

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 8 Julai, 2010

(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO PAMOJA
NA NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Pamoja na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**MHE. FATMA ABDULLA TAMIM (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadiryo ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI (K.n.y. WASEMAJI WAKUU WA
KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA
MICHEZO PAMOJA NA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA
VIJANA):**

Taarifa ya Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadiryo ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezopamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. JOEL N. BENDERA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):

Randama ya Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa muujibu wa Kanuni ya 38 (5) inapotokea kwamba Waziri Mkuu kwa udhuru maalum hayupo basi hayapo maswali kwa Waziri Mkuu. Hiyo ndiyo hali iliyojitekeza leo. Kwa hiyo, tunaendelea. Tuna maswali tu ya kawaida ambayo tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, swali linaulizwa na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 186

Askari wa Usalama Kuhesabu Kura wakati wa Uchaguzi

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi ya askari wa usalama n katika kipindi cha Uchaguzi ni kusimamia upigaji kura na sehemu ya kupigia kura, na kwa kuwa, Askari hao hawapaswi kujihusisha na kuhesabu kura:-

Je, Serikali inasema nini juu ya Askari ambao huhesabu kura kwenye Uchaguzi mbali mbali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa hakika swali hili limekuja wakati muafaka kwa sababu tunaelekeea kwenye Uchaguzi Mkuu hivyo napenda kusema kwamba kwa mujibu wa sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 sura ya 343 na sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 sura ya 292.

Askari wa Usalama waliopangwa kazini kuhakikisha taratibu za Uchaguzi zinazingatiwa, wanawajibu wa kulinda usalama katika vituo vya kupigia kura, vituo vya kuhesabia kura na pia vituo vya kujumlishia kura. Wakati wa kutekeleza kazi hiyo askari wa usalama wanatakiwa kuwa nje ya vyumba au umbali wa kuweza kushuhudia vile vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura.

Endapo itatokea vurugu kwenye kituo, Askari hao wa Usalama baada ya kupata maelekezo kutoka kwa msimamizi wa kituo au msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi anaweza kuingia ndani ya chumba cha kura au kwenye kituo na kushughulikia vurugu hizo.

Mheshimiwa Spika,kwa mujibu wa sheria ya Uchaguzi, msimamizi wa kituo akisaidiwa na msimamizi msaidizi wa kituo ndiye mwenye jukumu la kuhesabu kura zilizopigwa na wapiga kura kwa kituo hicho na kazi hii hufanyika mbele ya Mawakala wa Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi husika na watu wengine waliotajwa kwenye sheria za Uchaguzi.

Aidha, Serikali haijawahi kupokea malalamiko yoyote kuhusu Askari wa Usalama waliopangwa kulinda vituo vya kupigia kura kuhusika katika zoezi la kuhesabu kura. Hata hivyo, ikitokea Askari anaiingilia mchakato wa kuhesabu kura,atakuwa amevunja sheria za uchaguzi kama mtu mwengine yejete, hivyo Askari huyo atawajibishwa kwa mujibu wa sheria za uchaguzi kama mtu mwengine yejete. (*Makofî*)

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a)Kwa kuwa Askari hawa wa Usalama wanajua Mijini watu wameelimika kuhusu zoezi zima la kupiga kura na kuhesabu. Kwa hiyo, mambo haya zaidi wanayafanya Vijijini ambako wananchi wanawaogopa Askari. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu elimu kwa wananchi wetu wa Vijijini kuhusu hatua mbalimbali la kutoka zoezi la kupiga kura mpaka la kuhesabu kura na kumwondoa Askari ambaye hahusiki?

(b)Kwa kuwa, tunaambiwa kwamba Askari atakapokutwa anahesabu kura atawajibishwa. Je, watu hawa watakaomkuta Askari wapeleke wapi malalamiko yao wakati wananchi wetu hususani wa Vijijini wanaogopa Askari?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwanza sio kweli hata kidogo kwamba Watanzania Mijini na Vijijini wanaogopa Askari Polisi, Askari Polisi wanalinda usalama wa Raia na ni kimbilio la Raia muda wote, amjasikia habari hizo na sio kweli hata kidogo kwamba Watanzania wanaogopa Askari polisi.

Pili Msimamizi Mkuu wa kituo ndiyo mtu mwenye mamlaka yote wakati huo. Kwa hiyo, matukio yejete ya uvunjaji wa sheria za uchaguzi ikiwa ni pamoja na yale ambayo pengine yatatendwa na Askari Polisi, basi yapelekwe kwa Msimamizi wa Kituo au Msimamizi Msaidizi au Msimamizi wa uchaguzi wa Wilaya au Jimbo.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa sasa tumeshuhudia kwa macho yetu, nimeshuhudia mwenyewe Kiteto, nimeshuhudia Busanda, nimeshuhudia Biharamulo wananchi wanapojoitokeza wakakutana na Askari kabeba bunduki, wanarudi kule walikotokea.

Haya tumeyaona kwa macho anaebisha abishe, nimeyaona Tarime wananchi wanakimbia hata mikutano hawahudhurii kwa sababu hawakuzoea kuona Vijijini

Maaskari wenyе silaha, Waziri analieleza nini Taifa kwamba elimu kutolewa kwa Askari ni jambo muhimu ili wananchi wasiwaogope hawa Maaskari?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, Askari wanaolinda usala wa raia nchini kwetu wamekuwa wakitenda shughuli zao kwa muda mrefu sana. Tumeogopa wale wa kikoloni lakini sasa ni zaidi ya miaka 50 toka tuwe na Askari wetu wenyewe. Hivyo, basi iwapo kuna raia anamwogopa Askari basi anajidhania kwamba pengine ana makosa. Raia mwema ana sababu gani kumwogopa askari?

Lakini la msingi hapa ni kwamba katika swalı la msingi tuliulizwa kama tuna taarifa. Sisi taarifa tulizonazo ni kwamba wananchi wanaelewa vyema kabisa wajibu wa Askari kuwa ni kulinda usalama wao. (*Makofi*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Mimi nina swalı moja tu la kumwuliza. Katika majibu yake ametaja askari wa Usalama, sasa Askari wa Usalama katika mazingira ya Uchaguzi maana yake ni nini, ni Askari Polisi au ni Askari wa Usalama wa Taifa pamoja na polisi au hata Jeshi anaekuja pale pia ni Askari wa Usalama? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa maana ya sheria ya Uchaguzi, askari wa Usalama ni Askari mwenye sare. (*Makofi*)

Na. 187

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu - CDA

MHE. EPHRAIM N. MADEJE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali bado inayo dhamira ya kuufanya Mji wa Dodoma uwe Makao Makuu ya Serikali; lakini bado inaendelea kuimarisha miundombinu na kujenga majengo mbalimbali Mkoani Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali haioni kwamba haitimizi dhamira yake na kwamba hali hiyo inaweza kuwafanya wananchi wakose imani na Serikali yao?

(b) Kama dhamira ipo. Je, Serikali inashindwaje kuweka bayana mikakati thabiti ya kujenga miundombinu muhimu kwa ajili ya kuhamisha Makao Makuu kuja Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swal la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) napenda nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Serikali ilianzisha Programu ya Ustawishaji Makao Makuu ambayo ilikuwa inalenga kukamilisha uhamishaji wa Mako Makuu yake kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 1973. Katika kipindi hicho, Serikali ilikuwa imojiwekeea mkakati wa kuwezesha utekelezaji wa programu kwa kutenga shilingi za wakati ule milioni 370 kila mwaka kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1973.

Kwa bahati mbaya sana lengo hili halikuweza kufikiwa kutokana na uhaba wa Bajeti ya Serikali iliyosababishwa pamoja na mambo mengine Vita vya Kagera, kupanda kwa bei ya mafuta miaka ile ya 1980 na pia changamoto nyingine mbali mbali.

Hii iliathiri sana uharakishaji wa ukuaji wa Makao Makuu ya Serikali Mjini Dodoma kwa vile huduma muhimu na miundombinu mbalimbali ambayo ingewezesha uhamishaji wa Makao Makuu katika Mji wa Dodoma hazikuweza kujengwa. Kutokana na changamoto hizi, Wizara nyingi zimelazimika kuendelea kubakia Dar es Salaam.

Sasa baada ya maelezo haya napenda kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa nijibu swal la Mheshimiwa Ephraim Madeje, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Dhamira ya Serikali ya kuhamia Mji wa Dodoma bado iko pale pale na itaonekana wazi wazi kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambayo itazinduliwa hivi karibuni.

Kwa sasa Serikali inaweka juhudi kubwa kuiwezesha *CDA* pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi iweze kuchangia katika ujenzi wa Makao Makuu kwa kuweka huduma na miundombinu mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kuhamia Dodoma.

Aidha, Seriakli imelazimika kuendelea kuweka miundombinu na majengo Jijini Dar es Salaam ili kukidhi mahitaji yake kwa sasa wakati ikisubiri kuhamia Dodoma. Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha biashara, majengo hayo yanaweza kukodishwa kwa matumizi mengine pindi Serikali itakapokuwa imehamia Dodoma. (*Makofii*)

(b) Serikali ipo katika mchakato wa kutunga sheria ya Makao Makuu ambayo itabainisha mikakati thabit ya kuhamia Mjini Dodoma baada ya ujenzi wa miundombinu na huduma muhimu kukamilika. Kwa sasa kwa utaratibu wa ushirikishwaji wa sekta mbalimbali au utaratibu ambao unajulikana kwa jina la *Public Private Partnership* ambayo sheria yake tutaiwasilisha hapa Bungeni wiki ijayo.

MHE. EPHRAIM N. MADEJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal moja la nyongeza.

Katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 tuliahidi kwamba sheria hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameizungumzia ingetungwa katika kipindi hiki. Sasa naomba uhakikisho kwamba sheria hii sasa italetwa lini kwenye bunge lako Tukufu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Madeje kwanza kama Mkurugenzi wa *CDA* na pia Mbunge wa Dodoma Mjini kwa jitihada zake za kutaka kuhakikisha kwamba angalau Makao Makuu yahamie Dodoma haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, moja wapo ya nyenzo za kuharakisha uhamiaji wa Makao Makuu Dodoma ni kuwa na sheria ambayo inaweka bayana utaratibu wa kuhamia Dodoma, lakini mgawanyo wa kazi kati ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu na Manispaa ya Dodoma.

Sheria hii kama sheria zingine hufuata mchakato wa utungaji wa sheria kwanza kwa utafiti wa awali kufanyika kwa maana ya sera kuangaliwa, kazi hiyo imekamilika, tumewasilisha rasimu ya Sera kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu yaani *IMTC* na imeifanya kazi waraka wa Baraza ili Muswada uandaliwe nao uko tayari na wakati wowote unaweza ukajadiliwa na Baraza la Mawaziri na nina hakika sheria hii itatungwa wakati wowote kuanzia sasa.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali kwa hivi sasa ninavyozungmza Serikali inaendelea kujenga majumba ya Idara na Mashirika kule Dar es Salaam na mawizara. Je, kwa nini Serikali ikiwa ina nia thabiti ya kuhamia Dodoma, majengo hayo hayajengwi hapa Dodoma yanajengwa kule Dar es Salaam na badala yake Mheshimiwa Waziri anasema baadaye huko mbele sijui yatakuja kukodishwa. Kwa nini sasa hivi yasijengwe hapa Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeeleza kwamba ni kweli majengo mapya ya Serikali yanajengwa Dar es Salaam kukidhi haja ya sasa ya Serikali wakati ikifanya maandalizi ya kuhamia Dodoma hapo baadaye. Tumeeleza kwamba Dar es Salaam bado ni kitovu cha biashara na tuna hakika majengo hayo yatatumika na tukumbuke hatimaye Serikali ikihamia Dodoma siyo kwamba kila Idara ya Serikali imehamia Dodoma. Kuna baadhi ya Idara za Serikali zitabaki pale kwa ajili ya umuhimu wa kuwa pale kwa maana ya Dar es Salaam kuwa kitovu cha biashara kuwa na bandari, kuwa ndiyo vianzio vya reli na barabara na kadhalika.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza. Pamoja na kwamba majengo ya Serikali bado yanaendelea kujengwa Jijini Dar es Salaam. Lakini kwa kuwa hivi sasa Serikali imeamua kujenga Makao Makuu ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu hapa Dodoma. Je,

uamuzi huo upo na kama upo Ofisi hiyo ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu itaanza kujengwa lini hapa Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga Makao Makuu ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali hapa Dodoma. Tumetenga hekari 20 kwa ajili ya Makao Makuu ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na nataka kutoa taarifa rasmi hapa kwamba katika muda wa siku 10 zizazo wataalam kutoka nchi rafiki ya China kuja kuangalia ramani ya eneo hilo na ramani ya awali ya majengo ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa sababu nchi hii baadaye ndiyo itatupatia sehemu ya fedha zitakazotumika katika ujenzi wa Makao Makuu ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Pia nitoe taarifa kwamba katika wiki ya kwanza ya Agosti, mwenyewe nitampokea Waziri anayehusika na uchapishaji wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China hapa nchini, atakuja hapa nchini na katika mikataba ambayo tunatarajia kuiwekea sahihi ni mkataba wa ujenzi wa Makao Makuu ya Mpiga Chapa wa Serikali hapa Dodoma.

SPIKA: Wakati tukiendelea na suala hili, na mimi nitumie tu uzoefu wangu kwa sababu tunamwomba Mungu hapa kwamba tujadili mambo kwa dhati. Sasa kila kuhamia Dodoma, Serikali ijithahidi tu ituondolee hii aibu tu, maana yake hakuna utekelezaji wa dhati kuhusu dhamira hiyo. Ndiyo ukweli tu. Basi wengine huwa wananchukia nikisema hivyo. (*Makofi*)

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Lakini kwa kiasi fulani umenifilisi. Kwa kuwa Serikali kama ina nia ya dhati kabisa ya kuhamia Dodoma. Mfano tunao, nia ya dhati ya kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) hakina mfano duniani na kimefanywa na Serikali ya Tanzania. Ni dhati kabisa ambayo inaonekana kwamba Serikali ilikusudia kujenga Chuo na kimewezekana. Je, ni lini Serikali sasa iwaambie wananchi itahamia Dodoma, Mji Mkuu utakuwa Dodoma, na tuiache Dar es Salaam ibaki kuwa mji wa kibiashara kwa dhati, siyo kwa nadharia? (*Makofi*)

SPIKA: Mimi nadhani majibu utayapata yale yale. Kwa hiyo, tuendelee. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 188

TBC Kusikika Nchi Nzima

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Kwa kuwa vyombo vya habari ni muhimu sana katika kuwaelimisha wananchi na kutoa habari mbalimbali na kwa kuwa radio ya *TBC Taifa* ni namba moja kwa ubora wa kutoa habari lakini ni mikoa kumi na mbili (12) tu ndiyo inayosikika nchini na chombo hicho na mikoa mingine inakosa matangazo hayo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa chombo hiki kinasikika nchi nzima?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Redio ya *TBC* Taifa, ni namba moja kwa ubora katika kutoa habari hapa nchini. Ili wananchi wengi waweze kupata habari zinazotangazwa na *TBC* Taifa, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbali mbali za kuboresha huduma hiyo kwa kufunga mitambo mipyä na kukarabati ile ya zamani katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kuwa chombo hiki kinasikika nchi nzima ni kuendelea na ufungaji wa mitambo mipyä kwenye mikoa ambayo haipati vizuri au haipati kabisa matangazo yanayorushwa na *TBC* Taifa.

Kutokamilika mara moja kwa utekelezaji wa mkakati huo kunatokana na matatizo ya kifedha. Bajeti ndogo inayotolewa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mipyä na ukarabati wa mitambo iliyochakaa katika baadhi ya mikoa inachangia kwa kiasi kikubwa kuendelea kuwepo kwa tatizo la kutopata matangazo ya *TBC* Taifa katika baadhi ya mikoa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ufungaji wa mitambo mipyä na ukarabati wa mitambo iliyochakaa umekuwa ukifanika kwa awamu kutegemea na kiasi cha fedha kilichopatikana. Mwaka huu wa fedha maka (2009/2010) jumla ya shilingi bilioni mbili tu zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kurushia matangazo katika masafa ya kati yaani (*FM*) ambazo zilipangwa kufungwa katika mikoa ambayo matangazo ya *TBC* Taifa hayasikiki.

Mikoa hiyo ni pamoja na Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Tanga, Ruvuma, Shinyanga na Zanzibar. Mkoa wa Pwani na Pemba itawekewa mitambo yake ya Redio mwaka ujao wa fedha 2011/2012. Kwa sasa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani na Pemba inapata matangazo kutoka vituo vya Kisarawe na Tanga.

Hadi sasa ninavyozungumza mkoa wa Rukwa tayari unapata matangazo ya *TBC* Taifa na mkoa wa Singida unapokea matangazo ya *TBC* I na *TBC* Taifa. Mitambo hiyo ya kurushia matangazo tayari imeagizwa kutoka nchini Afrika ya Kusini na itawasili nchini wakati wo wote. Mara tu itakapowasili itafungwa kwenye mikoa niliyoitaja. Ni matarajo yetu kuwa hadi Septemba mwaka huu ufungaji wa mitamob hiyo utakuwa umekammilika.

Hata hivyo, lengo la Serikali bado linabaki pale pale, kuhakikisha kwamba *TBC* Taifa inasikika nchi nzima. (*Makofi*)

MHE. MGENI JADI KADIKA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hata hivyo namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Je, mikoa hiyo iliyokuwa haisikiki atahakikisha vipi kuwa watapata mawasiliano wakati wa uchaguzi ili wapate kuelimika wapiga kura?

Swali la pili, kwa kuwa chombo hiki cha redio na *TV* ya *TBC* ni chombo muhimu sana. Lakini ni kwa nini kiko nyuma sana kuelimisha waadili ya Watanzania kuhusu mavazi na kuhusu kutunza mazingira? (*Makofi*)

SPIKA: Hilo la pili naona limechomekewa hapo. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri najua uwezo wako, basi lifahamishe Taifa.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi. Naomba kumtoa wasi wasi Mheshimiwa Mbunge na Watanzania. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba chombo hiki cha Umma kinasikika nchi nzima na ndiyo maana juhudu kubwa inafanyika kama ambavyo nimezungumza. Ifikapo mwisho wa mwezi wa Septemba, 2010 nataka kumhakikishia kabisa kwamba ile mikoa yote ambayo bado haina usikivu itapata. Kwa sababu tayari vyombo vipo vimeshanunuliwa, mitambo imeshaingia, kilichobaki ni kufungwa.

Kama nilivyooleza mikoa hiyo itafungwa mwisho wa mwezi wa Septemba, 2010 tayari nchi nzima sasa *TBC* Itakuwa inasikika. Kwa hiyo, wale wapiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu na kila kitu kitakuwa kimekuwa tayari na bahati nzuri *TBC* imeweka mikakati mizuri sana ya kuhakikisha kwamba suala la Uchaguzi Mkuu tunalipa kipaumbele ili wananchi waweze kupata habari. Kwa hiyo namtoa wasi wasi. (*Makofi*)

Swali la pili, kuhusu maadili. Nataka niseme tu kwamba suala la maadili limekuwa likizungumzwa humu ndani ya Bunge kwa muda mrefu, hasa kuhusu vyombo vyetu vya redio, vyombo vya magazeti na televisheni. Ukweli wenyewe ni kwamba tunajitahidi tuna kipindi maalum cha kuzungumzia maadili ya Taifa ambacho kinarushwa na Kurugenzi yetu ya Utamaduni kuelezea utamaduni wa Mtanzania.

Hili ni somo kwa Watanzania waelewe. Lakini tukumbuke kuna suala la utandawazi ambalo halizuliki. Si lazima *TBC* peke yake viko vyombo vingine. Kuna *CNN* kuna vyombo vingine vya dunia ambayo yanaonyesha. Suala la utandawazi nalo ni tatizo ambalo sisi wote katika dunia lazima tuweze kuona kwamba hali hiyo ni ngumu na haiwezi kuzulikia. Tutajitahidi sisi kama Wizara husika kutoa elimu ili Watanzania wabadilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba sitatenda haki kama sitakupongeza wewe mwenyewe. Napenda nichukue nafasi hii kwa sababu ni mahali pake kwa uamuza wako wa busara wa kuweza kuamua kwamba Bunge badala ya kipindi chake kionekane

muda unaostahili lakini ukasema kwa sababu ya *World Cup* basi Watanzania waone. Huo uamuzi ulikuwa ni wa busara na tunakupongeza sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa Redio Tanzania mpaka ikawa *TBC* na vyombo vingine vya habari vimefunga mitambo yao katika Wilaya ya Kisarawe, Mkao wa Pwani. Na kwa kuwa mitambo hiyo inawezesha redio hizo na vyombo vingine vya habari kusikika nchi nzima. Lakini kwa mkao wa Pwani na Mheshimiwa mwenyewe, Naibu Waziri amethibitisha hawawezi kusikia vizuri.

Je, haoni kwamba hawatendei haki watu wa Mkao wa Pwani pamoja na nia nzuri ya kutoa eneo la kujenga mitambo hiyo? Analiable nini Bunge lako Tukufu na watu wa Pwani watapata matangazo yao lini?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli Pwani kuna tatizo la usikivu, mitambo yote iko Kisarawe. Tena siyo ya *TBC* tu ni ya vyombo vyote. Minara iko pale Kisarawe itakuwa imejaa.

Lakini kama angenifuutilizia vizuri kwenye jibu langu ni kwamba hivi ninavyozungumza mkao wa Pwani unapata matangazo ya *FM* ya *TBC* kutoka Kisarawe yenye kipimoja na Tanga. Lakini nataka nimhakikishie kwamba jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba mkao huu ambao mitambo yote ipo tunaitendea haki kwa kupata usikivu. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, siruhusu tena swalii la nyongeza kuhusu hili. Ila nilikuwa nataka tu kwamba katika majibu haya nimeona jambo ambalo si vyema tukaendelea nalo. Tunapotaja mikoa ya Tanzania tusijumuise Zanzibar kama ni Mkao. Kwa sababu Zanzibar siyo mkao. Hii inawezekana ikawa ni moja ya kero ya Muungano. Kwa sababu unaposema Morogoro, Mtwara, Tanga, Ruvuma, Shinyanga na Zanzibar kuna baadhi ya watu unawaleta hisia ambazo ni ngumu.

Kwa hiyo, nimeona katika baadhi ya machapisho ya Serikali maandiko kama haya. Zanzibar kuna mikoa mitano. Kwa hiyo kama unakusudia mikoa utaje, ama uweke, umalizie pale Shinyanga halafu useme na huko Zanzibar yaani iwe ni kitu tofauti, hii itatusaidia. Ahsante sana, tunaendelea. (*Makofi*)

Na. 189

Tatizo la Umeme Katika mji wa Kahama

MHE. JAMES D. LEMBELI aliuliza:-

Kwa kuwa mji wa Kahama unakuwa kwa kasi kiuchumi lakini upanuzi wa huduma ya umeme umeshindwa kwenda sambamba na kasi hiyo hivyo kusababisha usumbufu mkubwa:-

- (a) Je, ni sababu gani za msingi kwa shirika la *TANESCO* Kahama kuwafanya wananchi kusubiri kati ya mwaka mmoja hadi minne kuunganishiwa huduma hiyo?
- (b) Je, ni lini maeneo ya Kata ya Kahama Mjini, Nyihogo na Kata ya Mhunga yatapata umeme kwa utaratibu wa kawaida?
- (c) Je, ni lini Serikali itaunganisha umeme wa Buzwagi na mji wa Kahama ili kuondokana na tatizo la umeme unaotoka Ibadakuli kwenda Kahama ambao hukatika mara kwa mara?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, waombaji wa huduma ya kuunganishiwa umeme walioko kwenye maeneo yaliyo na miundombinu ya umeme, hupata huduma hiyo katika kipindi cha wiki moja hadi mwezi mmoja toka wanapoomba. Katika maeneo yasiyo na miundombinu ya umeme huduma hiyo hutegemea mipango na Bajeti ya Shirika kwa eneo husika. Aidha, kama kuna wananchi wa Kahama ambao miundombinu ya umeme imefika maeneo yao na wameomba kuunganishiwa umeme miaka minne iliyopita mpaka sasa hawajapata huduma hiyo, naomba taarifa zao ili Wizara yangu iweze kushughulikia.
- (b) Mheshimiwa Spika, Kata ya Kahama mjini ina umeme tangu mwaka 1982. Kata ya Nyihogo ina maeneo yenye umeme na kwa sasa kuna mradi wa kusambaza umeme ambao ujenzi wake unaendelea. Huduma ya umeme katika Kata ya Mhungula itapatikana kulingana na upatikanaji wa fedha. Nitamwomba Mheshimiwa Lembeli atusaidie jina hapo baadaye kwa kuhusu Kata ya Mhunga ama Mhungula kuna tofauti katika kumbukumbu zetu kuhusu usahihi wa jina hili. Lakini atuwie radhi kama hatujalipatia.
- (c) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuunganisha umeme wa Buzwagi na mji wa Kahama upo na tathmini ya mpango huo inaendelea. Kazi zinazotarajiwa kufanywa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kupozea nguvu ya umeme wa gridi kuutoa kwenye msongo wa 220/33kV Wilayani Kahama kitakachokuwa na ukubwa wa MVA 30. Katika kutekeleza mpango huo *TANESCO* imetenga shilingi bilioni nne katika Bajeti yake ya mwaka huu 2010 kwa kazi za awali ikiwa ni pamoja na gharama za kumtafuta Mshauri Mwelekezo wa Mradi (*Consultant*).

MHE. JAMES D. LEMBELI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwanza kwa niaba ya wananchi wa mji wa Kahama napenda kuipongeza Serikali kwa kuanza

mchakato wa kuwezesha umeme unaotumika mjini Kahama na hivyo kuondoa kero ya muda mrefu ya kukatika umeme mara kwa mara katika mji huo.

Pamoja na shukrani hizo nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa yapo maeneo mengi ya mji wa Kahama kama vile ya Majila, Kasela, Igomelo na Nyakato tayari yana mtandao wa umeme.

Je, ni kwa sababu gani za msingi wananchi wenyе vipato vya chini wanaoishi katika maeneo hayo hukumbana na matatizo na vikwazo mbalimbali vya kuunganishwa umeme ukilinganisha na watu wenyе vipato vizuri, matajiri, na watumishi wa Serikali ambao nao pia wanaishi katika maeneo hayo hayo? (*Makofī*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni utaratibu wa Shirika la *TANESCO* kuwashudumia wateja wake, ama wateja wataratiwa kwa usawa.

Ninachoomba ni kumwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kahama endapo kuna jambo linalowakwaza la kiutendaji atupatie taarifa hizo moja kwa moja ama kwa siri tunafahamu uovu ama vitendo visivyoendana na maadili ya kazi katika baadhi ya wafanyakazi wa shirika letu limekuwa likijitokeza katika maeneo kadhaa lakini kwa kushirikiana na wananchi tumefanikiwa kupunguza eneo hilo kwa kiasi kikubwa sana.

Kwa hiyo, niombe pia wananchi wa Kahama watupe hizo taarifa kwa siri kwa kuwatambua ambao wanahusika na mchezo mchafu.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Taifa kwa ujumla kwamba tutaendelea kuchukua hatua kali kuhakikisha kwamba hawa wachache tunawadhibiti na kuondoa kabisa katika shirika. Ahsante sana. (*Makofī*)

Kuongeza Mtandao wa Usambazaji Umeme – Mbinga

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Kwa kuwa uwezo wa mashine za kuzalisha umeme Mbinga ni mkubwa ikilinganishwa na matumizi halisi ya sasa hasa kutohana na kukosekana/upungufu wa mtandao wa usambazaji wa umeme (*Low voltage distribution network 0.4 kV na high voltage 11Kv*):-

Je Serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao huo kwa mwaka 2009/2010?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kama tulivyoeleza hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, tarehe 21 Aprili, 2010, ni kweli Mbinga imeshapata uzalishaji wa umeme wa jenereta mbili zenyne uwezo wa kuzalisha jumla ya *MW 2.5* ingawa kwa sasa matumizi ya juu hayazidi *MW 1*. Hata hivyo maeneo yote ya Mbinga yametathiminiwa na mahitaji makubwa zaidi ya matumizi ya hivi sasa kulingana na shughuli za kiuchumi na jamii hasa zile za wakulima wa kahawa, ambao kwa sasa wanatumia nishati ya gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* katika Bajeti yake ya ndani ya mwaka 2009, ilitenga shilingi 150,000,000/= kwa ajili ya kuongeza mtandao wa umeme katika mji wa Mbinga. Fedha hizo zilitumika kujenga njia za umeme wa msongo wa *KV 11* yenye urefu wa kilometra 1 na kufunga *transfoma* yenye uwezo wa *KVA 100* na kujenga njia ndogo yenye urefu wa km 2, ili kusambaza umeme katika maeneo ya Makita na Tanki La maji. Vile vile zilitumika kufunga *transformer* yenye uwezo wa *KVA 100* ili kusambaza umeme maeneo ya Matarawe na Ruhuwiko na kujenga njia ndogo yenye urefu wa kilometra 5 ili kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali katika mji wa Mbinga; kazi hizi tayari zimekamilika. Kazi inayoendelea sasa ni ya ujenzi wa njia ndogo yenye urefu wa kilometra 2 ili kusambaza umeme maeneo ya Matarawe na Ruhuwiko na kujenga njia ndogo yenye urefu wa kilometra 1.5 ili kusambaza umeme Mbambi na Kiwandani.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupanua mfumo wa usambazaji umeme katika Wilaya ya Mbinga umo katika utekelezaji wa mradi wa njia kuu ya msongo wa *KV 132* Makambako – Songea. Katika mradi huu maeneo yaliyojumuishwa katika usambazaji umeme ni pamoja na Kata za Uilambo na Maposeni, Matomondo, Liganga, Kitai, Amani Makoro, Masuguru Gam, Mkako, Kigonsera, Lipumba, Mtama na kuongeza mtandao wa umeme katika mji wa Mbinga; inakadirwa kuwa jumla ya wateja 4,273 wataunganishiwa umeme.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa kuna upungufu wa kujaza jenereta hizo. Na kwa

kuwa, kazi hii ya kusambaza umeme imekuwa ikichukua muda mrefu, jambo ambalo mimi ninaona ni hasara kutembeza jenereta ambazo zinatumia mafuta ya bei mbaya wakati kuna wateja wengi tu wanaozunguka mji huo.

(a) Je, katika Bajeti yake ya mwaka huu atatoa kipaumbele angalau kwa maeneo yale ya karibu sana na hizo jenereta?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kuna fununu ambazo jana nimezisoma kwenye magazeti juu ya tatizo la msongo wa umeme wa *KV 132* kutoka Ubungo mpaka Makumbusho, ambao inadaiwa kwamba umeshindwa kuwaka vizuri kutoptaka na hoja za Mheshimiwa Mzee Kakobe. Je, unaweza pia ukatufafanulia jambo hili ili kututoa katika mkanganyiko?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli kama tulivyosema kwamba mji wa Mbinga tunaupa kipaumbele na hasa kwa kuzingatia kwamba uwezo wa mitambo iliyopo ni mkubwa kuliko matumizi ya sasa. Na ndio maana katika jibu la msingi tumeelezea juhudzi zilizopo na zinazoendelea kufanywa na Shirika la *TANESCO* kwa ajili ya kutanua ule mtandao, malengo ikiwa ni kuhakikisha kwamba tuna *maximize* matumizi; tunautumia umeme wote huo uliopo pale kwa ajili ya manufaa ya wananchi. Hili la pili kuhusu matatizo aliyoyasikia; kwanza nikiri tu kwamba mimi sijaiona hiyo taarifa kwenye vyombo vya habari, lakini masuala ya usambazaji wa umeme ni Sayansi na hatutarajii kwenda kwa imani yoyote ile katika mazingira hayo, iwe ni imani ya kiroho au imani nyingine, tuseme *super natural power*. Lakini tunachosema tu ni kwamba mradi ule unaendelea vizuri na uko katika hatua za mwisho kabisa. Tunaamini kwamba hivi karibuni tutautangazia Umma kuhusu kuanza kazi au kuwashwa kwa umeme; uboreshwaji wa usambazaji wa umeme kwa kutumia huo msongo wa *KV 132* kama vile ambavyo Serikali kwa kupitia Shirika la *TANESCO* imepangilia kwa miaka kadhaa.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TV* zinafanya kazi tu kwenye maeneo ambayo yana umeme, kwa sababu sijawahi kuona *TV* ambayo inatumia betri. Katika kuhakikisha kuwa *TBC* inasikika nchi nzima kama ilivyoainishwa leo asubuhi, Wizara ya Nishati na Madini itashirikiana vipi ili kuhakikisha kuwa maeneo yote ya pembezoni hasa katika Mkoa wetu wa Manyara ambako sasa hivi hakuna *TV* na hata Redio katika maeneo mengine, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki yao ya msingi ya kupata habari?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Martha Umbulla. Mbunge Viti Maalum - Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mipango inapopangwa na Serikali katika sekta mbali mbali, inapangwa kwa kuoanisha na kuainisha na mahitaji na vitu vingine ambavyo vinawezesha jambo moja kufanyika. Kwa mfano katika hili la *TBC* kueneza

huduma ya upatikanaji wa masafa yake katika sehemu mbalimbali za nchi; kwa vyovoyote vile pia linaendana na juhudi zinazofanywa na Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini, katika kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, ambacho ninaweza kusema ni kwamba wote tunafahamu juhudzi za Serikali zinazofanywa sasa hivi. Juzi hapa tumetoa taarifa kwa Kauli ya Serikali, katika mikoa 16 ya Tanzania, ambayo tunasambaza umeme katika maeneo mbalimbali na mionganoni mwa maeneo haya ni yale ambayo yako katika Mkoa wa Manyara. Lakini si hiyo tu miradi inayosambazwa kwa kupitia wakala wa nishati vijijini peke yake, kuna miradi pia inayofanywa na Shirika la *TANESCO* lenyewe kwa kutumia Bajeti zake. Lakini pia tuna miradi ambayo hivi karibuni nimeisema; tuna miradi ambayo inafadhiliwa na *African Development Bank* (Benki ya Maendeleo ya Afrika), inaihusu mikoa kama minne hivi, miradi inayofadhiliwa na *MCC*, ambayo nayo kwa pamoja zinaongeza ufikishaji na usambazaji wa umeme katika maeneo mbali mbali ya nchi. Kwa hivi, nina mhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, *TBC* kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini tunafahamu umuhimu wa kuwafikishia wananchi huduma hii muhimu, kuwawezesha kupata kile ambacho wanakitarajia. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa ni matangazo tu. Naanza na wageni. Leo tunazo Wizara mbili kwa hiyo orodha ni ndefu kidogo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchika, Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo ni kama ifuatavyo. Ndugu Seti Kamuhanda – Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo – yule pale. Ahsante sana na karibu sana Katibu Mkuu. Katibu Mkuu, amefuatana na Wataalam Waandamizi wafuataao, Bwana Gasper Mwembezi – Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Alhaji Adam Kiama – Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bwana Tido Mhando – Mkurugenzi Mkuu wa *TBC*, Bwana Habi Gunze – Mkurugenzi wa Utangazaji Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TICRA*), Bwana Clement Mshana – Mkurugenzi wa Idara ya Habari, Bwana Raphael Hokororo – Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari, Profesa Herman Mwansoko – Mkurugenzi wa Idara ya Utamaduni, Bibi Angela Ngowi – Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Utamaduni, naona wasaidizi labda wamekaa sehemu nyingine; Bibi Rose Lukindo – Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Utamaduni, pia wako upande huu, ahsante sana na wote kwa ujumla wenu karibuni sana. (*Makofi*).

Wageni wengine ni Ndugu Leonard Thadeo – Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Michezo, Bibi Juliana Yasoda – Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mawendeleo ya Michezo, Bibi Recho Koweya – Mkurugenzi Msaidizi pia Idara hiyo hiyo, Ndugu Iddi Kipingu – Mwenyekiti wa Baraza la Michezo, Bwana Alex – Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo – Malya. Dr. Anna Kishe – Katibu Mtendaji Baraza la Kiswahili la Taifa, Ndugu Wilfred Nyachia – Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utangazaji la Taifa, Ndugu Mkumbwa Ally – Kaimu Mhariri Mtendaji wa Shirika la Magazeti ya Serikali; haya mambo ya Kukaimu kaimu nimeyazungumza humu ndani. Kuna watu wanakaimu mwaka, miaka, sijui kuna nini sijui? Lakini ahh, basi bwana! Bibi Joyce Fiso – Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu, Ndugu Juma Bakari – Mkuu wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo na Ndugu Gonche Materego – Katibu

Mtendaji wa *BASATA*, yule pale ahsante. Wote kwa ujumla wenu karibuni sana. Wageni binafsi wa Mheshimiwa Waziri, *Captain* Mstaafu Mkuchika, ni Bibi Anna Ernestina – Mkewe Mheshimiwa Waziri, yule pale ahsante sana. Wanamichezo wa watu wenye ulemavu wa kusikia, viungo na ulemavu wa ngozi, nadhani Mkalimani anaendelea nao pale na Bwana Kassim Mapili – Mwenyekiti wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania. Karibu sana Bwana Kassim; ahsante sana kwa kudumisha muziki tangu enzi zetu zileee! (*Makofi*).

Sasa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ni kama ifuatavyo. Kwanza Bibi Kijakazi Mtengwa – Katibu Mkuu, yule pale Bibi Edin Mangesho – Naibu Katibu Mkuu, naona hapa jinsia inazingatiwa kweli Katibu Mkuu na Naibu wote ni wanawake, ni jambo zuri tu. Ndugu Sauli Kinemela – Kamishna wa Kazi, Ndugu Ernest Ndimbo – Mkurugenzi wa Ajira, Bibi Joyce Shaidi – Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana, Bibi Doroth Uwiso – Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Ndugu Haji Janabi – Mkurugenzi Mipango na Sera, wote karibuni sana. Sasa viongozi wengine katika Taasisi za Wizara hii ya Kazi ni Ndugu Cosmas Msigwa – Mtendaji Mkuu wa *CMA*? Ndugu Elieza Mwasele – Mtendaji Mkuu wa *TAESA*, Ndugu Hamisi Kitumbo – Mtendaji Mkuu wa *OSHA*, Ndugu Ferdinand Kasege, – Mkurugenzi wa *NIP* na Ndugu Leonidas Rwejuna – Mkurugenzi wa Fedha na Utawala *NIP*, wote ahsante sana na karibuni sana. (*Makofi*).

Wapo Viongozi wanne wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), ambao wameongozwa na Ndugu Abubakar Rajab – Mwenyekiti wa Bodii ya *NSSF*, Ndugu Ramadhani Dau – Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF*, yule pale. Hongera sana *NSSF* kwa kazi nzuri sana mnayoifanya katika sekta nyingi sana hapa nchini. Wapo Viongozi 16 wa Vyama Vya Wafanyakazi na Waajiri, ambao wanaongozwa na Dr. Aggrey Mlimuka – Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri (*ATE*), ahsante. (*Makofi*)

Basi baada ya hao sasa, inaelekea Mheshimiwa Kapuya, Waziri wa kazi, hana wageni binafsi anao tu hawa wakutoka Wizarani na Taasisi. Kwa hiyo, tunaendelea na matangazo. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge wa Ilala, anao wageni wake ambao ni wanafunzi sita kutoka Chuo cha Biashara(*CBE*) Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Evodia Bonifas. Ahsanteni sana na karibuni sana, tunawatachia mafanikio katika masomo yenu. Kuna wageni wa Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, wanafunzi wanenye, lakini hakuwataja na wala hakusema wanasona wapi, wageni wa Mheshimiwa Zulekha, wale pale, karibuni sana ahsanteni sana, sijui wanatoka Zanzibar au wapi sijui. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa John Cheyo, eeh, mchanganyiko huu hata haueleweki vizuri. Mheshimiwa Susan Lyimo na John Cheyo, *anyway*, mimi kazi yangu jamani ni kutangaza tu. Kwa hiyo, ni Ndugu Lydia Lipuba Mawala – *Program Officer* wa *UDP* - Makao Makuu na Ndugu Samson Mwenda – Mkurugenzi wa Kampuni ya *Solar Energy*, ambaye pia atakuwa na maonyesho, eneo la maonesho na panapouzwa magazeti hapa Bungeni. Wapo pia wanafunzi 88 wa mwaka wa nne wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki. Wanaosomea Shahada ya kwanza ya udaktari na sasa hivi wanafanya mazoezi katika Hospitali ya Mirembe. Wale pale Wataalam wetu, ahsante sana. Tunawatachia mafanikio katika shughuli zenu tuna

upungufu mkubwa sana wa Madaktari nchini. Kwa hiyo, basi mfanye bidii muungane na madaktari wengine ili tupunguze tatizo la kutokuwa na madaktari wakutosha hapa nchini. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Paul Kimiti, ambaye ni Ndugu Julius Mtuka. Wapo wageni wa Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Miundombinu, ni Ndugu Sifaeli Kiwoli – Katibu Tawala Msaidizi, Mipango na Uratibu, Ndugu Abdallah Mwambi – Mhasibu wa Mkoa, nadhani ni Mkoa wa Dodoma basi. Ndugu Samuel Mashindike – Mchumi Mkuu na Ndugu Hebeneza Mlinga na yeye ni Mchumi, ahsante sana na karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Wabunge, leo pia wapo wageni wa Mheshimiwa Mwanawetu Zaraffi, ambaao ni Bwana Goodluck Selemani, sijui yuko upande gani? Ndugu Halima Saburi na Salma Abdul, wako *Basement*. Kuna Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo wa Kata ya Haneti, wakiongozwa na Mheshimiwa Ibrahim Mnduli – Diwani wa Kata hiyo ya Haneti, wale pale; karibuni sana .Pamoja na wale wageni wa Mheshimiwa Profesa Kapuya, Waziri wetu wa Kazi, kumbe wapo viongozi wa *TUCTA* na *SIBUKA*. Viongozi wa *TUCTA* bahati mbaya sikupewa majina lakini popote popote walipo.

Basi hao ndiyo wageni wetu kwa leo nadhani nimemaliza orodha yote. Lakini matangazo ya kazi ni haya yafuatayo.

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba leo saa tano asubuhi Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi mkutane ili kuzingatia baadhi ya Shughuli za Miswada ambayo inakuja mbele yetu. Kwa hiyo, Kamati ya Fedha na Uchumi Mkutano katika Ukumbi Namba 231 saa tano asubuhi leo. Mheshimiwa Elietta N. Switi Katibu wa Chama cha Wabunge Wanawake Tanzania anaomba Wabunge wote wanawake ambaao hawakuchukua aha! Sasa hii basi bahati mbaya nimeanza kuisoma lakini tangazo hili lah! Wale ambaao hawakuchukua vitengeta vya TAWLA wakachukue kwa Angelina Sanga, Chumba Namba 320. Hili tangazo siyo mh! Basi tu, lakini mngeweza kuarifiana wenyewe tu. Hivyo vitengeta ni kwa Angelina Sanga, Chumba Namba 320, Jengo la Utawala, ghorofa ya tatu.

Waheshimiwa Wabunge kuna maonyesho ya Chuo Kikuu cha Mzumbe ambayo yanaeendelea katika viwanja vya maonyesho vya Bunge na yapo machapisho mbalimbali na ya aina nyingi tu, ukizingatia taaluma. Kwa hiyo, mnaombwa Waheshimiwa Wabunge muweze kufika pale na kuweza kujipatia elimu hii na taalima hiyo muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya kulenga Shabaha anaomba kutangaza kwamba katika zoezi la kulenga shabaha jana huko Makutupora matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Kulenga shabaha kwa kutumia *sub machine gun*, ah! Hivi naruhusiwa kuwa na *sub machine gun* kumbe! Basi aliyepata alama za juu au nianze na wa chini kidogo Mheshimiwa Issa Kassim Issa, ana alama 95, Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami ana alama 99 na Mheshimiwa Parmukh Sigh Hoogan ana alama 102. Huyu ndiye bingwa wetu hapa Bungeni kwa kulenga shabaha kuwa kutumia SMG. (*Makofi*)

Sasa kundi la pili ni wale walenga shabaha kwa kutumia bastola, wa tatu ni Parmukh Sigh Hoogan inaonekana huyu silaha sijui anazo ngapi maana yake ana bastola na *SMG*. Halafu Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami amepata alama 10 na bingwa ni Mheshimwa Said Juma Nkumba, amepata alama 12. Hongera sana wote kwa mafanikio hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba leo saa saba wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane katika ukumbi namba 227. Kwa hiyo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji sasa saba mchana katika Ukumbi namba 227.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo naomba sasa Katibu atuelekeze katika hatua inayofuata.

KAULI ZA MAWAZILI

Tatizo la Uchakachuaji Mafuta Nchini

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007, kanuni namba 49, naomba kutoa kauli ya Serikali kuhusu tatizo la uchanganyaji wa mafuta ya Petrol nchini yaani uchakachuaji kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Mfumo wa uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini. Ili kuielewa biashara ya mafuta ya petroli nchini ni vizuri kuelewa namna ya uagizaji na usambazaji wa bidhaa hiyo unavyofanyika. Mfumo wa uagizaji na usambazaji ndiyo uti wa mgongo wa biashara hii ya mafuta hasa katika kuhakikisha kuwa mafuta yanapatikana sehemu zote za nchi, kwa wakati wote na kwa bei stahili. Mfumo uliopo hivi sasa umeweza pamoja na kuhitaji ufanisi katika maeneo mbalimbali kuhakikisha bidhaa hii inapatikana katika maeneo yote ya nchi na kwa wakati wote. EWURA kama Mamlaka ya Udhhibitii ndiyo chombo cha usimamizi wa biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, uagizaji wa Mafuta. Inakisiwa kuwa Tanzania inatumia kiasi cha tani milioni 1.7 za mafuta ya petroli kwa mwaka. Mafuta mengi yanayoingizwa hapa nchini huagizwa kutoka nchi za Mashariki ya Kati yaani *Arabian Guff*. Kwa mwaka 2009 makampuni yapatayo 25 ndiyo yaliyohusika na biashara ya kuagiza mafuta hapa nchini. Makampuni haya yanaagiza mafuta yaliyosafishwa kulingana na mahitaji yanayokidhi umiliki wao katika soko. Mchanganuo wa kiasi cha bidhaa za mafuta yaliyoagizwa mwaka 2009 yanaonyeshwa katika jedwali ambalo kwa sababu taarifa hii itasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge basi wataona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Takwimu za Biashara ya Mafuta. Katika kipindi cha mwaka mmoja kati ya Julai, 2008 – Juni 2009, makampuni ya mafuta yaliingiza nchini bidhaa ya mafuta kiasi cha tani milioni 1.52. Katika kipindi cha Julai ,2009 – Aprili, 2010 kiasi cha tani 1.1 milioni za mafuta ya petroli kiliingizwa nchini na inakisiwa kuwa kufikia

mwisho wa July 2010 takriban tani milioni 1.4 za mafuta zitakuwa zimeingizwa nchini. Taarifa za mwaka 2008 kuanzia mwezi Januari – Desemba zinaonyesha kuwa jumla ya mafuta yaliyoingizwa nchini kiasi cha tani milioni 1.69 kati ya hizo kiasi cha tani 578,689 karibu theluthi moja ya jumla iliingizwa kama mafuta ya nchi za jirani yanayopitishwa kwenye bandari ya Dar es Salaam. Hata hivyo, tani 217,331 sawa na 40% kati ya hizo ziliingizwa katika soko la ndani baada ya kuhalalishwa yaani *localisation*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto za udhibiti wa sekta ya *Petrol* ni pamoja na waombaji kutotimiza masharti ya leseni, uuzwaji wa mafuta yasiyokidhi viwango, uuzaji wa mafuta yaendayo nchi za nje isivyo halali yaani *dumping*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Uchakachuaji. Changamoto kubwa ambayo *EWURA* inapambana nayo ni tatizo la uchanganyaji haramu au uchakachuaji hasa wa mafuta ya taa au ya ndege kuchanganywa na *petroli* au *Diesel* unaofaywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kwa lengo la kupata faida kubwa inayotokana na udanganyifu kwa wateja kwa kuwauzia bidhaa iliyochanganywa na isiyokidhi viwango kama *petroli* au *Dizeli* halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa chanzo au kishawishi cha uchakachuaji kiko kwenye mfumo wa kodi ambapo bidhaa ya *Petrol* inatozwa kodi ya Shilingi 539, *Diesel* inatozwa kodi ya shilingi 514 wakati mafuta ya Taa yanatozwa kiasi cha shilingi 52 na mafuta ya ndege hayatozwi kodi kabisa. Hivyo kuna tofauti kati ya shilingi 539 hadi 462 kwa kila lita ya mafuta inayochanganywa kama faida kwa mfanyabiashara. Serikali ilichukua hatua ya kupunguza kodi ya mafuta ya taa ili kutoa nafuu kwa wananchi wenye kipato kidogo ili waweze kumudu kupata nishati hiyo muhimu katika maisha na kuokoa misitu na mazingira kama njia kuu ya kupata nishati kwa wananchi wenye kipato kidogo hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika jedwali ambalo litaonekana kwenye taarifa tofauti ya kodi za Serikali kati ya mafuta ya *Diesel* na mafuta ya Taa ni wastani wa shilingi 462 kwa lita moja. Kwa kuchanganya mafuta ya Taa na *Diesel* na kuyauza kama *Diesel*, kiasi cha shilingi 462 kwa kila lita zikiwa ni kodi za Serikali hukwepwa na wafanyabiashara wasio waaminifu kwa nia ya kujitajirisha na kuikoseha Serikali mapato. Tathmini ya hasara inayotokana na uchakachuaji wa *damping* hajafanyika nchini, lakini kulingana na taarifa mbalimbali inakisiwa kwamba uchakachuaji mpaka mwezi June 2010 umesababisha hasara ya kati ya shilingi bilioni 100 na 200. Uchakachuaji katika nchi za jirani kama Kenya na Uganda umepungua sana ikilinganishwa na Tanzania kutokana na nchi hizo kutumia mfumo wa mabomba kusafirishia mafuta na vifaa vyta kisasa vyta *Making System* kama tunavyotarajia kutumia kuanzia mwezi August 2010 hapa Tanzania. Kenya wanatumia mabomba kusafirishia mafuta na *Making System* ambapo Uganda wanatumia *Making System* pia.

Mheshimiwa Spika, Uchanganyaji wa Mafuta au Uchakachuaji. Tangu kuanza juhudzi za kupambana na tatizo la kutokomeza uchakachuaji mwezi May 2007, *EWURA* imekagua vituo na maghala 454 ya mafuta, magari 35 na imechukua na kupima sampuli 1289 kutoka sehemu hizo. Kati ya hizo sampuli 368 sawa na 30% hazikukidhi ubora wa mafuta uliotakiwa, mnamo mwezi Mei, 21 – 25 2010 *EWURA* ilifanya ukaguzi wa kushtukiza katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro uliohusisha vituo 47 na matokeo ni kuwa vituo 21 havikukidhi viwango na vilipewa adhabu stahiki kisheria.

Mkoani Arusha 50% ya vituo havikukidhi viwango na kilimanjaro 37% havikukidhi viwango. Vituo vingi sawa na 44% Mkoani Arusha vilikuwa na mafuta yasiyokidhi viwango. Vilevile katika ukaguzi wa maghala uliofanyika November 2009 Maghala ya *BP Tanzania Limited* na *ORXY Oil* yalikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango na walipewa adhabu ya faini ya shilingi milioni 10 na vituo kuamuriwa kufungwa kwa miezi 12 kila moja. Hata hivyo, adhabu hiyo ilibatilishwa baada ya Baraza la Ushindani yaani *Fare Competition Tribunal* kuzikubali rufani za kampuni na *depots* hizo.

Mheshimiwa Spika, wote waliokutwa wanaiza au kusafirisha mafuta yasiyokidhi viwango waliadhibiwa kwa mujibu wa Sheria na hasa *EWURA Petroleum Sampling and Testing Rules Government Notes 31* ya mwaka 2008. Adhabu hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kwa wafanyabiashara wa rejareja faini ya shilingi milioni 3 kwa kosa la kwanza, shilingi milioni 5 pamoja na kusimamishiwa leseni kwa kipindi kisichozidi miezi 12 na kufutiwa leseni kwa kosa la tatu.

(b) Kwa wafanyabiashara wa jumla faini ya shilingi milioni 5 kwa kosa la kwanza, shilingi milioni 10 pamoja na kusimamishiwa kwa leseni kwa kipindi kisichozidi miezi 12 kwa kosa la pili na kufutiwa leseni kwa kosa la tatu.

(c) Kwa wasafirishaji mafuta faini ya shilingi bilioni 3 kosa la kwanza, faini ya shilingi milioni 5 na kusimamishiwa kwa leseni kwa kipindi cha miezi 12 kwa kosa la pili na kufutiwa leseni kwa kosa la tatu.

Mheshimiwa Spika, kanuni mpya za uchukuaji na upimaji wa sampuli za mafuta yaani *Petroleum Sampling and Testing Rules* na zile za kuweka vinasaba na kudhibiti ubora wa mafuta yaani *Petroleum Making and Quality Control Rules* ambazo zimeanza kufanya kazi tarehe 11 Juni, 2010 zimeongeza adhabu kwa yejote atakayekutwa akiuza mafuta yasiyokidhi ubora kama ifuatavyo;

(a) Kwa wafanyabiashara wa rejareja faini ya shilingi milioni 7 kutoka shilingi milioni 3 ilivyokuwa awali kwa kosa la kwanza na shilingi milioni 25 kutoka milioni 5 ilivyokuwa awali kwa kosa la pili na kufutiwa leseni kwa kosa la tatu. (*Makof*)

(b) Kwa wafanyabiashara wa jumla faini ya shilingi milioni 10 kwa kosa la kwanza kutoka shilingi milioni 5 ilivyokuwa awali, faini ya kiasi kikubwa kati ya shilingi milioni 100 au 20% ya thamani ya mafuta yaliyochafuliwa kutoka shilingi milioni 10 kama ilivyokukwa awali na kusimamishwa leseni kwa miezi 12 kwa kosa la pili na kufungiwa ghala au sehemu ya ghala kwa kipindi cha miezi 12 pamoja na faini ya shilingi milioni 100 kwa kosa la tatu.

(c) Kwa wasafirishaji mafuta faini ya shilingi milioni 7 kutoka shilingi milioni 3 ilivyokuwa awali kosa la kwanza, kiasi cha kikubwa cha faini kati ya shilingi milioni 15 au 20% ya thamani ya mafuta yaliyokamatwa kutoka shilingi milioni 5 ilivyokuwa awali na kusimaishwa kwa leseni kwa miezi 12 kwa kosa la pili na kufutwa kwa usajili wa kusafirisha mafuta kwa gari lililokamatwa kwa kosa la tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii tumeainisha vituo vya mafuta 12 vilivyofungiwa na *EWURA* kwa mwaka mmoja kutokana na kosa la kuchanganya mafuta kwa mara ya pili kati ya mwaka 2007 hadi sasa. Vituo hivyo na maeneo vilipo vituo hivyo ni kama ifuatavyo:-

Abdulatif Twalib Mohamed Station ya Morogoro, *Kobil Abdulatif Twalib Petrol Station* ya Morogoro, *Mohamed Twalib Petrol Station* ya Morogoro, *Oilcom Kihonda Petrol Station* ya Morogoro, *Sadiq Gapco Super Service Station* ya Morogoro, *Madafu Petrol Station Muro Investment* ya Pwani, *Vigwaza Petrol Station* ya Pwani, *African Motors Petrol Station* ya Dodoma, *New ORIXY Petrol Station* ya Kilimanjaro, *Rafiki Petrol Station* ya Kilimanjaro, *Mount Meru Uchira* ya Kilimanjaro, *Clemence J. Mushi Filing Station* ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na *EWURA* kiwango cha sampuli zilizochukuliwa mwanzoni kiwango cha kufeli kilikuwa 80% kwa mwaka 2007 ambacho kimeshuka mpaka 40% kwa mwaka 2010. *EWURA* itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti tatizo la uchakachuaji ikiwa ni pamoja na kupitisha kanuni mpya kwa ajili ya usafirishajiwa mafuta na kuanzisha teknolojia ya kisasa ya vinasaba yaani *XRF Detection Technology*.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwezi June, 2010 uchakachuaji haramu wa mafuta uliyakumba magari ya msafara wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Moshi. *EWURA* ilitoa maelekezo kuwa kituo husika na gari lililosusha mafuta kwenye kituo hicho viwe chini ya ulinzi mpaka sampuli ya mafuta husika zichukuliwe kitaalamu na *EWURA*. Matokeo ya uchunguzi yamedhihirisha kuwa mafuta ya *Petrol* ya vituo vitatu vya Rafiki, *Mount Meru*, Uchira na Rahisi yalikuwa hayakidhi viwango vya ubora vinavyoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* imechukua hatua za kisheria kwa vituo vya Rafiki na *Mount Meru Uchira* kulipa faini kila kimoja ya shilingi milioni 5 na kufungiwa vituo hivyo miezi 12 kwa kosa la mara ya pili. Kituo cha Rahisi kimelipa shilingi milioni 3

kwa kosa la kwanza. Adhabu hizi ni kwa mujibu wa kanuni za *EWURA Sampling and Testing Rules* za Mwaka 2008 kwani kosa hili lilitendeka kabla ya kuanza kwa kanuni mpya ambazo zimeanza kazi tarehe 11 Juni, 2010 ambazo zimeongeza adhabu.

Mheshimiwa Spika, Suala la magari ya kusafirisha mafuta kurudishwa kutoka Rwanda. Hivi karibuni malori 18 yenye shehena ya mafuta ya *Petrol* yamerudishwa kutoka nchini Rwanda baada ya kubainika kuwa yalikuwa yamebeba mafuta yasiyokidhi viwango nya ubora. *EWURA* baada ya kupata taarifa hizi kutoka kwa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera tarehe 9 June, 2010 ilipeleka Maofisa wake huko Rusumo kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi na uhakiki wa ubora na zoezi hilo la kuchukua sampuli lilianza mara moja tarehe 11 Juni, 2010, sampuli zilipelekwa kwenye maabara kwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi yamebainisha kuwa mafuta yote yaliyorudishwa hayakukidhi viwango vinavyotakiwa, *EWURA* imeshawasilisha taarifa ya matokeo hayo *TRA* ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe. Pamoja na kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* itachukua hatua stahiki dhidi ya waharibu hao, *EWURA* inasubiri maelekezo kutoka *TRA* ili nayo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria zilizopo. *EWURA* inasubiri maelekezo ya *TRA* kwa sababu suala la mafuta yanayosafirisha kwenda nje ya nchi yaani *Transit* linasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Katika kuangalia suala hili na kulifanya tathmini na kulinganisha utaratibu na hali ya nchi jirani yafuatayo yanajitokeza.

Kwanza, habari zilizopatikana kutoka nchi ya Rwanda zinazelea kuwa mafuta yaliyopitia nchini Kenya hadi Uganda hayakuwa na uchafuzi wowote na yalikidhi viwango. Nchi ya Uganda inatumia mbinu ya kisasa ya vinasaba kama *nilivyosema XRF Detection Technology* kung'amua mafuta haramu yaliyochanganywa au yasiyolipiwa kodi, teknolojia itakayoanza kutumiwa na *EWURA* hivi karibuni na hasa mwezi ujao.

Pili, changamoto nyingine inahu kuitishwa kwa mafuta nchi jirani, hili linatokana na uvunjifu wa sheria unaotokana na baadhi ya wafanyabiashara kuyashusha mafuta ya nchi jirani ambayo hayalipiwi kodi hapa nchini. Kiasi cha mafuta kilichoshushwa kinyemela hujaziwa kwa mafuta ya taa, hii inapelekea nchi kutumia mafuta yasiyolipiwa kodi na hivyo kukosa mapato ya kodi na hivyo inachafua mafuta yanayopelekwa nje ya nchi. (*Makofi*)

Tatu, tatizo hili la uchakachuaji pia linaifanya nchi yetu kukosa sifa na kupoteza biashara katika ushindani na nchi za jirani, si Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* wala *EWURA* wenye takwimu kamili ya kiasi cha mafuta yanayoshushwa kinyemela, lakini vyanzo mbalimbali vinakisnia kuwa kodi inayokosekana kwa kupatikana ni mabilioni ya shilingi mbali na uharibifu wa magari, kudhoofisha ushindani wa bei na kuharibu mazingira.

Nne, *EWURA* na Wizara ya Nishati na Madini kwa pamoja waliitisha mukutano na wadau katika usafirishaji wa mafuta ya *Petrol* wakiwemo *TRA*, Chama cha Wafanyabishara Wasafirishaji wa Mafuta TAMAC na TATOA Chama cha Wasafirishaji tarehe 11 Juni, 2010 ili kujadili kwa kina tatizo la kuchanganya mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi na mbinu za kulikomesha. Hatua zinaendelea kuchukuliwa na Serikali pamoja na *EWURA* kukabiliana na uchakachuaji.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* ikiwa ni mamlaka ya udhibiti kwa kushirikiana na Serikali tumechukua hatua zifuatazo.

Kwanza, imeagiza kwamba makampuni ya mafuta na wamiliki wa mafuta wafuate taratibu za kukabidhiana mafuta, kumbukumbu zionyeshe viwango vya mafuta na sampuni zilizofungwa kwa lakiri yaani *Sealed Sample* zitunzwe kama ushahidi.

Pili, magari ya kubebea mafuta yazibwe sehemu zote zinazoweza kupakia na kushusha mafuta yanayosafirishwa na pia yawekewe kifaa kinachoonyesha ratiba ya usafiri hadi yaendako yaani *Tracking System*.

Tatu, kuanzia mwezi August 2010, *EWURA* itaweka na kuanza kutumia mfumo wa kung'amua mafuta yaliyochanganya au yasiyolipiwa kodi.

Nne, kuendeleza na kuongeza nguvu, ukaguzi wa mara kwa mara wa kushtukiza kwenye vituo vya mafuta maghala ya mafuta na magari yanayosafirisha mafuta.

Tano, *EWURA* iko kwenye mchakato wa kuunda kikosikazi yaani Taskforce kitakachoshirikisha taasisi mbalimbali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*, Jeshi la Polisi, *PCCB*, *TA*A, *TPA* na *TBC* kitakachopendekeza suluhihisho la kudumu la uchakachuaji.

Sita, kuanzisha *register* ya takwimu ya biashara ya mafuta kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta sura ya 392 ili kuoanisha kiasi cha mafuta yanayoingia nchini na kiasi kinachotumika hapa ndani ya nchi na kinachokwenda nje ya nchi yaani *transit*.

Saba, Serikali ya Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na *EWURA* walitoa notisi ya siku 30 kwa wamiliki wote wa vituo vya mafuta vyenye maghala nyuma yake katika Mkoa huo. waliagizwa wawe wamevunja maghala hayo ifikapo tarehe 26/6/2010. Kwa sasa uongozi wa Mkoa wa Pwani unafanya tathmini kujiridhisha vituo vilivyotii maagizo na visiviyotii kwa hatua zaidi za kisheria.

Nane, kwa kuwa ni dhahiri kwamba vitendo hivi vya uchakachuaji haramu wa mafuta ya *Petrol* unaathiri sana uchumi wa nchi yetu, Serikali imelazimika kufanya mapitio ya sheria zote zinazohusika zikiwemo sheria za biashara ya mafuta, *UWURA*,

uhujumu uchumi na sheria nyingine zote kwa lengo la kuziboresha kwa kuongeza makali ikiwa ni pamoja na maeneo ya usimamishwaji wa leseni, ufutwaji wa leseni na usalama wa utendaji. Zoezi la kupitia sheria hizi linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani vikali kitendo cha uchakachua ji kinachofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, Serikali inafanya kila liwezekanalo kudhibiti huo mchezo mchafu ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria husika, kama nilivyosema kwa kadri itakavyohitajika kwa madhumuni ya kukomesha kabisa uchanganyaji haramu wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge nimepata udhuru kidogo kwa hiyo nitamwita sasa Mheshimiwa Naibu Spika, ili aendeleze shughuli zilizosalia.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Asasi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. (*Makofi*)

Kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena leo kwa mara ya tatu nikiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa mzima wa afya. Aidha, sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano walionipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kikamilifu. Napenda kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima aliyonipa ya kunitfea kuwa Waziri anayesimamia majukumu ya Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo.

Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Newala kwa moyo wao wa upendo kwa kuendelea kunisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu kama Mbunge wao. Pia, ninawashukuru Watanzania wote hususan Wanamichezo,

Wasanii na Wanahabari kwa ushirikiano mzuri walionipa. Vilevile, nakishukuru Chama changu, Chama Cha Mapinduzi, kwa kunitfea kuwa mgombea wa Jimbo la Newala na kwa imani kubwa niliyopewa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 nikiwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara). Hali kadhalika, ninaishukuru familia yangu, hasa mke wangu mpendwa, Anna Ernestina ambaye yuko hapa, watoto wangu na wajukuu wangu Eveline na Ethan, kwa uvumilivu wao wa kukosa kuwa nami wakati mwingi ninapokuwa ninatekeleza majukumu ya kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa hotuba yake nzuri ambapo ameeleza kwa ufasaha utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Aidha, ameainisha malengo ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, Malengo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II) na miongozo mingine ya Kitaifa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kadhalika, namshukuru Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri ya Hali ya Uchumi Nchini na Mipango ya Maendeleo ambayo imetoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo wa hali ya uchumi wa nchi na mapato ya Serikali.

Aidha, imeonyesha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika bajeti hii hasa ile mikakati ya kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani ambazo tayari kwa namna moja au nyingine zimeathiri baadhi ya sekta hapa nchini.

Wizara yangu imeendelea na mchakato wa kubainisha maeneo yanayoathirika na mtikisiko huu ambapo Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2010/11 – 2012/13 pamoja na bajeti ya mwaka huu vyote vimezingatia namna ya kukabiliana na athari hizo zote. Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri walionitangulia. Maoni yao yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali, zikiwemo Sekta zinazosimamiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuiongoza nchi yetu vizuri kuanzia mwaka 2005. Tumeshuhudia mambo mengi mazuri yaliyofanyika katika kipindi chote hasa katika nyanja za siasa, uchumi na jamii. (*Makofi*)

Tunatoa pongezi za pekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutia saini Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Na.1 ya Mwaka 2010 tarehe 17 Machi, mwaka huu ambayo imeanza kutumika. Aidha, naomba nimpongeze kwa jinsi alivyoiwezesha Nchi yetu kufikia

kwenye ufanisi mkubwa wakati ulipofanyika Mkutano wa 20 wa Kimataifa kuzungumzia hali ya Uchumi kanda ya Afrika (*World Economic Forum for Africa*) jijini Dar es Salaam mwezi Mei, 2010.

Kadhalika, nampongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri alizozifanya tangu alipoingia madarakani mwaka 2008. Wote tumeona na kushuhudia utendaji makini, uadilifu, unyenyekevu kwa watu wote, na ushupavu wa Waziri Mkuu wetu katika kipindi hiki kifupi hasa alivyoshughulikia suala la kubana matumizi ya Serikali. Aidha, Waziri Mkuu alilivalia njuga suala la kupiga vita mauaji ya kikatili ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*Albino*) hasa kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa Mjini Iringa mwezi Mei, 2010. Vilevile, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, natumia fursa hii kumpungeza kwa dhati kwa maagizo yake mbalimbali likiwemo lile la kuagiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) la kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya shughuli za utamaduni na michezo kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu pia niwapongeze viongozi wote walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Mikoa, Wilaya, Mashirika na Taasisi mbalimbali za Serikali. Pongezi za pekee ziwaendee Wabunge wapya walioteuliwa na ambao wamejunga nasi hivi karibuni katika Bunge hili Tukufu ambao ni Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kutoka Chama cha Wananchi (*CUF*) na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene kutoka Chama Cha Mapinduzi (*CCM*). Nitumie fursa hii pia kumpungeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kufungua ukurasa mpya wa siasa nchini kwetu hasa kutokana na maridhiano ya kisiasa yaliyopatikana huko Zanzibar. Pongezi zangu pia ziende kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Amani Abeid Karume, kwa kuwateua Wawakilishi wawili kutoka *CUF* kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ikiwa ni hatua nzuri ya utekelezaji wa maridhiano ya kisiasa Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Taifa lilipatwa na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuriko yaliyotokea Same - Kilimanjaro, Kilosa - Morogoro na Chato - Kagera kwa watu kupoteza maisha na kuwaacha wengine bila makazi. Aidha, tarehe 31 Desemba, 2009 Taifa lilimpoteza mpigania uhuru wake, Waziri Mkuu na Makamu wa Rais Mstaafu, Hayati Mzee Rashidi Mfaume Kawawa, maarufu kama Simba wa Vita. Pia, mwaka huu Taifa lilikumbwa na misiba mikubwa ya kuwapoteza wananchi wake kutokana na ajali za barabarani na mapigano baina ya koo mkoani Mara. Vilevile, Taifa lilimpoteza Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa mkoani Lindi. Naungana na wenzangu walionitangulia kusoma hotuba zao kutoa salamu za pole kwa wale wote waliofikwa na majanga na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutumia fursa hii kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ambayo inaongozwa na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa Jenista Joakim

Mhagama na Makamu Mwenyekiti wake Mbunge wa Jimbo la Koani Unguja Kusini, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa kuendelea kuishauri Wizara yangu katika masuala mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitano tangu Wizara hii ilipoanzishwa mwaka 2006. Ushauri wa Kamati hii umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha utendaji wa Wizara na Sekta kwa jumla. Pia, naishukuru Kamati hiyo kwa kujadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 04 Juni, 2010. Pongezi zilizotolewa na Kamati hii kwa Wizara katika bajeti ya mwaka 2009/2010, zimetusaidia sana katika kuongeza ufanisi wa kazi za Wizara kwa jumla. Wizara yangu inaendelea kuufanya kazi ushauri pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti ya mwaka huu ili kuendelea kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: Sehemu ya kwanza itajikita katika kutoa maelezo ya majukumu ya Wizara, ilihali sehemu ya pili itahusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sehemu ya tatu inahusu utekelezaji wa majukumu yaliyoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010. Sehemu ya nne inahusu majukumu na maombi ya fedha ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Wizara. Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa na kutekeleza Sera za Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kuandaa Mipango ya ukuaji wa sekta za Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vyombo vya Habari katika maeneo ambayo hayavutii sekta binafsi;
- Kuandaa na kusimamia viwango na ubora wa kazi za sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kukuza na kuimarisha fani mbalimbali za utamaduni nchini, hususan sanaa za maonyesho, filamu, muziki na sanaa za ufundi wa mikono kama kielelezo cha uitaifa na chanzo cha ajira;
- Kuenzi kazi zilizotia fora katika Sekta ya Utamaduni;
- Kuimarisha na kukuza Kiswahili na matumizi ya lugha za asili ambazo ni vijenzi vya lugha hiyo na kutoa mafunzo ya lugha za kigeni kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa;
- Kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo nchini;
- Kukuza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika fani za Habari, Utamaduni na Michezo kitaifa na kimataifa;

- Kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kusimamia Maendeleo ya Watumishi katika sekta za Habari, Utamaduni na Michezo; na
- Kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maendeleo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza utekelezaji wa mambo muhimu kwa Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Habari. Kuendeleza uhuru wa vyombo vya Habari kwa mujibu wa Sheria. Kuhusu kuendeleza uhuru wa vyombo vya Habari, Wizara imesajili magazeti na majarida 710 hadi mwezi Mei, 2010. Vipo vituo vya Redio 59 na Televisheni 28 ambavyo vimesajiliwa kurusha matangazo yake hapa nchini, Kiambatisho Na. VII. Marekebisho ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 yamekamilika kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wamiliki na waendeshaji wa vyombo vya habari na asasi zisizo za kiserikali. Aidha, Wizara imekamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM) kuhusu Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Wizara pia imeanzisha Tovuti ya Wananchi ambapo hadi mwezi Mei, 2010, Tovuti hii ilikuwa imepokea maoni na hoja zipatazo 16,596. Hoja zote zinazoihusu Serikali zimeshughulikiwa kwa kupelekwa katika Wizara na Asasi husika ili kupatiwa ufumbuzi. Hoja nyingi zilihu kero mbalimbali za wananchi na ushauri kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kueneza Usikivu wa Redio na Televisheni kupitia Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC). Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na Televisheni ya Taifa (TVT) ziliunganishwa na baadae kuwa Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC) mwaka 2007. TBC imeanzisha Idhaa za TBC1, TBCTaifa, TBCFM na *TBC International* na vipindi vipyta na kuboresha vipindi vyake kwa lengo la kuvutia wasikilizaji na watazamaji na pia kuongeza usikivu. Hivi sasa, TBC inasikika na kuonekana moja kwa moja katika nchi nyingine duniani kwa kupitia DSTV mkondo 143. TBC inakamilisha mchakato wa kuhama kutoka katika mfumo wa analogia kwenda dijitali ili kukamilisha mabadiliko hayo ifikapo 2015. Aidha, TBC imeanza kurusha matangazo yake ya televisheni kwa teknolojia ya dijitali katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza tangu mwezi Juni, 2010.

Katika kuboresha usikivu wa matangazo yake ya redio, TBC imekamilisha uwekaji wa mitambo ya *Frequency Modulation (FM)* katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Tabora, Kigoma, Mwanza, Mara, Kagera, Tanga na Lindi.

Ujenzi wa mitambo ya FM katika mkoa wa Singida na mjini Sumbawanga, mkoani Rukwa umekamilika na vituo vinafanya kazi. Mitambo ya FM kwa ajili ya mikoa ya Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Rukwa na Mtwara; na pia Zanzibar imeshaagizwa na inatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Septemba, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utamaduni. Kuendelea kuenzi na kulinda historia, mila na desturi nzuri za watu wetu na kuzitokomeza mila na desturi mbaya. Wizara yangu imeendelea kuenzi, kuhifadhi na kulinda historia, mila na desturi nzuri za Watanzania na kutokomeza mila na desturi zilizopitwa na wakati. Utafiti wa mila na desturi wa kubaini dhana ya sheria za mila na desturi umefanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza na Kigoma. Aidha, uchambuzi wa torwi (*data*) umeonyesha baadhi ya mila kuwa zinatafaa na hivyo matokeo ya utafiti yatasambazwa na kuendelezwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya awali ya ujenzi wa mradi wa Jumba la Utamaduni katika kijiji cha Kiromo wilayani Bagamoyo yamekamilika. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uthamini wa ardhi, mazao na mali zilizopo katika eneo la mradi na barabara kutoka barabara kuu hadi eneo hilo. (*Makofi*)

Aidha, michoro ya kiusanifu wa majengo ya mradi tayari imeshakamilika. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya jamii yetu. Wizara kupitia Taasisi ya Sanaa na Utamaduni, Bagamoyo (*TaSUBa*) inaendelea kutoa nafasi za mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa vijana na elimu kwa jamii. Jumla ya wanafunzi 121 walidahiliwa kwa ajili ya mafunzo ya stashahada na wasanii 100 walio kazini walijunga na mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) linaandaa na kurusha vipindi 52 vya Lughya ya Taifa, vipindi 52 vya Kumepambazuka katika Radio, na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kwenye Televisheni kila mwaka.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitoa mafunzo ya ukuzaji vipaji kwa wasanii 560 katika Mikoa ya Ruvuma (Wilaya ya Tunduru), Tanga (Manispaa), Tabora (Manispaa), Dar es Salaam (Ilala na Kinondoni), na Dodoma (Chamwino). Wasanii 124 na wanawake wajasiriamali 19 kutoka Mikoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam walitambuliwa na kushiriki katika mafunzo ya sanaa za ufundi yaliyoratibiwa na BASATA na kuendeshwa na *'The Great Lake Consortium for International Training and Development'* na '*The Arts Council Lake Erie West*' kutoka Marekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuweka mipango ya kuwatambua wasanii wa aina mbalimbali pamoja na wasanii wasomi na kuimarisha mipango ya mafunzo ya sanaa hadi

Chuo Kikuu. Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo imekamilisha mpango wa kuboresha Programu ya Mafunzo na Utafiti kwa kuandaa mitaala ya kufundishia yenyenye lengo la kuwaandaa wanafunzi kupata Shahada ya Kwanza. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ilibaini shule 15 zilizoshirikisha walimu 27 na wanafunzi 250 katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma na kuendesha mafunzo ili kuibua vipaji na ubunifu za mafunzo darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuweka mipango ya kukiimrisha Kiswahili kama kielelezo cha utamaduni wetu. Wizara yangu ilifanya utafiti wa Lugha za Asili ili kubaini maneno yanayoweza kutumika katika Kiswahili badala ya yale yenyenye kutatanisha katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Dodoma Mbeya, Iringa, Mara, Manyara, Mwanza, Ruvuma na Singida.

Aidha, mafunzo kuhusu utumiaji wa lugha fasaha ya Kiswahili yalitolewa kwa wahariri na waandishi wa habari zaidi ya 150 nchini. Zaidi ya hayo, Wizara yangu ilitoa Tamko la kusisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zote rasmi za Serikali wakati wa kikao cha Bunge lako tukufu. Aidha, ninapenda kulikumbusha tena Taifa kwa kupitia kikao hiki cha Bunge kuwa, ni muhimu sote tukazingatia kwa dhati maelekezo ya Tamko hilo ili kuienzi lugha yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Agizo lingine ni kuweka mipango ya kuimrisha, kuendeleza na kudhibiti maadili katika tasnia ya filamu. Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Jukwaani imekagua filamu na kanda 345, imepitia tungo 50 za filamu na kutoa vibali vya utengenezaji picha 10 kutoka ndani na nje ya nchi.

Aidha, Bodi imefanya zoezi la kukusanya takwimu ili kujuu hali halisi ya maonyesho ya filamu, kumbi rasmi za filamu, maktaba, maduka na maeneo yasiyo rasmi yanayotumika katika maonyesho ya filamu. Zoezi limefanyika katika mikoa 11 ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Mtwara, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Iringa na Mbeya. Mkoa wa Dar es salaam pekee una vibanda zaidi ya 750 visivyo rasmi. Zoezi hili litaendelea katika mikoa 10 iliyobakia ili kupata picha halisi. Vile vile, Bodi imekamilisha mchakato wa kuandaa Kanuni za Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa sheria hiyo. Bodi imeendelea kutoa ushauri kwa wadau wake ili kuboresha kazi zao kimaadili, ubora na viwango. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Michezo. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudhi na msukumo aliota ili kuhakikisha kwamba Tanzania inapiga hatua katika Sekta ya Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na msukumo huo, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Kuendelea kusimamia mchakato wa awamu ya pili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo. Aidha, imefanya ukarabati mkubwa katika jukwaa kuu sehemu ya paa la Uwanja wa Uhuru, kazi ambayo inaendelea hivi sasa.

Kukamilisha ujenzi wa Jumba la Michezo ya Ndani katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na kuanza ujenzi wa dahalia (bweni) ambayo imekamilika kwa asilimia 70.

Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatenga bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Michezo.

Kukusanya taarifa mbalimbali za Maendeleo ya Michezo katika mikoa 15 na wilaya 24. Sambamba na zoezi hilo, Wizara yangu imetua ushauri kwa mamlaka mbalimbali kuhusu uhifadhi na kuendeleza maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya Michezo.

Kugharamia timu ya Taifa ya Ngumi kwenda kwenye michezo ya kujipima nguvu huko New Delhi - India mwezi Februari, 2010 ili kufuzu kwa ajili ya mashindano ya Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika huko New Delhi - India mwezi Oktoba, 2010.

Kutembelea baadhi ya Halmashauri za mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Arusha, Singida, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kigoma, Mara na Kagera kufuatilia utengaji wa bajeti kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya maendeleo ya Michezo.

Kutoa mafunzo kwa wanachuo 24 katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa kiwango cha Stashahada. Mafunzo hayo yamemalizika mwezi Aprili, 2010. Aidha, mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wadau zaidi ya 200 katika vituo vya michezo Arusha na Songea.

Kusajili jumla ya Vyama na Vilabu vya Michezo 363, na shule za michezo (*Sports Academies*) sita.

Kutoa huduma za Kinga na Tiba kwa wadau wa Michezo zikiwemo timu mbalimbali za michezo katika mikusanyiko na Matamasha ya michezo. Aidha, mafunzo ya uzoezaji viungo vya mwili (*Physiotherapy*) yametolewa na Mtaalamu kutoka Ujerumanii katika vituo vya Arusha na kliniki ya tiba na kinga ya Dar es Salaam ambapo zaidi ya Madaktari wa michezo 75 walipata mafunzo hayo.

Kuratibu shughuli za Siku ya Michezo Tanzania kwa mwaka 2009 ambapo jumla ya vikundi au timu 140 za michezo zilishiriki katika shughuli za kitaifa mkoani Arusha.

Kuajiri makocha wanne wa michezo: Makocha wawili wa Riadha, kocha mmoja wa michezo wa ngumi za ridhaa na kocha mmoja wa Judo. Aidha, Wizara imepata kocha mmoja wa michezo wa kuogelea kutoka Korea ikiwa nchi mshirika. Hii ni katika kufanikisha mpango wa kuendelea kutafuta walimu wenyewe ujuzi na uzoefu wa kimataifa kufundisha timu za taifa za michezo mbalimbali kupitia mikataba ya ushirikiano na nchi rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilitekeleza kazi zifuatazo:-

Kuendesha mafunzo ya ufundishaji Michezo kwa Jamii kwa Walimu 386 wa Michezo mbalimbali katika Halmashauri za Wilaya 10 za Tanzania Bara ambazo ni Sengerema, Kigoma vijijini, Magu, Ksimba, Iramba, Muheza, Same, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Tandahimba na Korogwe.

Kufanya tathmini ya mahitaji na miundo ya Utawala katika Vyama vitano vya Michezo vya Kitaifa.

Kuwezesha Wafanyakazi tisa wa BMT kupata mafunzo zaidi ya kazi zao.

Kuendesha mafunzo ya uongozi kupitia Michezo kwa walimu 338 kwa ushirikiano na *UK Sport International* na kwa wanafunzi 1,529 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Ruvuma.

Kuwezesha uanzishwaji wa Kituo cha Kimataifa cha Uongozi wa Vijana kupitia michezo kwa ushirikiano na *UK Sport International* na *IDS* zote za Uingereza, ambapo Makao Makuu ya Kituo hicho yapo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

Kusimamia chaguzi za Vyama vitano vilivyoohusisha fani za Kuogelea, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Mikono, na Mashirikisho ya Michezo, kama vile SHIMUTA kwa ajili ya kuimarisha Utawala Bora kwenye fani ya Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Raslimali Watu. Wizara imeendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wanaostahili kulingana na Miundo ya Utumishi ya kada zao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010 watumishi 17 walipandishwa vyeo, watumishi 22 walithibitishwa kazini na watumishi tisa walajiriwa katika nafasi mbalimbali. Aidha, Sekretarieti ya Ajira inaendelea na mchakato wa kujaza nafasi 32 zenyе vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeweza kutoa mafunzo kwa Watumishi 151 kati ya hao waajiriwa wapya 32 walipatiwa mafunzo elekezi pamoja na kufanyiwa upekuzi (vetting), watumishi 18 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Aidha, watumishi 43 wamehudhuria mafunzo ya kudhibiti vihatarishi mahali pa kazi (Risk Management), wajumbe wanane wa Bodi ya Zabuni ya Wizara pamoja na watumishi 12 wa Kitengo cha Ugavi wamehudhuria mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi Na. 21 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu imewaelimisha na kuwahamasisha watumishi wake 198 juu ya ugonjwa wa UKIMWI na athari zake. Vilevile Wizara yangu imeendelea kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI waliojitokeza, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali kupitia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 2006, kuhusu huduma kwa watumishi wa umma wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wenyе UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya mkutano wa wafanyakazi wote na vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi kwa lengo la kuwawezesha watumishi kushauri uongozi wa Wizara juu ya mambo mbalimbali yanayoihusu Wizara na maslahi yao. Wizara imeendelea kupokea ushauri kutoka tawi la TUGHE na Baraza la Wafanyakazi ili kutekeleza malengo yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha rasilimali za Wizara zinatumika vizuri na kwa madhumuni yaliyowekwa, Wizara imeendelea kutumia Kamati ya Kuratibu, Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali pamoja na Kamati ya Ukaguzi ya Wizara kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha zilizotengwa kutekeleza shughuli mbalimbali.

Aidha, Wizara imeendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2001 kwa lengo la kupunguza mianya ya rushwa na kutoa huduma zenyе viwango vinavyokubalika. Hali hiyo, imewezesha Wizara yangu kupata hati safi kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo tangu iundwe mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ni miongoni mwa Wizara zilizotekeliza Programu ya Pili ya Maboresho katika Utumishi wa Umma. Kupitia programu hiyo, Wizara iliboresha muunganiko wa kompyuta na vifaa vingine vya mawasiliano vilivyounganishwa katika mtandao mkubwa wa kompyuta (wide area network) kwenye idara na makao makuu ya Wizara kwa kutumia mkongo wa mawasiliano (optic fibre). Maboresho katika njia ya mawasiliano ya barua pepe kwa kutumia anwani zenyе utambulisho wa kipekee katika mfumo wa mtandao kwa ajili ya mawasiliano (domain) ya Wizara yamekamilika. Uboreshaji huu umefanya Wizara iwe

na vifaa vya kisasa kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki katika Jumuiya Mbalimbali. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/10 Wizara iliendelea kushiriki katika Mikutano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kukuza ushirikiano kati ya Sekta za pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Wizara ilishiriki katika vikao viliyofanyika katika miji mbalimbali ya Afrika Mashariki. Ushiriki wa Wizara katika vikao hivi, pamoja na mambo mengine, ulilenga zaidi kujiandaa kuingia katika Soko la pamoja la Afrika Mashariki ambalo limeanza rasmi tarehe 1 Julai, 2010. Kwa sasa Wizara inaanisha maeneo yatakayofunguliwa kwa ajili ya soko hilo kutoka katika Sekta 12 zilizopendekezwa ndani ya Itifaki hiyo, Wizara yangu ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Sekta ya Habari. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inatarajia kupitisha Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Pamoja na mambo mengine, Sheria hiyo itaiwezesha Serikali:-

Kuanzisha chombo huru kitakachosimamia viwango vya elimu na taaluma ya habari pamoja na maadili ya taaluma hiyo kitakachoitwa Bodi ya Usimamizi wa Taaluma ya Habari.

Kufuta Sheria za Vyombo vya Habari zilizopitwa na wakati na ambazo zinalalamikiwa na wadau.

Kuweka utaratibu bora zaidi wa usajili na umiliki wa vyombo vya habari unaoendana na hali ya sasa ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Kuendelea kuchapisha Jarida la Nchi Yetu baada ya kuliboresha, kuandika habari na makala pamoja na kupiga picha za matukio mbalimbali ya kitaifa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara, Idara na Wakala mbalimbali wanaohusika na Tovuti ya Wananchi. Wizara pia, itaendesha mafunzo kwa watendaji wa ngazi za mikoa wakiwemo Makatibu Tawala wa Mikoa na wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya, kuhusu Tovuti hiyo.

Kuendeleza mradi wa picha kwa kuanzisha mtandao wa kulinda na kuuza picha popote duniani kupitia E-commerce Project. Mtandao huu utawawezesha wadau kupata picha hizi kwa gharama kidogo kutoka katika maktaba yetu. Aidha, katika mradi huu, picha muhimu za kumbukumbu za kitaifa na kimataifa zitahifadhiwa katika “CD” na kutunzwa katika sehemu nyingine ili kuondoa uwezekano wa kupoteza kumbukumbu hizo endapo kutatokea janga lolote kama moto katika maktaba ya picha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 *TBC* imejipanga pamoja na shughuli zake za kawaida, kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kufunga mitambo ya matangazo ya redio ya *FM* ya *TBC* na *TBC FM* katika mikoa ifuatayo: Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Rukwa, Mtwara na Ruvuma; na pia Zanzibar.

Kufanya ukarabati na kuboresha Studio tano za redio zilizopo makao makuu ya *TBC*, Barabara ya Nyerere Dar es Salaam.

Kupanua usikivu wa matangazo ya televisheni kwa mfumo wa dijitali kwenye mikoa mitano ikiwemo Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro; na pia Zanzibar.

Kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu upigaji kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2010.

Kuimarisha mkondo mpya wa matangazo wa *TBC* ulioanzishwa kwa mfumo wa dijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na *TCRA* imejipanga kuelimisha wananchi na watumiaji wa huduma za utangazaji nchini juu ya mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analogia kwenda dijitali. Hivyo tutafanya yafuatayo:-

Kuelimisha wananchi faida za mfumo wa utangazaji katika teknolojia ya dijitali kuitia televisheni, redio, vipeperushi, warsha na njia nyingine zitakazowezesha wananchi kuelewa mabadiliko hayo.

Kuweka utaratibu utakaowawezesha wananchi kupata kwa urahisi na kwa bei nafuu ving'amuvi vitakavyotumika kupoolea matangazo ya dijitali.

Kuendelea kuratibu na kusimamia vyombo vyote vya utangazaji nchini na kutathmini mchango wa vyombo hivyo katika maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kufanya kazi zifuatazo:-

Kununua mashine ya pili ya *Computer to Plate (CTP)* ili kuongeza uwezo wa mtambo wake wa kuchapa magazeti.

Kununua machine za kuchapa vitabu, kalenda, vipeperushi na kadhalika.

Kukamilisha ununuzi wa majengo ya mtambo wa uchapaji na chumba cha habari.

Kufuatilia mazungumzo na wabia ili kuendeleza viwanja vya Kampuni vilivyopo Dar es Salaam na Dodoma.Kukamilisha ukarabati wa jengo la Ofisi Barabara ya Mandela.

Kukamilisha na kuzindua maktaba ya elektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utamaduni. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

Kusambaza matokeo ya utafiti uliofanywa mikoani na kuchapisha vijarida vya mila na desturi.

Kuendesha mafunzo ya mbinu za kufanya Utafiti na Uhifadhi wa kumbukumbu za Mila na Desturi kwa Maofisa Utamaduni wa Kanda ya Kusini (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma).

Kuendelea kufanya utafiti wa Mila na Desturi zinazochochea au kudhibiti kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mwanza.

Kufanya utafiti wa lugha za asili katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kilimanjaro na Rukwa.

Kuendesha mafunzo ya Lugha ya Kiswahili sanifu kwa waandishi na wahariri wa vyombo vya habari.

Kuratibu na kuendesha mpango wa kuibua vipaji kwa watoto wa shule za msingi katika fani mbalimbali za sanaa.

Kuanzisha kanzidata (data base) za wasanii wa kazi za mikono kwa lengo la kuzitambua, kuzitangaza na kuingizwa katika soko.

Kuongeza idadi ya vikundi vya asili kushiriki katika maadhisho ya sherehe za kitaifa.

Kuratibu na kusimamia Maadhisho ya Siku ya Utamaduni Duniani Mei 21, 2011.

Kusimamia na kuendesha Tamasha la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania litakalofanyika mwezi Septemba, 2010.

Kusimamia ujenzi wa Jumba la Utamaduni eneo la Kiromo, Wilaya ya Bagamoyo.

Kusimamia na kuendesha Mkutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni unaofanyika kila mwaka.

Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya Redio kuhusu maadili ya Mtanzania.

Kusimamia ujenzi wa Mradi wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitoe ufanuzi kwa kifupi kuhusu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Ikumbukwe kuwa, nchi yetu imechangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa uhuru katika nchi kadhaa Barani Afrika. Hivyo, Mradi huu unaoungwa mkono na *UNESCO* pamoja na Umoja wa Afrika, umelenga kuweka kumbukumbu muhimu za harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika katika kituo kimoja mahususi kwa ajili ya ukumbusho wa sasa na vizazi vijavyo.

Kituo hicho kitajengwa Tanzania yalipo makao makuu ya mradi, ingawa kila nchi mshiriki wa mradi huo itakuwa na kituo kidogo nchini mwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza kazi zifuatazo:-

Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili katika televisheni.

Kuendelea kusoma miswada ya vitabu vya taaluma na kuipatia ithibati ya lugha.

Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kitaifa na kimataifa na shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi.

Kuendelea kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho yake.

Kuchapisha vitabu viwili Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu na Kamusi ya Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa.

Kukarabati na kuboresha baadhi ya majengo yaliyonunuliwa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi hatimaye BAKITA ihamie katika majengo hayo na kuyatumia kama ofisi zake mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Sanaa la Taifa litatekeleza kazi zifuatazo:-

Kufanya utafiti wa Sanaa za Jadi katika Mkoa wa Mwanza. Kuendeleza uhamasishaji na uratibu wa uundaji wa Mashirikisho manne na mitando ya Wasanii.

Kuendelea kuendesha mafunzo na maonyesho ya sanaa kwa watoto 200 wa Shule za Msingi kwa kuwapatia stadi za uchoraji, utambaji wa hadithi na maonyesho katika Wilaya za Kinondoni, Temeke, Ilala na Korogwe.

Kuandaa, kuratibu na kuendesha Tamasha la Siku ya Wasanii Tanzania. Kuanzisha Mfuko wa Sanaa Tanzania. Kuendesha mafunzo kwa vikundi 20 vya wasanii juu ya urembaji wa vitambaa kwa mtindo wa batiki, uchapaji na mafundo katika mkoa wa Singida.

Kuendelea kusanifu, kuboresha na kuhifadhi maelezo ya wasanii katika kanzidata ya BASATA.

Kuandaa na kuratibu mijadala 52 ya sanaa kupitia Jukwaa la Sanaa kwa wasanii, waandishi wa Habari na Wadau wapatao 1,000.

Kuendelea na utafiti wa Mchango wa Sanaa katika kuongeza pato, ajira na kuondoa umaskini katika wilaya za Dodoma Mjini, Kibaha, Kinondoni na Morogoro Mjini. Kuanzisha mashindano ya uandishi wa Tamthiliya na Maonyesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani itatekeleza kazi zifuatazo:-

Kusambaza Kanuni za Sheria Na 4 ya mwaka 1976, katika mikoa na halmashauri zote nchini, kuendesha vikao vya wadau wa filamu ili kuzifahamu Kanuni hizo, kuimarisha sekretarieti ya Bodi kwa kuongeza watendaji na vitendea kazi vya kisasa.

Kukamilisha zoezi la kukusanya takwimu kuhusu maonyesho ya filamu, kumbi rasmi na zisizo rasmi, maduka na maktaba za filamu yanayotumika kwenye maonyesho ya filamu katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Ruvuma, Rukwa, Shinyanga, Mwanza, Musoma, Kagera, Manyara na Tanga pamoja na kukamilisha mpango mkakati wa Bodi.

Kuendelea kuhamasisha wadau wa filamu kuhakikisha wanakagua filamu zao kabla ya kutumika kwa maonyesho ya hadhara na wanaonyesha kwa kuzingatia madaraja na viwango.

Kuendelea kuelimisha jamii juu ya wajibu na majukumu ya Bodi, wajibu wao kama wadau kupitia kipindi cha Maadili ya Mtanzania kinachorushwa hewani na *TBCI*.

Kusimamia mapato yanayotokana na tasnia ya filamu ili kuongeza pato la Taifa na kuongeza ajira.

Kuendelea na juhudi za kupata sheria mpya itakayokwenda na wakati na hivyo kuendelea kulinda maadili ya Taifa kwa kukagua filamu, kanda za video, majumba ya sinema na kushiriki vipindi vya maadili katika radio na televisheni.

Kuimarisha sekretarieti ya Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Jukwaani kwa kuongeza wataalamu na vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TaSUBa*). Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 TaSUBa itatekeleza kazi zifuatazo:-

Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 120 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini.

Kukamilisha mtaala wa shahada ya kwanza na kuanza kuutumia katika mwaka wa masomo 2011/2012.

Kuendesha Tamasha la 29 la Bagamoyo la Sanaa litakalofanyika Septemba hadi Oktoba 2010 ambapo kauli mbiu yake ni “Sanaa na Utamaduni katika kukuza na kuimarisha Demokrasia”.

Kuimarisha kituo cha utafiti na uhifadhi wa ngoma na muziki wa Kitanzania.

Kujenga jengo la utawala ikiwa ni sehemu ya mpango kabambe wa *TaSUBa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Katika mwaka 2010/2011 Mfuko wa Utamaduni Tanzania umekusudia kutekeleza yafuatayo:-

Kuendeleza utaalamu asilia wa usukaji kwa akina mama waishio vijijini kwa lengo la kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika maeneo yao.

Kuendeleza Vituo vya Utamaduni na Masoko katika mikoa ya Dodoma na Morogoro.

Kuendeleza viwanda vidogo vidogo asilia vya nguo katika mikoa ya Tanga, Singida, Ruvuma; na pia Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Michezo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara yangu itatekeleza kazi zifuatazo katika Sekta ya Michezo:-

Kukamilisha marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Michezo.

Kuendeleza mchakato wa awamu ya pili ya Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo.

Kuratibu maandalizi na ushiriki wa timu za taifa katika michezo ya Jumuiya ya Madola mwezi Oktoba 2010 huko New Delhi, India na mashindano ya Vijana wenyewe umri chini ya miaka 20 kwa nchi za SADC yatakayofanyika mwezi Desemba, 2010 huko Swaziland.

Kuhamasisha mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya michezo.

Kuhamasisha mamlaka mbalimbali kuboresha viwanja vya michezo inavyomiliki na kujenga viwanja vipya.

Kutoa mafunzo ya stashahada ya elimu ya ufundishaji michezo na stashahada ya uongozi na utawala wa michezo kwa wanachuo wa Chuo cha Michezo Malya watakaodahiliwa mwezi Septemba mwaka huu.

Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo katika vituo vya michezo kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea).

Kuendelea kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu miundombinu na vifaa bora vya michezo kwa wadau.

Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

Kutoa huduma za Kinga na Tiba kwa Wanamichezo kwa kupima afya na kuendesha kliniki za wazi.

Kuhamasisha wanawake kujihusisha zaidi katika michezo ili kuongeza ushiriki wao ikiwa ni pamoja na kugombea nafasi za uongozi katika Vyama na Vilabu vya michezo.

Kushirikiana na Wizara za Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI katika kuimarisha somo la Elimu kwa Michezo shulen na vyuoni.

Kutafuta walimu wa michezo (makocha) wenyewe ujuzi na uzoefu wa kimataifa katika kufundisha timu za taifa za michezo mbalimbali.

Kuratibu shughuli za Siku ya Michezo Tanzania inayoahimishwa tarehe 21 Septemba kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Michezo la Taifa litatekeleza kazi zifuatazo:-

Kuendelea kuhamasisha jamii kushiriki michezo na kutoa huduma bora kwa wadau wa michezo.

Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundishaji kwa walimu wa michezo wapatao 900 katika wilaya 20 za Tanzania Bara.

Kuandaa na kuendesha mafunzo ya uongozi kwa vijana kupitia michezo kwa washiriki wapatao 2,000 na pia kuwashirikisha katika bonanza watoto wapatao 6,000 kwa kushirikiana na *UK Sport International*.

Kumalizia ujenzi wa darasa moja la mafunzo ya uongozi kwa vijana kupitia michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa kushirikiana na *UK Sport International*.

Kuendesha mafunzo ya utawala Bora, Mpango wa kazi kwa viongozi wa vyama 30 vya michezo vya Taifa kwa lengo la kuimarisha utawala Bora katika michezo.

Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Baraza.

Kushiriki katika mikutano, matamasha na mashindano yanayoandalowiwa na wadau wa ndani na nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Raslimali Watu. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara imekusudia kutekeleza yafuatayo:-

Kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kutokana na mahitaji ya mafunzo yaliyoainishwa na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa Wizara.

Kufanya mapitio ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi (*Training Needs Assessment*).

Kuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi kutokana na mahitaji ya mafunzo yaliyoainishwa.

Kupandisha vyeo watumishi wa Wizara walio na sifa kwa mujibu wa Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi za mwaka 2002 pamoja na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, toleo la mwaka 1999 na 2008.

Kuelimisha Watumishi kuhusu rushwa na maadili sehemu za kazi na kutoa mafunzo kwa wajumbe wanane wa Kamati ya Maadili ya Wizara.

Kufanya mafunzo ya mpango wa maendeleo ya rasilimali watu na maandalizi ya mfumo wa taarifa za kiutumishi na mshahara (*Human Capital Management Information System (HCMIS)*).

Kuendesha kampeni ya ushauri nasaha na kupima VVU/UKIMWI kwa hiari na kutoa huduma ya lishe na madawa kwa watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Idara itatekeleza yafuatayo:-

Kuratibu na kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 pamoja na Sheria za BAKITA, BASATA, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani na Baraza la Michezo la Taifa.

Kuendelea kuratibu vikao vya ushirikiano kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Tanzania Bara na Zanzibar kwa ajili ya maendeleo stahiki na sawia kwa pande zote mbili.

Kutekeleza vikao vya Kuratibu, Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Wizara.

Kuratibu uandaaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala.

Kuendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelawa chini ya Wizara.

Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitatu (2010/2011 – 2012/2013).

Kuratibu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayohusu sekta za Wizara, ikiwa ni pamoja na kubaini fursa za ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Kkupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Serikali itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo ili Sekta hizo ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Serikali inaanini kuwa Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo zina nafasi katika kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi yetu.

Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kuleta amani na furaha katika jamii. Pamoja na kuwa katika kutumia fursa hizo bado kuna changamoto ambazo ni lazima zipatiwe ufumbuzi ili kutumia fursa hizo ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Ninaanini kuwa changamoto zilizopo zitaendelea kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua na hasa kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)* na wadau wengine wa maendeleo. Ni matarajio yangu kuwa, tukidhamiria inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani. Naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 katika kutimiza malengo yetu. Utekelezaji wa majukumu na

malengo ya Wizara yangu umewezezana kutokana na ushirikiano mzuri uliopo mionganii mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara.

Shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mjini na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambaye amekuwa wa msaada mkubwa kwangu na hasa shughuli za hapa Bungeni; Ndugu Sethi Kamuhanda, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalamu, na Watumishi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Asasi zilizo chini ya Wizara yangu kwa juhudii walizofanya kuhakikisha kwamba wanatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wametuunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Nawashukuru wahisani wote ambao wametusaidia na nina imani wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Sweden, Norway, Uingereza, Denmark, Ujeruman, Japan na Finland; Mashirika ya kimataifa ya *UNICEF* na *UNESCO*. Pia, ninapenda kuzishukuru Kampuni za *Vodacom*, *Tigo*, *Zain*, *Zantel*, *TTCL*, *Tanzania Breweries Limited (TBL)*, *Serengeti Breweries Limited*, *NMB Bank*, *NBC Bank*, *CRDB*, *Standard Chartered Bank*, *Stanbic Bank*, *Exim Bank*, *Mohamed Enterprises (T) Limited*, *SBC Limited*, Benki ya Posta, *Coca Cola Africa - Kanda ya Tanzania na IPP Ltd.*

Aidha, navishukuru vyombo vyote vya habari nchini kwa kufanya kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu. Ninaamini vyombo hivyo vitaendelea na kazi ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha hususan wakati wa Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2010. Kadhalika, ninamshukuru sana Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau pia vituo vya Televisheni ambavyo kwa namna ya pekee vimerusha hewani Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2010/2011:-

Mapato : Mwaka 2010/2011 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 561,556,000 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida:

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imetengewa Bajeti ya Shilingi 14,261,820,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- Mishahara ya Wizara – Shilingi 1,506,132,000
- Mishahara ya Taasisi – Shilingi 4,623,818,000
- Matumizi Mengineyo ya Wizara – Shilingi 4,588,037,000
- Matumizi Mengineyo ya Asasi – Shilingi 3,543,833,000

Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara upo katika Kiambatisho Na.IV Aidha, Kiambatisho Na.V kinaonyesha mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida kwa kila Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 4,482,562,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, zote ni fedha za ndani. Mchanganuo kamili upo katika Kiambatisho Na. VI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa mwaka 2010/2011. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2010/2011, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 18,744,382,000 ambapo kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 14,261,820,000 na shilingi 4,482,562,000 ni fedha za miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizi upo katika viambatisho nilivyovitaja hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.hum.go.tz. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambaye anaendelea Kukaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011
Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya
Vijana wa Fedha

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayohusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa likubali kujadili Mpango wa Kazi na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri husikiki vizuri.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Haroub Masoud Mbunge wa Koani, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu tarehe 3 Juni, 2010. Hotuba yangu imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu tangu alipochaguliwa kushika wadhifa huo mwaka 2005. Katika uongozi wake ametekeleza yale aliyoahidi kwa wananchi wakati wa uchaguzi na mengi yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Mheshimiwa Rais amesimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa.

Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesa kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuja nchini kwetu na wadau wa maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu kwa miaka mingine mitano ambayo tuna hakika watanzania watampa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais kwa kumsaidia na kumshauri Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo.

Nampongeza pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuendelea kuongoza vyema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Hotuba aliyoitoa ndani ya Bunge lako Tukufu imeonyesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2010/2011. Nampongeza vile vile Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa Hotuba yake ambayo imemeanisha misingi na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa taifa kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Kwa namna ya pekee naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais akiwemo Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (CUF) na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (CCM). Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa (CCM), Mbunge wa Biharamulo Magharibi kwa kuchaguliwa kwake. Naamini kuwa michango yao imeongeza ufanisi wa Bunge lako katika kuwatumikia wananchi wa taifa hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake na heshima kubwa aliyonipa ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mawaziri wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia

na jamaa za Waheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, mmoja wa waasisi wa Taifa letu, aliyefariki dunia tarehe 31 Desemba 2009 na Sigfrid Seleman Ng'itu aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa aliyefariki dunia tarehe 2 Novemba, 2009. Pia natoa pole kwa wote walioondokewa na wenzi wao, ndugu, jamaa na marafiki katika kipindi hiki, akiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Tunamwomba Mwenyeze Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi na awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya awali naomba sasa kuelezea majukumu ya Wizara yangu, mapitio ya utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, utekelezaji wa Mpango wa kazi wa Mwaka wa Fedha 2009/2010, mpango wa Kazi wa mwaka 2010/2011 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wizara. Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imepangiwa kazi na majukumu yafuatayoambayo tumeyafafanua katika ukurasa wa 5 ambayo ni pamoja na:-

- (a) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Kazi.
- (b) Kuzuia migogoro ya kikazi kwa kufanya kagazi na kutoa elimu katika sehemu za kazi.
- (c) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya ukuzaji wa ajira nchini, hususan upatikanaji wa ajira mpya zisizopungua milioni moja ifikapo mwaka 2010.
- (d) Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, kuratibu Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira, hususan mpango wa mikopo yenyenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo na wa katil.
- (e) Kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ya vijana kiuchumi, kisiasa na kijamii.
- (f) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru nchini.
- (g) Kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri.
- (h) Kusimamia mipango ya usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi (*Occupational Health and Safety*), kuititia Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (*OSHA*)
- (i) Kusimamia mipango ya uboreshaji wa tija na ufanisi kazini kuititia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*).
- (j) Kuratibu na kusimamia masuala ya Hifadhi ya Jamii nchini.

(k) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia kazi za Wakala na Taasisi zifuatazo:-

- (i) Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*);
- (ii) Shirika la Tija la Taifa (*NIP*);
- (iii) Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (*OSHA*);
- (iv) Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*);
- (v) Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*); na
- (vi) Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri (*RTU*).

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa majukumu haya Wizara inaongozwa na Sheria, Sera na Miongozo ifuatayo:-

- (a) Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025);
- (b) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA);
- (c) Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010;
- (d) Malengo ya Maendeleo ya milenio (*MDGs*);
- (e) Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008;
- (f) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007;
- (g) Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003;
- (h) Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri ya mwaka 2005;
- (i) Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2010;
- (j) Sheria za Kazi ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004;
- (k) Sheria ya Malipo ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaouumia Kazini (*Workers' Compensation Act*) Na. 20 ya mwaka 2008; na
- (l) Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (Social Security Regulatory Authority Act) Na. 3 ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Miiongoni mwa maeneo muhimu ambayo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005 hadi 2010 inaielekeza Wizara yangu kutekeleza ni:-

Mheshimiwa Spika, Kuendelea kuwa Karibu na Wafanyakazi na Kuhakikisha kuwa Serikali inayashughulikia kwa Ukamilifu na kwa Wakati Matatizo ya Wafanyakazi. Serikali imeendelea kuwa karibu na wafanyakazi na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Pamoja na mambo mengine Sheria mbili za Hofadhi ya jamii zimetungwa na kuitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hizo ni:-

- (i) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (Social Security Regulatory Authority Act) Na. 8 ya mwaka 2008. Sheria hii inakusudia kupanua wigo wa huduma za hifadhi ya jamii nchini na kuweka utaratibu wa kudhibiti sekta hifadhi ya jamii. Aidha, Serikali ipo katika hatua mwisho za cunda Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii.
- (ii) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (Workers Compensationa Act) Na.20 ya mwaka 2008. Sheria hii inakusudia kuanzisha Mfuko wa Fidia. Pamoja na mambo mengine Mfuko utatathmini na kuboresha viwango vya fidia vitakavyolipwa kwa wafanyakazi wanaoumia, kupata magonjwa, kufariki wakiwa kazini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi; ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya Mwaka 2004. Vile vile imesimamia uundwaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi ili kuwawezesha kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayowagusa. Vyombo hivyo ni pamoja na Baraza la Kazi, Jamii na Uchumi (*LESCO*) na Bodi 8 za Mishahara za Kisekta ambazo ni Kilimo, Huduma za majumbani, Viwanda na Biashara, Madini, Mawasiliano na Uchukuzi, Afya, Uvuvi na Usafiri wa Baharini na Huduma za Ulinzi Binafsi. Aidha, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) imeundwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhimiza maelewano mema baina ya waajiri na wafanyakazi, na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya usuluhishi na uamuzi.

Jumla ya migogoro ya kikazi 20,021 ilipokelewa na kusajiliwa. Kati ya hiyo migogoro 16,161 ilimalizika, ambapo migogoro 12,748 imemalizika kwa njia ya usuluhishi na migogoro 3,413 imemalizika kwa njia ya uamuzi. Muda wa utatuzi wa migogoro umepunguzwa na kufikia wastani wa siku 30. Aidha, jumla ya Mabaraza ya wafanyakazi 184 yalisimamiwa kuundwa mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa usalama na afya mahali pa kazi. Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2010 imetungwa na kupitishwa. Aidha, jumla ya kaguzi za kawaida 16,054 na kaguzi maalumu 38,435 zilifanyika. Wafanyakazi 35,063 walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari wanazozipata kutokana na maeneo wanayofanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea pia kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za wafanyakazi na waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za vyama vya wafanyakazi na waajiri. Jumla ya vyama 6 vya wafanyakazi, chama kimoja cha waajiri na shirikisho moja la vyama vya wafanyakazi limesajiliwa. Lengo ni kuongeza na kuboresha wigo wa ushiriki, majadiliano na utetezi wa haki za waajiri na wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na azma ya kuzalisha ajira milioni moja. Mpaka kufikia mwezi Aprili 2010 jumla ya ajira mpya 1,313,561 kutoka sekta mbalimbali zimepatikana kama ifuatavyo: Serikalini (128,174) na Sekta Binafsi (1,185,387). Aidha, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 1997 na kuandaa mpya iliyopitishwa rasmi mwaka 2008. Programu ya Ajira ya Taifa ya mwaka 2007 ilikamilishwa na kuanza kutekelezwa. Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Ajira upo katika hatua za mwisho kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha mchakato wa kuainisha *SACCOS* mbili kwa kila Halmashauri/Manispaa zote za Tanzania Bara ambazo zimepewa fedha za Mfuko wa Vijana na kisha kuwakopesha vijana. Vile vile mwongozo mpya unaozielekeza Halmashauri/Manispaa za Wilaya juu ya matumizi bora zaidi ya fedha za Mfuko wa Vijana katika Wilaya zao umeandaliwa na kusambazwa katika Halmashauri zote za Wilaya za Tanzania Bara. Uhamasishaji wa Vijana kuanzisha *SACCOS* umeendelea kwa kutumia fursa zote zinazojitokeza. Vile vile Vijana wameendelea kuhamasika na kujiunga katika *SACCOS* mbalimbali nchini.

Jumla ya *SACCOS* 238 zimekopeshwa kiasi cha Shilingi 1,190,000,000 kutoka mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa lengo la kuwawezesha Vijana kmtaji. Aidha, Serikali imekamilisha mapitio ya Sera mpya ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 na kuzinduliwa rasmi mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa kutokomeza ajira mbaya ya mtoto katika wilaya 18 za Tanzania Bara na Wilaya 2 za Tanzania Visiwani. Mpango huu umewezesha watoto wapatao 38,211 kuondolewa katika ajira mbaya na kupewa huduma mbalimbali zikiwemo Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) 15,110, elimu ya msingi 3,358, elimu ya awali 1,856, elimu ya ufundi 12,770, msaada wa kisaikolojia 2,216 na msaada wa vifaa vya shule 2,901.

Aidha, masuala ya utumikishwaji wa watoto yamehuishwa katika mipango ya Halmashauri za Miji na Wilaya, ambapo Mpango wa Kitaifa wa mwaka 2008 wa kuratibu na kusimamia utumikishwaji wa watoto umekamilika. Uelimishaji juu ya athari za utumikishwaji wa watoto umefanyika katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Iringa, Dar

es Salaam na Zanzibar na ukaguzi wa jitihada za kupambana na utumikishwaji wa watoto umefanyika katika Wilaya za Urambo, Kwimba, Simanjiro, Ilemela, Arusha, Iramba na Igunga.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2005/2006 mpaka kufikia mwezi Mei 2010, Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) limewekeza jumla ya Shilingi milioni 994,611.4 katika vitega uchumi mbalimbali, ujenzi wa majengo na kutoa mikopo katika miradi ya maendeleo ya Serikali na makampuni kama ifuatavyo: mikopo Shilingi milioni 40,907.5, miradi ya Serikali Shilingi milioni 216,793.9, dhamana za Serikali Shilingi milioni 194,581.8, hisa Shilingi milioni 68,287.7, amana za muda maalumu Shilingi milioni 274,490.0 na majengo na ofisi Shilingi milioni 199,550.5.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea na utekelezaji wa mpango wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kukuza kipato na kuongeza ajira. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2010 mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 45,436.73 imekopeshwa. Kati ya mikopo hiyo, Shilingi milioni 37,169.88 zilikopeshwa katika Awamu ya Kwanza ya Mpango na Shilingi milioni 8,266.85 zimekopeshwa katika Awamu ya Pili

Jumla ya benki na asasi za fedha 12 zimeshiriki kutoa mikopo kwa wananchi katika awamu ya pili ambazo ni Benki ya *CRDB*, Benki ya Akiba, Benki ya Posta, Benki ya Wakulima – Kagera, Benki ya Ushirika – Kilimanjaro, Benki ya Uchumi, Benki ya Jamii - Mwanga, Pride, Mfuko wa Dhamana wa Rais, *SCCULT*, Dunduliza na Benki ya Azania. Aidha, jumla ya Wajasiriamali 72,113 (44,224 katika Awamu ya Kwanza na 27,889 katika Awamu ya Pili) wamefaidika na mikopo hii wakiwemo wanaume 45,852 na wanawake 26,261. Aidha *SACCOS* zipatazo 192 na vikundi vyta uzalishaji mali na kiuchumi vipatavyo 86 vimefaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea pia kusimamia fedha za Mfuko wa Dhamana (*Revolving Loan Fund*) wa mradi wa Usawa wa Jinsia na Ajira Bora kwa Wanawake. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,229,369,125.05 imetolewa kwa wajasiriamali walengwa 3,800 kupita *SACCOS* za wanawake na Mfuko huu wa Dhamana una akiba ya fedha zenye thamani ya Dola za Kimarekani 261,336.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Sheria za Kazi, yaani Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Madhumuni ya Sheria hizi ni kutoa haki na wajibu kwa wafanyakazi na waajiri, ili kuongeza tija, ufanisi na uhusiano mwema katika sehemu za kazi. Hivi ni vigezo muhimu katika kukuza uchumi na ajira kwani vinavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kazi moja kubwa iliyofanywa katika kipindi hiki ni kukamilisha kanuni za Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Na. 20 ya mwaka 2008 na kukamilisha taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanywa na Wizara ni utekelezaji wa Sera na kukamilisha Programu na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini ambayo itakuwa ndiyo dira ya kuongoza mapambano dhidi ya tatizo la ukosefu wa ajira, hasa mionganoni mwa vijana. Mheshimiwa Spika, sura kamili ya kazi zilizofanywa na Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara imetekeliza kazi zifuatazo:-

- § Vima vya chini vya mishahara katika sekta binafsi vimetangazwa mwishoni mwa mwezi Aprili, 2010 kupitia Tangazo la Serikali Namba 172 la mwaka 2010 na kuanza kutumika tarehe 01 Mei, 2010.
- § Wajumbe wapya wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*) wameteuliwa na Baraza jipya kuzinduliwa rasmi tarehe 13 Agosti 2009. Aidha Baraza limefanya vikao viwili kujadili masuala mbalimbali, ikiwemo mapendelekezo ya vima vya chini vya mishahara yaliyotolewa na Bodi za kisekta za mishahara, pamoja na notisi ya mgomo iliyotolewa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*).
- § Kaguzi za kazi 1,374 zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini pamoja na kutoa elimu ya Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri ili kuwajengea uelewa zaidi juu ya viwango bora vya kazi.
- § Mchakato wa kumpata Mtendaji Makuu wa Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii pamoja na Bodi upo katika hatua za mwisho.
- § Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Na. 20 ya mwaka 2008 zimekamilika na sasa zipo katika hatua ya kujadiliwa na wadau. Aidha Mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi utafanyika katika kipindi cha mwaka 2010/2011. Aidha, jumla ya Shilingi 6,480,000/= zimelipwa kwa wafanyakazi wa umma wapatao 60 walioumia au kupata madhara wakiwa kazini.
- § Jumla ya rufaa 278 kati ya 653 zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana zimetolewa uamuza. Rufaa 375 zilizosalia na migogoro ya kikazi 270 iliyowasilishwa kwa Kamishna wa Kazi, imewasilishwa kwenye Tume ya Usuluhuhishi na Uamuza. Hii ni baada ya kumalizika kwa kipindi cha mpito cha miaka mitatu kilichowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

- § Waajiri na wafanyakazi wameendelea kuhamasishwa kufanya majadiliano ya pamoja ili kuongeza tija, uzalishaji na kupunguza migogoro mahala pa kazi. Jumla ya Mikataba 28 ya makubaliano ya pamoja kati ya vyama vya wafanyakazi na waajiri ya kuboresha maslahi na haki za wafanyakazi imepokelewa.

- § Kwa kushirikiana na wadau na Jamii kwa ujumla, Wizara imetoa mafunzo kwa Halmashauri za Miji na Wilaya juu ya namna bora ya kuhuisha masuala ya ajira mbaya ya mtoto katika mipango yao ya kazi. Aidha tathmini na ufuutiliaji juu ya vita dhidi ya ajira mbaya ya mtoto umefanyika katika Wilaya za Urambo, Kwimba, Simanjiro, Ilemela, Arusha, Iramba na Igunga.

- § Mpango Kazi wa Kitaifa wa kupiga vita ajira kwa watoto (*National Action Plan on Elimination of Child Labour*) wa mwaka 2008 umeandaliwa. Vilevile Wizara imefanya upembuzi na kuainisha kazi zote hatarishi kwa mtoto.

- § Uelimishaji juu ya madhara na vita dhidi ya utumikishwaji wa watoto umefanyika katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Iringa, Dar es Salaam na Zanzibar.

- § Wizara imeshiriki mikutano mbali mbali ya kimataifa ikiwemo vikao viwili vya Baraza la Utawala la Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), ambalo pamoja na mambo mengine lilijadili mbinu mbalimbali za kukabiliana na mtikisiko wa uchumi duniani ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta ya kazi na ajira. Aidha Wizara ilishiriki kikamilifu katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vilivyopelekea kusainiwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kuratibu na kukamilisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii.
- § Kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali ya kazi kwa lengo la kutatua na kuzuia migogoro ya kikazi sehemu za kazi.
- § Kusimamia na kuratibu shughuli za Bodi za Mishahara za Kisekta.

- § Kuratibu shughuli za Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii.
- § Kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini.
- § Kusimamia majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri kwa lengo la kukuza uchumi, ajira, tija na kulinda kazi za staha.
- § Kusimamia na kuratibu ukamilishaji wa Kanuni za Sheria ya Fidia na uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi.
- § Kusimamia na kuratibu shughuli za Ukomeshaji wa Ajira ya Mtoto nchini.
- § Kushiriki na kuhudhuria mikutano ya kimataifa kuhusu masuala ya kazi ambayo ni ILO, AU, EAC, ARLAC na SADC na kushiriki katika shughuli mbalimbali za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kwa kushirikiana na wadau wengine Wizara imeendelea na utekelezaji wa mpango wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kwa kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2010 mikopo yenyenye thamani ya Shilingi milioni 45.436 imetolewa. Kati ya mikopo hiyo, Shilingi milioni 37.169.88 zimekopeshwa katika awamu ya kwanza ya mpango na Shilingi milioni 8.266.85 katika awamu ya pili.
- § Jumla ya wajasiriamali 72,113 wamefaidika na mikopo hii wakiwemo wanaume 45,852 na wanawake 26,261. Kati yao 44,224 katika awamu ya kwanza na 27,889 katika awamu ya Pili. Aidha, SACCOS zipatazo 192 na vikundi vya uzalishaji mali na kiuchumi vipatavyo 86 vimefaidika na mpango huu.
- § Rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira 2008 kwa kipindi cha miaka mitano (2011 - 2015) imekamilishwa. Kipaumbele cha Mkakati huu ni kukabiliana na ukosefu wa ajira, ajira zisizokidhi viwango na tija ndogo mahali pa kazi.
- § Rasimu ya Mswada wa Sheria mpya ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2010 imekamilishwa na kujadiliwa na wadau kwa lengo la kupata maoni yao kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (LESCO) kwa majadiliano zaidi na kuitishwa.
- § Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), mafunzo ya kujenga uwezo yanetolewa kwa Kamati za Kukuza Ajira za Mikoa ya Lindi na Mtwara juu ya

namna bora zaidi ya kuzingatia masuala ya ukuzaji wa ajira katika mipango ya Serikali ngazi ya Mikoa. Aidha mafunzo yametolewa kwa Wakurugenzi wa Sera

na Mipango na Wachumi kutoka Wizara 13 kuhusu namna ya kuzingatia masuala ya ukuzaji ajira katika mipango ya maendeleo ya Serikali ngazi ya Wizara.

- § Hadi kufikia Aprili 2010, jumla ya vikao 16 vya kujadili maombi ya vibali vya ajira kwa wageni vilifanyika. Jumla ya maombi 3,771 yalipokelewa ambapo kati ya hayo, maombi 2,402 yalikuwa mapya na 1,369 yalikuwa ya kuongeza muda. Maombi 2,962 yalikubaliwa, 474 yalikataliwa na maombi 335 yalisitishwa ili kupata taarifa zaidi za makampuni yaliyoomba. Aidha, jumla ya makampuni 68 yamefanyiwa ukaguzi ili kubaini wageni wenye vibali vya ajira na wasio na vibali hivyo na utekelezaji wa sharti kwa makampuni kuandaa wazawa ili kurithi nafasi za wageni watakapo ondoka.
- § Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa kujenga usawa wa jinsia na ajira bora kwa wanawake ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2010 mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,229,369,125.05 ilitolewa kwa *SACCOS* za wanawake katika Wilaya za Tukuyu, Kinondoni, Ilala na Temeke.
- § Jumla ya wajasiriamali 478 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wamewezeshwa kushiriki katika Maonesho ya 11 ya Nguvu Kazi/Jua Kali kwa nchi za Afrika Mashariki, yaliyofanyika Arusha na Dar es salaam mwezi Novemba 2009.
- § Wizara imeratibu mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvu Kazi (*Labour Migration Policy*) ambayo itasaidia kudhibiti uhamaji wa nguvu kazi ndani ya nchi na hivyo kuwa na mtazamo wa kimaendeleo zaidi. Aidha itasaidia kuwalinda watanzania waendao kufanya kazi nje kuhusu maslahi yao ya kikazi, ikiwa ni pamoja na nchi yetu kuwa na mikataba na nchi nyingine (*Bilateral Agreements*) kuhusu maslahi ya nguvu kazi.
- § Mpango wa Takwimu wa Kiwizara kwa Sekta za Ajira na Kazi kama sehemu ya Mpango wa Takwimu wa Kitaifa ambao umeainisha mfumo rahisi wa upatikanaji wa taarifa na takwimu za soko la ajira umeandaliwa.
- § Rasimu ya Kamusi ya Kazi (*Tanzania Standard Classification of Occupations (TASCO)*) imekamilika na kuanza kutumika kwa majaribio kwenye tafiti na masuala yanayohusu ajira, kama vile shughuli za vibali vya ajira kwa wageni, soko la pamoja la ajira la Afrika Mashariki na kwenye utafiti wa majaribio wa hali ya utumishi.

§ Kwa kushirikiana na Tume ya Mipango na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, maandalizi ya awali ya utafiti wa hali ya utumishi kwa nchi za Afrika Mashariki yamefanyika. Hii ni pamoja na majoribio ya utafiti huu kwenye mikoa sita ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

§ Kukamilisha rasimu ya muswada wa Sheria mpya ya Ajira na kuuwasilisha Bungeni.

§ Kuendelea na mchakato wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri ya mwaka 2005 na kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvu Kazi ya mwaka 2010.

§ Kukamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na kuratibu utekelezaji wake.

§Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira, ikiwa pamoja na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira.

§ Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo wadogo wa sekta isiyo rasmi katika maonesho ya 12 ya Nguvu Kazi/Jua Kali yatakayofanyika nchini Uganda.

§ Kuratibu mchakato wa uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Mafunzo kuhusu masuala ya ajira (*National Centre of Employment Studies*) ambacho kitasaidia kutoa elimu na taarifa kuhusu masuala ya ajira kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Halmashauri, Taasisi za Serikali na Binafsi, Vyuo, *NGOs* na Washirika wa Maendeleo.

§Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani, itaendelea na utekelezaji wa masuala ya Kukuza ajira kuititia mpango wa pamoja wa mashirika ya umoja wa mataifa (*One UN Joint Programme*).

§ Kwa kushirikiana na wadau, itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kujenga usawa wa jinsia na ajira bora kwa wanawake. § Kufanya kaguzi katika sehemu za kazi hu-

§ Kuratibu vikao vya Kamati ya utatu vya kujadili maombi ya vibali vya kazi kwa wageni wanaofanya kazi nchini.

§Kuanza kutumia mfumo wa ‘*digitization*’ katika mchakato wa kushughulikia vibali vya ajira za wageni.

§Kuratibu miongozo, viwango na mifumo ya kukusanya, kuchambua na kutangaza takwimu na taarifa za soko la ajira kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na wadau wengine.

§Kuendelea kuratibu matumizi ya Kamusi ya Kazi kwa wadau mbalimbali kama vile waajiri, Wakala wa Huduma za Ajira, Idara ya Uhamiaji, vyuo na taasisi za elimu na watafiti.

§Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa taarifa na takwimu za soko la ajira kwa ngazi za taifa, mikoa na wilaya nchini kwa kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Wilaya.

§Kushiriki kikamilifu katika utafiti wa hali ya utumishi katika nchi za Afrika Mashariki na katika maandalizi ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (*Labour Force Survey*).

§Kutengeneza utaratibu wa kutunza takiwmu (*Database*) za maendeleo ya kijamii na uchumi kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za viashiria vya Kazi na Ajira kwa kutumia mwongozo wa (*Tanzania Social Economic Database (TSED)*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeendelea kuimariswa ikiwa ni pamoja na kuandaa na kusambaza mwongozo mpya wa ukopeshaji wa fedha za mfuko wa Vijana, kupitia SACCOS katika Halmashauri za Wilaya na Sekretariati za Mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, jumla ya Shilingi 1,190,000,000 zimetolewa kwa SACCOS 238 ili kuweza kuwakopesha vijana.

Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2009 zimeratibiwa na kukimbizwa katika mikoa yote 26 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya kauli mbiu: “Piga Vita Ukatili wa Kijinsia, Albino na Watoto”. Mbio hizi zimetumika kuwashamasisha wananchi hasa vijana kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa pamoja na kuanzisha na kujiunga na SACCOS, kupambana na umaskini, maradhi ukiwemo ugonjwa hatari wa UKIMWI, dawa za kulevyta, rushwa na ukatili wa aina zote.

Kupitia mbio hizo, jumla ya miradi 1,781 yenye thamani ya Shilingi 103,161,477,757 ilizinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi. Miradi hii ilitokana na nguvu za wananchi, wahisani na michango ya Serikali.

Vijana kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu walishiriki katika Wiki ya Vijana, Kilele cha Mbio za Mwenge pamoja na maonesho ya wajasiriamali na waelimishaji vijana yaliyofanyika katika viwanja vya Butiama Mkoani Mara. Jumla ya taasisi 116 za vijana na wadau wa vijana walishiriki maonesho hayo.

Katika wiki hii, watu walielimishwa juu ya masuala mbalimbali ya afya yakiwemo masuala ya VVU/UKIMWI pamoja na afya ya uzazi ambapo jumla ya watu 4,086 walijitokeza kupima VVU kati yao wanaume walikuwa 2,284 na wanawake 1,802. Kati ya watu wote waliopima, 115 sawa na asilimia 2.8 walikutwa na maambukizi ya VVU kati yao wanaume walikuwa 35 na wanawake 80.

Wizara imeratibu na kufanikisha uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2010/2011 ambao umefanyika Mkoani Manyara tarehe 29 Mei 2010. Jumla ya viongozi 300 wa vikundi vya vijana kutoka Mkoa wa Dar es Salaam walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na uongozi katika vikundi vya vijana. Aidha, vijana 45 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walipelekwa katika ziara ya mafunzo nchini China.

Vijana hawa walitoka Umoja wa Vijana wa Vyama vya Siasa vya CCM, *CUF*, CHADEMA na *UDP*. Washiriki wengine walitoka vyuo vikuu, shule za sekondari na taasisi za vijana wajasiriamali.

Mwongozo wa Stadi za Maisha kwa Vijana nje ya shule umekamilika na kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Aidha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 imechapishwa katika lugha ya kiswahili kwa lengo la kurahisisha uelewekaji wake.

Kwa kushirikiana na taasisi nyingine za vijana, Wizara imeendesha kambi kazi za vijana na matamasha. Takribani Vijana 2,500 kutoka mataifa ya Uingereza, Ujeruman, Ireland, Ugiriki, Canada, Denmark, Korea Kusini, Marekani, Kenya, Malawi, China, Bolivia, Rwanda, Uganda, Ethiopia, Zambia, Malaysia, Ghana na wenyeji Tanzania walishiriki katika shughuli za kujitolea na kujenga moyo wa uzalendo.

Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za vijana, Wizara iliadhimisha Siku ya Kujitolea Duniani. Sherehe hizo zilifanyika mkoani Dar es Salaam katika Shule ya Watoto Viziwi ya Buguruni, ambapo shughuli mbalimbali za kujitolea zilifanyika. Shughuli hizo ni pamoja na usafi wa mazingira, kupanda miti ya matunda na kivuli pamoja na kutoa msaada wa vifaa vya usafi na kilimo.

Wizara imefanikisha uzinduzi wa Ripoti ya Kamisheni ya Afrika ya mwaka 2009. Ripoti hii inaeleza kwa kina mikakati mbalimbali ya kuwawezesha vijana kiuchumi na kijamii hasa katika masuala ya kukuza ajira.

Utekelezaji wake utakwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya mtandao wa Ajira za vijana Duniani (*YEN*), kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Jumla ya watanzania 300 wakiwemo vijana walihuduria uzinduzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

Kuratibu mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana kwa mwaka 2010.

Kuwawezesha Vijana kiuchumi kupitia mfuko wa Maendeleo ya Vijana chini ya utaratibu wa kuziwezesha *SACCOS* zinazo wakopesha Vijana. Kuendeleza ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi za kimataifa na kuwezesha ushiriki wa vijana na watendaji wa masuala ya vijana katika mipango na mikakati ya Jumuiya za Kimataifa.

Kuwahamasisha vijana kushiriki katika kambi kazi na shughuli za kujitolea katika maeneo yao.

Kukamilisha mkakati wa kitaifa wa ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.

Kuhakikisha kuwa vijana wanapatiwa huduma ya kuunda taasisi/vikundi vyao kisheria.

Kuwaandaa wawezeshaji wa stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule kwa lengo la kuwa na ufahafamu wa matumizi ya mwongozo mpya wa stadi za maisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara imetekeliza kazi zifuatazo:-

Jumla ya watumishi 137 wa Wizara wamepata mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wao. Hii ni pamoja na watumishi 23 waliopata mafunzo ya muda mrefu na 114 mafunzo ya muda mfupi.

Wizara imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi kama vile ulinzi, usafi na matengenezo madogo madogo ya vifaa vya ofisi.

Wizara ilishiriki kikamilifu katika michezo ya SHIMIWI ya mwaka 2009/2010 iliyofanyika mkoani Morogoro.

Kazi ya ukarabati na kuzipatia vitendea kazi ofisi za kazi za Mikoa na Wilaya na baadhi ya majengo katika vituo vya maendeleo ya vijana imeendelea kutekelezwa katika mikoa ya Lindi, Tabora, Kagera, Tanga, Morogoro, Kilimanjaro na Dodoma. Mafunzo yametolewa kuhusu maadili katika utumishi wa umma, vita dhidi ya rushwa na utawala bora, kwa watumishi 124 wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi za ulinzi, usafi na matengenezo madogo madogo ya vifaa vya ofisi katika kuboresha utendaji kazi.

Kufanikisha mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa Wizara.

Kutoa mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukimwi.

Kusimamia na kuratibu ushiriki wa Wizara katika michezo ya SHIMIWI.

Kushiriki katika maonyesho ya wiki ya utumishi wa umma, saba saba na nane nane ili kuelimisha umma juu ya kazi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri imetekeliza kazi zifuatazo:-

Chama kimoja cha wafanyakazi cha “*Finance, Industrial, Banking Utilities, Commercial and Agro-Processing Industries*” - (*FIBUCA*) kimesajiliwa na kufanya idadi ya vyama vya wafanyakazi vilivyo sajiliwa kufikia 24

Kagazi 36 za kumbukumbu za wanachama zilifanyika katika vyama vya wafanyakazi katika Mikoa saba ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam. Aidha, vyama hivi vilishauriwa kuhusu utaratibu wa utunzaji wa kumbukumbu kwa mujibu wa sheria.

Wadau mbalimbali walipatiwa ushauri juu ya taratibu za kujiunga na kuanzisha vyama vya wafanyakazi na waajiri. Vyama vilivyopatiwa ushauri ni *Road Transport*

Workers Union (ROTWU), Tanzania Drivers Trade Union (TDTU) na Communication and Transport Workers Union (COTWU (T).

Migogoro mbalimbali iliyotokana na uanzishwaji wa matawi katika sehemu za kazi, uhamaji wa wanachama kutoka chama kimoja kwenda kingine na utaratibu wa vyama zaidi ya kimoja kuwepo katika sehemu moja ya kazi, ilishughulikiwa kwa njia ya vikao vya majadiliano na wahusika kutakiwa kuzingatia sheria, kanuni na katiba zao. Migogoro hii ilivihusu vyama vya TEWUTA, COTWU (T), TUPSE, TUGHE, TALGWU, TASIMU, TUICO, FIBUCA, TASU na TMW-UNION.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri, kutoa ushauri wa kisheria juu ya taratibu za uanzishwaji wa vyama pamoja na umuhimu wa kujunga na vyama vilivyopo.

Kufuatilia utekelezaji wa sheria za kazi kwenye vyama kwa kufanya kaguzi za kumbukumbu za wanachama na hesabu za mwaka.

Kushughulikia kesi zinazovihu vyama vya wafanyakazi na waajiri na utekelezaji wa sheria za kazi.

Kufuatilia migogoro inayosababishwa na uanzishwaji wa matawi ya vyama katika sehemu za kazi na kutoa ushauri wa kisheria kwa wahusika. Kufanya vikao na majadiliano ya pamoja na vyama kwa lengo la kutoa maelekezo na kubainisha kwa pamoja matatizo yanayotokana na utekelezaji wa sheria za kazi na kanuni zake. Kutayarisha mwongozo wa utendaji bora wa vyama vya wafanyakazi na waajiri kwa kushirikiana na vyama. Kushughulikia masuala ya janga la UKIMWI na masuala ya jinsia kwa kushirikiana na vyama vya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Jumla ya kaguzi 6,180 za kawaida na kaguzi 12,544 maalum ambazo zinajumuisha kaguzi za umeme, boilers, mitungiya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira zilifanyika. Aidha wafanyakazi 9,400 walipimwa afya zao. Imeratibu na kufanikisha maadhimisho ya siku ya usalama na Afya mahali pa Kazi Duniani iliyofanyika mjini Morogoro tarehe 28 Aprili, 2010.

Ofisi ya Kanda ya Kati iliyopo Dodoma imekamilika na kufunguliwa. Aidha maandalizi ya ukarabati wa ofisi ya Kanda ya Kusini umeanza mjini Mtwara.

Mchakato wa ununuvi wa magari ili kurahisisha na kupanua wigo katika zoezi la ukaguzi umeanza.

Kozi tatu za wiki tatu za Afya na Usalama zimefanyika kwa maafisa wa afya na usalama mahali pa kazi kwa wafanyakazi wapatao 63.

Mafunzo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi yamefanyika mara mbili kwa wafanyakazi wa makampuni yanayoagiza mafuta. Hali kadhalika mafunzo ya huduma ya kwanza yamefanyika katika awamu sita ambapo jumla ya wafanyakazi 200 kutoka sehemu mbalimbali za kazi walimenufaika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Kufanya kaguzi 7,000 za kawaida na kaguzi 14,000 maalumu za kisheria za afya na usalama mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi 10,000 katika sehemu mbalimbali za kazi.

Kutoa mafunzo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi hususan namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

Kuanzisha na kuimarisha mifumo mbalimbali ya utendaji kazi, kwa kuripoti na kutoa taarifa za mara kwa mara za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi.

Kuwaelimisha wafanya biashara wadogo na wa kati katika mikoa mitano ya Tanzania Bara ili waweze kuboresha mazingira ya kazi. Kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO Conventions*) ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

Kuunda Baraza la Taifa la Afya na Usalama Mahali pa Kazi. Kukamilisha kanuni sita za utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2010. Kuanzisha tovuti ya *OSHA* itakayoisaidia jamii kuongeza uelewa wa masuala ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi. Kuendelea kuimarisha ofisi za kanda ikiwemo makao makuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira nchini (TaESA) ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Ofisi za kanda ya kaskazini katika Mkoa ya Arusha na Kanda ya Kati, Dodoma zimefunguliwa.

Jumla ya watafuta kazi 2,770 wameandikishwa. Kati yao 1,212 waliunganishwa kwa waajiri wenyewe fursa za ajira na 86 walithibitika kuajiriwa ndani na nje ya nchi. Watafuta kazi 1,107 walijengewa uwezo na mbinu mbalimbali za kutafuta kazi na kuujajiri.

Aidha watafuta kazi 584 walipewa ushauri juu ya uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi zinazo wastahili kulingana na sifa walizonazo ili kuongeza uwezo wa kuajiriwa/kuajirika (*vocational guidance and employment counseling*).

Jumla ya nafasi 672 za kazi zilisajiliwa na waajiri 211 walitembelewa.

Mkataba wa maridhiano kati ya waajiri wa nje ya nchi na Wakala umeandaliwa (*Cross Border – Bilateral Recruitment Agreement*).

Jumla ya watumishi 17 walihudhuria mafunzo ya uongozi na 49 walihudhuria mafunzo elekezi. Aidha jumla ya watumishi 22 walihudhuria mafunzo mbalimbali katika nyanja za uhasibu, ununuzi, mipango na tathmini, utunzaji wa Kumbukumbu na Uhazili, kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

Wakala ulikagua Wakala binafsi 17 wa huduma za Ajira na kuzitambua Wakala 16 kati ya hizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kupanua wigo na kuboresha utoaji huduma za ajira nchini.

Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ajira nje ya nchi (*cross-border placement*).

Kuboresha mifumo ya huduma za uendeshaji katika kuwe

Kuwajengea uwezo watumishi kwa njia ya mafunzo ili kuongeza ufanisi.

Kuweka na kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi.

Kupambana na ugonjwa hatari wa UKIMWI mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara kuitia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Mapato ya Shilingi milioni 495,254.9 sawa na asilimia 100.9 yamekusanywa ikilinganishwa na lengo la kukusanya Shilingi milioni 490,674.3.

Ujenzi wa mabweni matano na madarasa katika Chuo Kikuu cha Dodoma yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 5,000 umekamilika. Aidha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo mengine kwa ajili ya wanafunzi 15,000 unaohusisha mabweni, madarasa, mabwalo ya chakula, majengo ya ofisi na viwanja vya michezo unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2010.

Awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba za polisi 24 katika maeneo ya Ziwan Baracks, Unguja na Limbani Pemba umekamilika na kukabidhiwa. Aidha nyumba 96 zilizopo Barabara ya Kilwa Dar es salaam, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia

na Kupambana na Rushwa na ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Mbozi umekamilika.

Ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Kigoma na katika Wilaya za Njombe na Kahama unaendelea na unatarajiwu kukamilika mwezi wa Juni na Septemba 2010.

Ujenzi wa Kituo cha Biashara (*Business Park*) cha wafanyabiashara ndogondogo (*Machinga Complex*) katika Manispaa ya Ilala umekamilika na kukabidhiwa mwezi Mei, 2010.

Ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi katika Jiji la Arusha umeanza mwezi Mei 2010 na unatajiwa kukamilika mwezi Februari 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara kupitia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kukusanya jumla ya shilingi milioni 767,194.0 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo.

Kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii.

Kufanya upembuzi yakinifu ili kuona uwezekano wa kuangalia upya mahitaji ya wanachama wake kulingana na mahitaji ya Hifadhi ya Jamii.

Kukamilisha uwекaji kompyuta katika ofisi zake za mikoa na wilaya na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika.

Kuboresha uwекaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu vya kuweka kumbukumbu hizo katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Mara. Kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi ya vitega uchumi katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Mbeya, Morogoro na Shinyanga na ujenzi wa ofisi ya Wilaya ya Kahama.

Kuendelea na miradi ya ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Tanzania jijini Nairobi nchini Kenya, ujenzi wa nyumba za Polisi awamu ya pili, ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (*TPDF*), ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi, Dar es Salaam na Bugarika Mwanza.

Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni, kujenga hoteli ya kisasa Mwanza, Hospitali ya Apollo jijini Dar es Salaam, Chuo cha Nelson Mandela Arusha, jengo la Shirika la Utangazaji Tanzania, ofisi za *RITA*, jengo la Mzizima jijini Dar es Salaam, jengo la Maadili Dar es Salaam, Jengo la Maduka Moshi (*Shopping*

Mall), na ujenzi wa majengo katika maeneo ya Ilala Mchikichini na Magomeni Kondoa Dar es Salaam.

Kushirikiana na wadau wengine katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam hadi Chalinze Mkoani Pwani na mradi wa uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara kuitia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Mafunzo 73 ya kuboresha ufanisi na tija yametolewa kwa taasisi na mashirika ya umma na binafsi na kuwanufaisha washiriki 1,106.

Huduma za uelekezi zimetolewa kwa Taasisi 37.

Tafiti 2 kuhusu uboreshaji wa tija sehemu za kazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Shirika imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kuendesha mafunzo 80 ya uongozi yatakayo hudhuriwa na watumsihi 1,300 kutoka taasisi za umma na binafsi.

Kutoa huduma za ushauri kwa wateja 40 katika sekta za umma na binafsi.

Kufanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayo lenga kukuza tija.

Mheshimiwa Spika, Tume hii ni moja kati ya Taasisi zilizoundwa kutohana na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 na inafanya kazi katika Kanda 11. Jukumu kubwa la Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ni kusuluhisha na kufanya uamuzi wa migogoro sehemu za kazi. Aidha, upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Tume unaweza kupeleka shauri hilo katika Mahakama ya Kazi ambayo ni kitengo chini ya Mahakama Kuu. Pia kusimamia uanzishwaji na uimarishaji wa mabaraza ya wafanyakazi mahali pa kazi, Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu kuitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilitekeleza malengo yafuatayo:-

Migogoro 12,573 ilipokelewa na kusajiliwa, ambapo migogoro 6,737 ambayo ni sawa na asilimia 53.6 ilishughuligulikiwa na kumalizika. Kati ya hiyo migogoro 4,378 sawa na asilimia 65 ilitatuliwa kwa njia ya usuluhishi na migogoro 2,359 sawa na asilimia 35 ilitatuliwa kwa njia ya uamuzi. Aidha, Migogoro 5,836 inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

Mabaraza ya Wafanyakazi 72 yalisimamiwa kuundwa. Semina 62 za mafunzo kuhusu Sheria za Kazi, yaani Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya

mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 yametolewa na ushauri kuhusu masuala ya ushirikishwaji wa wafanyakazi ultolewa kwa Taasisi 35.

Tume imeratibu ufasiri wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 kuwa katika lugha ya Kiswahili.

Jumla ya watumishi wapya 33 wameajiriwa katika nyanja mbalimbali ili kuboresha utendaji wa Tume.

Aidha, Watumishi 13 walipata mafunzo ya stashahada ya uzamili katika fani ya usuluhishi na uamuza Sheria. Imehudhuria mikutano ya kitaifa na kimataifa inayohusu utekelezaji wa Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara kupitia Tume itafanya kazi zifuatazo:-Kupokea na kusajili migogoro mipy ya Kikazi, kusuluhiha kwa njia ya mazungumzo na kuandaa Kupokea na kusajili migogoro Kuandaa taarifa za migogoro iliyoshindikana kusuluhihswa na kuipeleka katika Kitengo cha Uamuza kwa hatua za Uamuza.Kufanya utafiti juu ya migogoro ambayo haijatolewa taarifa katika Tume na kuishughulikia.

Kuendesha mafunzo ya uelewa kwa waajiri na wafanyakazi juu ya matumizi ya Sheria za Kazi.

Kujenga uwezo wa Tume kwa kutembelea nchi zinazoendesa shughuli za utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa lengo la kujifunza.

Kuandaa mchakato wa kuwatumia wasuluhihi binafsi (*Private Mediators*).

Kutoa ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya matumizi ya Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu.

Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudzi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na taifa.

Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga (Mb), Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa msaada na ushauri wake wa karibu.

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Hajjat Kijakazi Rajabu Mtengwa na Naibu Katibu Mkuu, Bibi Edine Mangesho,

pia kwa Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao, ambao wameshirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wemetuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Kwa njia ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*), Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama vyta Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Naishukuru pia *TACAIDS* kwa misaada mbalimbali kwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yake.

Kwa uchache naomba shukrani za dhati ziende kwa Serikali ya nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Benki ya Dunia (*WB*), Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA* na *CYP*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Spika na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki ambapo kwa kipindi cha miaka mitano limetoa maamuzi mazito yaliyothibitisha uwezo wake katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini.

Natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ya mara kwa mara kuhusu Wizara yangu na vile vile wananchi wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Urambo Magharibi kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia kwa kipindi chote cha miaka mitano ambao kwa kiasi kikubwa umeniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa. Ushirikiano huu hatimae kwa kushirikiano na wenzetu wa Urambo Mashariki, umewevesha Jimbo letu kuwa Wilaya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuiteua Kaliua kuwa mionganoni mwa Wilaya mpya. Tunaahidi kufanya kazi kwa mshikamano zaidi, ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi ili kuleta maendeleo makubwa zaidi ndani ya miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2010/2011, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 15,646,578,000/= kwa Fungu 65. Kati ya fedha hizo Shilingi 9,005,921,000/= ni

kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 1,824,503,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi 7,181,418,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha kiasi cha Shilingi 6,640,657,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo Shilingi 1,545,433,000/= ni fedha za hapa nchini na Shilingi 5,095,224,000/= ni fedha za nje.

Vile vile naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha Shilingi 2,034,676,300/= chini ya Fungu 15 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, ambapo shilingi 457,926,300/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 900,250,000/= ni kwa matumizi mengineyo. Aidha, kiasi cha Shilingi 676,500,000/= ni fedha za nje kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Hawajasikia.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono lakini imesomwa kama cherehani. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati au Mjumbe wa Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti. Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir. Kuna ndugu zake hapa, Khalfani, Herieth, Munira Kwegyir, Faida Kuwelu, Hidaya Omar, Rehema Kwegyir, wako wapi. Wamevaa sare kabisa msikilizeni mama yenu anavyosoma hii hotuba.

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai hadi siku hii ya leo. Aidha namshukuru Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunitua kuwa Mbunge katika viti vyake kumi vya uteuzi. Namtakia kila la kheri kwenye uchaguzi ujao ashinde kwa kishindo, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii naomba kusoma taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kubwa kuchukua fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11) Toleo la Mwaka 2007 kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa fedha 2009/2010 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011; kwa Fungu 65 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati naomba nitumie fursa hii kutoa Salam za pole kwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, (Mb) kwa kufiwa na mume wake. Aidha, natoa Salam za pole kwa Mjumbe mwenzetu wa Kamati Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, (Mb) kwa kufiwa pia na mume wake. Wote kwa pamoja tunawapa pole na kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze pema peponi roho za marehemu na kuwatia nguvu na ujasiri wenzetu katita kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya majukumu ya Kamati hii ni Kupitia na Kuchambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na kuisimamia na kuishauri Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 04 Juni 2010, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam na kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2009/2010. Wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ilitoa ushauri kuhusu maeneo mbali mbali kwa Wizara na Taasisi zake ikiwa ni pamoja na Serikali kuongeza ruzuku kwa Shirika la Utangazaji Tanzania na Udhagini wa Serikali katika kutoa mkopo ili Shirika liweze kukarabati majengo yake yaliyoko Mikocheni, BAKITA kushirikiana na Hazina ili kuandaa vitabu vya Bajeti kwa Lugha ya Kiswahili, Serikali kutenga fedha katika kila Bajeti ya Mwaka kwa ajili ya Maafisa Utamaduni, Uhuishaji wa Sheria ya Hatimiliki, na mwisho Mapato na Matumizi yanayotokana Uwanja wa Taifa yakaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanzia Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara imejitahidi kutekeleza na kuzingatia ushauri wa Kamati isipokuwa kikwazo kikubwa ni ufinyu wa Bajeti inayotengwa ndio umekuwa ukikwamisha utekelezaji wa malengo Wizara iliyojiwekea na ushauri unaotolewa na Kamati. Hata hivyo Kamati inaendelea kuisihi Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati ili kuweza kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara ykwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2010/2011, Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati Malengo ya Asasi zilizo chini ya Wizara hii kwa Mwaka 2010/2011. Asasi hizo ni Kampuni ya

Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya kuigiza, Balaza la Sanaa la Taifa (BASATA), Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Taasisi ya Sanaa za Utamaduni Bagamoyo(*TaSUBa*) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Katika maelezo hayo majukumu ya jumla ya kila Asasi na malengo yake kwa mwaka 2010/2011 yalielezwa.

‘Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara, Kamati imeridhishwa na malengo yaliyopangwa na kila Asasi kama yaliyoyelezwa na Mheshimiwa Waziri alipokutana na Kamati. Aidha, Kamati inasisitiza utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011. Ili kutekeleza vyema majukumu yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 18,472,194,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 14,261,820,000.00 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 4,482,562.00 kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa Mwaka 2010/2011. Baada ya kupitia mafungu yote, Kamati inaunga Mkono hoja ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011. Kwa kuzingatia majukumu ya Wizara hii, pamoja na malengo yaliyowekwa kwa kila Asasi, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Habari. Katika hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Waziri alieleza Bunge lako Tukufu kuwa “kwa kuzingatia umuhimu wa Vyombo vya Habari katika Maendeleo ya Nchi yetu, Mchakato wa kutunga Sheria ya kusimamia Vyombo vya Habari umeanza. Mchakato huo upo katika hatua ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Kuhusu pendekozo la kutunga Sheria ya kusimamia Vyombo vya Habari, tunaamini kuwa Baraza litaridhia pendekozo hili ili Muswada wa Sheria hiyo uweze kuletwa katika Bunge lako Tukufu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo ya Waziri, Kamati yangu ilishauri kuwa, wakati huu ambapo tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, ni vyema Serikali ikapitisha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari pamoja na ile ya Haki ya Kupata Habari ili kuwawezesha waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa Uhuru zaidi. Aidha, wananchi pia wangkuwa na nafasi pana ya kufanya maamuzi sahihi zaidi kuhusu Mgombea wanayemtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeona ni vyema kuweka bayana kuwa Uhuru wa Habari kwa sasa unatishiwa zaidi na hali ya kisiasa. Hii ni kwa sababu Wanasiwa wameamuwa kujiingiza katika umiliki wa Vyombo vya Habari, hali ambayo inaleta mkanganyiko na kuwafanya wananchi wapate taarifa zenye mtazamo wa Mwanasiwa husika tu. Vyombo vya namna hii wakati mwingine hushindwa kutekeleza Kanuni na Maadili ya uhandishi wa Habari na kujikuta vikianguka katika falsafa za Wanasiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri huu wa Kamati haukuzingatiwa, na kwa kuwa Mkutano huu wa 20 ni wa mwisho, ni dhahiri kuwa Muswada wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Habari hautajadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri na kuwasihii Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wote wa Umma na Serikali kuanzisha mahusiano mazuri na Vyombo vya Habari ili kufahamu namna Waandishi wa Habari wanavyofanya kazi zao badala ya kuwaona kama maadui.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia *TBC* kwa uanzishaji na uboreshaji wa huduma mpya ya ving'amuzi kwa Mikoa minne ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Arusha. Ubunifu huu utalionezea Shirika na Serikali mapato. Kamati inashauri Wizara kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) kujizatiti zaidi na kujipanga vizuri ili kuhakikisha huduma hii inafika Mikoa yote na upungufu uliojitokeza katika Mikoa hii minne ya mwanzo ufanyiwe kazi, hasa yale yanayohusisha uhaba wa ving'amuzi wakati soko lipo la kutosha.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuona jinsi itakavyo imarisha vituo vyote vinavyotoa huduma katika kuongeza mapato. Ipo haja ya kuanzisha vyanzo vipyta vya mapato vyenye tija na kutoa huduma za uhakika katika zama hizi za biashara ya kiushindani. Aidha, Kamati imesikitishwa na Serikali kutotoa udhamini kwa *TBC*, ingawa kwa muda wote wa uhai wa Kamati wa Kipindi cha miaka mitano, Kamati imekuwa ikiombwa na kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuidhamini *TBC* ili iweze kukamilisha ujenzi wa majengo yake yaliyoko eneo la Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inamaliza muda wake kwa masikitiko makubwa kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza ushauri huu wa Kamati hata pale ambapo *TBC* imekiri mbele ya Kamati kuwa inauwezo wa kurudisha pesa hizo za udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utamaduni. Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Kamati ilitoa maoni kwa Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kuwa Kiswahili kinatumika wakati wote kwenye shughuli za Serikali. Ikiwa ni pamoja na mawasiliano.

Napenda kuipongeza Wizara kuptitia Kauli ya Serikali kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu katika shughuli za Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 19/4/2010 kuwa lugha rasmi ya mawasiliano ya Serikalini ni Kiswahili. Aidha, Kamati ilishauri kuwa BAKITA isaidie kuandaa vitabu vya Bajeti kwa Mwaka 2010/2011 kwa Lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi kuelewa muelekeo wa hali ya Uchumi na Mapato ya Serikali na maeneo yaliyopewa kipaumbele. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kauli zake na kuhakikisha kile kinachotamkwa kinatekelezwa na Watendaji wote wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kauli hii ya Serikali kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli rasmi za Serikali haikuanza leo, kunako tarehe 10/12/1962 muda mfupi baada ya Uhuru Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamuhuri ya Tanganyika, alihutubia Bunge kwa Lugha ya Kiswahili, hatua ambayo ilisababisha kutolewa matamko mbalimbali na Viongozi wa Serikali kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili.

Mwaka 1967, aliyezeka Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, Hayati Rashidi Mfaume Kawawa, alitoa Waraka wa matumizi ya Lugha ya Kiswahili.

Mwaka 1974, aliyezeka Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, Utumishi Ndugu J.D. Mganga alitoa Waraka wa Utumishi Na. 1 wa 1974 ulioelezea Kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Ofisi za Serikali. (*Makof*)

Mei 2005, aliyezeka Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera), Mheshimiwa William Lukuvi, aliagiza Taarifa za Mikutano, Semina na Warsha nchini zitolewe kwa Lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya wananchi.

Pia taarifa za miradi inayohusu wananchi ni lazima zitolewe kwa Lugha ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na vipeperushi na nyaraka zinazohusu miradi hiyo.

Aidha, katika kikao cha Baraza la Mawaziri tarehe 18.02.2010, Makamu wa Rais. Dr. Ali Mohamed Shein, alisisitiza suala la matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na kuwakumbusha Watendaji Serikalini kuzingatia Waraka wa Hayati Mzee Kawawa alioutoa alipokuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa kuzingatia matamko haya na umuhimu wa Lugha ya Kiswahili, ikiwa sasa pia ni Lugha ya Kimataifa inayotumiwa mathalani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika.

Kamati inaishauri Wizara kuptitia Serikali kufuata hatua moja baada ya nyingine kuhusu Utekelezaji wa kauli zake, na siyo kutoa kauli tu ambazo Watendaji na wananchi wanaona hazina uzito na hivyo kutozitekeleza, hatimaye Serikali yenye kushindwa kusimamia maagizo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maarifa yanaweza kutolewa katika Lugha yoyote ile nchi kama China, Urusi, Japan, Korea na nchi nyingine nyingi zimepata maarifa kwa kutumia Lugha zao na kupata elimu ya juu katika teknolojia kwa Lugha zao na sasa watu wake wanawenza kufanya kazi popote pale duniani na kujipatia maarifa na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa letu lingetumia matamko haya ya Serikali kikamilifu leo tungekuwa hatuna mjadala wa Lugha gani kati ya Kiswahili na Kingereza itumike Shulenii na Vyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa. wakati wa hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010 Mheshimiwa Waziri alilieleza Bunge lako tukufu kuwa Baraza liliendeleza na kukuza vipaji kwa Wasanii 560 na wakati akiwasilisha maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010 na Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Waziri alilieleza Kamati kuwa Wizara imeweza kutoa Mafunzo ya Sanaa kwa Watoto 200 wa Shule za Msingi kwa kuwapatia stadi za uchoraji na utambaji wa hadithi katika Wilaya za Kinondoni, Temeke, Ilala na Korogwe.

Aidha mafunzo ya sanaa kwa wasanii 200 katika Wilaya za Bunda na Ukerewe yalitolewa kwa lengo la kuwapatia stadi za kuzalisha sanaa bora, kukuza ujasiriamali, uelewa wa hakimiliki na masoko ya sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri hii iliyofanywa na Wizara kuitia Baraza la Sanaa, Kamati inaushauri kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko ihimize kuitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Hati Miliki, upatikanaji wa Sheria hii utasaidia ukuaji wa pato la Wanamuziki na Serikali kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri wa Fedha na Uchumi akiwasilisha katika Bunge lako Tukufu mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011, Wabunge wengi na wananchi wameilamu Serikali kwa kushindwa kuonyesha vyanzo vipyta ya mapato. Uchambuzi wa Kiuchumi wa Sekta ya Muziki uliofanywa na Idara ya Uchumi Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, umebaini kuwa mara Sheria ya Hatimiliki itakapopitishwa na Bunge lako Tukufu itakuwa ni moja ya chanzo kipyta na kizuri cha mapato ya Serikali kwani utafiti umeonesha kuwa:-

- Pato la Taifa linalotokana na Sanaa ya Muziki hapa Tanzania lilikadiriwa kuwa Sh.71 bilioni, ikiwa ni karibia 0.5% ya jumla ya pato lote la Taifa (*GDP*);
- Mapato yanayopatikana kwenye Sekta ya Muziki, yanatoka katika 12% tu ya kiwango kilichotakiwa kulipiwa Kodi ya Mapato kwenye sekta hiyo;

□ Hasara inayotokana na ulipaji mdogo wa kodi kwa Taifa (kwenye sekta ya muziki) inakadiriwa kuwa 0.1% ya *GDP* na hii ilitegemewa kuongezeka kwa kiasi cha 11% katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2007;

□ Kama Sheria ya Hatimiliki ikitekelezwa, faida kwa Wadau wa Sekta ya Muziki itakuwa kama ilivyoaainishwa hapa:-

1. Itaongeza kipato kwa Wadau wote wa Sekta hii, ikiwemo Serikali.

2. Ongezeko la kipato litakuwa kwa wale walioajiriwa katika muziki kwa sasa na pia hilo litavutia ajira mpya kwenye muziki.

3. Makadirio ya waliodumu katika Sekta ya Muziki ni 48% ya wale wote wanaojishughulisha na muziki, wakati 52% ya wanaofanya shughuli za muziki, huzichukulia tu kama kazi ya ziada.

4. Kipato kitakuwa zaidi ya mara dufu na hii itafanya wengi kwenye Sekta ya Muziki kufanya kazi hiyo kuwa ya kudumu, (wataifanya na kuithamini – kazi inayowalipa vizuri).

5. Idadi kubwa zaidi inaweza kuajiriwa katika Sekta ya Muziki hapa nchini na kuongeza kipato kwa Wanamuziki na Serikali pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa katika Kujadili na Kupitia Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2010/2011. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti na Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mgeni Jadi kadika, Mheshimiwa Salim Abdullah Khalfan, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Anna L. Lupembe, Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Elietta Nandumpe Switi, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Al- Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Kapt. John D. Komba na Mheshimiwa Mwajuma. H. Khamis. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Mwenyekiti wa Kamati, kwa umahiri wake wa kuiongoza vyema Kamati. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Kapt. George H. Mkuchika, (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel N. Bendera, (Mb), Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Katibu Mkuu, Ndugu Sethi

Kamuhandha pamoja na Watendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali kwa kuandaa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, naomba nikushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika mkisaidiwa na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa Spidi na Viwango. Kwa hakika Bunge hili la Tisa, chini ya Uongozi wako mahiri, litabaki kuwa Bunge la Kihistoria katika nchi yetu.

Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge wakisaidiana na Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Elieka Saanya kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa kusoma vizuri taarifa hiyo. Sasa nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, ndiyo unatafutwa uzoefu namna hiyo.

MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Amani, kwa kutuwezesha sote kumaliza Bunge hili la Tisa tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upizani, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Kambi, kwa imani waliyokuwa nayo kwangu kwa kunitfea kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi kwa Wizara hii. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano ambao wamenipatia kwa kipindi chote cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa, nawashukuru wananchi wote wa Wilaya ya Kilwa, Chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*), kwa ushirikiano ambao wamenipatia ndani na nje ya Bunge kwa kipindi chote cha uwakilishi wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru sana mume wangu mpenzi, Ndugu Selemani Bungara (BWEGE) na watoto wangu Abbasi Selemani, Hassani Selemani na Goodluck Selemani, kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote ambacho nimekuwa nje ya familia nikifanya kazi za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa juhudzi zao katika kuhakikisha mipango ya Wizara inakwenda kama ilivyopangwa. Sambamba na hilo, nawapongeza Wanamichezo na Wanahabari wote katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata kile wanachostahili katika tasnia nzima ya michezo na habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tasnia ya habari, katika hali ya Tanzania, ni vigumu kutaja habari na umuhimu wake bila ya kujielekeza kwanza kwenye Katiba ya nchi, ambayo ndiyo Sheria Mama. Hivyo basi, marekebisho yoyote yale ya sheria ambayo yanalenga kutoa mwongozo katika tasnia ya habari, ni lazima ijkite katika misingi ile inayoelezwa na Katiba. Misingi hiyo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kila mtu:

- Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;
- Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;
- Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na
- Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirisha kuwa kupata habari ni moja ya haki za msingi za raia. Serikali ina jukumu la kusimamia haki hii na kutetea haki za wananchi wake. Hivyo, kusambaza habari ni jukumu la Serikali, ingawaje hata vyombo binafsi vinayo majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya sekta ya habari na utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na yombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majorida, televisheni, filamu, video, intaneti, picha, vipeperushi, katuni na mabango. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano yamerahisisha upataji na utoaji habari. Hii ina maana kwamba Serikali inatakiwa kuzipitia na kuzihuisha sheria zote zinazokataza kutolewa kwa taarifa zenye manufaa kwa umma ingawa kupata na kutoa taarifa ni haki ya msingi ya Mtanzania, kinyume chake ni Tanzania inaendelea kuvunja haki ya msingi na kutotambua ipasavyo haki hiyo ya uhuru wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wa tasnia ya habari wamekuwa wakiilalamikia Serikali kwa kile kinachoitwa mgongano wa maslahi, kwani Serikali ni mmiliki wa vyombo vya habari, msajili ya vyombo vya habari, mtunga sera, msimamizi na mwisho ni mshindani kwenye tasnia nzima ya habari. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri alieleze Bunge, kwa njia hii haki na usawa mionganoni mwa vyombo vya binafsi na Serikali inaweza kupatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa taaluma ya habari ni moja ya nguzo muhimu sana katika jamii, kwa nchi zingine duniani sekta ya habari nayo inachukuliwa kama nguzo ya nne katika utawala mzima wa nchi, nguzo zingine zikiwa ni Bunge, Serikali na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu, ni hatua gani zimechukuliwa kufuta Sheria Kandamizi ya Magazeti ya mwaka 1976 ambayo inampa mamlaka Waziri wa Habari kufungia chombo chochote cha habari ambacho yeye anaona kimeandika taarifa asiyopenda. Sheria hii, inampa mamlaka Waziri kuamua kwa utashi wake nini kibaya na nini kizuri. Hii ni mionganoni mwa sheria 40 ambazo Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza zifutwe. Leo, ni zaidi ya miaka 17 Serikali bado haijafuta na haionyeshi dalili za kuifuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni mazoea kwa Serikali yetu kuitumia vibaya sheria hii, ambapo pale chombo cha habari binafsi kinapoandika habari ambayo Mhariri

na Mchapishaji wanaweza kuzithibitisha, Serikali haitoi nafasi kwa wahusika kujitetea na kuthibitisha habari hiyo. Badala yake Serikali inatumia sheria hii kufungia gazeti au chombo cha habari isichokitaka na kunyamazia inachokipenda. Lakini pili, Serikali imekuwa ikiitumia sheria kukandamiza vyombo vyahabari ambavyo vinaonekana havitakiwi na watu fulani ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko humu Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wenzetu wamekuwa wakituhumu baadhi ya magazeti kuwachafua na kuwazushia habari za uwongo hasa katika kipindi hiki cha kuelekeu uchaguzi, lakini Serikali haijawahi kuchukua hatua zozote angalau kukemea vyombo hivyo au kutoa ushauri kwa wahusika kutafuta haki yao Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili ambalo wewe unaliongoza, kulikuja malalamiko yaliyotolewa Novemba 2008 na Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, kwamba gazeti la Serikali – Habari Leo, limedhalilisha Bunge kwa kuchapisha habari iliyotuhumu Wabunge kujipanga kuchukua hatua dhidi ya Mheshimiwa Rais kutokana na hatua za Rais kutaka wezi wa fedha katika Akaunti ya Fedha za Kigeni (*EPA*) ndani ya Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) wasishtakiwe.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, aliomba Mwongozo wako na kutaka Bunge hili lipewe taarifa sahihi ya habari hiyo, chanzo chake na kiini chake. Alimtaka Waziri wa Habari amuagize Mhariri wa Habari Leo, kukanusha taarifa hiyo. Waziri aliliambia Bunge hili, kwamba tayari Serikali imemjulisha Mhariri malalamiko hayo. Pamoja kupewa malalamiko hayo bado maelezo hayo hayajatolewa na wala gazeti halijaomba radhi, hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya gazeti hili la Serikali. Hali hii inatoa ujumbe gani kwa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, alitangaza hapa Bungeni kwamba Mhariri Mtendaji na Bodi ya Wakuregenzi ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) wangeteuliwa hivi karibuni. Hata hivyo, ni bodi tu iliyoteuliwa na anayeongoza kampuni hivi sasa amekaimu kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kama hana sifa zinazohitajika kwa nini asitafutwe mwenye sifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujuu kazi ya Wizara hii ni kufungia magazeti tu au kuendeleza tasnia ya habari? Tunasema haya kwa sababu, tangu Wizara hii iliporejeshwa miaka mitano iliyopita, Watanzania hawajaona kitu chochote cha mpango wa maendeleo ya sekta ya Waandishi wa Habari kama kuondoa sheria kandamizi na kuleta sheria mpya ambayo tayari imeridhiwa na wadau walioleta Rasimu Mbadala ya Muswada wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka Mheshimiwa Waziri kueleza kazi ya Idara ya Habari Maelezo hasa. Idara hii imekuwa ikitumika kutisha vyombo vyahabari na Wahariri wake badala ya kuvilea. Hali hii imetokana na Serikali kuanzisha Idara za Mawasiliano katika kila Wizara na hivyo MAELEZO ikajikuta imegeuka mahali pa watu wasio na kazi wenye kuja kazini asubuhi na kusoma magazeti. Tija yao kwa Taifa inapimwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Habari MAELEZO kwa mfumo wake wa sasa, haina tofauti na shirika la Serikali lililofungwa la SHIHATA. Kama Serikali imefunga SHIHATA kwa kukosa kazi, Kambi ya Upinzani inauliza kwa nini isiifunge

Idara hii ambayo inaongeza mzigo wa ukubwa wa Serikali na badala yake kupeleka baadhi ya shughuli zake Wizarani kwa kuweka Kitengo cha Mawasiliano na Wahariri?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kwa takwimu ni jinsi gani imeinua ubora wa taaluma ya habari kwa kushirikiana na vyombo vyao vya binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tasnia ya mila, desturi na utamaduni. Naomba kunukuu Sera ya Taifa ya Utamaduni, inasema:-

"Ingawa sekta ya utamaduni imekuwa katika mfumo wa Serikali tangu mwaka 1962, nafasi ya sekta ya utamaduni katika maendeleo ya Taifa letu bado haijatambuliwa kikamilifu. Mipango ya maendeleo imekuwa ikibuniwa na kutekelezwa bila kujali utamaduni wa wananchi, mfano matumizi ya uzoefu, stadi na elimu ya jadi havitiliwi maanani. Utamaduni haupewi dhima katika maamuzi na mipango ya maendeleo". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nukuu hiyo ni dhahiri kuwa Serikali siyo kama haielewi umuhimu wa utamaduni katika mipango ya sekta mbalimbali za uchumi katika nchi yetu, bali inafanya makusudi tu na hili lifanywalo ni kwa manufaa ya nani? Je, tamaduni zetu zinahusishwa vipi katika mpango mzima wa maendeleo ya michezo mathalani kulenga shabaha, kuruka kwa upondo, bao na riadha hapa nchini? Kambi ya Upinzani inasema kuwa Tanzania tutakuwa tunashindwa kwa sababu ya kutokuthamini na kuvienzi vile vya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu mwingi uliopo katika sekta hii, Maafisa Utamaduni hufanya kazi za Maafisa Michezo na Maafisa Vijana, hii inawazidishia mzigo wa kazi na hawana marupurupu yoyote, wao wanabakia kufanya kazi tatu kwa pamoja. Kweli huku ndiyo kuwekeza ili kuibua vipaji? Pamoja na hilo, kutokana na ukubwa wa Wilaya zetu bado tumekuwa tukiona matatizo makubwa wanayoyapata katika kutimiza majukumu yao. Sote tunajua ukubwa wa Wilaya zetu, matatizo yetu ya miundombinu tunayafahamu, lakini tunamsaidia vipi mtumishi huyu? Kambi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Wizara husika kutoa takwimu zinazoonyesha, je, nchi yetu ina Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo na Vijana wangapi katika Wilaya zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya filamu, sekta hii inakuwa kwa kasi sana, kwani ndiyo njia rahisi sana kufikisha ujumbe katika rika zote kwenye jamii. Aidha, ni kivutio kikubwa zaidi kibiashara. Filamu ni njia nyepesi ya kuutangaza na kufikisha ujumbe lengwa na mtayarishaji wa filamu. Sambamba na hilo, filamu inaweza kutumiwa kuharibu kabisa maadili na tamaduni za jamii husika kama hakutakuwa na chombo cha kudhibiti sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, filamu, video na vielelezo vinaweza kuchochea vitendo vya uvunjaji maadili katika jamii na pia inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kuielimisha jamii uzuri wa mila na tamaduni zetu. Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa wahusika katika sekta hii ya filamu wameshindwa kutumia uhalisia wa mila na tamaduni za makabila yetu katika filamu na badala yake wale wenye makabila hayo wanaona kama wanadhalilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hivi kwa kuwa wengi wamekuwa wakijaribu kutengeneza filamu za makabila mbalimbali lakini, je, waigizaji wako sawasawa na wanawiana na jamii husika au ni bora iende tu? Hii ni kasoro kwani ujumbe unaofika sio ule uliokusudiwa. Hivyo basi, tunawaomba wahusika hili walifanyie kazi kwa makini kama kweli lengo ni kutangaza mila na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko Wa Utamaduni kwa kipindi kirefu umekuwa ukifanya kazi zake kwa msaada mkubwa wa ufadhili kutoka mashirika ya nje. Mfuko huu umekuwa ni kitovu cha kuendeleza sanaa na utamaduni wa Mtanzania. Aidha, sambamba na hilo, Mfuko huu kwa upande mwingine umekuwa ni chanzo kimojawapo cha ajira kwa wajasiriamali wengi hapa nchini kupitia sanaa zao wanazozitengeneza na kuziua pamoja na sanaa zinazoonyeshwa majukwaani. Kwa kufanya hivyo, tunaamini kabisa tutakuwa tumeongeza ajira na kuiongeza Serikali wigo wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tasnia ya michezo. Mpira wa miguu, ni kati ya michezo inayopendwa na wananchi wengi hapa kwetu kulinganisha na michezo mingine. Hivyo basi, kufanya vyema kwa mchezo huo kwa ngazi ya vilabu na Taifa, ni faraja sana kwa wapenzi wa mchezo huo. Nafasi ya Mwalimu katika soka ni jambo nyeti sana kwa maendeleo ya mchezo huo hapa nchini na duniani kote. Kwa nini tunasema haya. Ni kwa sababu, kuna kasumba kubwa iliyojenga hapa nyumbani na katika Bara hili la Afrika la kupendelea kuwatumia Makocha wa kigeni ambao wengi wao hawana msaada mkubwa sana kwa soka letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tathmini fupi kuhusu makosa ya mchezo huo Barani Afrika. Nchini Nigeria, pamoja na kwamba Kocha Mzalendo Shaibu Amodu, ndiye aliiwezesha Super Eagles kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (2010) nchini Angola na kufuzu kwenda Afrika Kusini, aliondolewa na nafasi yake akapewa Lars Lagerback wa Sweden.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na imani ya viongozi wa soka kwa Makocha wa Kigeni, lakini kuna ushahidi uliowazi kwamba Makocha wa Kizalendo wamezipa timu mafanikio makubwa. Misri, kwa mfano, imetwaa Kombe la Mataifa ya Afrika mara saba, lakini mara tano chini ya wazalendo; 1957 alikuwa Mourad Fahmy, 1959 ni Pal Titkos wa Hungary, 1986 ni Mike Smith wa Wales, mwaka 1998 alikuwa Mahmoud El-Gohary na kuanzia 2006, 2008 na 2010 ni Hassan Shehata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ghana imetwaa mara nne Kombe la Afrika ambapo mara tatu ni chini ya wazalendo; 1963 na 1965 alikuwa Charles Gyamfi, 1978 alikuwa Fred Osam Duodo na 1982 alirejeshwa Charles Gyamfi na akatwaa kombe. Congo ilitwaa kombe mwaka 1972 chini ya mzalendo Amoyen Bibanzulu na Algeria ilimtumia vizuri Abdelhamid Kermali akatwaa kombe mwaka 1990. Mwaka 1992, Ivory Coast ilitamba ikiwa na Yeo Martial na Afrika Kusini Clive Barker akaipa ubingwa mwaka 1996. Kwa hiyo, japokuwa Morocco ilimtegemea Gheorge Mardarescu wa Romania mwaka 1976, Nigeria iliwiwa chini ya Otto Gloria wa Brazil mwaka 1980 na Clemens Westerhof wa Uhollandi mwaka 1994, wazalendo ndio wamekuwa wakiivusha hadi kwenye fainali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi mwagine ni kwa Tanzania. Walioiwezesha Taifa Stars kutwaa Kombe la Challenge kwa mara ya kwanza mwaka 1974 walikuwa wazalendo na ndio hao waliipeleka kwenye fainali za Kombe la Mataifa Huru ya Afrika mwaka 1980, ni hayati Paul West Gwivaha na Mheshimiwa Joel Bendera ambaye leo yuko hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaliomba Bunge hili Tukufu kutambua mchango wa Makocha hawa wawili, Mheshimiwa Bendera na Gwivaha na Serikali itoe Tunzo ya Heshima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisubiri hadi mwaka 1994 Syllersaid Mziray alipoiwezesha Taifa Stars kutwaa kombe hilo kwa mara ya pili. Mwaka 2001 ni Mziray na Boniface Mkwassa waliotwaa Kombe la Castle. Hata aliyetuea kikosi kilichokuja kunolewa na kocha Mbrazil na kufika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani alikuwa Dk. Mshindo Msolla. Baada ya kikosi hicho kusambaratishwa, kila mmoja aliona matokeo yake. Hata sasa timu ya Taifa ya Wanawake inacheza Fainali za Kombe la Afrika ikiwa na makocha wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazalendo wana uchungu, uwezo mkubwa wakipewa kila aina ya msaada, huduma, mshahara mzuri na vifaa kama kwa Makocha wa Kigeni. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kwamba baada ya mrithi wa Maximo, Jan Borge Poulsen wa Denmark kuanza kazi, Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*) litawashirikisha kina Mziray, Mkwasa na wazalendo wengine ili pale atakapoondoka, basi Makocha wetu wabaki na ujuzi utakaosaidia kuendeleza timu yetu. Hivi ndivyo inavyofanyika katika nchi nyingi. Tusikubali Makocha wa Kigeni kuja na wasaidizi wao wote na kuondoka na ujuzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinua michezo Tanzania, tunahitaji kutambua matatizo yanayoikabili sekta hii ambayo ni:-

(i) Ukosefu wa mikakati endelevu inayoteklezeka na kuboresha michezo licha ya kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Michezo. Kwa mfano, hakuna vyombo madhubuti vinavyowaandaa vijana kuwa wachezaji wazuri tangu wakiwa na umri mdogo yaani (*Sports Academy*);

(ii) Ufinyu wa bajeti na matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya michezo na hivyo kushindwa kuandaa mashindano ya kutafuta vijana wenye vipaji toka Mikoani; na

(iii) Migogoro ya mara kwa mara ndani ya Vyama vya Michezo nchini na vilabu mbalimbali vya michezo. Migogoro hii inatokana na ubinafsi wa Viongozi wenye nia ya kujinufaisha na siyo kuendeleza michezo kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya utaratibu unaoendeshwa na Chama cha Riadha Tanzania, kwa kutumia Wanariadha Wakongwe kuwa wao ndio Waratibu Wakuu katika kadhia nzima ya kuendeleza michezo

huo nchini. Aidha, tabia ya wachezaji hao kila mmoja kuwa na kundi lake la wachezaji na hivyo kufanya kila awezalo inapofikia muda wa mashindano ya kitaifa au kitaifa, washiriki wakubwa ni wale wanaofundishwa na wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu ambao umewekwa na viongozi wa chama hicho, unashindikana kwa kocha wa Taifa kuweza kuwafundisha wachezaji wote kama timu moja, linalotokea ni timu kufanya vibaya kila mashindano kutokana na umimi wa viongozi hao ambao ni Wanariadha Wastaifu. Kwa mtindo huu, haina maana kwa Serikali kuleta wataalam wa mchezo huo kutoka nje ya nchi kwa fedha za walipa kodi kama hawezi kuchagua vijana wazuri wanaoweza kutuletea ushindi?

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), kutakiwa kukabidhi viwanja kadhaa vyta michezo Serikalini. CCM imeng'anga'ania kwamba viwanja kama Kirumba kule Mwanza, Jamhuri mjini Dodoma, Sokoine kule Mbeya, Majimaji kule Songea, n.k. eti ni vyta kwake! Viwanja vyote hivyo ni vyta Watanzania wote na vilijengwa kwa kodi zao na hata nguvu zao za moja kwa moja pia fedha zao kupitia michango yao mbalimbali enzi zile za Chama kimoja. Kwa kweli kinachofanyika ni dhuluma. Viwanja hivyo havina matunzo wala uangalizi wa uhakika na vimechakaa vikiwa vinahitaji matengenezo makubwa. CCM ione busara ya kuvirudisha Serikalini viwanja hivyo ili angalau vifanyiwe matengenezo na viwe na menejimenti ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ni mtindo wa CCM kujimilikisha maeneo mengi ya wazi na kuyafanya mali yake na kuwa maeneo ya kulaza magari na kuegesha magari mabovu na hivyo kuleta kero kwa watoto kukosa viwanja vyta kuchezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Kiswahili Taifa (BAKITA), kuhusu maendeleo ya Kiswahili, Tanzania ndiyo inasifika kwa kuongea Kiswahili na chimbuko lake, lakini leo ukiingia katika tovuti yoyote duniani, ukiuliza Kiingereza utaambiwa asili yake ni Uingereza, Kifaransa asili yake Ufaransa, Kijapan asili yake Japan, Kijerumani asili yake Ujerumani, Kispanyola asili yake Hispania, lakini unapouliza Kiswahili, wanasema asili yake ni Kenya. Hivi tumeshindwa hata kulinda haki hii na huu utamaduni wetu wa asili? Kwa sababu hata juhudhi ambazo Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) wanazifanya kuendeleza Kiswahili duniani, zinaishia kuwa wanafanya hivyo kwa niaba ya Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilifarijkla kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa hapa Bungeni kuhusiana na matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika vikao vyote rasmi vitakavyoandaliwa na taasisi yoyote ya Serikali. Pia aliagiza sheria zote ziandikwe kwa Kiswahili ikiwa ni pamoja na kutafsiri zile zilizoandikwa kwa lugha za kigeni. Kambi ya Upinzani inalipongeza hilo japokuwa juhudhi zake hizo zinaweza kukwamishwa na hali halisi ya utendaji katika Serikali kwani taasisi za Kiswahili ambazo ndizo muhimili mkubwa katika kufanikisha agizo hilo bado hazijapewa motisha ya kutosha kufanyakazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutembea kwenye maneno yake, kwani kutoa tamko bila ya kuwepo na nyenzo za utekelezaji wa tamko hilo ni sawa na kuwatania Watanzania na kwa kuwa limetolewa Bungeni pia ni kuwadhihaki Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kengele ya pili.

MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. FATMA OTHMAN ALI (K.n.y) MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni ya 114(7), nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, naomba nitumie fursa hii, kutoa Salamu za pole kwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kufiwa na mumewe. Hali kadhalika, natoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kwa kufiwa na mumewe. Tunawapa pole na kuwaombea kwa Mwenyenzi Mungu awapeku na ujasiri katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge (2007), majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kufikiria na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Tarehe 3 Juni, 2010, mjini Dar- es Salaam, Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Katika kikao hicho, Kamati ilipata maelezo ya Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2009/2010 na malengo yaliyomo katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika kufikiria taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2009/2010 na bajeti ya mwaka 2010/2011 ilizingatia miongozo muhimu ya Wizara ikiwa ni pamoja na dira, dhima, majukumu na malengo ya Wizara. Katika kikao hicho, Kamati iliweza kuhoji kuhusu utekelezaji katika sekta mbalimbali za Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Vilevile ilihoji kuhusu Bajeti ya mwaka 2010/2011, malengo yaliyowekwa na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati kwa bajeti ya mwaka 2009/2010. Katika mwaka wa Fedha uliopita wa 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali na hasa yanayohusu:-

(i) Mkakati wa Serikali wa kuibua Ajira Mpya milioni moja ifikapo mwaka 2010;

(ii) Umuhimu wa fedha za uwezeshaji kupelekwa moja kwa moja kwenye *SACCOS* na Asasi za kifedha;

(iii) Wizara kuwa na utaratibu wa kufuatilia matumizi na urejeshwaji wa fedha hizo ili ziweze kukopeshwa kwa wajasiriamali wengine na hivyo kukuza ajira na kuondoa umaskini;

(iv) Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa fedha hizo zinawafikia walengwa. Aidha, Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia katika mabenki kujua kama fedha hizo zimekopeshwa kwa walengwa;

(v) Ili kuleta mafanikio katika kukuza ajira, ni lazima wafanyabiashara ndogondogo (*Wamachinga*) kupewa mafunzo ya ujasiriamali;

(vi) Kuendeleza zoezi la kutambua vijiwe vyा vijana na kuwawezesha kiuchumi kwa kuwasaidia fursa mbalimbali, ili kupunguza watu wasio na kazi;

(vii) Wakati umefika kwa Serikali kukamilisha mkataba wa mpango wa ujenzi wa daraja la Kigamboni, kwa udhamini wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*);

(viii) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) uangalie uwezekano wa kujenga majengo ya wafanyabiashara ndogondogo (*Machinga*) katika majiji ya Mwanza na Arusha kama liliojengwa Manispaa ya Ilala Dar es Salaam; na

(ix) Serikali kuongeza fedha kwa ajili ya uimarishaji wa Tume ya Usuluhihi na Uamuza (*CMA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ufanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, inaonesha kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imewajibika kwa kufanya kazi baadhi ya ushauri na maelekezo ya Kamati na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudii zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Katika Mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi 16.7 bilioni. Waziri alielezea Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Baadhi ya shughuli zilizotekelzwa na mafanikio yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Vima vyा chini vyा mishahara katika sekta binafsi vimetangazwa mapema mwezi Aprili, 2010 kupitia Gazeti la Serikali Namba 172 la mwaka 2010 na kuanza kutumika tarehe 01/05/2010;

(ii) Wajumbe wapya wa Baraza la Masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*), wameteuliwa na Baraza jipya kuzinduliwa rasmi tarehe 13/8/2009. Aidha, Baraza limefanya vikao viwili kujadili masuala mbalimbali ikiwemo mapendekezo ya vima vya chini vya mishahara yaliyotolewa na Bodi za mishahara kisekta pamoja na notisi ya mgomo iliyotolewa na Shirikisho la Vyama (*TUCTA*);

(iii) Kaguzi 624 zimefanya katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini pamoja na kutoa elimu ya Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri ili kuwajengea uelewa zaidi juu ya viwango bora vya kazi;

(iv) Wizara imefanya kaguzi za kazi 893 katika Sekta Binafsi;

(v) Jumla ya wajasiriamali 72,023 (44,224 katika awamu ya kwanza na 27,799 katika awamu ya pili) wamefaidika na mikopo hii ikiwemo wanaume 45,794 na wanawake 26,229. Aidha, *SACCOS* zipatazo 192 na vikundi vya uzalishaji mali na kiuchumi vipatavyo 86 vimefaidika na mpango huu;

(vi) Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa kujenga usawa wa jinsia na ajira bora kwa wanawake ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2010 mikopo yenyeye thamani ya Shilingi 1,229,369,125.05 ilitolewa kwa *SACCOS* za wanawake katika Wilaya za Tukuyu, Kinondoni, Ilala na Temeke;

(vii) Wizara imeratibu mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Uhamiaji wa Nguvu kazi (*Labour Migration Policy*) ambayo itasaidia kudhibiti uhamiaji wa nguvukazi ndani ya nchi na hivyo kuwa na mtazamo wa kimaendeleo zaidi. Aidha, itawasaidia Watanzania waendao kufanya kazi nje kuhusu maslahi yao ya kikazi, ikiwa ni pamoja na nchi yetu kuwa na mikataba na nchi nyingine (*Bilateral Agreements*) kuhusu maslahi ya nguvu kazi; na

(viii) Rasimu ya Kamusi ya Kazi (*Tanzania Standard of Occupation (TASCO)*), imekamilika na kuanza kutumika kwa majaribio kwenye tafiti na masuala yahusuyo ajira kama vile shughuli za vibali vya ajira kwa wageni, Soko la Pamoja la Ajira la Afrika Mashiriki na kwenye utafiti wa majaribio wa hali ya utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio, kuna changamoto za namna ya kuhakikisha kuwa huduma za Hifadhi ya Jamii zinazingatia Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii na njia bora ya kuwafikia walengwa katika ngazi zote hadi vijijini.

(i) Kukabiliana na tatizo la UKIMWI sehemu za kazi ili kupunguza/kuokoa kupotea kwa nguvu kazi za Taifa;

(ii) Uwezo mdogo (Bajeti finyu) wa kuwafikia vijana wote mijini na vijijini kwa lengo la kuwahamasisha, kuwaelimisha na kuwajengea uwezo wa kujajiri;

(iii) Kuhakikisha kuwa mikopo ya wajasiriamali inawafikia walengwa kwa wakati hasa vijijini; na

(iv) Upatikanaji wa takwimu sahihi za ajira mpya zinazozalishwa kote nchini hasa katika sekta binafsi zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2010/2011, imeomba kiasi cha shilingi 16,523,077, 900 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na kiasi cha shilingi 2,034,676,300 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 15. Baada ya kupata taarifa na maelezo ya kina ya malengo ya kina na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha Bajeti ya Wizara. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara hii. Hata hivyo Kamati ilitoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, ujenzi wa daraja la Kigamboni. Suala la ujenzi wa daraja la Kigamboni, limekuwa ni suala la muda mrefu bila kutekelezwa na kumekuwa na majibu mbalimbali ikiwemo la ujenzi wa daraja hili upo kwenye mchakato wa kuidhinishwa na Serikali ambapo Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa. Waraka ambao unataka NSSF ishirikiane na Mbia wa Sekta Binafsi kujenga daraja hilo. Aidha, tuliamiwa kwamba Waraka huu umepitishwa na Kamati ya Makatibu Wakuu (*IMTC*) na sasa upo tayari kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri. Suala hili limecheleweshwa na Serikali kutotoa udhamini wa ujenzi na matokeo yake tumepoteza asilimia 50% ya gharama za ujenzi wa daraja toka kwa wahisani ambayo ni sawa na fedha za Ulaya €22.5 milioni. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali iharakishe mchakato huu ili kazi ya ujenzi wa daraja hili uanze mapema iwezekanavyo;

(ii) Serikali iweke muda wa kuanza kazi ya ujenzi wa daraja hili (*timeframe*) badala ya kuendelea kusema kwamba ipo kwenye mchakato. Utafutaji wa Mbia uharakishwe ili kazi ya ujenzi ianze mara moja;

(iii) Mara kazi ya ujenzi wa daraja utakapoanza, Serikali iweke mikakati ya kukabiliana na changamoto ili kazi ya ujenzi iweze kuwa na manufaa kwa Taifa; na

(iv) Ili mradi uweze kuwa na manufaa kwa Taifa, Serikali iweke mikakati ya kujenga barabara za kuunganisha Daraja la Kigamboni na mji wa Dar- Es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kuboresha usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi. Kwa kuwa Serikali imeonesha juhudi katika kuimarisha usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi na kwa kuwa usalama na afya za

wafanyakazi ukiwa ni mbaya inaweza kuongeza gharama za matibabu, kuongezeka kwa majeruhi, kupungua kwa uzalishaji, kuongezeka kwa gharama za fidia, kuongezeka kwa gharama za ukarabati na kupungua kwa ubora. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Uongozi wa OSHA uweke mikakati madhubuti ya kukamilisha utaratibu wa kufanya marekebisho katika Sera na kutunga Sheria ya kutekeleza Sera hiyo;

(ii) Serikali itenye fedha za kutosha ili OSHA iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuharakisha uanzishwaji wa ofisi za kanda sita nchi nzima ili OSHA wajihushe kikamilifu katika kudhibiti madhara mbalimbali yanayotokea katika viwanda na maofisi mbalimbali;

(iii) Kwa kuwa siku ya tarehe 28 Aprili kila mwaka ni siku ya usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi, Kamati inashauri Serikali kutumia siku hiyo kutoa elimu kwa umma kuelezea mambo mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi;

(iv) Uongozi wa viwanda uweke utaratibu wa kupima afya za wafanyakazi wao mara kwa mara ili kubaini afya za wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi, aidha, Serikali iweke mikakati ya kuboresha usalama mahali pa kazi; na

(v) Kwa kuwa OSHA ndio taasisi inayopaswa kufanya kazi ya ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi, OSHA walete taarifa ya ukaguzi wa viwanda 10 bora vinavyozingatia usalama na afya mahali pa kazi na viwanda 10 visivyozingatia. Hii italeta chachu na changamoto kwa viwanda vingine na mashirika kujenga tabia ya ushindani katika kuimarisha mazingira ya kazi na afya za wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), umefanyika bila udhamini wa Serikali. Serikali bado hajatoa dhamana kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) pamoja na mifuko mingine na hivyo kufanya kazi bila dhamana ya Serikali kwa awamu zote mbili. Aidha, *NSSF* pamoja na mifuko mingine inayofanya kazi hii ya ujenzi, wako tayari kuendelea na ujenzi kwa awamu ya pili lakini Serikali inakwamisha udhamini wa ujenzi huo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kutoa udhamini huo mapema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi za Jamii kushiriki kwenye ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Kwa kuwa Katika kipindi kifupi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), umefanikiwa kujenga nyumba za kisasa na za bei nafuu ambazo zinategemewa kuuzwa kwa bei nafuu kwa wananchi wa hali zote nchini, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Mifuko mingine ya Hifadhi za Jamii kama vile *PSPF*, *LAPF*, *PPF* iwezeshwe ili ujenzi wa nyumba hizo uongezeke kwa kasi na kupunguzia wananchi adha ya kukosa makazi bora; na

(ii) Serikali itoe dhamana kwa mifuko hiyo ili kuipa mazingira mazuri ya kufanya kazi hizo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Jamii nchini. Kamati ilifanya kikao cha kujadili huduma zitolewazo na Hifadhi ya Taifa ya Jamii na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ibadili maamuzi yake ya mwaka 2001 ya kwamba Mifuko ya Jamii iendelee kushindana kwa sababu kushindana huko haitakuwa na manufaa kwa wanachama wala kwa mifuko; na

(b) Pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Hifadhi za Jamii, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuboresha mafao ya wanachama. Aidha, mifuko itafute namna ya kumsaidia mwanachama hata kabla ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Shirika lake la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), imefanya kazi nzuri ya kujenga jengo kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga (*Machinga Complex*) na kwa kuwa jengo hilo limeshakabidhiwa kwa wahusika ambao ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Kamati inashauri Serikali kupitia Halmashauri iharakishe kukamilisha taratibu za kukabidhi jengo hilo kwa uongozi wa Wafanyabiashara ndogondogo ili waweze kuanza kulitumia ili waachane na biashara za kutangatanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Athumani Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga na Wataalam wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Kijakazi R. Mtengwa, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2009/2010 na bajeti ya Mwaka 2010/2011. Kamati inawashukuru na kuwataenia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana. Ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti na Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Fatma O. Ali, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Zuleikha Y. Hajji, Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Mch. Dkt. Gertrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa

Kiumbw M. Mbaraka, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Mohamed A. Said. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah na Ofisi yake, kwa kuiwezesha Kamati yangu kufanya kazi ya kuchambua na kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rachel Nyega, kwa kuratibu kazi za Kamati hadi maoni kutoka kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuniskiliza, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa majaliwa yake ya uzima kwetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha Hotuba yetu ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati, kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa kuniamini kunipa nafasi hii kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Aidha, natoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa salam za pole kwa Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kwa kuondokewa na waume zao. Mungu awape moyo wa ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu cha mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa shukrani kwa wananchi na wanachama wote wa Jimbo langu la Tumbe, bila kusahau viongozi wa Chama changu cha Wananchi (*CUF*), kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kipindi chote cha miaka mitano, nasema ahsanteni sana na tuendelee kujenga na kukiimarisha Chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, natoa shukrani na pongezi kwako wewe Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyevit wa Bunge, kwa kazi kubwa ya kuliongoza vyema Bunge hili. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia majukumu ya Wizara japokuwa kuna upungufu wa hapa na pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu ikaeleweka kwamba Wizara tunayoijadili leo ina umuhimu mkubwa sana kwa mustakabali wa Taifa letu hasa ikizingatiwa kwamba imepewa dhamana ya kusimamia kizazi ambacho licha ya uwingi wake kitakwimu, ndicho kinachoongoza kwa kuishi katika ufukara wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi, Tanzania ya leo inaundwa na raia wake ambao asilimia 65.2, (sawa na watu 24,772,648) wana umri chini ya miaka 24 . Halikadhalika, idadi ya watu wenyewe umri kati ya miaka 25- 64 ni asilimia 32 ya watu wote (sawa na watu 13,202,267). Vilevile asilimia 3.4 tu ya watu wote wenyewe umri zaidi ya miaka 65 (sawa na watu 1,378,309) ni watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi, Taifa letu, ni Taifa la vijana, tunapaswa kubadili mtazamo wetu kuhusu vijana na kuwatazama kama suluhisho badala ya tatizo. Kwa asili, vijana ni kundi muhimu kiuchumi kama wazalishaji wakuu. Kwa asili, vijana ndio wenyewe uwezo wa kulisukuma Taifa mbele kutokana na nguvu, nishati na ubunifu wao. Ndio maana maendeleo ya vijana inapaswa kuwa agenda mtambuka (*cross cutting*) kwa sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwawezesha wazee, tunajenga Taifa lipitalo, kwa kuwalea watoto tunajenga Taifa la kesho, kwa kuwawezesha vijana, tunawekeza katika Tanzania ya leo na kesho. Suala la msingi la kujuliza, ni kama kuna uwiano baina ya idadi yao na hali zao za kiuchumi, halikadhalika ushiriki wao katika vyombo mbalimbali vya maamuzi. Hii ni changamoto kubwa kwa Wizara yenye dhamana ya kuwasimamia vijana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya kazi za Wizara, ajira na uwezeshaji wa wananchi. Kutokana na matokeo ya uchambuzi ya utafiti wa nguvukazi na ajira, inaonyesha kwamba asilimia 11 ya watu wote hawana ajira. Hali hii inatokea wakati ambapo malengo ya MKUKUTA, ambayo pia ni sehemu ya Ilani ya CCM ni kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kufikia 6.5% ifikapo mwaka 2010. Hapa Ilani imeshindwa!

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 ilitamka kwamba, imekisikia na kukipokea kilio cha ajira cha wananchi, hasa vijana. Ilani hiyo iliendelea kubainisha kwamba lengo la CCM ni kuona kwamba ajira mpya zaidi ya milioni moja zinapatikana katika kipindi cha miaka mitano (2005-2010). Tafsiri ya ajira kwa mujibu wa Ilani ya CCM ni zifuatazo:-

- (i) Ajira katika maana ya kazi ya kulipwa mshahara katika sekta ya umma (Serikali na vyombo vyake) na katika sekta binafsi (iliyo rasmi na isiyo rasmi); na

(ii) Ajira katika maana ya kujajiri binafsi katika kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, biashara, kuchimba madini, udereva, ufundi, Ualimu, Uhasibu, kuendesha mgahawa, ushonaji, Uandishi, Uanasheria, Uhandisi, Ukandarasi n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani, mwaka 2008 Serikali ilianzisha Wakala wa Huduma za Ajira ili kusaidia kutoa huduma bora zinazohusu ajira hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha watu wanaotafuta kazi na waajiri wa ndani na nje ya nchi. Kwa mujibu wa kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa mwaka 2008, ajira mpya takribani 1.3 milioni zilanzishwa. Swali kubwa hapa ni kuwa hizo ni ajira za aina gani? Je, zinaendana na viwango vya ubora wa kazi na ziko katika kundi la *decent work?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira mpya zilizoanzishwa, kwa mujibu wa Kitabu cha Serikali cha Hali ya Uchumi, ajira mpya zilizozalishwa ndani ya miaka mitano ya utawala wa CCM ni kama ifuatavyo:

Fursa Mpya za Ajira			
sekte	Idadi	Asilimia	
Serikali	85,571	6.7	
Mashirika ya Umma	965		0.1
Sekta binafsi (isiyo rasmi)		1,233,747	97.0
Sekta binafsi (iliyo rasmi)		-48,360	-3.8
Jumla	1,271,923	100	

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia takwimu husika, ni wazi kwamba sekta isiyo rasmi, ndio iliyozalisha ajira kwa wingi zaidi ya asilimia 97 ya ajira zote. Sekta binafsi iliyo rasmi ambayo ilikuwa inategemewa kuongeza ajira yenyе kipato cha uhakika kutokana na ubinafsishwaji wa viwanda na mashirika ya umma uliotekelawa kwa kasi kubwa na Chama cha Mapinduzi, ilishindwa vibaya sana kwa kupunguza ajira 48,360. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie basi, ni kwa kiasi gani Serikali ilishiriki katika kutengeneza asilimia 97% ya ajira kama inavyojipambanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira (kuwawezesha wananchi kujajiri wenyewe) A.K. na Mabilioni ya JK, uliana rasmi mwaka 2006/2007 kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya kutengeneza ajira milioni moja. Katika kufanikisha hilo, Tshs. Bilioni 21 zilitengwa na Serikali kwa ajili ya kutoa mikopo yenyе masharti nafuuu ili kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu ulitekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza TShs.10.5 bilioni zilitolewa kwa benki za CRDB na NMB (TShs.5.25 bilioni kila moja). Awamu ya pili ilitolewa Desemba 2007 ambapo TShs. bilioni 9.9 ziligawiwa kwa asasi 14, TShs.2.56 bilioni zilitolewa kwa dhamana na TShs.7.3 bilioni zilitolewa kwa ajili ya kukopesha moja kwa moja kwa walengwa na

TShs.600,000,000/= zilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya mpango wa uwezeshaji na kuongeza ajira. Ni ajira kiasi gani zilizalishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *BOT* iliyotolewa tarehe 22 Agosti 2008, hadi kufikia 30 Juni 2008, Mikopo ya *CRDB* imetolewa kupitia *SACCOS* 181 na vikundi 127 vyenye jumla ya wajasiriamali 26,266. *NMB* imetoe mikopo kwa wajasiriamali 21,955 kupitia wakopaji binafsi, *SACCOS* na Vikundi. Jumla ya wajasiriamali waliokopa ni 48,221 kati yao wanawake ni 13,782 na wanaume ni 34,439.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, kwa kuangalia tu takwimu husika na taarifa za *BoT* juu ya watu waliowezeshwa kiuchumi katika dhana ya kujiajiri ni wazi kwamba Serikali kwa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi, mpaka kufikia Agosti 2008, umeweza kutengeneza/kuboresha ajira zisizo rasmi 48,221 tu. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iwapambanulie Watanzania, hizo ajira zingine zimetokea maeneo yapi yasiyo rasmi na kwa kiwango gani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe takwimu zilizo halisia hasa kutokana na ukweli kwamba kilimo ambacho ndicho kinachoongoza kwa kutoa ajira, kimekua kwa asilimia 3.5% badala ya 20% tofauti na malengo na ahadi ya CCM wakati ikijinadi kwa mbwembwe mwaka 2005. Zaidi ikizingatiwa kwamba mikopo iliyotolewa kupitia Halmashauri na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, haizidi hata watu 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo mojawapo la Wizara katika kipindi cha mwaka 2007/2008, ilikuwa ni kujenga uelewa juu ya viwango bora vya kazi (*Labour standards*) mionganoni mwa jamii na kusimamia mpango wa “*decent work*”. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge, je, ajira zilizoahidiwa na kutolewa kwa mujibu wa Wizara zinakidhi viwango bora vya kazi na hivyo zinaweza kuwa katika kundi la “*decent work*”?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kusaidia kuwezesha vikundi vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) kuhakikisha vinapata fedha za kuvii marisha toka kwenye Mabenki na zingine toka Serikalini. Ilani ya CCM inasema, nanukuu:-

“*Ushirika na Uwezeshaji. Ushirika ndio njia kuu ya uwezeshaji kwa wananchi walio wengi. Ushirika ni njia ya kukusanya nguvu. Ushirika uko wa aina nyingi. Lakini ushirika wa kuweka na kukopa una umuhimu wa kimkakati katika harakati za kukuza uchumi na kutokomeza umaskini kwa sababu unawawezesha wanachama wa ushirika huo kuwa na chombo chao cha kuwapatia mikopo kwa uhakika na kwa masharti nafuu*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona kuwa tatizo linalowakabili wananchi ni riba kubwa kiasi kwamba badala ya kuwasaidia wananchi inachangia kuwaongezea umaskini. Tunaomba ufanuzi, je, masharti nafuu maana yake ni nini kwa wananchi kuwapa hayo yanayoitwa masharti nafuu lakini riba ni asilimia 30-50, je,

tunawasaidia au tunawaibia? Kwa njia hii, tunasaidia kumuondolea umaskini Mtanzania kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yetu hiyo inapata nguvu zaidi pale Taarifa ya Hali ya Umaskini inapoonyesha kuwa uwezo wa Mtanzania wa kawaida kufanya manunuzi kupungua kutoka asilimia 62 mwaka 2001 na kufikia asilimia 59 mwaka 2007. Kwa takwimu hizi, kuna uwezekano kabisa kuwa takwimu hizo zimezidi kupungua zaidi kutockana na hali halisi ya mseleleko wa shilingi yetu kulinganisha na Dola ya Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kadhia nzima ya kuwawezesha wananchi (uwezeshaji wa mitaji), Serikali ilitenga eneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Mgusu, Wilaya ya Geita. Tukumbuke kuwa, wananchi hawa sio wakulima, sio wafugaji na vilevile sio wavuvi, wao wanaendesha maisha yao ya kila siku kwa kutegemea uchimbaji wa dhahabu tu. Lakini kwa makusudi, viongozi wa Serikali wa Wilaya na Mkoa wanakwenda kinyume na Ilani ya Chama iliyoiweka Serikali madarakani, kwa kuwakataza wananchi kuendesha shughuli zao za uchimbaji madini katika eneo hilo. Tunaomba Serikali iltoe ufanuzi kuhusu hatma ya wajasiriamali hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana na elimu, mtaji pekee wa nchi maskini, ni kutengeneza Taifa lenye vijana wasomi, ili washiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa. Hata hivyo, hali ya ufaulu wa vijana wetu inatia mashaka sana na kuna hatari Tanzania yetu ikawa zilio la vijana wajinga. Hii itakuwa hatari sana kwa amani na usalama wa nchi yetu. Ripoti ya Serikali ya mwaka 2009, ya Hali ya Umaskini inaonyesha kwamba kuna anguko kubwa sana la ufaulu wa wanafunzi wa sekondari. Idadi ya wanafunzi waliofaulu Kidato cha Nne (*Division 1-3*), imeporomoka kutoka 35% mwaka 2006 na 2007 kufikia pungufu ya 27% mwaka 2008. Hali kadhalika taarifa zinaonyesha kwamba kati ya hao wanafunzi asilimia 80% waliofaulu Kiswahili, wakati ni robo yao tu (1/4) waliofaulu Hesabu. Hii ni hatari sana kwa Taifa. Lazima tujitazame upya, hasa katika elimu na kufanya maamuzi mazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa hivi, ni suala la kawaida kabisa kwa wanafunzi kumaliza Darasa la Saba na asijue kabisa kusoma wala kuandika na ni jambo la kawaida sana kwa mwanafunzi kumaliza Shahada ya Kwanza pasipo kujua kuandika barua ya Kiingereza kwa ajili ya kuomba kazi. Lazima tujitazame upya. Tufanye maamuzi magumu kukikomboa hiki kizazi ambacho kinatengeneza asilimia kubwa ya Taifa letu. Hatutaki Tanzania iwe nchi iliyoundwa na vijana wanaofanyabiashara ndogo ndogo tu. Lazima tuwe na vijana katika sekta zote za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanamuziki wa kizazi kipyaa, katika kuepuka kuwa wazururaji na vibaka mitaani, kuna kundi la vijana wa Kitanzania ambao kwa nia thabiti kabisa wameamua kuisaidia Serikali kwa kujitengenezea ajira (*informal employment*) kwa kufanya sanaa ya muziki. Kwa kiasi kikubwa sana, vijana hawa wamefanikisha kubadilisha muziki wa kitanzania, halikadhalika kubadilisha fikra za Watanzania kuhusu

muziki wa nyumbani. Kinyume na mafanikio yao katika soko la muziki, vijana hawa wamekuwa wakiishi katika mazingira ya kifukara na umasikini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewatelekeza huku ikiwaacha mafisadi papa na nyangumi wakitajirika kupitia mgongo wa vijana hawa. Si Wizara ya Kazi na vijana wala Wizara ya Utamaduni na Michezo iliyosimama kidete kuwatetea vijana hawa. Kila siku ni porojo nyingi kuliko vitendo. Inachojua ni kuwatumia wakati wa kampeni za kisiasa kwa lengo la kuteka kundi la vijana kwa ajili ya kura. Baada ya hapo, wanawatelekeza. Kambi ya Upinzani inataka jibu toka Serikalini ni lini hasa watacaa na hawa vijana na kuwasikiliza na sio kutumia 'kakikundi' ka watu wachache amba wako karibu na CCM kuwakilisha mawazo ambayo sio hasa tatizo halisi la wanamuziki hawa? Tunaambiwa Serikali ni sikivu, kwa nini haiwi sikivu kwa vijana hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija la Taifa, Wizara ilitakiwa kusimamia mipango ya uboreshaji wa tija na ufanisi kazini ili kukuza uchumi nichini kupitia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*). Kambi ya Upinzani, inataka kufahamu tathmini ya tija kwa watumishi inapimwa vipi? Kwani suala kubwa ambalo bado linasumbua katika sekta ya umma ni utumishi usiokuwa na tija. Aidha, Kambi inapenda kufahamu ni kwa vipi tija inaweza kupatikana bila ya kuwepo na motisha? Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, imebainisha kwamba matatizo ya ubadirifu yanayojitokeza, yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na watumishi kutokuwa na motisha ya kazi wanayoifanya, jambo linalopelekea wizi na udokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ni muhimu sana kwa maslahi ya wastaafuli. Ili kuwa na ufanisi, mifuko hii inapaswa kutunza vizuri fedha za wafanyakazi na ili kuongeza thamani, inategemewa kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Kuhusu uwekezaji, tunatoa pongezi kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kuanza kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo, mradi mkubwa zaidi ukiwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Chuo hiki ni zalio la akiba za wazazi, dada na kaka zetu wanazodunduliza kwa madhumuni ya kujipatia malipo ya uzeeni mara wanapostaafu. Hivyo, Watanzania waliopewa dhamana ya kusimamia mifuko hii, wana wajibu wa kuhakikisha kwamba zinasimamiwa ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Majukumu yake makubwa, ni kukusanya michango, uwekezaji wa michango na kulipa mafao kwa wanachama. Kambi ya upinzani inapenda kuipongeza *NSSF* kwa juhudi hizo za kutimiza wajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *NSSF*, bado yapo maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka. Shirika la *NSSF* ambalo fedha zake zinatokana na fedha zinazowekezwa na wafanyakazi, wanachama wa Mfuko huo kwa ajili ya mafao yao, lilitoa Mkopo wa Dola za Kimarekeni US\$ 7,000,000 (Tshs Billioni 8.4) kwa Kampuni ya Makaa ya Mawe na Nguvu za Umeme, Kiwira, fedha ambazo wala hazijulikani kama zitarudi kwa kutokuwepo ushahidi wowote wa dhamana iliyowekwa iwapo mkopaji atashindwa kurejesha (*Collateral*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo huu ultarajiwa kulipwa baada ya miezi sita lakini hadi 26 Machi, 2009 ulikuwa haujalipwa. Isitoshe, Mkataba huo, katika kifungu cha 10.5 unasema kuwa mkopo huo umedhaminiwa na Serikali kwa asilimia 100 pamoja na Benki ya *CRDB*. Hii inashangaza kwani fedha zenyewe ni za wafanyakazi wa Tanzania na Serikali yao inadhamini kwa asilimia 100 ili wakopaji wakishindwa, Serikali yaani wananchi wa Tanzania wakiwemo wanachama wa *NSSF* watalipa deni hilo kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* ni moja kati ya Mashirika yetu ya Hifadhi ya Jamii yaliyoshiriki kwa 100% kufanikisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *NSSF* ilichangia sehemu ya TShs.800 bilioni zilizochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kukijenga chuo husika. Cha kushangaza Serikali mpaka sasa hivi haijaingia mkataba wowote wa kimaandishi na mifuko husika (*NSSF* ikiwa mmoja wao) utakaothibitisha kwamba mabilioni ya fedha za wastaa fu watarajiwa yako katika mikono salama na yatalipwa. Serikali imekuwa ikipiga danadana kuingiwa kwa mkataba husika, hali ambayo inaleta mashaka juu ya usalama wa fedha za Watanzania hawa maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri mwenye dhamana ya kusimamia shirika hili atueleze, wamechukua hatua gani kuisukuma Serikali kuandaa mkataba wa makubaliano, baina yake na mashirika husika ili kuondoa usumbufu wa malipo siku za usoni na mchakato umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Daraja la Kigamboni na *NSSF*, kwa muda mrefu sasa, tumekuwa tukiuzungumzia mradi wa daraja la Kigamboni ambao kutokana na uzembe na urasimu uliokithiri katika kufanya maamuzi, Serikali imejikuta inalazimika kutumia gharama kubwa zisizo na msingi wowote. Kwa makisio ya mwaka 2005 ambapo ndipo mradi husika ulikuwa uanze, jumla ya gharama za ujenzi wa daraja husika ulikuwa EURO milioni 45. Mradi ambao ungefanikishwa kutokana na msaada kutoka Uholanzi (*Grant*) wa EURO 22.5 milioni na Mkopo nafuu (*soft loan*) EURO15 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na urasimu huo, Serikali imepoteza kiasi cha UEROs milioni 22.5 ambazo zingekuwa ni msaada na vilevile gharama za ziada kwa kuwa sasa gharama za ujenzi wa daraja hilo unakadirwa kuongezeka kufikia hadi EURO's milioni 60. Inasemekana kwa sasa Serikali iko katika mchakato wa kumpata mbia binafsi atakayeshirikiana na *NSSF* katika kutekeleza mradi husika. Kambi ya Upinzani inataka tamko toka Serikalini, mchakato husika umefikia wapi na utaanza lini? Je, gharama za awali za upembuzi yakinifu zitafidiwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Vijana la Taifa, kwa sababu ya uwingi na nguvu zao, ni lazima wawe na chombo kinachowaunganisha bila ya kujali itikadi za vyama vyao. Tunafahamu kwamba mbinu nyingi zinafanywa na watendaji Serikalini kuhakikisha kuwa Baraza hilo haliundwi kwa misingi ya vijana wenyeve yaani ushirikishwaji wa makundi ya vijana wenyeve na asasi mbalimbali za vijana ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kuwa ni miaka zaidi ya kumi na tano imepita na suala la Baraza linazidi kuwa ahadi isiyotekelzeza. Kuna hofu ya kitu gani? Tarehe 16 Februari 2006, Mheshimiwa Halima Mdee, aliuliza swali kuhusiana na uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa (BAVITA). Swali ambalo lilijibowi na aliyekuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsazugwanko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akijibu swali husika, Mheshimiwa Nsazugwanko alibainisha kwamba suala la uundwaji wa Baraza la Vijana lilikuwa katika mchakato na kwamba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imeandaa nyaraka za Baraza la Mawaziri na zimekwishajadiliwa katika ngazi mbalimbali za Kiserikali na hatua inayofuata sasa ni kujadiliwa katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. Aidha, baada ya hatua hiyo, hatua zitakazofuata ni pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) ambao utawasilishwa katika Bunge hili Tukufu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata taarifa sahihi juu ya uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa. Lughya ya “muendelee kuwa na subra” haiwasaidii Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wizara hizi ni muhimu sana lakini zitapatwa na matatizo ya muda. Kwa hiyo, kwa muda nilionao hapa, naweza kumuita Mheshimiwa Faida Bakar na Mheshimiwa Martha Umbulla. Kama hayupo atafuatiwa Grace Kiwelu. Wanaweza kuongea wawili tu.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Hotuba ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwanza, naomba kuunga mkono hoja kwa hotuba zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha hapa leo tukiwa na afya njema na salama. Napenda kwa heshima na taadhima, kutoa shukrani za dhati kwa wapigakura wangu, Wanawake wa UWT wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa heshima kubwa ambayo walnipatia na tukawa tunafanya kazi pamoja kwa muda wote wa kipindi cha miaka mitano kwa ushirikiano mkubwa na nawaomba muda ukifika basi nikichukua fomu wanichague tena tuendelee kufanya kazi kwa pamoja ili kukidumisha Chama chetu cha Mapinduzi na Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwashukuru wapigakura wangu wanawake wa UWT wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa huzuni kubwa, napenda kutoa pole kwa

Mwenyekiti wangu wa Mkoa wa Kusini Pemba, UWT, mama Raya Talib kwa kufiwa na mume wake asubuhi ya leo. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapa pole wanawake na wananchi wote wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa ujumla kwa kufiwa na baba yetu Bwana Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache tu, muda kama unavyojuu ni mdogo. Kuhusu Waandishi wa Habari, napenda kuipongeza Serikali ama napenda sana kupongeza Waandishi wa Habari wa Tanzania. Waandishi wa Habari wa Tanzania ni kama kioo. Maana ukijiangalia kwenye kioo ukijiona leo umependeza au hukupendekeza basi ndiyo Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana hasa Waandishi wa Habari wa Tanzania. Waandishi wa Habari wa Tanzania wana kazi kubwa sana. Wanafanyakazi nyakati tofauti, nyakati ngumu sana lakini hawarudi nyuma pamoja na matatizo mengi ambayo wanayakabili kama vile nyenzo duni, elimu duni, kukosekana kwa bima za ajali na kadhalika lakini Waandishi wa Habari hawarudi nyuma wanaelimisha jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya Waandishi wa Habari, leo hapa hatuwezi kwenda mbele katika nchi yetu ya Tanzania kwa sababu kila siku binadamu anahitaji apate habari. Kwa hiyo, nawapongeza Waandishi wa Habari kwa kazi nzito wanayoifanya. Naiomba Serikali waendelee ama wazidi kuwathamini Waandishi wa Habari kwa kuwapatia nyenzo, elimu ya ziada na vilevile kuwawekea bima katika kazi yao hasa katika vyombo vya habari vya kujitegemea, naomba sana Waandishi wa Habari na wao vilevile wapewe uwezo mkubwa katika kazi zao. Kwa kusema hayo, napendekeza ile sheria basi ya kusimamia vyombo vya habari iletwe hapa Bungeni, Bunge litakalokuja, tukianza tu hapa Mwenyezi Mungu atujalie turudi wote basi wote tuje tuipitishe hiyo sheria ili waweze kuwa huru kufanya kazi zao za kila siku. Napenda kupongeza *television* za Tanzania, magazeti ya Tanzania, redio mbalimbali kwa sababu wanaelimisha jamii. Kila siku redio na TV zinafanya kazi na sio TV tu za Serikali hata za binafsi zinafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia fedha za Mfuko wa kuwasaidia wajasiriamali, vijana na wanawake, kwa jina la JK na AK au mabilioni ya Kikwete. Shukurani kwa uamuji mzuri wa Serikali yetu ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuamua kwa makusudi kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2005/2010 kwa kuweka Mfuko huu. Madhumuni ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Amani, ni kuwakomboa wananchi hususanii vijana na wanawake. Mabilioni haya ya Kikwete na Amani Karume yanatolewa, hatuelewi watendaji wana kigugumizi kiasi gani hata kufikia wananchi wengi hawapati fedha hizi za mikopo ya JK na AK? Mheshimiwa Waziri wakati akija kufanya majumuisho naomba jibu kwa sababu mimi kule kwetu Pemba sioni fedha hizi zinatolewa kwa nani. Nikienda kwenye vikundi vya ushirika, wananiambia Mheshimiwa hatupati mkopo kutoka kwenye

Mfuko huu, nikienda pale Benki wanasema watu walishapata, nawauliza nani aliyepata, aah, wapo tu watu waliopata, watu mmoja mmoja, lakini kama tunavyoju, vikundi vya Ushirika, *SACCOs*, kampuni mbalimbali za wanawake na vijana ndio zinazokwamua maisha ya wananchi na ndio ajira za kujitegemea binafsi lakini sio vijana wengi wala sio wanawake wanaopata fedha hizi hasa kule kwetu Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe hapa tarehe 11/4/2010, niliuliza swali Na.5092, kwamba kuitia huu Mfuko wa JK, Kusini Pemba wamepewa watu wangapi mikopo hasa wanawake? Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu, kikundi kimoja tu na watu 22. Nataka njue hicho kikundi kimoja, hebu *imagine* kikundi kimoja ni haki kweli? Kusini Pemba nzima kipewe kikundi kimoja mkopo huu wa JK? Wanawake wangapi wana vikundi vya ushirika, wana makampuni yao mbalimbali, wana *SACCOs* mbalimbali, wanajitahidi na sisi Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wawakilishi tunajitahidi kuwasaidia lakini huu Mfuko ni wa kwao, kwa nini wasipatiwe mikopo hiyo? Fedha hii imekwenda wapi na mwaka 2010 umeshamalizika, tujue wameziweka wapi au wana madhumuni gani? Wanawake, vijana walengwa haziwafikii, lazima tuseme ukweli. Mheshimiwa Rais alitaka kuwakomboa wananchi wa Tanzania lakini kwa nini tunamuangusha? Watendaji tusimuangushe Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kuna vikundi vya walemovu, kuna hiki Jumuiya inaitwa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA). Tawi lao liko kule Pemba, nilivyokuwa nawatembelea katika ziara zangu, niliwauliza wakasema wao hawajapewa pesa hata siku moja, kwa nini huu Mfuko unabagua watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu? Kwa nini huu Mfuko unabagua, wanapewa watu amba ni matajiri, mimi naamini wanapewa matajiri, wanaongeza utajiri zaidi, maskini wanawekwa nyuma. Kwa hiyo, naomba Mfuko huu kwa kule Pemba uwape mikopo walemovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sasa, nitamwita Mheshimiwa Grace Kiwelu na nafikiri nitampa Mheshimiwa Idd Azzan kwa sababu leo ni siku yake ya kuzaliwa na watoto wote 68 kutoka Shule ya Kumbukumbu, Dar es Salaam, Kinondoni wako hapa. Hebu simameni watoto wote na Walimu, wanakuja kumpamba Mbunge wao. (*Makofi*)

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ambazo zimeweza kuwasilisha hotuba yao hapa ndani ya Bunge.

Kwanza, nianze kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hizo pamoja na Manaibu Mawaziri wao na watendaji wote wakuu wa Wizara hizo. Kipekee nimpongeze Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel Bendera ambaye ni Kocha

wa Timu ya Bunge, ambaye ameweza kuifundisha vizuri timu ya Bunge na mashindano yote waliyoweza kushiriki walishinda vizuri. Nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Naibu Waziri wa Wizara hiyo, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza aliyekuwa Kocha wa Timu ya Taifa, Marcio Maximo, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kuweza kuifundisha timu yetu ya Taifa na tunajua kuwa mtoto hawezi kuzaliwa siku moja na kutembea siku moja, ameweza kujitahidi kuifikisha timu yetu ya Taifa ilipofika. Kwa hiyo, ninampongeza na ninamtakia kila la kheri kule anakokwenda aweze kufanikiwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nichukue nafasi hii kuipongeza timu ya Twiga Stars, timu ya wanawake ambayo imeweza kufanya vizuri na kufikia hatua iliyofika sasa. Ninawapongeza sana kina dada hao na hii inaonesha kwamba akina mama wanawenza wakipewa nafasi. Kubwa ninaloliomba hapa ni maandalizi mazuri ya timu yetu hii ya Twiga ili iweze kufanikiwa na kuweza kuleta kombe hilo katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika kuzungumzia mpira wa miguu. Tumeona timu yetu inavyoshiriki katika mashindano mbalimbali na Kocha aliyeondoka ameweza kujitahidi na imeweza kufanya vizuri. Lakini kuna upungufu ambao umejitokeza kutokana na timu yetu kutokuandaliwa vizuri. Kumekuwa na mtindo wa mara kwa mara kuingiza timu zetu kwenye kambi bila kuijandaa na matokeo yake, timu zetu zinaenda kufanya vibaya kwenye mashindano hayo. Kwa hiyo, tunawaomba *TFF* pamoja na Wizara wawe na ratiba maalum ambayo wataipa timu yetu ya Taifa kukaa kwenye kambi ili iweze kufanya vizuri kama timu za nchi nyingine zinavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahamia kwingine, napenda nitoe masikitiko yangu, lakini nipongeze wote walioshiriki kuileta timu ya Brazil kuja katika nchi yetu ya Tanzania, lakini ninayo masikitiko makubwa kwa sababu timu ile ilipokuja hapa, Watanzania wengi maskini waliotaka kuiona timu ile walishindwa kuiona na kwa sababu viingilio vilikuwa ni vikubwa sana na tunajua Watanzania wengi ni maskini, hata mlo mmoja kwa siku unawashinda na kiingilio cha chini kilikuwa ni shilingi 30,000, Watanzania wa kawaida walishindwa kuingia. Pamoja na sababu zote zilizotolewa na *TFF*, lakini mimi bado sikubaliani nazo kwa sababu walikuwa na nafasi ya kuwashawishi wale waliokuwa wadhamini ili Watanzania waweze kushiriki kuiona timu ya Brazil ambayo walikuwa wanaiyona tu kwenye TV na kwa bahati nzuri iliweza kufika katika nchi yetu lakini walishindwa kuiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililosikitika, walituahidi kungekuwa na ulinzi mkubwa sana katika siku ile ya mechili, lakini kwa bahati mbaya ulinzi haukuwepo. Sisi ni mashahidi, tuliona shabiki aliyeingia katikati ya uwanja na alitimiza dhamira yake ya kumshika KAKA, lakini tuliambiwa ulinzi ungekuwepo! Sikubaliani na kitendo

alichokifanya kijana yule lakini kama ulinzi ungekuwa wa kutosha jambo lile lisingeweza kutokea. Tumeona kwenye viwanja vya wenzetu, Askari Polisi huwa wanatazama watazamaji na ulinzi mzuri unakuwepo, lakini Askari Polisi wa Tanzania nao wanakuwa watazamaji wa mpira, wanaacha kuangalia ulinzi wa wachezaji na watazamaji. Kwa hiyo, tunaomba tujifunze kama wenzetu wanavyofanya tusiige machache mengine tuache, tuige yote ambayo tunaona yana manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tuna uwanja mzuri, lakini utaratibu wa siku ile ulikuwa ni mbovu, mpangalio wa ukaaji haukua mzuri. Katika uwanja ule, iko milango mingi ya kuingilia, viti vya kukalia vina namba, lakini sijui ni kwa nini tiketi zile zisingekuwa zinaonyesha *seat number* na lango la kuingilia, ingepunguza usumbufu ambao watazamaji walipata siku ile. Kulikuwa kuna waongozaji wa kuonesha mahali pa kukaa, lakini baada ya timu kuingia uwanjani, wale waliochelewa walishindwa kuelewa wakae upande gani. Kwa hiyo, tunaomba tutumie ule uwanja wetu vizuri na kwa bahati mbaya katika nchi yetu tunao uwanja huo pekee tofauti na nchi nyingine. Kwa hiyo, basi tuutumie uwanja ule vizuri ili uweze kuleta tija kwa Watanzania wote na watazamaji wote wa mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa kuweza kurudisha michezo mashulenii lakini bado tuna changamoto nyingi sana kwa sababu baadhi ya shule hazina viwanja vya michezo. Kama tunavyojua, viongozi wetu hasa wa kisiasa wameshiriki sana kuuza maeneo ya wazi na hata viwanja ambavyo vinazunguka shule na hii imechangia sana watoto wetu kukosa maeneo ya kuchezea. Mbali na viwanja vya michezo, pia hatuna Walimu wa Michezo katika shule zetu. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Habari na Utamaduni na Wizara ya Elimu zishirikiane ili hivi vyote viweze kupatikana na watoto wetu waweze kupata mafunzo mema katika sekta ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la haki za wasanii. Mara kwa mara tumekuwa tukisikia Wasanii wetu wakilalamika kwamba kazi zao zinaibiwa na tukumbuke kwamba Wasanii hawa katika nchi zilizoendelea ni matajiri lakini Wasanii wetu wameendelea kuwa masikini, wana vipaji, wanavitumia vizuri, wanatoa elimu kwa njia ya sanaa, kwa njia ya nyimbo na hata filamu lakini bado wameshindwa kunufaika na kazi zao. Tunaiomba Serikali iletu Sheria ya Hatimiliki ndani ya Bunge hili Wasanii hawa waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka, sasa nzungumzie vazi la Taifa. Miaka hamsini sasa nchi yetu toka imepata uhuru, lakini ni aibu kutokuwa na vazi la Taifa. Ninakumbuka Bunge lililopita la 2000/2005, ulipita mchakato wa vazi la Taifa na fedha nyingi za Serikali zilitumika lakini mpaka leo vazi la Taifa halijapatikana. Tunataka Waziri atuambie hatma ya vazi la Taifa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu TV ya Serikali, *TBC*. Viko vipindi vizuri vinavyotolewa na *TBC* lakini kiko kipindi kimoja cha *CHEREKO*,

tunakwenda kwenye uchaguzi, tumejitisha Sheria mpya hapa ya Gharama za Uchaguzi, wananchi hawaijui vizuri na hata baadhi ya wagombea hawaijui. Mimi nafikiri vipindi hivi vingepewa nafasi katika *TV* ya Taifa kuwaonesha Watanzania kuliko vipindi vyta CHEREKO kwa sababu hawa wameshapendana, wameoana, wanakwenda kuanza maisha yao, yapo mambo ya msingi ambayo Watanzania wanatakiwa kuyafahamu kuitia *TBC* ya Taifa. Kwa hiyo, ndugu zangu na ninamuomba Tido Muhando atuwekee vipindi vyenye tija kwa maslahi ya Watanzania wote na sio vipindi vyta CHEREKO ambavyo ni kwa masilahi ya wachache na sidhani kama vina tija kwa Taifa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Azzan, *Happy Birthday.* (*Makofit*)

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ni kweli leo ni siku yangu ya kuzaliwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mdogo, niende kwenye pointi. Kwanza kabisa, niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza michezo, utamaduni pamoja na mambo ya habari, hongereni sana. Lakini katika majumuisho yao nitapenda sana wanieleze ama walieleze Taifa, ile aibu tulivoipata siku ile ya mechili na Brazil ya Wimbo ya Taifa, Mheshimiwa Rais amesimama zaidi ya dakika tano, Wimbo wa Taifa haupatikani badala yake tunaona sindimba kwenye *screen* na makelele ya ngoma za kienyeji badala ya Wimbo wa Taifa. Ile kwetu ni aibu kwa sababu ile mechili likuwa inaoneshwa karibu nusu ya dunia. Kwa hiyo, tunataka tupate maelezo ni kwa nini kilitokea kile na kwa kwa nini msiombe radhi kwa lile lililotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nitapenda pia nielezwe, timu yetu ya Taifa imeshindwa tena kucheza mashindano ya CHAN, mashindano ya Afrika ambayo tulitakiwa kuitoa timu moja tu ya Rwanda, lakini uzembe uliofanyika tena naweza kusema ni uzembe wa makusudi. Mechili yetu ambayo tulicheza Dar es Salaam ambayo tulitakiwa tushinde, watu walizembea, watu hawakujituma na matokeo yake tukapoteza michezo ule, tulivyoenda kurudiana nao kwao wakatufunga, tukapoteza. Laiti tungetumia vizuri michezo ule ambaao ulifanyika kwetu, nina hakika Tanzania tungecheza mashindano ya CHAN 2012, lakini hilo limefanyika kwa uzembe. Zinapokuja timu, imekuja Cameroon hapa, wamekuja Ivory Coast hapa, wamekuja Brazil hapa lakini angalia viongozi wenu wa *TFF* walivyoshughulikia mechili hizo na kuzisimamia kweli kweli ili ziende vizuri kwa sababu kule kuna hela lakini ilipokuja Rwanda hapa, hakukuwa na hamasa yoyote, hakukuwa na kazi yoyote ya maana iliyofanyika ya kufanya timu yetu ishinde, matokeo yake tumejeteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoea fedha kwa ajili ya Kocha ili tufanye vizuri katika miaka hii, lakini matokeo yake mpaka 2012 hatupo kwenye mashindano ya Afrika. Napenda kujua ni nini kinafanyika na kwa nini wasichukuliwe hatua. Tunao Viongozi wa *TFF* ambaao wamechaguliwa pamoja na Rais Tenga, nampongeza kwa kazi

nzuri, lakini wapo watendaji ambao wameajiriwa, walipaswa kufanya kazi hizi kwa umakini mkubwa ikiwemo Kamati ya Ufundu, kuna Mkurugenzi wa Ufundu, wanafanya kazi gani pale ikiwa timu yetu ya Taifa haifanyi vizuri? Kwa hiyo, naomba tupate maelezo ya kutosha ni kwa nini timu yetu haikufanya vizuri na ni hatua gani ambazo zinachukuliwa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana timu ya Twiga Stars, timu ya miguu ya wanawake, wamefanya kazi nzuri na hii ni aibu kwetu wanaume maana tumeshindwa kupeleka timu ya wanaume ambayo tumeiandaa kwa gharama kubwa sana, lakini timu ya wanawake ambayo haikuandaliwa kwa maandalizi ya kutosha sana, hela walikuwa wanaombaomba pale, lakini wameweza kufanya vizuri na leo watacheza fainali za Afrika. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa kazi nzuri waliyofanya, nimpongeze Rais kwa sababu amejitolea zaidi ya shilingi milioni 50 kuwasaidia kwa maandalizi yao hayo na nijipongeze mwenyewe kwa sababu Tanzania, ligi ya mpira wa miguu kwa wanawake ilifanyika Kinondoni, ndio tulipoanzia, wakati huo ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira Kinondoni, kama hamtaki kunipongeza basi najipongeza mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ligi ya miguu kwa wanawake imeanzia Kinondoni, ndio tunapocheza na ndio haya mafanikio ambayo tunayaona hivi sasa. Basi twende na kwenye Mikoa mingine, ligi hii ya mpira wa miguu kwa wanawake ifanyike na kwingine ili tuweze kupata wachezaji wazuri wataoweza kuja kulisaidia Taifa hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Baraza la Michezo, tuliambiwa hapa muda mrefu itabadilishwa, ni ya mwaka 1971 kama sikosei au 1974, tunaomba tujue imefikia wapi, marekebisho yatafanyika lini? Vipo Vyama vya Michezo hivi sasa ambavyo haviko kwenu kwa maana ya Wizara, vinasajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, michezo ya ngumi za kulipwa, *kickboxing* n.k basi turekebishe sheria hii ili sasa michezo yote tui-*accommodate* huku, yote muwe mnaisimamia ninyi, iwe chini ya sheria hiyo ya Baraza la Michezo. Lakini tumeendelea kuiacha michezo hii matokeo yake hata maswali mengine hapa yanayohusu vyama vya michezo hii ya kulipwa, majibu yake tunapata tabu kuyapata. Lakini hata huu mpira wa miguu tunaoendanao sasa inawezekana hatujafika kuwa mpira wa miguu wa kulipwa lakini angalau tumeshaffika hata nusu yake, tupo kwenye *semi-professional*, sasa tujaribu kurekebisha sheria zetu ili twende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka kukisema ni kuhusu Waandishi wa Habari. Kwanza niwapongeze Waandishi wote wa Habari pamoja na vyombo vyote vya habari, kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Lakini kwa upekee kabisa, niwapongeze sana wale wanaoitwa *Global Publishers* ambao wanatoa magazeti ambayo tunaita ya Udaku, lakini mara nyingine mimi naita ni magazeti ya uchunguzi. Yapo mambo mazuri wanayafanya na wakifanya vizuri, lazima tuwasifie, wanapofanya vibaya kama tunawakosoa, wanapofanya vizuri tuwasifie. Wanatoa habari za kichunguzi kama sio wao kutoa habari zile, umefanya baya au la hovyo hovyo ambalo ni nje ya maadili wakalionna, likaandikwa leo maadili yetu yangezidi kuvunjika mno, lakini leo

hata ukifanya jambo lako la hovyo hovyo, la kukiuka maadili unaanza kuogopa eeh, kuna *Paparazi* hapa. Naomba waendelee lakini watende haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa sababu pia pamoja na hela wanazokusanya wanazirudisha kwa wananchi wetu. Wanafanya mashindano, wanatoa magari, wanatoa vitu mbalimbali. Nawaomba wakiendelea kufanya mashindano hayo waangalie na vitu vingine vya kutoa, wanaweza kutoa hata majembe au hata *power tillers* wasaidie wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, *Happy Birthday to you.*

Sasa Waheshimiwa Wabunge hata mimi sipaswi kutoa maneno zaidi kwa sababu muda wangu umeisha pia. Tukirudi mchana hapa tutakuwa na Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni mmoja hapa, yupo Bwana Julius Mtuka, huyu ni Katibu wa Mheshimiwa Paul Kimiti, alipoona anastaafu amempeleka kusoma Chuo cha Mwalimu Nyerere Kivukoni miaka mitatu na amepata Diploma ili na yeye aendelee kufanya kazi zake wakati Mzee huyu kastaafu. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi nilikuwa nimewataja Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwamba wataanza kuchangia, Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Mwanne Mcchemba atafuatia. Mheshimiwa Martha Umbulla. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hoja ya Wizara hizi mbili ya Habari, Utamaduni na Michezo na ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga unakaa huku. Sasa nashangaa Mawaziri wanaohusika hawapo. Mheshimiwa Mahanga unakaa mezani. Mheshimiwa Mbunge uanze tena.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupatiwa fursa hii ya kuchangia hoja ya Wizara hizi mbili ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kuweza kusimama mahala hapa saa hii na kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Napenda kwanza niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuandaa vyema na kuwasilisha hotuba ya Wizara hizi kwa ufanisi kwa umakini na nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kweli kwa kuziendeleza sekta hizi na kupiga hatua katika kuelimisha wananchi katika masuala mbalimbali yanayohusu jamii, siasa pamoja na uchumi wa nchi yetu na hasa pia katika sekta ya michezo na pamoja na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa sababu hatua ambayo tunaiona sasa hivi haiwezi kulingana kabisa na miaka mitano, kumi iliyopita. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee naomba pia kupongeza sekta binafsi na kipekee niipongeze Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*) kwa kuweza kuibua maovu na kuyakemea kwa njia ya kufanya maigizo, kwa mfano Fataki na Sidanganyiki. Ni michezo ambayo kusema kweli imeweza kupunguza maovu yanayofanyika katika nchi yetu kwa kiasi fulani. Vilevile nawapongeza kwa kuwa wameweza pia kukemea maovu mbalimbali ambayo yanahamasisha uonevu na unyanyasaji wa kijinsia na hivyo imeweza kupunguza kasi ya maovu haya kwa kiasi fulani na tuna kila sababu ya kuapongeza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kueleza matatizo mbalimbali kwa kusikitika kabisa kwamba maeneo mengi ya nchi yetu na hususan vijijini na hasa Mkao wetu wa Manyara bado kuna matatizo makubwa sana ya kufikisha habari kwa wananchi na hivyo kuna giza kubwa kwa wananchi kuelewa mambo mbalimbali. Tunavyoolewa *information* ni *power* na *knowledge* na kwa hivyo bila watu kuelewa masuala mbalimbali bado maendeleo yao yanaweza kuwa nyuma. Nasikitika kwamba maeneo mengi ya mkao wetu bado kuna matatizo makubwa na utakuta wananchi wanapata habari hizo pengine kutokana na mikutano ya hadhara kama ya Mbunge ama Mwenyekiti wa Kijiji ama *DC* na mikutano hiyo siyo wananchi wote wanahudhuria na hususan wanawake amba wengi wanabaki nyuma katika fursa mbalimbali na kwa hivyo, ningependa kusisitiza na kuiomba Serikali kwamba namna *effectiveness* ya kupata habari isiwe kwa jinsi ambavyo nimeeleza bali iwe kupitia *public medium* kwa maana ya radio, televisheni, magazeti na kadhalika, suala ambalo sasa hivi kwa maeneo mengi ya Mkao wetu hayajaweza kufikiwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba basi Serikali kwa maana ya Wizara hii ishirikiane kwa haraka kabisa na Wizara ya Nishati na Madini kufikisha huduma hii kwa

wananchi wa vijijini katika Mkoa wetu kwa sababu utakuta kwamba matatizo haya yanakwenda sambamba na ukosefu wa umeme na kama kutakuwa na umeme wananchi wengi watahamasika kutumia vyombo hivi nya TV, Redio ili kuweza kujipatia habari kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tabia pia ya Wizara na hasa sekta binafsi kuelekeza nguvu za kutekeleza huduma hizi katika maeneo yanayofikika au *accessful areas*. Tunajua kuna shida kubwa ya miundombinu na hasa katika mkoa wetu kuna tatizo kubwa kwa sababu hata baadhi ya Wilaya zina shida ya barabara zinazounganisha Mkoa na Wilaya zake na kwa ajili hiyo utakuta huduma mbalimbali zikiwepo hizi za kupeleka habari zinakuwa na matatizo na tunaomba Serikali iweze kuangalia pia maeneo haya yasiyofikika yasiachwe nyuma na kuambiwa kwamba wao wasubiri na miaka nenda rudi wanabaki nyuma bila kupata huduma na vilevile nawasihi waandishi wa habari pia waweze kuwa wanatafuta habari zilizo ngumu, siyo zile rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutoa mfano kwamba wafugaji wanapohama na ng'ombe zao ni mfano mmoja, wanapata shida kubwa sana. Watoto wao kule porini wanaliwa na wanyama na wakati mwingine hata wao wenye we wanaliwa na wanyama na ng'ombe wanaofugwa pale na wanaoswagwa kupelekwa maeneo mengine kutafuta maji na malisho, utakuta wanafika mahali amebakiwa na asilimia hamsini tu na hakuna waandishi wa habari kule na hata wakifika wanafichwa kwa sababu wafugaji wanadhani kwamba Serikali haipendi hiyo tabia ya wafugaji kuhama. Nadhani waandishi wa habari watakapoibua habari hizi ngumu ambazo zinaweza kuleta hisia kwa wananchi na kurekebisha mambo fulani fulani na wenye we watajijengea heshima ya kuweza kusaidia jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichangia Wizara ya Kazi, Ajira, na Maendeleo ya Vijana, naomba tu kusitiza suala la ubunifu kwa Maafisa Michezo wa nchi yetu. Naelewa tatizo kubwa la kutokuwa na nyenzo. Lakini nazishauri Halmashauri zetu ziweze kutenga Bajeti ya kutosha ili kuwawezesha Maafisa Michezo kuibua vipaji mbalimbali nya wanafunzi wa shule za msingi kwa sababu tukitegemea Wizara ya Elimu peke yake, wao *syllabus* na mambo mengi na hawawezi kusaidia sana katika eneo hilo na basi Maafisa Michezo waweze kuwezeshwa kushughulikia suala la michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuibua vipaji, nimechangia mara nyingi sana kusema kwamba Serikali ingeshauriwa kujenga *centre* ya michezo Mkoani Manyara kwa sababu kubwa tu ya kwamba wachezaji wengi hasa kwa michezo ya riadha wanatoka huko. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ni kengele ya pili. Ahsante.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu leo hii kuchangia hoja ambazo ziko mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, kwa jinsi walivyowasilisha mada zao ambazo kama zitatekelezwa ipasavyo basi zitaweza kuleta maendeleo makubwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimpongeze Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kiwango kikubwa katika mwaka 2005/2010 na hasa katika kuinua vipaji kwa wanamichezo wa Tanzania na sasa tunakwenda pole pole katika kukuza vipaji vyetu na kutambulikana Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie suala la ajira nchini. Suala la ajira ni muhimu sana katika nchi yetu. Tunakumbuka kwamba sasa hivi nchi yetu tunaingia soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunaendelea na harakati za kuanzisha soko la Jumuiya hii na tukumbuke kwamba kuanzishwa kwa soko hili tutakuwa na mwingiliano wa nchi na nchi katika mizunguko mbalimbali na wananchi mbalimbali kuingia huku na kule katika kutafuta maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukumbuke kwamba baadhi ya waajiri wa sekta binafsi huwa wanapendelea sana kuajiri wageni zaidi kuliko wazalendo ingawa Serikali sasa hivi inajitahidi sana lakini tuone kuwa lipo hilo na wanakuwa na makusudi maalum kama wawekezaji wa sekta binafsi kupendelea sana kuwaajiri wageni kwa kuangalia vigezo mbalimbali ambavyo wanahisi kama Tanzania hawanavyo. Naiomba sana Serikali kuliangalia sana suala hili. (*Makofi*)

Lakini pia ningependa kuishauri Serikali kujitahidi kuanzisha kwa namna moja au nyingine vyuo ambavyo vitaweza kuwaendeleza watumishi au wafanyakazi wa sekta binafsi, kimaadili pamoja na kizalendo ili kuweza kukaribisha wageni katika nyanja mbalimbali mfano kupatiwa mafunzo ya *customer care* na mengineyo.

Tutakopofanya hivi wawekezaji hawataweza kutofautisha vigezo ambavyo wanavikuta kule na hapa kwetu. Kwa hiyo, vijana wataweza kuajiriwa kwa wingi na tutaweza kufikia lile lengo ambalo tumelikusudia la kuongeza ajira nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iendelee kusimamia ajira na kuendelea kuratibu ajira za wageni kama nilivyo sema iwe kwa upana zaidi. Vilevile naendelea kuishauri Serikali na kusema kwamba kitengo cha wakaguzi kiongezewe Bajeti zaidi ili kiweze kufanikisha kazi zake kwa ufanisi katika maeneo mbalimbali kwa sababu tutakapoongeza Bajeti katika kitengo hiki wataweza kupata usafiri na mambo mengine ya kuwawezesha kufika kule ambako wanataka kufanya ile kazi. Lakini kwa kusikia tu kama iko sehemu fulani, wafanyakazi wamefanywaje, wamedhalilishwa wamefanyaje kwa kusikia tu, hii itakuwa haina tija zaidi. Lakini kama watakwenda wenyewe na kushuhudia itaweza kuleta maana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba Serikali iweze kuzisimamia bodi za kisekta kuzisimamia na kuziendeleza kufanya maboresho ya mishahara ya watumishi wa sekta hizi kuititia wadau wenyewe yaani kuwashirikisha wadau wenyewe. Kwa sababu tunakumbuka kwamba sekta ziko nyingi binafsi ambazo zinashughulikia nyanja nyingi,

kuna ma-house girl, kuna wafanyakazi wa viwandani, kuna wafanyakazi wa maeneo mbalimbali katika sekta binafsi. Kwa hiyo, hizi bodi kila moja ilekee upande wake na kutathmini katika vikao mbalimbali vya bodi. Kuweza kupanga mishahara na vilevile kuangalia fidia za wafanyakazi pale wanapopata matatizo. Kwa hiyo, hapa wataweza kupata tathmini nzima ya mishahara na itaweza kutofautiana, siyo kupanga tu vima vya mishahara katika maeneo kwa pamoja. Hii inatokana na sheria kama alivyosema Waziri katika kitabu chake cha Bajeti kuwa Sheria ya Ajira Na. 6 ya mwaka 2004 na kutolewa katika taarifa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu migogoro ya wafanyakazi. Utakumbuka kwamba waajiri wengi nchini hawatekelezi majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kuwafanya wafanyakazi hasa katika sekta binafsi kuweza kuleta malalamiko ya aina mbalimbali. Utakumbuka kwamba wapo waajiri ambao hujamulia wenyewe tu kutokana na kuwa hawana sheria maalum inayowaongoza. Mtumishi anapoumia kazini wanamsimaisha kazi na wanaona kuwa hawezi kufanya kazi ambayo imekusudiwa pale. Kwa hiyo, mwajiri yule akishamfukuza yeze anatafuta mfanyakazi mwingine bila kujali kuwa anahitaji kitu gani mfanyakazi yule. Lakini wafanyakazi waliopo pale ndani wanaangalia hatma yao itakuwaje kutokana na athari alizozipata mfanyakazi mwenzaao.

Kwa hiyo, hapa ndipo panapotokea mgogoro wa wafanyakazi na hapa waajiri hawa wanapofutiliwa wanasema kwamba sisi tunatumia kigezo cha Tangazo la Seiikali la mwaka 2010 kupitia *Government Notice No.172*. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kulifuautilia kwa kina hili suala ili waajiri hawa wasiweze kuwadhalilisha wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya muda, naomba nichangie kuhusu fidia za wafanyakazi, kama nilivyoeleza kwamba kuna mashirika mengi au sekta nyingi hazifuati sheria kwa mujibu wa sheria za sekta binafsi hatuna hasa sheria ambayo inaongoza mwajiri wa sekta binafsi. Kama ingekuwepo sheria hii angeweza kufikiria na kubana kuwa kama sikulipa fidia basi inakuwaje. Vima viko chini sana ambavyo wanavipanga wao wenyewe vya fidia. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifuatile kwa kina na tukiangalia kwamba wafanyakazi wengi si wanachama wa vyama vya wafanyakazi. Kwa hiyo, hawana kile kitengo maalum ambacho kinaweza kumtetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawaomba sana wananchi wenzangu pindi mtakapopata ajira nawaomba mjiunge na vyama vya wafanyakazi popote vilipo nchini ili kuweza kutetea maslahi yenu na kuyasimamia zaidi ili kuleta maendeleo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache kwenye Wizara hizi mbili na hususan Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza

Mawaziri wote wa Wizara hizi mbili na Naibu Mawaziri wa Wizara zote hizi, Makatibu Wakuu wote na wataalam wote wahusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hotuba zao ni nzuri na za kina, zimetoa ufanuzi kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kipindi chote cha miaka mitano. Awamu ya Nne imefanya kazi nzuri kwa ujumla, kwenye michezo pamoja na ajira. Ushindi upo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nianze kwa kuchangia, kwanza kutoa pongezi kubwa sana na shukrani kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuipatia Wilaya Mpya ya Kiliua ambayo imekuwa ni mgogoro mkubwa na kero kubwa kwa wananchi. Kwa hiyo, nimpongeze na nimshukuru sana kwa kuona kero hiyo kwa wananchi wa Urambo, hususan Kaliua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo mimi niombe tu kuzungumzia suala zima la ajira na migogoro kazini. Nianze moja kwa moja kuchangia suala zima la Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora. Ni kiwanda pekee ambacho kiko Mkoani Tabora, niwapongeze pia wawekezaji. Lakini pia kuna mgogoro wa muda mrefu baina ya mwekezaji na wafanyakazi. Mwekezaji huyu aliwaachisha wafanyakazi kwa njia ya ujanja, kulikuwa na mgogoro wa wafanyakazi kwa muda mrefu tangu mwaka 2008 aliwapa likizo bila malipo na kupoteza haki za wafanyakazi wale, lakini pia nimpongeze Waziri wa Kazi, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya amelifuatilia sana na Waziri wa Viwanda na Biashara amelifuatilia sana. Sasa naomba nifahamu jeuri anayoipata huyu mwekezaji, hawa watu wote wamezungumza, wamekuja wamefanya vikao na vikao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado matatizo yako pale pale hayajapata ufumbuzi. Ajira ya wafanyakazi wale na haki zao imepotea. Wamefuata huku na huku wametembea kila sehemu, imekwama. Mimi leo naomba Mheshimiwa Waziri atupe jibu kamili la mgogoro huu kwa sababu wale wanaume wana watoto, wana wake zao na kuna wafanyakazi wanawake ambao yaani wengine walikuwa wajawazito, wamejifungua kwa matatizo kwa kukosa fedha na haki zao. Nyumba zingine zimeyumba, watu wameachana kwa sababu ya kukosa haki zao. Kwa hiyo, sasa hivi mimi niombe Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, mimi najua ni msikivu sana na ni muelewa sana na una uchungu na maendeleo ya watu wa Mkoa wa Tabora, tenda haki, ionekane. Hawa wafanyakazi wa Kiwanda cha Nyuzi walipwe haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mapungfu basi kaeni na wale wafanyakazi waliopewa *notice* ya kusimamishwa kazi kwa kipindi chote kile, ili muone kuna tatizo gani? Maana mnasikiliza upande mmoja, hawa wafanyakazi waliokuwa wameachishwa kazi, hakuna aliyewaita akawauliza matatizo yao ni nini? Wapo takribani 300, sasa watu 300 ni wengi sana; ingawa Serikali imeshafikia kiwango kile cha ajira ya wafanyakazi ambacho tulitoa ahadi kwenye Ilani ya Uchaguzi, tumeshaitimiza na hatuna tatizo, sasa tukiwapunguza hawa 300 bado kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niombe kwa kero kubwa ambayo inatusumbua ni matatizo ya Kiwanda cha Nyuzi. Mimi likiisha hili nadhani nitalala

usingizi, kwa sababu wale watu wamekuja, wamefukuzwa kodi, wengine wameshindwa hata kurudi makwao, wanahangaika, hili suala ni vyema sasa Serikali ikafikia tamati, tuhakikishe kwamba haki inatendeka kwa pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukarabati wa Ofisi ya Kazi; niipongeze sana Wizara, kwa kweli sasa hivi iko katika hali nzuri. Niombe wapewe vifaa au nyenzo za kisasa kulingana na jengo lilitivo; kwa hiyo likamilike, kuwe na uzio, wapate na gari ili hatimaye kazi hiyo iweze kukamilisha hadhi iliyokuwepo kwa hivi sasa. Lakini lingine ni Mahakama za Kazi, niziombe kesi za wafanyakazi zinapokwenda zifanyiwe kazi ya haraka sana wayamalize matatizo ili kuondokana na migogoro. Migogoro mningi makazini ni kutokana na Mahakama ya Kazi kutofanya kazi kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, kunakuwa na tatizo na kuzalisha migogoro ambayo sio ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mikopo kwa vijana. Serikali imefanya vizuri sana, lakini ni vizuri ikakamilisha kutoa elimu mbalimbali hasa kwa wajasiriamali vijana wadogo wadogo na hususan wale ambao wanashughulika na kilimo cha umwagiliaji; hawa nao pia wangepewa mikopo, hasa vijana ambao mnasema wapo vijiweni lakini hawapo vijiweni, wakipata kazi, wakipata mikopo, watafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Suala lingine ni kuhusu michezo; bado mimi nitaendelea kupiga kelele ya michezo. Kiwanja cha Tabora, mimi nadhani suala hili la kusema kiwanja hiki ni cha CCM si kweli. Tutafute uwezekano wa kukiboresha kwa kutafuta angalau basi michezo mikubwa mikubwa iwe inafanyikia kule. Sherehe mbalimbali zifanyikie pia na Tabora, kiwanja kile ni kikubwa kwa Tanzania nzima, kinafuatana na kile cha Taifa kilichopo Dar es Salaam.

Kwa hiyo, mimi niombe kiwanja hiki nacho kiangaliwe, kisiachiwe ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika, naomba pamoja na Mheshimiwa Joel Bendera, wote ni wanamichezo, hebu kiangalieni kwa jicho la huruma ili angalau hata timu nyingine kubwa kubwa zipangiwe ziweze kuja Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa kuokoa muda, nilikuwa nataka nichangie hayo lakini pia nipende kutoa salamu kwa wananchi hasa wanawake wa Mkoa wa Tabora, niko nao pamoja. Lakini wengi wananiulizaauliza maswali, wanasema mama Mcemba, vipi? Mbona hueleweki? Hapana, wakati bado, Bunge likivunjwa nitatangaza nia. (*Makofi*)

Mimi sasa hivi bado ni Mbunge, lakini ukifika wakati nitatangaza, Jimbo litakapokuwa wazi tarehe 16 Julai, 2010, ni kweli nitagombea Tabora Mjini, lakini sio wakati wake. Mimi ninagombea Jimbo la Tabora Mjini, lakini sio wakati wake; isipokuwa nilichotaka tu kuzungumzia ni kwamba, ikifika tarehe 16 Julai, 2010 baada ya Bunge kuvunjwa rasmi, sasa ndio nitakuwa na nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninapozunguka pale ninatumia nafasi yangu kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kwa hiyo ni nafasi yangu, ninapita

kwenye chama kuhamasisha akinamama na watu wengine wajitokeze kugombea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine mimi bado ni Mbunge wa Viti Maalum, ila wakati muafaka ukifika nitatangaza nia. Ila msifuate haya maneno ya watu wanaosema kwamba Mama Mchemba anayumba, hatagombea, si kweli. Mimi nitagombea Jimbo la Tabora Mjini pale tu itakapokuwa imetangazwa rasmi kwamba Bunge limevunjwa. Mimi ninaunga mkono hotuba hizi zote mbili asilimia mia moja. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Pamoja na pongezi za Wizara, lakini napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Wizara, hasa kwa ule ujenzi wa mitambo ya *TBC Fm* pale Singida. Sasa hivi mambo ni barabara, kwa hiyo, tunashukuru na tunaipongeza sana Serikali. Lakini pia bado nipongeze timu ya mpira kutoka Mkoa wa Singida, ambayo walikuwa washindi wa *Taifa Cup*, kwa hiyo, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe pongezi na shukrani za dhati kwa *TCRA*, kwa namna ambavyo wameweza kufanya kazi vizuri na vyombo vyahabari na hasa kuwahimiza kutoa ile mirahaba kwa wasanii. Kwa kweli, napenda kuwapongeza sana *TCRA*, naomba msichoke, muendelee kutusaidia ili vyombo vyahabari, hasa TV pamoja na redio waweze kulipa kile kinachostahili kwa wasanii. Lakini kuna tatizo kidogo labda kwenye *TBC*, nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri unisaidie; *TBC* wakati huo ilikuwa ni Redio Tanzania, wasanii, wanamuziki wa zamani waliweza kurekodi nyimbo zao pale na sasa hivi nyimbo zile zimekuwa zinaitwa zilipendwa, lakini bado zinapendwa kweli na zinazwa kutoka pale. Sasa nataka kujua je, mauzo yale, zile pesa ni za nani? Na je, wale wenye zile nyimbo zao kama akina Mbaraka Mwinshehe, Ali Hamadi Kipande, *Kilwa Jazz*, Salum Abdallah na wengine wengi, je, wanapata mrahaba kutoka kwenye mauzo yale? Na kama hawapati, kuna utaratibu gani? Nilikuwa naomba niweze kupata jibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kumetokea unyanyasaji wa hali ya juu sana katika maonesho yanayoendelea kwenye Viwanja vyahabari. Wasanii wamepata unyanyaswaji wa hali ya juu kwa kukatazwa kufanya shuguli zao za sanaa eti kwa sababu wanapiga kelele wakati miaka yote wamekuwa wakiendesha shughuli zao kama kawaida tangu maonesho yale yaanzishwe; iweje sasa hivi ndio wazuiwe? Je, huko ni kukuza sanaa au ni kubagua wasanii? Naomba nipate maelezo sawasawa, kulikoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia labda niulize, hivi Serikali inatambua kwamba kazi za sanaa ni sawa na mgodi wa dhahabu au almasi? Je, ni hatua gani inachukua? Mimi nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo anapigania haki za wasanii, mkubwa akiongea ametoa maagizo. Wakati ule anazindua mradi wa Malaria Haikubaliki, Mheshimiwa Rais, aliongea juu ya wasanii na alizungumza mambo mengi na akatoa ahadi na akasema kwamba kuna mambo moja, mbili, tatu, nne, tano, yatafanyika, lakini

mpaka sasa hivi sifahamu kuna hatua zipi, maana ameishaongea. Je, Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliskia? Na waliichukulia vipi kauli ya Mheshimiwa yule kuhusu wasanii? Ni jambo gani linaendelea sasa hivi? Nilikuwa nataka pia nipate ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niulize, je, ni kwa nini sasa Serikali haileti Muswada wa kuweza kuwasaidia wasanii hapa Bungeni? Kwa sababu tunasema kweli *COSOTA* ipo, ipo upande wa viwanda na sanaa au utamaduni upo Wizara ya Michezo, tuko wapi? Tunapigwa danadana. Sasa hiyo sheria italetwa lini ili tuweze kujua ni namna gani, tutalinda kazi zetu kutoka kwa hawa maharamia? Maana wasanii wanatoka jasho, wanaofaidika ni wengine. Kazi zinaabiwa mitaani, si *COSOTA*, si Waziri, si Wizara, si mtu yejote ambaye anakamata kazi hizi na kuhakikisha kwamba haki inatendeka. Akipelekwa Mahakamani faini ya shilingi 20,000/=, lakini kazi ile ilikuwa ni ya mamilioni ya pesa. Tunaomba haki itendeke kwa wasanii. Lakini pia bado nataka kusema kwamba hivi Wizara haioni kwamba kuishirikisha *TRA* ikaingia kwenye kazi za sanaa, ni kulipatia Taifa kipato kikubwa? Kwa sababu kazi ya sanaa itakapoingia kwenye *TRA*, ina maana msanii atapata haki yake lakini bado na Taifa litapata kutoka kwa sanaa ile ile, ndio maana nikasema ni sawa na mgodi. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana kuna wakati mwengine nilikuwa nasema basi ni heri Wizara hii itenganishwe, kwa sababu naona kitabu hiki kizima sana sana kimejaa habari za habari pamoja na mpira lakini mambo mengine hapa ni kidogo kidogo tu, kwa maana hakuna nafasi ya kile kitengo cha utamaduni. Lakini je, pale Wizarani kuna dawati lolote ambalo linashughulikia hata hiki kitengo kikashughulikia masuala ya uharamia? Kwa sababu sioni ni nani anasimamia haya? Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri, utusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pia niulize swali moja, hivi siku hizi ule wimbo wa Mzee Morris Nyunyusa, ule wimbo siku hizi haupigwi? Sielewi umekuwa na dosari gani? Kwa sababu ule wimbo mimi ninauhesabu kama ndio alama au nembo yetu wasanii wa Tanzania. Ni kwa nini ule wimbo hautumiki sasa hivi? Naona kuna mikwaruzo kwaruzo tu huko, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana niweze kupatiwa majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nataka niweze kuuliza, hivi ni nini hatma ya lile jengo la nyumba ya sanaa? Hatma yake ni nini? Niliwahi kuuliza hapa, lile jengo ni mali ya nani sasa? Kwa sababu pale kulikuwa na sanaa za aina mbalimbali zilikuwa zinaendelea, walemaru walikuwa wanakwenda pale, wanajifunza kazi mbalimbali za sanaa na zinawapatia ajira, sasa hivi imekuwa kama ni kakijiwe fulani hivi! Je, mapato yanayopatikana pale, ni nani anayeyatumia? Na kwa idhini ya nani? Na ni kiasi gani? Na ni mpaka lini? (*Makofi*)

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tujue, maana lile jengo lilianzishwa kwa ajili ya kazi za sanaa. Tunaishukuru Serikali, kweli pale BASATA kuna jengo zuri tu limejengwa kwa ajili ya kazi za sanaa na mimi nimefika na nimeliona na shuguli za vijana na sanaa zote zitakuwa zinafanyika pale. Lakini je, lile jengo lililobaki pale ni kwa nini hatupatiwi

majibu? Kuna nini au tuombe tume iundwe kuchunguza jengo lile? Kwa sababu lile ni mali ya Ikulu, vile viwanja. Lakini je, Ikulu inajua kwamba ni kitu gani kinafanyika pale? Na ni kitu gani kinaendelea na wanazalisha kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kuongea mengi, naomba niipongeze timu ya *Twiga Stars*; tukisema wanawake wanaweza, wanaweza kweli kweli. Wamejaribisha kidogo, mambo mnayaona, hakuna pesa, hakuna sijui nani, hakuna ufadhili wowote, lakini mambo yanakwenda kwa kuchangia watu kidogo kidogo, watu wanaojitolea. Tunaomba Wizara pia iishike ile timu isiiache pembeni, kwa sababu wale ndio watakaotangaza Taifa hili na wanapaa kweli kweli na watapaa mkiwapa nafasi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii, hasa ya Habari na Utangazaji, Wizara ambayo mimi ninahusika. Nimetoka huko, nilikuwa ni mtangazaji mahiri kweli kweli, wakati ule ni Redio Tanzania tu peke yake, hakuna tena redio nyininge katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kupongeza Wizara hii ya Habari na Utangazaji, inafanya kazi vizuri. Katika kipindi hiki vyombo vya habari vimeongezeka, redio, magazeti na kwa kweli ni Wizara ambayo inavumilia sana. Nasema hivyo kwa sababu tunaona mambo mengine yanakwenda pembeni, lakini Wizara hii haikurupuki, inajitahidi kuvumilia na ukiona imechukua hatua, basi ujue kwamba hizo habari zimekithiri. Kwa hiyo, napenda kuwapongeza katika hili na nawaomba muendelee hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuvipongeza vyombo vyote vya habari, vinafanya kazi nzuri sana ya kuwaelimisha Watanzania. Kazi za habari ziko tatu tu, kuelimisha, kufahamisha na kuburudisha, haya ndio maeneo muhimu ya vyombo vya habari. Sasa mimi nitazungumzia katika maeneo haya tu, hasa kwa upande wa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine mimi inanitia simanzi kubwa kabisa ninaposikiliza redio, ninapoangalia TV, ninaposoma magazeti, wapo baadhi ya wenzetu wa vyombo vya habari hawako tayari kufuata miiko ya uandishi wa habari na hata pale wanapokosea, baadhi ya vyombo hivi haviko tayari kuomba radhi hata kidogo na hapa ndipo tunaposema hivi vyombo vya habari, vilitie mkazo sana katika elimu. Kwa sababu vyombo hivi vinafanya kazi ndani ya jamii, vinataka kuelimisha, vinataka kufahamisha, vinataka kuburudisha, usipokuwa na elimu utakuwa unawaonea Watanzania ambao wanategemea sana vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuru umepatikana hatukatai hata kidogo, ruksa kwa kila mtu kuanzisha TV, kuanzisha redio na magazeti, lakini ruksa hii ni lazima iende sambamba na kujali elimu. Sio vyema hata kidogo leo mtu anakaa, anakurupuka tu, ana pesa zake, anakwenda kuanzisha chombo cha habari, hajali elimu, anachukua watu tu

hivi hivi na huyu ndiye anayetakiwa kuwahudumia Watanzania. Maana hapa ni lazima tujue, kama nilivyosema unapokuwa mwandishi wa habari, wewe huhudumii kile chombo cha habari peke yake, unawahudumia Watanzania. Sasa Watanzania ni lazima wapate habari za uhakika kwa sababu hakuna sehemu nyingine tena. Mahali wanapotegemea waburudike, wafahamishwe, wapate elimu, ni chombo cha habari, iwe redio, iwe TV, iwe magazeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja ilinitia simanzi kidogo, siwezi kutaja ni chombo gani cha habari, alitakiwa kumtaja Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, lakini akataja jina la mtu mwingine kabisa. Nikasubiri kwamba pengine anaweza akajisahihisha, hata kidogo mpaka kipindi kinamalizika ikabaki vilevile. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa hii ni hatari sana, ni hatari kwa sababu vipindi hivi vinasikilizwa na wengi. Wanaskiliza watu wazima, wanaskiliza wanafunzi, kwa mtu mzima sawa, lakini kwa mwanafunzi tena wa shule ya msingi anayetakiwa aelimike na chombo cha habari, leo anaambiwa kwamba Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ni fulani, si yule hata kidogo, akitoka pale anakwenda na yule yule. Sasa huu ni mfanano mmoja tu, iko mifano mingi sana. Sasa mimi nawaomba ndugu zangu, mimi ni mwandishi wa habari mwenzenu, enzi zetu sisi ulikuwa huwezi kukabidhiwa kutoa habari yoyote kama hujapata mafunzo ya uhakika, haiwezekani hata kidogo. Sasa siku hizi, sijui kuna kitu gani mpaka tunafika mahali tunataka kuiharibu fani hii ya Uandishi wa Habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi ninemekuwa nikisema uandishi wa habari *is a noble job*, lakini kuna wenzetu wanataka katuondoa hapo ionekane kwamba mwandishi wa habari ama habari sio kitu ambacho kinatakiwa kusoma, sio fani kama udaktari, sio fani kama mwalimu. Leo mwalimu hawezি kuingia darasani akaenda akafundisha bila kupata mafunzo, iwe ya mwaka mmoja, iwe ya miaka miwili, ama daktari hawezি kuingia *theatre* akaenda akampasua mtu bila kuwa na mafunzo. Iweje leo fani hii ya uandishi wa habari ionekane kwamba kila mmoja anaweza kuwa mwandishi wa habari? Hata kidogo, ni lazima tujirekebishe. Na ndio maana basi, ule Muswada wa Habari na uje hapa Bungeni, wala wasiwe na wasiwasi waandishi wa habari wenzangu. Kwanza mimi ikifika mahali nikiona kwamba hapa tunataka tuminywe waandishi wa habari, sitakubali hata kidogo, lakini ukija hapa, suala hili la elimu, tutatilia mkazo kweli kweli. (*Makofi*)

Napenda kuchukua nafasi hii niwapongeze waandishi wa habari wenzangu wa gazeti la Mwananchi. Nawapongeza sana kwa kutumia uhuru wa uandishi wa habari bila kujali mimi ni Mbunge wakaandika habari zangu, sina kinyongo hata kidogo na hivyo ndivyo inavyotakiwa. Naomba utaratibusi huu uendeleesi msiogope pale mnapoona kwamba kuna jambo mnataka kuandika, andikeni lakini ninachoomba mimi kabla ya kuandika lazima mchunguze kwa kina ili ukiandika unaandika kitu cha uhakika. Kwa hiyo, gazeti la Mwananchi liliandika habari zangu sina kinyongo na wao, walitumia uhuru wao na waomba waendeleesi hivyo. (*Makofi*)

Mwisho kabisa nimezungumza mara nyingi tu lakini hapa ningependa kutamka rasmi maana sidhani kama nitapata nafasi ya kuchangia tena, napenda kutamka rasmi kwamba nitagombea Ubunge katika Jimbo la Lulindi, sababu za kugombea ninazo. Mimi pamoja na wananchi wa Jimbo la Lulindi tumefanya mambo mengi sana, tumejenga shule katika Kata zetu 14 zote, kuna shule za sekondari na mengine mengi, kwa hiyo, namalizia kwa kuunga mkono Wizara zote, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru wewe lakini nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri mnazozifanya hapa Bungeni. Nipongeze Wizara zote mbili kwa kazi nzuri na Bajeti ambayo iliwasilishwa hapa leo. (*Makofi*)

Miaka ya nyuma tulikuwa na timu ya Tanzania kwenye michezo na tulikuwa na wachezaji wazuri sana ambao waliletea sifa kubwa sana Taifa letu wachezaji kama akina Kitwana Manara, akina William Mwajibe, Omar Zimbwe, Sunday Manara, akina Dilunga ni wengi sana. Hawa wanatakiwa wakumbukwe kwa sifa waliyoletea Taifa letu hili, Mtagwa aliwekwa mpaka katika *stamp*, leo anaumwa anasaidiwa saidiya na baadhi ya watu wachache wakiwemo Ndugu Leonard Tenga kiongozi wa *TFF* na baadhi ya watu ambao tunakutana naye anatupiga piga mizinga mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, upo umuhimu wa Wizara hii kwa kushirikiana na *TFF* sasa hivi kuweka bango maalum kwenye uwanja mpya wa Taifa na kukumbuka wachezaji wote walioletea sifa nchi hii kuanzia mwaka 1980 kushuka chini ili iwe hamasa kwa wachezaji wapya ili na wao waweze kutamani majina yao kubandikwa kwenye uwanja ule mpya. Ni kazi ndogo sana tu kwa hiyo, mimi nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuwakumbuka hawa kwa namna walivyoweza kuleta sifa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Niabu Spika, lakini nachukua nafasi hii kuwapongeza *TFF* wakiwa chini ya kiongozi wao Dr. Leonard Tenga kwa namna alivyobadilisha muundo wa mfumo wa uongozi wa *TFF* na kufanya mambo ambayo sasa hivi taasisi ile tunapata heshima ndani pamoja na nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia masuala ya tamthilia katika *TV*. Nchi zote duniani Wizara au chombo kinachohusika ni lazima zifuatilie hizi tamthilia na kuziwekea alama pale ambapo tamthilia hazitastahili kutizamwa na wanafunzi au watoto wenye umri wa miaka kumi na nane. Katika *TV* zetu zote karibuni michezo mingi ambayo wanafunzi au watoto chini ya miaka kumi na nane na cha ajabu wanaitwa kutazama michezo yenye usiku sana na wazazi na hakuna tahadhari yoyote kwenye *screen* inayoonyesha *parental guides*, naomba Wizara hili walichukulie maanani sana kuzuia vijana wadogo kutizama michezo au kutizama tamthilia ambazo haziendani na maadili na umri wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara katika shule nyingi za msingi na sitaki kutaja aina ya tamthilia zinazosemwa lakini karibu kila tamthilia niliyoitaja vijana hawa

ambao wana miaka kumi na mbili, kumi na moja mpaka tisa wanashabikia kuzitazama na kwa kuwa hakuna tahadhari katika michezo ile basi na wao wanatizama na wanaiga vitu ambavyo kwa kweli umri waliokuwa nao hawatakiwi kuiga, kuna mambo mengi watu wanatupiana tupiana madenda mle, sasa sidhani kama kuna haja ya wao kuanza kuona wakiwa katika umri mdogo kama huu wa sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kupongeza mifuko yote ya hifadhi kama *NSSF*, *LAPF* na *PPF*, kwa namna wanavyoshirikiana kuboresha na kuchangia mifuko hii katika maendeleo ya nchi yetu, nawapongeza sana. Nampongeza Dr. Ramadhani Dau, Mkurugenzi Mkuu, nampongeza Mkurugenzi wa *LAPF* na *PPF* kwa namna wanavyoboresha. Hawa wapewe fursa, wapewe fursa ya *ku-embark*, kuwa na miradi mingi zaidi, mwaka huu tulipata wageni, mabalozi fulani hivi, tulivyowapeleka *UDOM* wakawa wanauliza pesa hizi zimetoka wapi, hawakujua kama pesa hizi zilikuwa ni pesa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukidhamiria kufanya vitu vya ukweli tutafanya, tutumie mifuko hii mpaka kwenye miundombinu, waruhusiwe kuwekeza katika barabara ambazo wata-*return* pesa zao kwa *ku-charge road toll* na vitu vingine. Kwa kweli wamefanya mambo makubwa sana na mazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye masuala ya kumbukumbu za Mwalimu julius Nyerere. Mwalimu Nyerere tunamkumbuka mara moja kwa mwaka kwa maana kuna ziara ya kutembelea Butiama, si kila mtu anaweza kwenda Butiama watu wakitoka Meatu, Tandahimba, Nyarugusu hawawezi wote kwenda kule, kwa hiyo, upo umuhimu wa Serikali kuweka *Nyerere Square* kwenye kila miji na kuwe na ziara, kuna ziara za wanafunzi, majeshi, wafanyakazi, watumishi na wananchi kila wakati kwenda kutembelea na kuona mambo mazuri ambayo Mwalimu Nyerere aliyotuachia katika nchi hii. Kwa maana hii watu wataanza kubadilika, watakuwa wanaogopa, watakuwa wanashikwa na hamu ya kuiga yale aliyotuachia na yale ambayo ameyafanya. Kwa hiyo, mimi nilikuwa lazima Serikali itilie mkazo kuwa tuwe na *Nyerere Square* katika kila mkoa ili waweze kukumbuka na kuweza kuona umuhimu wa nini. (*Makofi*)

Lakini nipongeze vyombo vyote vya habari vya hapa nchini kwa namna na wao wanavyojitahidi kuboresha mawasiliano kuwfikia wananchi wote, nawapongeza vyombo vya habari vya magazeti. Magazeti mengi sasa hivi yameibuka lakini mengi nayo vilevile yanasaidia kuleta changamoto kwa wanasiasa, yana asili ya kuleta changamoto kwa Serikali na kufichua baadhi ya vitu ambavyo vinatakiwa vifanyiwe kazi ili tuweze kwenda mbele, navipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya nazungumzia sasa masuala rasmi ya Ilala, maendeleo ambayo Serikali sio Mbunge, maendeleo ambayo CCM na Serikali hii, maendeleo ambayo CCM nan Serikali hii iliyoleta katika maeneo ya Ilala, kama watu sasa hivi wanataka kutembelea maeneo ya Ilala kama vile Hospitali ya Amana, tunawakaribisha mje mtizame Serikali ilivyoboresha huduma katika hospitali na nawapongeza vilevile wahudumu na madaktari wa hospitali hii kwa namna wanavyowashughulikia wananchi kwa upenzi, yapo matatizo madogo yanatokea,

hatusemi kuwa mambo hayatokei, zipo *assaulted cases* ambazo zinaweza zikaibuka kutokana na *fatigue* ambao wafanyakazi hawa wanapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya narudia tena kupongeza Wizara zote mbili kwa kazi nzuri walizofanya, lakini naendelea vilevile kuiomba Serikali ifikirie sasa kutenga Bajeti ya michezo isiiachie tu hizi taasisi peke yao kufanya shughuli hizi, wanashindwa, wafadhili tumeona kwenye mfano wa timu ya mpira ya *TFF* wanakuwa na *excitement* pale tu timu ile inaposhinda sasa kocha anapokuja anakuwa na programu, hizi programu. (*Makofsi*)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante kengele ya pili.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. (*Makofii*)

MHE. ANNA K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikishukuru kwa kunipaita nafasi ya kuzungumza, nina uhakika kwa mara ya mwisho katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi hiki cha kwanza nilichofanya kazi ya kuleta maendeleo kwenye Jimbo la Same Mashariki nikishirikiana na wananchi ambao ndiyo walionichagua. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwashukuru wananchi wa Same Mashariki kwa heshima kubwa waliyonipa na kama wana uhakika kwamba niliwatendea haki kupitia kura zao wanirejeshe tena Bungeni humu nifanye kazi kwa kasi, ari na nguvu zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. kwanza umuhimu wa vyombo vya habari tunaelewa, vyombo vya habari ni muhimu sana kwa nchi yetu, sababu kubwa ni mbili, kwanza vyombo vya habari vinaelimisha, vyombo vya habari vinahabarisha na vyombo vya habari si kwa Taifa hata Kimataifa vinawafanya wananchi walioko vijijini na mijini waelewe nchi inakwendaje *Television*, Redio, Magazeti na vyombo vya habari vyote hivi ni muhimu sana kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kuna kitu ambacho kidogo kinanisumbua na ningependa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wakati anahitimisha hebu alizungumze hili. Mimi ninavyoolewa labda uelewa wangu ni mdogo kwamba vyombo vyta habari wamiliki wanakuwa wanamakusudi mawili, la kwanza kuelimisha wananchi, lakini pili ni biashara. Sasa kuna kitu huwa kinanisumbua kidogo hivi hawa

wamiliki wa vyombo nya habari ambao wanatoa magazeti yao bure hebu Waziri utueleze kidogo hapo kwa nini yatolewe bure kwa sababu wewe umetumia *cost* zako utake kutafuta habari, ukatengeneza habari ni hela nyingi kweli lakini magazeti hayo uyatoe bure! (*Makofi*)

Mimi ningependa Waziri hapa utueleze vizuri na Watanzania wakuelewe hivi hii iko kwenye sheria ipi uteleze vizuri maana yake magazeti haya unajua tumeshakuambia mara nyingi wapi na kuna kipengele gani kwenye sheria kinasema magazeti toeni bure na kwa nini wengine wauze wengine watoe bure, hawa wanatoa bure wana nia gani na kwa nini haswa wafanye hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Habari kwa kweli tutataka utupe maelezo mazuri kwa sababu limekuwa ni kero katika nchi. Mheshimiwa Waziri kuna jambo ambalo naomba waandishi wa habari nao wawe makini wanapoandika habari wafanye utafiti, *wa-balance story* japo mimi hiyo si fani yangu, lakini kwa kuwa Mwenyekiti wa Maadili nimekutana na kesi za magazeti *wa-balance story*, wawe na uhakika na wanavyoviandika, wakiandika vitu vyenye utata inakuwa ni matatizo sana huko kwenye majimbo yetu. Lakini kuna kitu Mheshimiwa Waziri umekizungumza jana kimeleta matatizo.

Mheshimiwa Waziri jana ulipokuwa kwenye uwanja wa *Nyerere Square* eti mimi mwenyewe sikuwepo, ulizungumzia ukasema wananchi waamini zaidi vyombo nya habari nya Serikali. Lakini pia vyombo nya habari nya watu binafsi Mheshimiwa vipo ambavyo viko makini sana na vinaelimisha sana na ndiyo vingi, sasa hili ni vyema ukalifafanua kwa sababu vyombo nya watu binafsi vimeanza kuingia wasiwasi kwamba labda Waziri ni Waziri wa vyombo nya habari nya Serikali tu, vyombo nya habari nya watu binafsi labda havitakiwi, sasa kwa sababu linazungumzwa sana ni vyema Mheshimiwa Waziri ukalieleza vizuri na kama kwa kweli hukulisema maana yake mimi sikusikia nimeona tu malalamiko ukalikanusha ili na wenzetu wa vyombo nya habari nya binafsi ambao ndio wengi wawe na amani wasione kwamba wao unawabagua. (*Makofi*)

Lakini kwa kumalizia ndugu zetu wa vyombo nya habari, ndiyo tunajua mnajiita ni mhimiili wa nne, hamjawa rasmi lakini naomba niseme kazi mnayoifanya kwenye nchi hii ni kubwa sana. Lakini inakuwa na maana pale mnapokuwa mnazungumza mambo ambayo ni ya ukweli, umeyafanyia utafiti, hamsingizii watu, hamuonei watu, basi mnakuwa mmefanya kazi inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri mimi nisingependa kuzungumza sana lakini nimalizie kwa kusema tuendelee kuwatia moyo watu ambao wanataka kuleta vyombo habari lakini vyombo nya habari ambavyo vitaelimisha wananchi mambo ya muhimu, mambo yanayohusu kilimo kwanza, mambo yanayohusu elimu, mambo yanayohusu teknolojia, mambo ambayo yatatufanya nchi yetu iendelee kuliko kuleta migongano na kuleta maneno yasiyo na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naunga mkono lakini nitaunga mkono hoja haswa nikishapata ufanuzi ule ambao nimeuomba, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuzungumza. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema yake na kunijaalia afya na uzima tele kwa kipindi chote cha miaka mitano katika kuitumikia jamii ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kwa familia ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mjumbe wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Maria Hewa, wote kwa pamoja kuwapoteza waume zao. Mungu awajalie uvumilivu katika kipindi hiki. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri.

Naomba nitumie fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuvitambua vijiwe vya vijana na kuwavezesha kiuchumi na kwa kuwasaidia fursa mbalimbali ni kupunguza idadi ya watu wasio na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuwafikia vijana huko vijijini ni suala la Afisa wa Utamaduni wa Wilaya. Wataalam hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na kazi wanayofanya ni kubwa kwa kuanzisha na kuhamasisha vikundi mbalimbali vya vijana na akinamama na wanaume pia lakini wanatembea kwa baiskeli. Hii ni aibu sana ukizingatia Afisa Kilimo na Afisa Maendeleo Wilayani wote wana usafiri wa pikipiki lakini Maafisa Utamaduni hawana usafiri. Kazi inakuwa ngumu na inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia magari Maafisa Utamaduni wa Wilaya hasa Wilaya ya Simanjiro ukizingatia kuwa jiografia ya Wilaya hiyo ni mbaya na pia wanyama wakali kuhatarisha maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa Vyuo vya VETA kwa kila Wilaya, Serikali kwa kupitia mpango maalum wa kuwaondoa watoto katika mazingira magumu ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Kazi Duniani, VETA Kanda ya Kaskazini, Shirika lisilo la Kiserikali la *Good Hope* kupitia mafundi jamii waliweza kupata mafunzo ya ufundi vijana wapatao 400, katika Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mji mdogo wa Mirerani una wakazi wengi wapatao 52,000 na kwa kuwa vijana ni wengi kuliko watu wazima na ambao hawana

ajira na Serikali ya awamu hii iliazimia kujenga Vyuo vya Ufundu katika kila Wilaya. Je Serikali haioni umuhimu wa kujenga Chuo cha Ufundu katika Mji Mdogo wa Mirerani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa ujenzi wa majengo ya wafanyabiashara ndogo ndogo (*Machinga complex*) katika Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam. Kwa kuwa Mkoa wetu wa Manyara ni mkoa mpya na una maeneo ya kutosha kabisa, tunaomba Shirika la *NSSF* kuja kuwekeza katika Mkoa wa Manyara. Karibu *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa Daraja la Kigamboni ni suala la muda mrefu kuanzia mwaka 2005 – 2010 hadi hivi leo hakuna utekelezaji wowote. Kwa kuwa waraka huu umepitishwa na Kamati ya Makatibu Wakuu (*MTC*) na upo tayari kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri. Je, ni sababu zipi zinazozua Serikali kutokutoa udhamini wa ujenzi huo hadi asilimia hamsini ya gharama za ujenzi toka kwa wahisani zimepotea bure? Je, Serikali itatoa lini udhamini huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali kuitia Mradi wa Daraja hili la Kigamboni kuna mpango gani wa kujenga barabara za kuunganisha Daraja la Kigamboni na Mji wa Dar es Salaam?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel Bendera. Vile vile niwapongeze Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote kwa pamoja nimewapongeza kwa kuandaa Bajeti nzuri kwa Wizara zote mbili kwani zimeweka mikakati mizuri ya kuboresha Wizara hizi. Hivyo basi ninawaombea Mungu ili wapigakura wao watambue juhudzi zao na wakati wa uchaguzi wawape kura za kishindo ili warudi tena Bungeni kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ambayo itaandaliwa na Rais wetu mpandwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ninawapongeza Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili pamoja na watendaji kwa kushirikiana vyema na Mawaziri wao katika kuandaa Bajeti hizi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Televisiuni ya Taifa na Redio ya *TBC 1*, kwa moyo mkunjuju ninaipongeza Serikali kwa kufunga mitambo ya Televisiuni ya Taifa pamoja na redio ya *TBC 1* katika Manispaa ya Singida, Kijiji cha Kititimo ambayo itatoa huduma Mkoa mzima pamoja na mikoa jirani. Hii inatokana na imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa wananchi wakiwemo wana Singida na usimamizi mzuri wa Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika, Mheshimiwa Joel Bendera na ndugu Tido Mhando na timu yake yote. Ninatoa shukrani kubwa sana kwa niaba ya wananchi wa Singida.

Msheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuwa mradi huu ni mkubwa sana na wa kihistoria Mkoani Singida naomba uzinduliwe rasmi kabla Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira ya maafisa utamaduni wa Wilaya na Mikoa, napenda kuipongeza Serikali kwa kutangaza rasmi kuwa kila Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Majiji pamoja na sekretarieti kuhakikisha wanaajiri Maafisa Utamaduni na Michezo wa Halmashauri na Mkoaa ili idara hii ianze kupata mgao wa fedha za kuendeleza idara hii ya Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijipongeze na mimi pia kwani tamko hili lilitokana na swalii langu la nyongeza katika Bunge hili la Tisa katika Mkutano wa Ishirini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kupeleka barua rasmi ya kuziagiza Halmashauri na Mikoa kuajiri Maafisa Utamaduni na Michezo na kufuatilia utekelezaji wake. Ni matumaini yangu kuwa itasaidia na kuinua utamaduni wetu pamoja na michezo mbalimbali nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana, napenda kuikumbusha Serikali kuwa nia njema ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha ndani ya miaka mitano vijana wengi wawe wamepata ajira halijatekelezeka kwa kiwango kikubwa. Naishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa mikopo kwa vijana ili wajajiri pia kutoa ajira kwenye maeneo ya wastaifu ama taasisi mbalimbali zinazofunguliwa mfano mpango wa ujenzi wa VETA kwa kila Wilaya hasa kwenye kada ambazo zina upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matumizi ya lugha ya Taifa ya Kiswahili, naipongeza Serikali kwa kutamka mara kwa mara kuwa lugha ya Kiswahili itatumika kwenye ofisi zote za Serikali likiwemo Bunge, warsha, makongamano na semina mbalimbali. Jambo la kusikitisha mpaka sasa tamko hili halijaanza kutekeleza ipasavyo kwani machapisho mengi ya Bunge bado yanachapishwa kwa lugha ya Kiingereza mfano vitabu vyta Bajeti, Miswada na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, naomba Bunge lijalo lugha ya Kiswahili itumike kwa asilimia mia ili lengo la Serikali litimie. Nitashukuru endapo Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika ambaye ni Waziri mwenye dhamana na Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera atasema neno lolote wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli yake ya utawala aliyoitoa kwa wafanyakazi walioitisha mgomo wakati tayari hoja yao ya madai ya kuongezewa mishahara ilikuwa kwenye meza ya majadiliano. Hata hivyo, nakubali kuwa mishahara ya watumishi ni midogo bado na haikidhi haja kwenye mahitaji yao ya msingi, vilevile hadi sasa ongezeko la mishahara bado halijakuwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuptitia Bajeti itamkwe rasmi kuwa kima cha chini cha mshahara ni shilingi ngapi. Hii itasaidia watumishi kujua Serikali imewasikiliza kwa kiwango gani. Vilevile naiomba Serikali iwe na utaratibu wa kukutana na uongozi wa *TUCTA* ili washirikishwe kutoa mawazo yao katika kuboresha mishahara na maslahi mengine ili kupunguza mizozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa vijana, napenda kuipongeza Serikali kwa kuwajali vijana kwa kupeleka fedha kwenye halmashauri zote nchini asilimia tano ili waweze kukopeshwa kwa lengo la kumsaidia Mheshimiwa Rais kuwapa vijana ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua ni kwa kiwango, kiasi gani mpango huu bado unatekelezwa kwa kupeleka fedha asilimia tano kwenye halmashauri ili vijana waweze kuendelea kukopeshwa kwa masharti nafuu na riba nafuu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanja cha michezo cha Namfua cha Singida Mjini. Kwa kuwa Serikali sasa inayo mikakati mahsus ya kuboresha michezo, ni vyema sasa ieleze ni kwa utaratibu upi kiwanja cha michezo cha Namfua cha Mjini Singida kitasaidia kukamilisha ujenzi wa kiwanja hiki ambacho kina miaka mingi kimesimama ujenzi wake. Ninayo sababu ya kuhimiza ujenzi huu kwa Mkoa wa Singida ni mionganoni mwa Mikoa yenye vijana wenye vipaji vya michezo ya mipira pamoja na mbio mbalimbali. Nasubiri majibu ya Serikali. Mwisho napenda kumalizia mchango wangu amba nina matumaini makubwa kuwa Serikali itatoa ufanuzi wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge leo wakati wa kikao cha jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja zote mbili kwa moyo mkunjufu na Mungu awape nguvu, afya na mshikamano katika kutekeleza mikakati yao.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni muda mrefu suala la kuhuisha Sheria ya BMT limezungumzwa sana. Nataka kufahamu ni lini sheria hiyo inabadilishwa ili hata vyama ambavyo vimesajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani viweze kupata usajili kutoka BMT/Msajili wa Vyama vya Michezo ili viwe rasmi kwenye Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa michezo wa kirafiki wa Kimataifa wa mpira wa Miguu kati ya Timu ya Taifa ya Tanzania na Brazil uwanja Mkuu wa Taifa Dar es Salaam lilitokea jambo la aibu sana mbele ya Rais wetu Jakaya Kikwete la kutokopigwa nyimbo za Taifa kwa takriban dakika zaidi ya tano na hata zilipopigwa hazikusikika na badala yake maspika makubwa na *screen* zikapiga na kuonyesha watu wanacheza sindimba, ile ni aibu kwa nchi yetu hasa ukizingatia michezo ule ulionyeshwa karibu dunia nzima. Naomba maelezo ni kwa nini baada ya tukio lile wananchi hawakueleza ni nini kilisababisha hali ile itokee na hatua zilizochukuliwa na pia kuomba radhi kwa tukio lile kwani halikufurahisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba Watanzania waelezwe baada ya Timu ya Soka ya Taifa *Taifa Stars* kutolewa kizembe kwenye mashindano ya *CHAN* ni hatua gani *TFF* imechukua ili timu yetu ipate mafanikio baadaye. Najua tumepata Kocha mpya, naomba na Kamati ya Ufundu ifanyiwe marekebisho makubwa. Pia nachukua fursa hii kuipongeza *Twiga Stars* kwa mafanikio waliyopata, nawapongeza sana *Simba Sports Club* kwa kuchukua ubingwa wa Tanzania hata kabla ya ligi kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imewasahau wanamichezo wa mpira wa miguu waliocheza mpira na kuiletea sifa nchi hii miaka ya 80, kama Kitwana Manara, Zimbabwe, Dilunga, Willy Mwaijibe na kadhalika. Kwa nini wachezaji hawa majina yao yasibandikwe kwenye Bango maalum Uwanja wa Taifa kwa kumbukumbu na hamasa kwa wachezaji chipukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *TV* tamthilia zinazoonesha michezo ambayo maadili yake hayafai kwa vijana chini ya umri wa miaka 18, hakuna tahadhari ya alama *PG* kuonekana (*Parental Guidance*) na kufanya wazazi na watoto wao kutazama pamoja. Je, hatua zipi sasa mtachukua?

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na iliyowasilishwa kwa umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri iliyofanywa ya tafiti ya mila ambazo zimepitwa na wakati na kuendeleza zile ambazo zinatafaa, ni matarajio yangu tafiti hizi zitafanywa kwa Mikoa yote nchini na vile vile, kuhakikisha vizazi vipya kupitia wazazi au walezi wao wanazienzi na kuwafundisha watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa upatikanaji habari ni muhimu kwa wananchi hasa wa vijijini na kwa kuwa Serikali imeliona hili, naipongeza kwa kuwa na mkakati ambao utawezesha Mikoa mingine ambayo haipati au *Radio* hazisikiki vizuri. Sambamba na kupatikana kwa *radio* ambazo hazitumii umeme na kuweza kupata *Radio* ambao zitaweza kutumia betri zinazoweza kutumia nguvu za juu zimefikia wapi? Hii itaweza kutoa ile fursa ya uhuru wa vyombo vya Habari. Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza na kuishauri Serikali katika suala la kutoa mafunzo kwa Waandishi wa Habari katika suala la uchaguzi kwa mtindo huo. Ushauri wangu, mafunzo hayo ni vyema yakagusa na masuala ya kijamii ili kutoa mchango katika maendeleo ya Taifa. Msisisitizo pia utelewe kwa wamiliki wa vyombo husika ili watoe mafunzo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naunga mkono hoja.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi zangu kwa Mkoa wa Rukwa kwa kupata Redio. *TBC* imekamilisha kujenga kituo cha redio cha *FM Mjini Sumbawanga*, tunatoa shukrani zetu nyingi sana wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamefurahi sana wamesema ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo Mkoa wa Rukwa bado tuko nyuma sana kwa sababu ya migogoro ya vyama, tunaomba Serikali ichukue hatua ya kumaliza matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba makocha wanawake kwa michezo ya Kandanda kwa ajili ya kujipima nguvu na soko la Kitaifa na Kimataifa kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kifupi Muko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) umefanikiwa kujenga nyumba za kisasa na za bei nafuu ambazo wananchi wa hali ya chini watafaidika kwa ujenzi huu pamoja na ujenzi wa majengo ya *UDOM*, kazi iliyofanyika ni kazi nzuri sana, naomba nitoe pongezi zangu kwa *NSSF* kwa kazi nzuri sana ya kujenga jengo kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga, bado Rukwa tunasubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke muda wa kuanza kazi ya ujenzi wa daraja ili uharakishwe na kazi ya ujenzi ianze mara moja pamoja na mikakati ya kujenga barabara za kuunganisha daraja la Kigamboni za Mji wa Dar es Salaam. Naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kupongeza kazi zinazofanywa na Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Joel Bendera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Bwana Tido Mhando Mkurugenzi wa *TBC* kwa kazi nzuri anayoifanya, ni kiongozi mzuri mwenye sifa zote za ujasirimali na uongozi. Tido anaweza hata kuanzisha redio yake Jangwani au kwenye Wimbi na maskini na bado akapata faida na redio hiyo kupendwa. Nawashukuru kwa aina ya pekee jinsi mnavyobuni program mbalimbali zenyе sura na mguso wa utamaduni wa Kitanzania, kama vile chereko na vipindi mbalimbali ambavyo vinachangia maendeleo ya Watanzania. Nashukuru pia kwa kipindi maalum cha kukemea mimba za utotoni, Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nijulishwe vipindi ambavyo vina mguso wa kijamii tunaweza kuvilipia pipi? Mfano, badala ya sisi Wabunge kuomba msaada tu, je, mnaweza kuona utaratibu wa kuweka kiwango maalum na muda maalum ambao Wabunge watakaobahati kurudi (nadhani nami nimo) kuweza kupata nafasi ya kuonyesha shughuli zao zenye ubora kwa malipo fulani? (yenye sura ya kiruzuku kidogo).

Mheshimiwa Naibu Spika, Uongozi ni jambo muhimu sana katika jamii. Je, hatuwezi pia kupata kipindi cha mafunzo ya uongozi ambayo yatasaidia kumotisha watu? Mfano, kwa watu wenye uzoefu kufundisha kuititia Televisheni au kuandaa siku maalum ya maongezi katika ukumbi fulani kama vile akina Robin Sharma na kadhalika. Hii itasaidia kuwa na viongozi wazuri kwani wakati wa uchaguzi wetu hupatikana kutoka *backgrounds* tosfauti na ili kulisaidia Taifa letu ni vema kuendelea kupata maboresho ili kuepusha makosa yasiyo ya lazima na pia viongozi wetu kuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, navishukuru vyombo vyote vya habari vilivyochangia kuniinua kwa kuonyesha kazi zangu kwa njia ya redio na *Television*, magazeti kama vile *TBG, TBC Taifa, Star TV, ITV, Redio Mlimani TV Maria, Clouds FM* na kadhalika. Magazeti yote yaliyoniadika *positively* na hata pale ilipokuwa hasi naamini ilikuwa kwa nia njema ya kuniboresha. Namshukuru pia Bwana Hamza Kasongo kwa kipindi chake. Taifa linakutegemea sana katika maendeleo yako, taarifa chanya ndio uhai wake hasa kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza *Twiga Stars* kwa kutuwakilisha wanawake. Hali kadhalika, navipongeza vikundi vya ngoma asilia toka Mkoa wa Ruvuma kama vile Beta, ambayo ngoma yake hupigwa na mwanamke mahiri, *Lizombe Shaba group* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na makumbusho ya Taifa Songea (Majimaji), naomba tusaidiwe kurekodi *CD* na *DVD* za vikundi angalau viwili tu vya ngoma toka Ruvuma mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha Ngoro ni utaalam maalum wa Tanzania wa kuhifadhi mazingira ya ardhi. Je, Tanzania tunayo haki miliki yake?

MHE. RAJAB HAMAD JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo machache yafuatayo ambayo yamenifurahisha zaidi katika mawasilisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo. Tanzania ina michezo mingi inayopendwa na wananchi wetu lakini michezo mingi haijapewa kipaumbele na Serikali. Mfano, bao, kuogelea, riadha na mbio za baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara iliagiza Baraza la Michezo la Taifa liwe na maoni mapana ili liweze kuimarisha michezo hiyo na mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Viwanja vya Michezo. Je, Wizara inao mpango wa kuongeza Viwanja vya michezo hapa nchini hasa katika Miji Mikuu ya Mbeya, Mwanza, Arusha na Dodoma. Tujitahidi kujenga Viwanja angalau vinne (4) kama vile Afrika Kusini. Tanzania iwe na lengo la kuwa hata kama *World Cup* isichezewe Tanzania lakini nchi mbalimbali zije kufanya mazoezi hapa nchini kwetu. Naunga mkono hoja.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne kwa kujenga Uwanja wa Michezo wa Kisasa Jijini Dar es Salaam. Pia nampongeza sana Rais Jakaya Kikwete kwa kuamua kumlipia kocha wa mpira wa miguu. Mambo haya mawili yatainua sana michezo katika muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosononesha ni kuwa, pamoja na Serikali kujenga uwanja mkubwa, pia wa kisasa na viti vina namba, lakini hamna mashine za kisasa za kukatia tiketi. Hii inatia mashaka sana na pia inaacha mwanya wa mapato kwenda kwenye mifuko ya watu. Hivi kweli Chama cha Mpira kinashindwa kununua mashine ya kisasa ya kukatia tiketi? Kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba Waziri aniambie ni kwa nini *TFF* hainunui mashine hizo wakati Serikali inatumia gharama kubwa sana kujenga uwanja.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Naibu Spika, katika kueneza usikivu wa *Radio* na *Televisheni* kupitia Shirika la Utangazaji la *TBC*, ni dhahiri kwamba chombo hiki kitajitahidi kutekeleza majukumu yake, lakini bado kinakabiliwa na changamoto nyingi sana hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa kutoka katika *Analog* kwenda *Digital*, sasa lazima *budget* yake iimarishwe kwa lengo la ufanisi kwa madhumuni ya kupata habari kwa Mikoa ambayo bado haijafanikiwa kupata taarifa ya chombo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa vyombo vya habari ni kutoa habari kutokana na tukio na wakati, kwa hivyo, tunaelekea katika uchaguzi mkuu wa Serikali hivyo chombo hiki kitoe fursa sawa katika kuzinadi sera za vyama vyote bila upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa huelimisha jamii kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini ipo haja ya kuziangalia baadhi ya sanaa ambazo maadili yake sio mazuri kwani huwa hazielimishi jamii na badala yake hupotosha jamii ya Watanzania na kuiga upotoshaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiswahili ni lugha ya Taifa, lakini Kiswahili hakitumiwi vizuri, hasa kwenye makongamano, warsha na matangazo. Hivyo, ipo haja

ya kutumia lugha hii kwani Watanzania ndio wanayoitumia na kuilewa zaidi na wala si Kiingereza kwani si lugha ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu zetu za Taifa huwa zinashiriki sana katika mchezo wa Kitaifa lakini baadhi ya timu zetu hazifanyi vizuri, mikakati iandaliwe kwani kuna vipaji vingi vya wanamichezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka kuwa na timu nzuri ya Taifa ipo haja ya kuwaandaa wachezaji wa umri wa miaka 17 kwani Waswahili husema kambare mkunje bado mbichi, hivyo vijana wetu hao wanaweza kufanya kama wale wenzetu wa Timu ya Taifa ya Ghana, ambao wamewekeza kwenye vijana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza hayo yote ipo haja ya *budget* ya Wizara hii kuongezwa na kuliondoshea Taifa aibu ya kushiriki tu na sio kushindana. Ahsante.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuchika pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Bendera, kwa kuhamasisha michezo hapa nchini. Juhudi zao zinaonekana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukru Mheshimiwa Waziri kwa kauli yake ambayo aliitoa hapa Bungeni ya kusema, shughuli za Bunge zote Semina zitumie lugha ya Kiswahili, hili ni jambo muhimu sana kwani watu wanaoangalia Bunge letu ni Watanzania na wengi wao hawajui hata kusoma Kiswahili na kukiandika pia. Hili ni jambo la maana lakini cha ajabu Sheria nyingi kama si zote za nchi yetu ziko kwa lugha ya Kiingereza, sasa wananchi hao ambao hawajui Kiingereza na ndio ambao sheria hutungwa kwa ajili yao ni vipi watazitambua huku ni sawa na kumpigia mbuzi gitaa. Naiomba Wizara hii itilie mkazo, pia sheria zitafsiriwe ili tuendane sambamba na wale wasiojua lugha ya kigeni. Kiswahili ndio lugha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kusema kuwa pamoja na utamaduni Tanzania bado hatujafikia utamaduni wa kuonyesha matendo au dalili za matendo ya ndoa. Kuna baadhi ya maduka ya dawa baridi yanauza kondom zenye picha ya mwanaume anamnyonya matiti mwanamke, mwanamke anashika utupu wake kwa mkono, mwanamume anashika matako ya mwanamke aliye uchi. Tukumbuke duka la dawa hata mtoto chini ya miaka kumi hutumwa hata kwa kununua panado, ni vipi anakuta picha kama hii. Picha hizi huwekwa kwenye kabati ya matangazo ya biashara. Ukihitaji Kondom hizo nitakupa maana nilizinunua na si kwa matumizi ila kwa ushahidi na ni hapa Dodoma. Hivyo, naomba Serikali ikemee hili si utamaduni wetu. Pamoja na Kondom kuwa ni kinga dhidi ya UKIMWI lakini tuzingatie maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara imesema imeendesha Kampeni ya ushauri nasaha na kupima VVU/UKIMWI kwa hiari na kutoa huduma ya lishe na madawa kwa watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI, kwa kuwa rasilimali watu wengi

wao wapo vijjni ni vipi uhamasishaji huo utawafikia na ushauri wa lishe kwa vyombo vya habari ukizingatia wengi wao hawana vyombo vya habari kama *TV* na *Radio*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ambayo ni hoja nzuri na ya muhimu kwa wananchi wetu hata tukizingatia maisha bora kwa kila Mtanzania. Napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Kapuya pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Makongoro kwa kufanya kazi zao japo lengo la maisha bora na ajira ni utata mtupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia Mfuko wa JK hakuna ubishi kuwa Mfuko huu ulikuwa ni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo (wajasiriamali) lakini lengo halikufikiwa kwani hapa tunasomewa takwimu lakini ukifutilia kwenye *SACCOS* nako ni utata, ukifutilia mtu mmoja mmoja huko ndio tatizo kubwa, hata ukokotoaji wa *BOT* hauonyeshi kama *SACCOS* na walengwa wamefikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi ajira 1000 hazikufikiwa, tunachokiona mfuko huu ungewasaidia wananchi waliokusudiwa bila shaka tuneona mabadiliko ndani ya vijana na akinamama, lakini tunachoona sasa ni ajira za kuokota machupa matupu ya maji na hata kushindwa kutofautisha kichaa na mtu mzima. Maana wote wanaokota taka, sasa basi tunaposema maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikanaje? Wakati vijana wapo vijiwi na kwenye madanguro, eti wafanye kazi, hiyo ni kazi gani na nani atawaajiri ukisema wajajiri mitaji iko wapi na ni nani atawapa mitaji hiyo. Hata ya JK hawakuipata, tukisema wakalime pembejeo watapata wapi, wakati hata ukiwa na mchanganuo mzuri na Serikali ya kijiji ikakiidhinisha na kukutambua haisaidii kama huna hati ya nyumba. Hii inapelekea vijana wengi kujihusisha na madawa ya kulevyta, wizi, ujambazi na hata uchangudoa. Tunaomba mijipange na muweze kuzitumia nguvu kazi hizi ambazo zinapotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekua ikitumia muda mrefu kwa kutoa uamuza, muda mrefu huo unatuingizia hasara sana, kwa mfano, ujenzi wa daraja la Kigamboni mwaka 2005. Daraja hilo lilikisiwa kujengwa kwa UR 45,000,000/= na 50% ni msaada hili hatukuliona kama ni jambo dogo na kwa sasa daraja hili linahitaji kujengwa kwa UR 60,000,000/. Kwa hiyo, hili ndilo tatizo tulilonalo Watanzania hebu tutazame tofauti UR 15,000,000/= jinsi zinavyopotea, huu ni urasimu mkubwa, ni uvutano au ni kwa maslahi ya nani? Kama hiyo haitoshi Serikali ilitumia Mfuko wa *NSSF* mamilioni ya shilingi na baada ya kucheleva kwetu, je, hasara iliyopata *NSSF* ya kufanya upembuzi yakinifu ni nani atawajibika? Hii ndiyo Tanzania ya nguvu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri zaidi Serikali ikaangalia vijana ambao wanafanya kazi kwa viwanda binafsi kama Samaki, Korosho (kubangua) na viwanda vinginevyo katika kuwapatia vifaa vya kutendea kazi. Pale ambapo Waziri au Kiongozi akitembelea kiwanda kwa kutoa taarifa utakuta mambo sawa. Je, ni lini viongozi walifanya ziara za kushtukiza ili kuona madhila wanayopata. Mimi niliyaona *vicfish* pale Mwanza. Hata hivyo, kama OSHA imeshindwa hata kutumia rungu lake kwa wale ambao wanazoa taka katika Jiji la Dar es salaam kutumia vifaa kama sheria inavyosema na wakabaki wakizoa taka kwa mikono mitupu hawana hata lapa mguuni na hawana hapa

Mase, hii ndiyo OSHA kwani hata haya wao hawa yaoni wala hawa yaonii au tunahitaji kiongozi wa OSHA atoke nje ya nchi ndio alione hili? Kama sisi hatujali watu wetu na wazoa taka wanafanana na vichaa hali zao, pia ni tatizo maana lolote linaweza kutokea, tetenasi ni karibu yako bila shaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na watekeleze maadili mema kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu mdogo. Kwa kuwa viwanja vingi vya michezo mikoa mingi ni vya CCM na mambo haya ya viwanja hivyo vilitolewa wakati wa chama kimoja. Je, kwa sasa wakati wa vyama vingi visibadilishwe kuitwa CCM?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali pamoja na Wizara inatoa jibu gani au ina mikakati ipi kuepukana na ujisadi wa viwanja angalau viitwe maji maji na ya viongozi kuliko chama hali ilishabadilika ni ya vyama vingi. Je, Wizara kwa nini isiwe inafuatilia mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kagera kuna mambo mengi ambayo yanaweza kutuingizia, kuna magofu ya Kyaka, Mtukura. Sehemu palipokuwa kwenye mapambano makubwa ya vita kwa Kanisa ipo karibu na Mto Kagera darajani, je, Wizara ina habari na hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza wafadhili wote kuhusu vifaa vya michezo, isingekuwa hawa tumekuwa tumekwishesahau michezo. Naomba kupata ufanuzi michezo ni mazoezi, michezo ni furaha pamoja na ajira. Kwa hiyo, tuienzi michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote kwenye Shule za Watoto wenye ulemavu na wanataka kucheza lakini vifaa hawana. Shule za Bukoba Ngeza, Mseto, pamoja na Tumaini, je, hizi shule Wizara inazijua? Je, ni msaada gani unaotolewa au tunasubiri wafadhili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo mashulenii hasa kuanzia shule za msingi, sekondari, kuna watoto wengi wenye vipaji. Serikali inaaniszha kitu baada ya kukiendeleza inakuwa vigumu UMISETA, UMISHUMTA iliishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyombo vya habari, nchi hii kuna sehemu ambayo hawasikii habari yoyote inayohusu nchi yao. Je, Serikali yenye kasi mpya pangekuwa na sehemu kama hiyo hasa tunavyo elekeea kwenye uchaguzi Mkoo wa Kagera hasa Vijijini magazeti wanayapata baada ya siku mbili hadi tatu, si kuwanyima haki hawa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makumbusho, Tanzania kuna sehemu nyingi ambazo zinaweza kutuletea kipato kama zitatengenezwa vizuri. Wizara inapaswa

kufuatilia mambo kama hayo, juzi tumesikia kuna jiwe Ukerewe linacheza. Matatizo ni kusubiri wafadhili wakija kutusaidia tuwe tumetoa chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kutoa ilani kuhusu michezo ya mpira wa miguu ya wanawake, tusijivunie timu moja ya TWIGA, tushuke chini kwenye Mikoa na Wilaya, wapo watu wenyewe vipaji, tuwainue wanawake kupitia michezo pamoja na afya zao. Ukarabati viwanja vya Bukoba Mjini, uwanja wa huru amba o uko kwenye mji katikati, huo uwanja una historia. Je, ni lini utakarabatiwa?

Mhesimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Tuendelee kuenzi michezo na utamaduni, ngoma za asili, mavazi ya asili, Mwfafrika anasifika kwa mavazi. Kuhusu wana muziki kucheza uchi mbona inaendelea hasa wanawake wanatudhalilisha? Kwa nini wanaume wanafunga suti? Je, huo ni uungwana? Kwa nini wasivue wote kama ni sheria yao?

Pia napenda kutoa mchango wangu, napenda kujua ahadi za ajira, naomba nijue ni lini ahadi zitakamilika, au ni propaganda za Kitanzania kwa sababu walio na ajira migogoro ni ya kila siku mara kuandamana, mara hawapati posho zao, je, hili tatizo litakwisha lini? Tusitegemee ajira za watoto pamoja na watu wazima kuokota chupa za maji, ni aibu kwa Mtanzania kuokota chuma yenyе kasi mpya, naomba ufanuzi kuhusu ajira. Idadi ya ajira ni ndogo sana vijana ni wengi. Naomba kujua jengo la Machinga Ilala, ili Wamachinga wapate ajira wasiwe wanapigwa na mgambo wanawadhalilisha vijana wetu ambao wana mitaji yao sio wezi, kwanza hilo jengo litaongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa matatizo ya vijana, *SACCOS* wanapata wachache na hata mikopo ya JK zilingizwa siasa. Kwa hiyo, wanaopata unakuta ni vijana wa CCM, naomba ikimewe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, zinatoka nafasi za ajira kwenye magazeti, ukifuatilia vijana wanatuma maombi yao hawapati, wanaweka kama geresha. Ukifuatilia unakuta nafasi hazipo, zilikwisha. Naomba ufanuzi, je, wanajaza watu wao, naomba kujuu kama wanakuwa wamekwishaweka watu wao kwa nini wanaweka kwenye magazeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, bomoa bomoa ya vibanda vya watu waliojajiri. Wafanyabiashara binafsi huu mchezo mchafu utakwisha lini? Ni kwa nini Serikali isiwaandalie mapema kuliko kuwavunja vibanda vyao mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. Tusiwategemee vijana watupe kura bila kujali ajira zao tuwaheshimu kwanza, baada ya hayo tuwaombe kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana wengi walijiunga na JKT wakapata mafunzo, baada ya kumaliza hawakupata ajira, je, hii si ni hatari na kuwa amejifunza kushika vyombo vya moto unategemea nini? Je, hawawezi kujiingiza kwenye ujambazi? Je, Wizara inajua hilo tatizo? Ni kwa nini wasitafutiwe ajira kuliko kuwatelekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi watoto wetu hasa vijana wanaosoma wanafikiria ajira, je, Serikali imewaandaa vipi kwenye maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejitahidi kujenga shule nyingi ili vijana wasome, bila ajira itawezekana? Ufutiliaji wa ajira ya wawekezaji vijana wetu wa Kitanzania wanateseka je, Wizara inajua?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kutoa hoja na kuwasilisha.

MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Naibu, Wenyeviti na watendaji wote kwa jinsi mnavyoliendesa Bunge hili kwa viwango vikubwa Mwenyezi Mungu akupeni nguvu zaidi ili mfanikiwe kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu na watendaji wake wote kwa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake na maoni kwa Serikali, naamini kama wanavyosema wenyewe Serikali, siku basi watayafanya kazi maoni ya upinzani ili tuweze kupeleka mbele Serikali yetu, tunajenga nyumba moja tusigombee fito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia kwanza naiomba Serikali iiongezee bajeti Wizara hii kwani bajeti yake ni ndogo sana kiasi kwamba wanashindwda kukamilisha majukumu ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni mingi sana na ambayo inaleta afya mwilini, kwa hiyo, ni lazima Serikali yenye mikakati ya makusudi kuhakikisha kuwa michezo yote inasaidiwa ili ipate mafanikio kama walivyosaidiwa mpira wa miguu na riadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpira wa *netball* ambao bado Serikali haijawasaidia kwa dhati wanawake, kitu ambacho kinawavunja moyo wanawake wengi. Vile vile mipira ya vikapu kwa wanaume, *table tennis* na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa ni muhimu sana kwa kuelimisha jamii, lakini bado vijana wetu wanakosa fursa ya nyenzo muhimu katika kuonesha vipaji vyao maana bado mambo mengi hawana fursa ya kuigiza uhalisia wake, kwa mfano, anapoigiza Polisi hapati fursa ya uhalisi wake, Mahakama vile vile hawapati fursa ya kuigiza. Naiomba Serikali ihakikishe inawapatia fursa hizo kama michezo ya wenzetu majirani au filamu za Kihindi na Kizungu kwani kufanya hivyo ni kuwaogezea ubora wa filamu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa busara kwa Wizara hii kuwajengea jengo zuri na kubwa la kufanya maigizo, likawa na sehemu mbalimbali za kufanya maigizo, ndio maana tukaomba bajeti ya Wizara hii iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kujenga mitambo mipy ya *digital* kwa kushirikia na wenzetu wa Kichina, mitambo mipy hiyo ambayo ni *TBC 2*, lakini naiomba Serikali bei ya manunuzi ni ghali kwa mwananchi wa kipato cha chini, vile vile kwa kulipa elfu tisa kwa mwezi wenzetu wengi watakuwa hawapati huduma hii na nzuri hasa kwa ulimwengu wetu wa sasa, sekta ya habari ni muhimu sana na kujua habari za dunia. Kwa hiyo, Serikali iangalie kwa jicho la huruma kwa kupunguza bei kidogo ili wananchi wengi wafikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu na Watendaji wake wote wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba hii iliyo mbele yetu ya Wizara ya Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ya kipekee, nampongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake na maoni kwa Serikali kwani sisi tunajenga nyumba moja, hatugombanii fito.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, nakupongeza wewe, Naibu na Wenyeviti wote kwa jinsi mnavyoliendesa Bunge hili kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kutoa bilioni moja kwa kila Mkoa lakini mpaka leo hii tunamaliza kipindi hiki bado walengwa hazijawafikia na hata ukiangalia jedwali bado ni kima kidogo kilichotoka. Ninaomba Serikali itekeleze ahadi yake kwani wananchi wamejenga matumaini makubwa kuhusu mpango huu wa Mabilioni ya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi vilevile itajenga daraja kabla ya kumalizika kipindi hiki cha miaka mitano lakini mpaka leo ni hadithi tu hatujalionna daraja la Kigamboni. Je, kwa nini Serikali inaahidi kitu ambacho utekelezaji wake hauonekani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi tunasifu Chuo Kikuu cha Dodoma kilichojengwa na fedha nyingi za walipa kodi lakini kibaya zaidi ambacho Wabunge wengi tunakipigia kelele ni kwa nini Serikali ina kigugumizi mpaka leo kufunga mkatuba ili kuhakikisha usalama wa pesa za walipa kodi wa nchi hii? Serikali ina dhamira gani hata inashindwa kufunga mikataba au haitaki kulipa? Tunaiomba Serikali iingie mkatuba haraka sana ili ituhakikishie kuwa fedha za walipa kodi zinalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni ajira kwa watoto, watoto bado wanatumikisha ajira mbaya na kudhalilishwa na waajiri wasiokuwa na huruma. Pamoja na juhudhi za Serikali kuhakikisha watoto hawatumikishwi lakini bado wanatakiwa waongeze jitihada ya kutoa elimu ndani ya vyombo vy'a habari na vipeperushi. Nashukuru sana. Ahsante.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Kapuya; Naibu Waziri Dr. Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Kazi ni muhimu sana ziboreshwwe kwa kupewa vitende kazi nya kisasa ili kuondokana na msongamano wa kesi na ucheleweshaji usio wa lazima na kusababisha migogoro kwenye maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu, kumekuwepo ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu na kusababisha malalamiko mengi ambayo imefanya wakate tamaa ya ufuatiliaji wa haki zao kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, ucheleweshaji wa haki zao kusababisha pia kukosa imani na Serikali yao hasa wananchi amba wako nje ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fidia kazini, kwa kuwa sheria iliyopo ni ya muda mrefu ambayo hunipa haki mfanyakazi kulipwa fidia aumiapo kazini. Ningeshauri Wizara kuandaa angalau sheria iletwe Bungeni mapema ili ifanyiwe marekebisho hasa ukizingatia ajali zinazotokea hivi sasa hasa kwa wale waajiriwa pia kumekuwepo viwanda vingi ambavyo ni nya watu binafsi na wawekezaji toka nje na hasa hivi tunavyoingia katika masoko na ajira kwa Afrika ya Mashariki ili wakute imekamilika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgogoro wa Kiwanda cha Nyuzi, Tabora, kumekuwepo na mgogoro wa muda mrefu kati ya mwajiri na mwajiriwa kiasi kwamba wafanyakazi hao kutolewanan na mwajiri na kusababisha wafanyakazi hao kupewa likizo bila malipo na kunyimwa haki zao za awali pia kuwa wafanyakazi amba walipewa barua za kuajiriwa na kunyimwa haki zao. Ningeshauri vema tatizo hilo likashughulikiwa ili haki itendeke kwa wote na kuondoa migomo kazini. Kwa kweli kutomalizika kwa tatizo hilo kutasababisha wawekezaji kuogopa kuja Tabora au waliopo kuondoka hasa ukizingatia ndicho kiwanda pekee katika Mkoa wa Tabora chenye kuajiri wafanyakazi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora kumekuwa na vijana amba wana *SACCOS* zinazoshughulikia kilimo na kilimo cha umwagiliaji, hivyo ningeshauri Serikali kuangalia jinsi ya kuwasaidia mikopo mbalimbali hasa ya kilimo kwanza kama vile Pembejeo ya Ruzuku yenye riba nafuu ili vijana wengi warudi vijijini hasa ipitishwe kwenye mifuko ya maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote amba wameandaa hotuba hii nzuri yenye mwelekeo wa maendeleo ya habari na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni afya, michezo ni furaha kwa Taifa letu Tanzania, lakini kwenye nchi zilizoendelea michezo pia ni ajira. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, wananchi wenye vipaji nya michezo ni vyema tukawaenzi kwa

kuwapatia ajira kwani utaratibu huu ulikuwepo siku za nyuma, vikosi vyetu nya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Askari Polisi, Magereza walikuwa wana utaratibu mzuri wa kuajiri vijana wenyе vipaji nya michezo, lakini sasa hivi wamepunguza kutoa ajira kwa wanamichezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa utaratibu huu ukarudi ili wananchi wetu wenyе vipaji wakapata moyo wa kuonesha vipaji vyao na wakaweza kuitangaza nchi yetu yenye amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mara kwa mara Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hupima viwanja na kupanga miji mipya ni busara sasa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kutenga viwanja nya michezo, viwanja vidogo vidogo na viwanja vikubwa kwani wakati mwingine watoto hutamani wawe na viwanja vidogo vidogo ambavyo wanaweza kucheza michezo mbalimbali ya watoto huwa havipatikani na kuwanyima haki ya kucheza watoto walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake yenye sura ya mafanikio katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa Wizara katika kukuza michezo hapa nchini, ukiangalia bajeti ya Wizara ni ndogo sana jambo ambalo litapelekea Wizara kushindwa kufanikisha azma yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mtazamo wetu wa kuona michezo nchini imekuwa bado dhana hii sio ya kweli. Asilimia kubwa ya michezo unaopendwa ni mpira wa miguu. Hii ndio sehemu iliyofanikiwa. Baadhi ya michezo imekosa wapenzi kutokana na Serikali kutoitupia jicho la rehema. Jambo ambalo hupelekea baadhi ya michezo kuonekana wakati maalum. Mchezo wa bao katika nchi yetu ungepewa umuhimu mkubwa kwani ni michezo ambao Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere aliuchenza na kuupenda. Lakini michezo huu hauna hata eneo maalum la kuchezza, badala yake ni vibarazani, ndio vilabu vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo ya kuigiza, michezo huu unapendwa sana, tatizo lililopo mara nyingi hukosa maeneo ya kuigizia na wakati mwingine na nguo. Mfano waigizaji wanapoigiza kama Polisi, Jeshi, hukosa vazi husika. Hivyo basi naiomba Wizara iwapatie sheria mahsusili ili waweze kufanya kazi zao ipasavyo. Pia na kuiwezesha michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wamejitokeza katika michezo wa *netball* na *football*, Wizara bado haijawasimamia ipasavyo wanawake hao. Mwisho, napenda

kuipongeza
nchi yetu.

Serikali kwa kuweza kurahisisha upatikanaji wa habari katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Kapuya (Mb), kwa hotuba yake yenyeye sura njema kwa vijana wetu hapa nchini. Mungu amjaalie Mheshimiwa Kapuya afanikishe azma yake. Ila napata wasiwasi kutokana na uhaba wa bajeti aliopewa kwani ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM iliahidi kuwapatia vijana ajira milioni moja. Pamoja na ufanisi wa Serikali juu ya ahadi hiyo bado vijana hawajapewa ajira ya heshima yenyeye uhakika, vijana wengi ajira yao si ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Kitanzania wameweza kujiajiri katika nyanja za Muziki wa Kizazi Kipyka kama sehemu ya ajira. Vijana hawa Serikali imeshindwa kuwasaidia kwa njia ya kuwakuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana na elimu. Kwa kuzingatia kazi yoyote inahitaji elimu, vijana walio wengi hapa nchini elimu yao kibashara ni ndogo sana. Tutawezaje kumuajiri kijana wakati elimu yake ndogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mashirika ya Hifadhi za Jamii, ni vizuri kuyapongeza mashirika haya kwa msaada wao nchini ambapo yameweza kusaidia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kufanikisha ujenzi huo kwa muda mfupi. Serikali mpaka leo imeshindwa kutoa dhamana (*guarantee*), hii ni kusema hadi leo hawajawa na uhakika wa fedha hizo za ujenzi wa Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* tuipongeze kwa kuweza kusaidia Serikali ujenzi wa nyumba za Polisi – Pemba, soko la Wamachinga Dar es Salaam, *UDOM* pamoja na gharama za tathmini juu ya Daraja la Kigombani, sidhani kama daraja hili limeulizwa. Mambo kama hayo kama Serikali haikutimiza wajibu wake, fedha za Watanzania zitatumika ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nasema ahsante.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara, kwa ushirikiano walionao wa kusimamia majukumu ya Wizara vema kwa manufaa ya Taifa. Kwa kweli, Wizara imetekeleza majukumu yake vizuri pamoja na ufuatiliaji mzuri kwa mafanikio yanayotokezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri katika hotuba yake katika kukuza lugha ya Kiswahili alisema utafiti umefanywa kwa maneno yanayoweza kutumika katika Kiswahili pia Wizara imetoea tamko la kusisitiza matumizi ya lugha hii katika shughuli zote rasmi za Serikali. Mipango hii ni ya kupongezwa sana.

Lakini wananchi wengi wanahofu kuwa suala hili haliwezekani kwa sababu maneno haya yalizungumzwa toka utawala wa Baba wa Taifa lakini hakuna lililotendeka. Kwa hivyo, ninaiomba sana Serikali hii ya Awamu ya Nne, inayoongozwa na Rais Kikwete, suala hili utekelezaji wake uonekane na kufuta usemi kuwa hakuna liwalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC*, licha ya kazi nzuri zinazofanywa na Shirika hili la kupanua usikivu wa idhaa zake za redio na *television* kwa kujenga vituo mbalimbali, lakini majengo yanayotumiwa na Shirika hilo hayafai na aibu kwa taasisi hii ya umma. Kama si ujasiri na ubunifu wa wafanyakazi wazalendo wanaopenda kazi yao na Taifa lao, hali ingekuwa mbaya zaidi. Kwa hivyo, ninaiomba Serikali katika kipindi hiki waipatie udhamini wa kujenga majengo yaliyopo kutoka katika Mifuko ya Pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri, pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake, kwa ushirikiano mzuri kwa kukamilisha hotuba hii kwa wakati. Nawaomba waendelee na ushirikiano katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi zilizofanywa na Mfuko wa *NSSF*, ni pamoja na majengo ya wajasiriamali (*Wamachinga*) kwa kuwasaidia kuondokana na biashara za kurandaranda. Wazo hili ni zuri na lilipokelewa na wananchi na wafanyakishara wenye kwa furaha sana lakini hadi leo jengo hilo lengo lililokusudiwa halijafanyika. Ninamuuliza Mheshimiwa Waziri, tatizo ni nini hadi leo jengo halijakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wachangiaji wengi wameeleza majengo mazuri ya Vyuo Vikuu yaliyoko Dodoma yaliyojengwa na Mifuko yetu hadi leo Serikali hajadhamini, ni sababu zifi zilizosababisha hadi leo Mifuko ambayo sote tunajua kazi nzuri iliyofanywa na inayoendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii.

ME. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kwa niaba ya wananchi wa Ranya, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, viongozi wa taasisi, mashirika na bila kusahau viongozi wa vilabu vya michezo hususan Klabu ya Simba, kwa kazi nzuri wanayofanya kuendeleza michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkuchika ni mkereketwa na mpenzi wa michezo. Naibu Waziri ni Kocha, mchezaji na mkereketwa wa michezo. Wote ni wapenzi wa *Yanga Sports Club*, nawatachia mafanikio na afya njema katika uchaguzi Mkuu 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kutoa maoni na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

(1) Ukurasa wa 52 – 54, sekta ya michezo. Nashauri kuwa Sera ya Michezo ya mwaka 1995, sasa ifanyiwe marekebisho na kuipitia upya ili iweze kukidhi matarajio ya wananchi kulingana na hali ya sasa ili Tanzania iweze kwenda na wakati katika nyanja ya michezo. Katika kupitia Sera hiyo, wadau katika ngazi mbalimbali washiriki kutoa michango yao.

(2) Ukurasa wa 55 – 56, kuhusu huduma za afya kwa wanamichezo. Chama cha Madaktari wa Wanamichezo (*Tanzania Sport Medicine Association*), ni chama cha kitaalamu kinachotambuliwa Chama cha Olimpiki Duniani. Chama hiki kilianzishwa rasmi katika miaka ya themanini. Chama hiki ni muhimu sana katika kutoa kinga na huduma za afya kwa wanamichezo. Wakati Chama hiki kilikuwa kinatoa huduma za afya kwa wanamichezo, Tanzania iliweza kuandaa wanamichezo wenyе afya bora. Nashauri TASMA ipatiwe wataalamu wenyе ujuzi, ofisi, *clinic* na ukumbi wa mazoezi ya viungo. Nchi nyingi zilizopiga hatua katika michezo, wamejenga hospitali na vifaa vya kisasa kwa ajili ya wanamichezo. Tuwezeshe TASMA ili tuweze kupata wanamichezo wenyе afya bora. Kama Rais wa Kwanza wa TASMA, niko tayari kutoa mchango wangu katika kufufua na kuimarisha TASMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, ila nawashauri wapunguze ushabiki wa Yanga.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa umahiri wao wa kunivumilia na kuniunga mkono pamoja na kasumba na ushawishi wanaoupata dhidi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, NSSF, kwa kazi walizotekeleza katika kipindi cha 2009 – 2010 ukiwemo ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Nyumba za Askari Bara na Visiwani. Suala hili limepunguza sana adha na shida za wanafunzi pamoja na shida kubwa ya makazi ya Askari. Kwa hivyo, ninaomba Serikali kuyapa nguvu mashirika haya kwa kuyatumia kwa ujenzi wa majengo mengine katika nchi nzima kwa sababu Mifuko hii kama itatumiwa vizuri ni ukombozi kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba ya Waziri imejitosheleza, naomba niishie hapo na naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100%. Ahsante.

MHE. DR. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ila napenda kutoa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara sasa ivalie njuga Wanahabari/Waandishi Makanjanja wasiaibishe fani ya Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wako baadhi ya Wandishi wanaonunuliwa kuandika habari za upande mmoja na habari za kupotosha na kukashifu upande wa yule anayewanunua. Mahali maalum pa kupokea rushwa kwa baadhi ya Waandishi wa Habari za Mahakamani, ni chini ya mwembe mkubwa wa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari vya *ITV* vinatoa habari kwa kupendelea wale walio karibu na wamiliki. Tunao wasiwasi hata wapiga picha wa magazeti ya baadhi ya wamiliki hawaandiki shughuli zinazofanywa na baadhi ya wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, si busara kuwapa leseni ya “*multiplex operator*” wale wanaomiliki vyombo vya habari mfano *TV* kwa vile kutakuwa na *conflict of interest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya habari inahitaji kupigwa msasa, kupatiwa mafunzo ya maadili ili iweze kutoa haki kwa wote (sawia) na bila ushawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza Rais Kikwete kwa kutupatia Kocha wa Mpira wa Miguu, sasa Wizara iangalie uwezekano wa kusaidia Makocha wa Mpira wa Kikapu na *Volleyball*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa michezo, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia shughuli mbalimbali za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhamasishe jamii yenye uwezo waanzishe Shule za Michezo, *Football Academy or Netball Academy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi *TBC* kwa kazi nzuri inayofanya bila ubaguzi. Tuendelee kuboresha maeneo ambayo hayasikiki vizuri mfano Rombo, Tanga, Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wasanii wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuelimisha jamii kwa michezo, ngonjera na kadhalika. Ila tutilie mkazo juu ya kuelimisha umma kuhusu kinga na maradhi mbalimbali ambayo yanaepukika kwa njia ya michezo au filamu ndogo ndogo. Tunanufaika kwa kuona filamu fupi fupi toka Afrika Kaskazini na Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari na maadili yetu. Hakuna uhuru usio na mipaka. Tunaona katika magazeti fulani fulani yakitoa vikatuni vyenye tasnia ya kufikisha ujumbe fulani kwa umma na huku tukijua waliochorwa ni viongozi wenye heshima zao, magazeti mengine hayachuji vya kutosha habari za kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wahariri wengine wakiwa na ugomvi na watu fulani basi chuki zao huishia kuwaandika wale wagomvi wao au wateja wa karibu katika magazeti. Hivi Mhariri wa Gazeti la Nipashe ni Mtanzania kweli? Anaumwa na nchi hii kweli au anafuata matakwa ya anayemlipa?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana, Waziri, Naibu waziri, Katibu Mkuu na watalamu wote wa Wizara waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii na kuiwasilisha hapa Bungeni. Hata hivyo, nina maeneo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo ameikuza sekta ya michezo nchini. Uamuzi wa kumwajiri Kocha (*Coach*) Maxio Maximo kutoka Brazil kwa ajili ya kuifundisha timu yetu ya Taifa ya mpira wa Miguuu, ni kielelezo tosha kuonesha dhamira njema ya Rais ya kukuza michezo nchini. Aidha, hivi karibuni Rais amekubali Chama cha Mpira wa Mikono (*Netball*) kumwajiri Mwalimu (*Coach*) kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kufundisha timu ya taifa ya Netball. Ni dhahiri Rais huyu amedhamiria kwa dhati kabisa kuona kwamba nchi yetu haiendelei kuwa kichwa cha mwenda wazimu katika sekta ya michezo. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia aliyekuwa Kocha wa Timu ya Taifa ya mpira wa miguu, Ndugu Maximo kwa kazi kubwa aliyoifanya, kwa mwenye macho haambiwi tazama. Maana kazi aliyoifanya imeonekana, kiwango cha mpira kwa timu yetu ya Taifa kimekuwa kwa kiwango cha kuridhisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, jitihada za kuimarisha michezo nchini ziendelezwe kwa ari kubwa zaidi, nguvu kubwa zaidi na kasi kubwa zaidi. Ipo siku tutafika huko ambako timu nydingine kama Ghana (*The Black Stars*) zimekwishafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, BAKITA na Kiswahili, naipongeza BAKITA kwa jitihada zake za kukuza na kusimamia maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, bado hawajafika ngazi za chini katika kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili hasa lugha fasaha inazunguzwa vizuri, shulenii, vyuoni na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zilizoanza kufanywa na Hayati Mwalimu Nyerere, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, za kuhakikisha kwamba Kiswahili kinapewa umuhimu mkubwa katika shughuli za Kitaifa, bado kuna maeneo ambayo Kiswahili hakipewi kipaumbele. Kwa mfano bado taasisi nydingi nchini zinaendesha semina zao kwa lugha ya Kiingereza. Kwa mwendo huu, lengo la kukuza Kiswahili litatimia lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, michezo katika ngazi za Wilaya. Pamoja na jitihada zinazofanywa na viongozi wakuu wa nchi katika kukuza michezo nchini bado ngazi za chini hasa Wilayani michezo karibu yote haijapewa uzito unaostahili. Vyama vinavyosimamia michezo kama vile mpira wa miguu viro lakini kama vile havipo, viongozi wake wengi wana upeo mdogo katika sekta ya michezo. Naomba Wizara ilifuatilie jambo hili ili michezo isitawi pia ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Sheria ya Kusimamia Sekta ya Habari, nampongeza Waziri kwa kuliarifu/kulifahamisha Bunge kwamba Muswada wa Sheria hiyo umekamilika na kwamba unaweza kuwasilishwa Bungeni muda wowote.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua hiyo. Hata hivyo, suala hili la kuletwa kwa Sheria hiyo Bungeni ni la muda mrefu sana. Naomba Serikali kupitia Wizara hii iwe na dhamira ya kweli ya kuhakikisha kwamba Muswada huo unaletwa Bungeni, kama alivyosema Waziri, ili Sheria itungwe kwa ustawi wa sekta ya habari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa Bajeti hii na kuimarisha hapa Bungeni. Hata hivyo, nina maeneo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kupitia Mfuko wa Mheshimiwa Rais, miaka mitatu iliyopita Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alidhiinisha zaidi ya Shilingi 21 bilioni kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wananchi hasa wale wa kipato cha chini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo. Hata hivyo, mikopo hiyo ambayo ilipaswa kuwa endelevu haionekani kuwa hivyo. Nasema hivyo kwa sababu mabenki yaliyotoa mikopo hiyo kwa niaba ya Serikali yamekuwa yanalamika sana kwamba, mikopo hiyo hairejeshwi ipasavyo. Urejeshwaji wa mikopo usioridhisha umefanya mabenki yasite kuendelea kutoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujua, je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba taasisi zilizokopa na watu binafsi wanarejesha mikopo hiyo kwenye benki husika ili zoezi la kutoa mikopo hiyo liwe endelevu? Aidha, tuliambiwa kwamba baadhi ya taasisi za fedha kama vile *Pride, Finca* na kadhalika zingetumika kutoa mikopo maeneo ambayo hayafikiwi na mabenki. Nataka kujua, je, zoezi hilo limefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, OSHA ni wakala muhimu sana katika kuhakikisha kwamba usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi zinazingatiwa. Wakala huu unatakiwa utembelee maeneo mbalimbali ya kazi, hasa viwandani ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya kazi yapo katika hali inayozingatia usalama na afya za wafanyakazi. Hata hivyo, Wakala huu unashindwa kufanya kazi zake nzuri kwa sababu moja, bajeti yake ni ndogo sana. Pili, wataalam wake ni wachache sana, aidha, watalam wengi wazuri hawakai katika taasisi hiyo kwa sababu ya maslahi duni. Nashauri bajeti ya taasisi iboreshwe. Pili, wataalam wengi zaidi na wenye sifa waaajiriwe. Tatu, Ofisi za Kanda za OSHA ziboreshwwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kima cha chini mshahara kwa watumishi wa Serikali na hata mashirika binafsi kipo chini sana ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya leo. Napongeza Serikali kwa kusikia kilio cha wafanyakazi na kukubali kwenda kuzungumza na *TUCTA* katika azma ya kuboresha mishahara ya watumishi. Ni kweli pia kwamba Serikali haiwezi kulipa kima cha chini cha mishahara cha Sh.315,000/= kwa mwezi kama inavyodaiwa na *TUCTA*. Jambo muhimu ni kwa Serikali kukubali kuzungumza na *TUCTA* na kuongeza kima cha chini cha mishahara kadri hali ya uchumi wa nchi yetu utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la vijana la Sasanda, Mbozi, linalokadirwa kuwa na ekari zaidi ya 800 bado halijatumika sawasawa. Aidha, majengo yaliyopo, yapo

kwenye hali isiyoridhisha hata kidogo. Nataka kujua nini mpango wa Wizara kwa mwaka huu wa fedha (2010 – 2011) katika kuendeleza kambi hiyo ya vijana ya Sasanda na kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa madhumuni hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawasilisha.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kero kubwa katika Idara ya Kazi ni migogoro ya mishahara ambayo kwa maoni yangu husababishwa na mambo makuu mawili, mosi, ni mtazamo wa kimapokeo kuwa mtu akishaajiriwa basi linalofuata ni mishahara yake na marupurupu bila ya kuzingatia tija inayomwezesha mwajiri kukidhi haki hii ya mfanyakazi. Jambo hili lilikuwa linawezekana enzi za uchumi hodhi lakini hali siyo hiyo katika mfumo wa soko ambapo uhai wa mwajiri unategemea tija na siyo ruzuku ya hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili ya migogoro ni tofauti kubwa iliyopo ya ufahamu wa kanuni na mbinu za majadiliano kati ya waajiri (*ATE*) na wafanyakazi (*TUCTA*) na hivyo wafanyakazi kuamua kufuata njia za mkato katika kutatua yanayowasibu katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara itilie mkazo suala la kutoa elimu ya uhusiano wa kuongezeka kwa tija na kuongezeka kwa malipo ya mishahara na marupurupu. Aidha, Wizara itilie mkazo suala la elimu ya mbinu za majadiliano maeneo ya kazi kwa Vyama vya Wafanyakazi na wafanyakazi wenyewe ili kuepusha migogoro inayoepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara ya Vijana. Hapana ubishi kuwa suala la vijana ni mtambuka na linaloratibwa na Wizara nyingi. Kwa bahati mbaya wananchi wengi hatuoni ukweli huu na hivyo kuamini kuwa Serikali haifanyi jitihada za makusudi katika kuwaendeleza vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya elimu ya sekondari, ufundi na elimu ya juu ni namna moja ya kuwaendeleza vijana katika matayarisho ya kujiajiri na kuajiriwa. Jitihada nyingine zinaonekana kupitia kilimo kwanza, ufugaji, uvuvi na biashara ndogo ndogo vinavyosimamiwa na Wizara mbalimbali na mamlaka za Miji na Halmashauri za Wilaya. Naishauri Wizara kwa kushirikiana na vyombo vingine vinavyoratibu shughuli za vijana, ziratibu kwa ushirikiano wa karibu matatizo yanayowakibili vijana na kubuni mbinu za kuleta suluhisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ina jukumu kubwa la kuelimisha, kuburudisha na kutoa habari zinazohusu mambo mbalimbali. Hivyo basi, ili jukumu hili lifanikiwe ipasavyo, ni lazima huduma za radio, televisheni, magazeti, vijarida, picha, sanaa na mengineyo viruhusiwe kuwepo na kupewa uhuru unaostahili. Ili azma hii iweze kutekelezeka, ni

lazima nchi itunge sheria, kanuni na miongozo itayosaidia vyombo hivyo kuweza kufanya kazi zake bila usumbufu au kuingiliwa na yelete.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba hadi leo hii Sheria ya Magazeti ya 1976 haijafutwa. Sheria ambayo inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Habari kufungia chombo chochote cha habari ambacho kwa maoni yake anaona kimeandika taarifa ambazo hazikumpendeza au hazifurahishi Chama kinachotawala. Nadhani ipo haja kwa Serikali kuitea sheria hii Bungeni ili ifanyiwe marekebisho kwa kukifuta kifungu hicho kandamizi kinachompa Waziri husika kuchukua maamuzi ambayo hayazingatii uhuru wa vyombo nya habari. Kuendelea kuwemo kifungu hicho kwenye sheria hiyo sio tu kinauwa uhuru wa vyombo nya habari lakini pia kinaenda kinyume na haki ya wananchi, haki yao ya kupata habari na hivyo imevunja haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa vyombo binafsi nya habari kwamba Serikali haiweki uwanja ulio sawa kwa vyombo nya habari binafsi kuingia katika ushindani. Lalamiko hili limekuwa linaelekezwa katika hoja kwamba Serikali ndiyo mtunga Sera ya Habari, Mtunga Sheria, Msajili wa Vyombo nya Pabari, pia ni Msimamizi wa Vyombo nya Habari. Lakini la kushangaza ni kwamba Serikali hiyo hiyo nayo inamiliki vyombo nya habari ambavyo vinapata fedha kutoka Serikalini. Hili si jambo halali, kwani ule ushindani wa kibashara kwa vyombo nya habari umekuwa na upendeleo kwa baadhi ya vyombo hivyo na hivyo kuviumiza kibashara baadhi ya vyombo binafsi nya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kuviacha vyombo nya habari nya Serikali kuingia katika soko la ushindani pasi na kupata ruzuku kutoka Serikalini. Vinginevyo Serikali itakuwa haivitendei haki vyombo nya habari binafsi hapa nchini na hivyo Serikali kukosa ile sifa ya kuwa mlezi bora wa vyombo vyote nya habari hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo kimsingi kazi yake ni kukusanya michango ya wanachama wake ambayo baada ya wanachama hao kustaafu hulipwa mafao yao yaweze kuwasaidia kuwaendeshea maisha, ni dhahiri kwamba ili mafao ya wastaafu yaboreshwe, michango ambayo inakusanywa na Mifuko hii huwekezwa katika ununuzi wa Hati Fungani, *Tresuary Bills*, kununua hisa katika makampuni yaliyosajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuziweka fedha hizo katika *Fixed deposit* katika mabenki mbalimbali. Hili ni jambo jema sana kwani kwa kuzingatia ukweli kwamba shilingi huwa mara nyingi inashuka thamani hivyo ingeliweza kuathiri mafao ya wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko hii ya Jamii pia inasaidia sana katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali hapa nchini. Mionganini mwa shughuli hizo ni pamoa kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe, Kiwira, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji umeme na kadhalika. Fedha nyingi sana zimetumika katika miradi hiyo ambayo Serikal imezikopa au kudhamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba fedha hizi ni za wanachama wa Mifuko hiyo na kwa hivyo ni lazima matumizi yake yawe yanayozingatia taratibu na Sheria za Fedha. Ni jambo la kusikitisha kwamba Serikali hadi hii leo imeshindwa kuheshimu taratibu za kisheria za matumizi ya fedha za Mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuingia mkataba na mifuko husika ili kuhakikisha fedha za wanachama wa Mifuko hiyo ziko salama. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni sababu zipi zilizopelekea hadi leo hii Serikali imeshindwa kuingia Mkataba wa Maandishi na Mifuko husika ilihali fedha nyingi zimeshatumika kadhalika atueleze ni lini basi Serikali itaaanza kulipa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa Daraja la Kigamboni limekuwa ni hadithi ya muda mrefu. Suala hili limegubikwa na ukimya mzito licha ya kufahamu umuhimu wa ujenzi wa daraja hilo, wananchi hatuelezwi ni hatua gani hadi sasa zimefikiwa kufanikisha ujenzi wa Daraja hilo. Ni vyema basi Serikali ikalieleza Bunge lako Tukufu, ni hatua gani hadi sasa imefikiwa katika mchakato wa ujenzi wa Daraja hili la Kigamboni ikiwa ni pamoja na wahuksika wataochangia ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama mahali pa kazi, ni jambo la msingi na muhimu sana. Nichukue nafasi hii, kuipongeza Wizara hii kwa juhudini ambazo inachukuwa katika kuimarisha afya na usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi. Hakuna asiyefahamu kwamba usalama mbovu na hali mbaya ya afya katika mazingira ya kazi yanapelekeza kuongeza ghamama za matibabu, kuongezeka kwa walemavu na vifo kazini ndiyo matokeo ya kadhia hiyo. Ni lazima mikakati madhubuti iandaliwe ili kuhakikisha kwamba madhara mbalimbali yanayotokana na kutozingatia ipasavyo usalama na afya za wafanyakazi wawapo kazini yanadhibitiwa.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kuwapongeza kwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya Waandishi kuhusu Sheria ya Habari yamekuwa ya muda mrefu bila ya utatuji, je, kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *TBC* kwa kuboresha huduma zake ingawa bado inatakiwa kupewa nguvu za fedha, nyenzo na miundombinu ili liwe Shirika la Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Wasanii mbalimbali kuibiwa kazi zao kwa ujanja ujanja hakijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa timu zetu za Taifa hasa mpira wa miguu na riadha, utazamwe upya kwa mtazamo wa kiushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wamiliki wa magazeti watahadharishwe ili waepukane na kuandika habari za kuchafuana. Nawapongeza mno kwa kuongoza Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, migogoro ya wafanyakazi inapaswa kuangaliwa kwa kina, malalamiko ya makato ya kodi na fedha wanazopata baada ya kustafu iangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ya kujajiri binafsi ni suluhisho katika ufumbuzi wa kuongeza ajira nchini uwepo uamuvi wa makusudi kuwekeza katika kilimo na ufugaji wenye mabadiliko ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa mbio za Mwenge unapendelea zaidi vijana wa Zanzibar (wakimbiza mwenge) mara nyingi wengi kutoka Zanzibar. Je, Watanzania hawawezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inayotolewa na Wizara ya Vijana haikidhi matarajio ya ujamaa iwapo wanawake wameanzisha Benki yao kuna kikwazo gani ianzishwe Benki ya Vijana? Hata hivyo, nawatakia heri na huko Majimboni mchaguliwe tena katika uchaguzi mkuu ujao mshinde.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa nafasi hii, pia naipongeza sana Wizara kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya kwani tangu tumeingia Bunge hili mwaka 2005 hadi leo mambo mengi ya maendeleo katika Wizara hii yanaonekana.

Pia naipongeza Wizara kwa kusimamia vyema mitambo ya *FM* ya *TBC* kwa ajili ya Mkoa wa Singida na hatimaye sasa hivi Singida hatuna tatizo la usikivu tena. Aidha, napenda pia nichukue nafasi hii kipongeza timu ya mpira ya Mkoa wa Singida kwa ushindi mkubwa iliyoipatia Singida yetu sifa kwa kutwaa kombe la Taifa.

Pia naomba pongezi ziende rasmi kwa *TCRA* kwa jinsi ambavyo wameweza kusimamia vyema vyombo vya habari vya *TV*, redio na kadhalika kuweza kulipa mrahaba kwa kazi za sanaa, muziki, filamu na kadhalika wanazotumia. Pamoja na pongezi hizo napenda kutoa mchango wangu mfupi kama ifuatavyo; swalii, kwa nini wasanii wa muziki na kadhalika wananyanyaswa kwenye maonyesho ya Sabasaba mwaka huu? Kwani wamezuiwa kufanya shughuli zao za sanaa eti wanapig kelele. Mbona miaka yote haikuwa hivyo? Naomba majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, *TBC (Radio Tanzania)* wamekuwa wakiuza nyimbo za zamani zilizorekodiwa kituoni kwao miaka ya zamani mfano nyimbo zilizoimbwa na Mbaraka Mwinshehe, Ali Hamadi Kipande, *Kilwa Jazz*, Salum Abdallah na kadhalika lakini inasemekana hawawalipi mrahaba wahusika, je, ni kweli na kama kweli kwa nini? Na Serikali inasemaje juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la tatu, je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya *COSOTA* na sanaa kwa ujumla ili kulinda kazi za wasanii na kuleta manufaa kwa wahisani hasa kuhusu maharamia wa kudumu na kuuza kazi za wasanii kwani sheria iliyopo inatoa mwanga mkubwa kuendeleza uharamia kwani hata faini wanazotozwa ni

ndogo sana. Je, kwa nini Wizara isiwe na kitengo kinachosimamia uharamia na kulinda maslahi ya wasanii? Kwa kuwa *COSOTA* naona wameshindwa, kwanza hawana hata bodi ya kusimamia kazi zao wasanii ni kama yatima tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inafahamu kuwa sanaa ya muziki na maagizo (Filamu) ni sawa na mgodi wa almasi na dhahabu sasa kwa nini *TRA* hawaingii katika fani hii ili kulipatia Taifa kipato na kuleta tija kwa wasanii. Je, ni lini hatma ya nyumba ya sanaa fedha zinazopatikana pale nani anakula? Kwa idhini ya nani?

Mheshimiwa Spika, mwisho si kwa umuhimu namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa namna anavyothamini maslahi ya kazi za wasanii kwa kuwa hata alipokuwa anazindua mpango wa Malaria Haikubaliki alizungumza maneno mazito na ya kutia moyo juu ya sanaa ya Tanzania hasa kwa upande wa muziki na filamu. Alitamka mambo mengi pamoja na kifaa ambacho ameletaa na akaahidi kujengwa kwa *center* ya wanasanaa. Je, Wizara na Waziri na Katibu Mkuu hawakusikia hotuba ile? Je, akisema mkubwa si ndio maagizo yamefikia, wapi yote aliyojasema ya kutia moyo wasanii? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru na ninawaombea Waziri Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika, Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera heri huko majimboni kwao ili wananchi wawarudishe na Mheshimiwa Rais awape tena dhamana katika Wizara hii ili mema yote haya mliyoyafanya yaendelee, kwani waswahili husema mnyonge myongeni haki yake mpeni, kazi mmefanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzingatia utamaduni wetu ni muhimu sana. Naomba uhamasishaji wa kudumisha utamaduni wetu hasa desturi nzuri uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana *Twiga Stars* kwa kuonyesha kwa vitendo kuwa wanawake wanaweza kwa kushinda mashindano ya mpira, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana Waheshimiwa, Waziri na Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maendeleo ya vijana ni muhimu sana na hivyo uwezeshaji kwa njia ya mikopo ni muhimu sana.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, tangu enzi za awamu ya tatu mpaka awamu ya sasa, Marais wanasisitiza kulinda Kiwanja vya michezo cha Moshi ambacho kina historia ndefu, *King George The V Memorial Grounds*, badala ya kuendelezwa kama viwanja vya michezo, Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Moshi

imegeuza uwanja huu kuwa soko, sielewi kwa nini Wizara inanyamazia uvamizi huu wakati Manispaa ya Mwanza ilipovamia uwanja wa Nyamagama, Wizara iliingilia na kusimamasha uwanja ule kutumika kama kituo cha uwekezaji.

Naomba Wizara itoe tamko juu ya hatma ya uwanja huu, kwani *Northern Zone* yote toka Tana hadi Arusha hakuna sehemu yoyote yenze nafasi kama hii hapa Moshi. Ni aibu kubwa kunyamazia uharibifu huu wa uwanja wa Moshi, kama Wizara haitatoa tamko kali, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imekwishakigawa hiki kiwanja na kukifanya soko na kiwanja. Kama wakikigawa hiki kiwanja ni wazi *zone* ya Kaskazini haitakaa iwe na kiwanja kinachokidhi masharti ya Kimataifa. Ni aibu kubwa au huu ni mkakati maalum wa kuhujumu maendeleo ya Moshi?

MHE. MATHIAS M.CHIKAWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba kuchangia sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni uwezekano wa Wizara kuifanya michezo kuwa ajira kwa vijana. Duniani sasa hivi michezo inalipa sana pengine kuliko sekta yoyote duniani na wachezaji ndiyo matajiri wakubwa kuliko wajasiriamali wowote wale. Wizara iweke mazingira ya kuifanya michezo kuwa ni sekta yenze kutoa utajiri zaidi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pamoja na sera zake zote iweke mazingira ya kufanya sekta ya utamaduni kuwa sekta ya kibashara sasa ni kweli sekta hii inafanyiwa biashara lakini hii haitoshi. Aidha, utamaduni ni roho ya Taifa kwa hiyo, pamoja na sekta hii kuwa ya biashara Wizara ni lazima iwekeze katika sekta hii ili kuona kuwa utamadiuni wetu hauharibiwi na tamaduni zingine za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, habari ni nyenzo muhimu sana kwa ajili ya kujua kinachoendelea katika ulimwengu huu, hakika bila mawasiliano tusingeweza kujua kinachotokea ndani ya jamii zetu na hata nje ya nchi yetu. Habari zimeweza kuchangia sana katika kuwahabarisha wananchi mambo yanayojitokeza, lakini pia kuelimisha jamii. Wizara ya Michezo kwa muda mrefu sana imejikita zaidi katika michezo na habari lakini suala la utamaduni halijapewa msukumo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kuwa nchi nyingi zina vazi la Taifa lakini sisi hatuna hata tunaposhiriki katika hafla mbalimbali imekuwa vigumu kutambua uwepo wa Watanzania kama ilivyo kwa nchi za wenzetu kama Waganda, Ghana, Nigeria, Cote de Voire na kadhalika. Pamoja na uwepo wa makabila mengi bado si sababu ya kutokuwa na vazi la Taifa kwani hata nchi tajwa hapo juu zina makabila mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni afya, ajira na pia kichocheo cha vijana kutokukaa vijiweni na kufanya mambo yasiyo na tija kwao na Taifa kwa ujumla. Ni

jambo la kusikitisha kwamba baadhi ya michezo inapewa kipaumbele huku mingine ikiachwa. Michezo kama *basket ball*, *netball*, ndondi, riadha na kadhalika huku ule wa *soccer* ukipewa makocha. Ni lazima tujue mchezo ni mchezo tu na unakuwa na tija pale unapoboreshw na uwepo wa utashi wa kisiasa. Wote tumeshudhudia jinsi timu ya Taifa (*Taifa Stars*) ilivyofanya vizuri baada ya Serikali kuingilia kati.

Napenda nitoe pongezi kwa timu ya *Twiga Stars* kwa kufika fainali za Kombe la Soka Barani Afrika. Tunaomba Serikali iangalie ni jinsi gani itasadia timu hii ili ishinde na kuleta kombe jambo ambalo litaitangaza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja vya michezo, michezo haiwezi kuchezwa kama hakuna viwanja, viwanja ndio sehemu pekee ya wanamichezo kuchezza au kufanya mazoezi yao. Ni jambo la kusikitisha kuona viwanja vikibadilishwa matumizi yake na kuwa soko kama uwanja wa *Moshi Memorium* lakini wote tunajua kuwa wanamichezo lazima wapikwe toka utotoni yaani katika shule za msingi kwa sasa hasa baada ya MMEM ambapo shule nyingi zimepanuliwa kwa kujegwa shule ya pili katika eneo moja, hali hii imepelekea maeneo ya viwanja vya michezo kuwa sehemu ya ujenzi wa shule mpya, kwa mantiki hii hatutaweza kupata vijana waliojengwa vyema ili wanapokuwa vijana wawe wameiva vizuri, tunaomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu wahakikishe viwanja vinatengwa kwa ajili ya watoto wetu wa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa habari tunaomba wanahabari wetu watoe habari bila upendeleo na wasome ili tasnia hii iweze kusaidia jamii yetu.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji na watumishi wote katika Wizara hii kwa hatua nzuri waliyofikisha Taifa katika Michezo, Habari na Utamaduni. Hotuba ni nzuri na kwa kiwango kikubwa inatia matumaini makubwa katika sekta zote tatu za Michezo, Habari na Utamaduni. Hongera sana katika kipindi hiki chote Waheshimiwa Mawaziri na watumishi katika Wizara hii wamekuwa wakifanya kazi kwa ushirikiano mkubwa! Matunda ya ushirikiano huo ndiyo ya mafanikio tunayoyaona. Hongera sana kutokana na ushirikiano mkubwa unaoleta manufaa haya makubwaa kwa Taifa na nawaombea kheri Waheshimiwa Mawaziri hawa ili kila mmoja wao ashinde katika uchaguzi ujao katika Majimbo yao ili warudi Bungeni humu na hatimaye Mheshimiwa Rais awarejeshe katika nyadhifa zao na kuwawezesha kuungana na watumishi katika Wizara hii, ninaamini kuwa mafanikio yafuatayo yataboreshw na kuongezeka kwa mafanikio haya ni kwanza viwango vya michezo vikiongozwa na michezo ya mipira wa miguu kwa wanaume na wanawake kuendelea kuwa bora.

Pili, usikivu wa redio na televisheni kuendelea kuwa bora na kuyafikia maeneo ambayo kwa miaka mingi ya nyuma yalikuwa hayajawahi kufikiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa ushirikiano huu ukiendelezwu utazidi kuleta mafanikio zaidi kwa Taifa letu, ndiyo maana naombea walioonesha

mshikamano mzuri katika miaka mitano hii inayomalizika waweze kuvuka kwa pamoja kuingia tena kwa pamoja katika kipindi kingine tena cha miaka mitano mingine. *Inshaalah.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu huo ninayo machache ya kuchangia, kwanza ni kuhusu lugha ya Kiswahili. Lugha hii ni tunu kwetu Watanzania, hatuna budi kuilea na kuikuza. Ni vyema Watanzania wakahamasishwa kutumia lugha ya Kiswahili tena sanifu katika vikao vyetu na katika mazungumzo ya kawaida, yapo maneno ambayo kwa mawazo yangu yangezuiliwa kutumika ni maneno ambayo vitendo vyake yana maana yake lakini yanapotumika yanaashiria kuwepo jambo au tendo lisilokatazwa hata kama tendo hili halikubaliki, yapo maneno mengi lakini kwa leo ningependa kuhoji matumizi ya neno kuchakachua ambalo matumizi yake yanazidi kuimarika! Maswali yangu ni nini hasa maana ya kuchakachua? Je, linapotumika kwa mafuta maana yake ni nini kwa nini tendo hilo litumiwapo kwa mafuta kwa nini Serikali itumie neno hilo kama tendo linalokubalika badala ya kusema uchafuaji wa mafuta kwa kuwa tendo la kuchafua halikubaliki? Kwa nini neno kuchakachua litumike (huku likificha tendo lisilokubalika) badala ya kuchafua? Ni vyema maneno mapya kwa matendo yasiyokubalika yanapoanza kuibuka na kutumika Serikali ijitokeze mapema kukemea badala ya matumizi yake yakaruhusiwa kuendelea kuenea nchi nzima huku yakiashiria kuhalalisha kitendo hicho huku maana ya neno kupoa polepole likihamisha maana au mantiki kutoka hisia za hasi kuwa chanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza Serikali kwa kuendelea kuutumia vizuri uwanja wetu mpya wa michezo kwa kuitangaza na kuitangaza nchi yetu. Aidha, ningetamani kufahamishwa hasa misingi ya utamaduni wetu ili hata tukiwa nje ya mipaka ya nchi yetu tujitambulisse kwa mambo mengi zaidi, lugha pekee yake naona tujipanue zaidi na mavazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Televisheni ya Taifa chonde chonde yakamilishwe yanafedhehesha. *TBC* iwezeshwe ili iyakamilishe yanatoa picha mbaya kwa Rais wa Awamu wa Pili aliyoyawekea jiwe la msingi ni aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo mbalimbali izidi kuimarishwa na mwisho sheria za habari ziletwe haraka Bungeni na elimu izidi kutolewa kwa vyombo vyaa habari na waandishi wa habari kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DR. BATILDA S. BURIAN: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika, pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera kwa hotuba nzuri lakini zaidi kwa kazi nzuri sana ambayo wanafanya kwa kushirikiana na timu yao ya wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mapendekezo katika maeneo machache kama ifuatavyo kwanza, Wizara iangalie jinsi ya kuboresha michezo mikoani na wilayani na ni vizuri tukaimarisha michezo kulingana na vipaji vinavyopatikana katika maeneo

mbalimbali. Kwa mfano Arusha na Manyara, tuna kipaji cha kukimbia (riadha) hivyo ni vizuri tukawa na chuo maalum cha mafunzo ili kukuza vipaji hivi, wenzetu wa nchi jirani za Kenya na Ethiopia wanafanikiwa kwa sababu ya mkazo mkubwa na uwekezaji katika mchezo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuipongeza timu ya *Mount Meru Worriers* ya Mkoa wa Arusha kwa kufanya vizuri katika Kombe la *Vodacom*. Hata hivyo mafanikio yataongezeka ikiwa shule za michezo ya mpira wa miguu zitaimarishwa. Tatu, Wizara iangarie jinsi ya kuwasaidia waandishi na wanahabari kupitia semina na warsha mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanapenda michezo na michezo ni ajira hivyo Wizara isaidie katika kuimarisha makampuni binafsi kusaidia michezo mikoani na siyo kwa timu mbili za Yanga na Simba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa na utamaduni zinachangia ajira na zinaweza kuongeza fursa kubwa ya kuongeza mapato Kimkoo na Kitaifa. Hivyo Wizara itusaidie mkoa wa Arusha na Jimbo la Arusha ili tuweze kuanzisha Tamasha la Kimataifa la Utamaduni ili tupate watalii watakaokuja kushiriki kwenye tamasha kama wanavyofanya wenzetu wa Zanzibar kupitia Tamasha la Sauti za Busara au wanavyofanya wenzetu wa Brazil au Jamaica kupitia *festivals* za *carnivals*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Alhaj Juma Kapuya, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga na timu ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mapendekezo machache kama ifuatavyo:-

(1) Ni ukweli uliowazi kuwa vijana ni zaidi ya asilimia 60% ya wananchi wote hivyo ni budi kuweka mikakati ya dhati ya kuimarisha vituo vyta kuratibu ajira Mikoani ili kurahisisha taarifa na upatikanaji wa ajira.

(2) Aidha, Wizara kwa kushirikiana na VETA iendelee kubuni maeneo ya mafunzo na stadi za maisha ili kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kulingana na mahitaji ya soko.

(3) Ni vizuri maeneo ya kufanya biashara kama vile "*Machinga Complex*" zikaanzishwa Mikoani ili kuwawezesha vijana walio katika sekta isiyo rasmi kufanya biashara zao katika maeneo yanayotambulika na ambapo hawatapata bughudha.

(4) Mikopo ya vijana iimarishe na kuboreshwa ili vijana wengi zaidi waweze kufaidika na mikopo hiyo.

(5) Vijana wengi wa Arusha Mjini wanategemea shughuli za madini, pamoja na utalii na biashara zingine ndogo ndogo kama vile biashara ya mitumba. Hivyo, Wizara iangarie jinsi ya kuwaendeleza vijana hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kuipongeza Wizara na kuunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi iliyotajwa, sijasikia mradi unaotarajiwa kufanyika katika bajeti ya 2010/2011, ya *NSSF* Kigoma. Serikali haijataja mradi utakaofadhiliwa na *NSSF* wa ujenzi wa stendi ya basi ya Kimataifa ya Mwandiga (*Mwandiga International Bus Stand and Motel*). Nadhani itakuwa imesahaulika. Naomba wakati Mheshimiwa Waziri akijibu atueleze kama mradi huo umo au umefutwa au umesahaulika na kama umefutwa kwa nini? Mradi huo ni wa Kigoma eneo la Mwandiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu, wakati wa Mkutano wa Kumi na Nane (18), Serikali ikijibu swalı langu la Mabilioni ya JK, nilitaka Serikali itoe taarifa kamili kuhusu vikundi na mtu mmoja mmoja aliyepata fedha hizo baada ya malalamiko ya wananchi na Wabunge humu Bungeni kuwa fedha hizo hazikuwafikia wananchi. Serikali kupitia Naibu Waziri wa Kazi, aliahidi kuleta taarifa hiyo kabla ya Bunge hili la Tisa halijaisha lakini mpaka sasa hakuna taarifa hiyo. Ni lini taarifa hiyo italetwa ili kutimiza ahadi hiyo iliyotolewa Bungeni? Inayoonekana kwenye hotuba yenu ni Wilaya si *SACCOs* na mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ndiyo maisha, bila ajira iliyorrasmi na isiyo rasmi hakuna kipato, hivyo maisha yanakuwa magumu zaidi. Naomba Serikali itueleze imejipangaje kuhakikisha kuwa wananchi wenyewe ulemavu hasa vijana walioelimika mfano wasioona na kusikia, wasioona, wasiosikia na wenyewe ulemavu wa viungo vingine wanapata ajira? Maana wanapata elimu lakini baada ya hapo hawana pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo nchi yetu imekuwa na kasumba ya kuwanyima vijana ajira kwa kuweka kigezo cha uzoefu wa miaka mitatu hadi mitano. Je, kijana atapataje ajira kwa kuweka kigezo hicho? Huo uzoefu ataupataje ikiwa hakupewa nafasi ili apate huo uzoefu? Jambo hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa kuwa haina ajira za kutosha, iwawezeshe vijana mfano '*graduate*' wa taaluma mbalimbali wajunge pamoja mfano Wanasheria wajunge pamoja kama watano au kumi ili wapatiwe mkopo wa kufungua '*Law Firm*' yao ili wafanye kazi ya kutoa huduma kwa kujiajiri wenyewe, vivyo hivyo na kwa taaluma zingine. Hii itaongeza ajira kwa kiwango kikubwa na itapunguza "*frustration*" za vijana walio-*graduate* bila kuwasahau wenyewe Ufundı, Diploma, Certificate na kada mbalimbali.

Mheshiniwa Naibu Spika, Shirika la *NSSF*, ni Shirika muhimu sana kama yalivyo mashirika mengine ya Hifadhi ya Jamii. *NSSF* imekuwa mstari wa mbele kukopesha Serikali ili kujenga/kutekeleza miradi mbalimbali. Inasikitisha kuwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Serikali haijasaini mkataba wa ujenzi, ni lini mkataba utasainiwa na lini Serikali itatoa dhamana?

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo Serikali haina tabia ya kurejesha pesa inazokopa *NSSF* na inasahau kuwa hizo ni pesa za wafanyakazi wa Tanzania wakistaafu inabidi walipwe mafao yao. Je, Shirika likifa lawana ziende wapi? Kumekuwa na uwekezaji usio na tija wa takriban Shs.62,789,093,299/= kwa mchanganuo ufuata:- Fedha zilizotolewa na *NSSF* kwa *Tanzania Oxygen Ltd.* shilingi 13,200,000/=, *Tanzania Housing Bank* shilingi 496,289,000/=, *First Adili Bank Corp. Ltd.* Ilipewa mkopo wenye utata wa shilingi 3,152,624,742.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni zingine *NSSF* imewekeza bila kupata gawio kwa kipindi chote ni *CDC Mbeya Cement*, shilingi 1,152,024,742, *Ubungo Plaza* shilingi 9,817,038,702/=, *TANRE Share*, shilingi 1,006,000,000/=, *HEP2 Quality Group Share*, shilingi 47,156,025,113/= na *PPL Pension Properties*, shilingi 3,500,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano hii ni michache inayoashiria udhaifu mkubwa katika upangaji wa miradi na uwekezaji wa *NSSF* na kwamba suala hilo lichukuliwe kwa uzito maalum ili kunusuru fedha za wanachama.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na kuunga hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuhusu Sheria ya Hakimiliki na na Hakishiriki iongezewe wakati. Jasho la urasamu ni jingi lakini kipato ni kidogo. Wezi wa kazi zao ndio wanaoneemeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya Kiswahili sasa iwe lugha rasmi ya kufundishia vyuo vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, watangazaji wazingatie weledi hasa katika kujua elimu ya dunia na kuwa na uhakika na wanachokisema. Wengi wameishia darasa la saba la zamani au *form four* ya sasa. Wengine wanashindwa hata mahojiano ya kawaida tu ya kiingereza hasa kwenye luninga.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* iboreshwe hasa majengo yake yaimarishwe ili kuleta hadhi ya taasisi hiyo. Nawapongeza *TBC* kwa kuwa makini katika vingi vya vipindi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa *BASATA* hasa wale waandamizi wahamishwe au wasomeshwe zaidi maana mawazo yao yamevia hivyo kushindwa kuleta mageuzi kwenye baraza. Nawasilisha.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba kuchangia ni kuhusu michezo shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 1960 – 1970 michezo iliitikiwa sana shulenii, lakini sasa hivi michezo haifanyiki. Michezo iliawezesha watoto pia kupunguza utoro,

kwa vile mwanafunzi mwingine huwa anaenda shule kwa kupendelea jambo fulani. Wengine walienda shule kwa vile alipenda mpira au kukiimbia au kuruka juu au chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo haifundishwi sana shulen na baadhi ya viwanja vya michezo vimeuzwa na kujengwa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni afya, michezo ni ajira, tutawapoteza wanamichezo wenyi vipaji iwapo michezo shulen itadorora. Bado narudia tena hivi Serikali inawapa tuzo gani wachezji wetu waliowakilisha nchi miaka ya 1960 kama Hemed Seif, Mweri Simba, Omar Zimbwe, Gibson Sembuli, Abdallah Kibadeni, Sharifa wa *TPC* ingawa wengine ni marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna waimbaji wa muziki wa dansi au taarab kama vile Shakila Said, Asmahan, John Kijiko, Mbaraka Mwinshehe na wengine ingawa wengine wamefariki, je, familia zao zinanufaika vipi na nyimbo zinazoendelea kupigwa kama vile wanavyonufaika watoto wa Bob Marley au Michael Jackson na wengine wa nchi za nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na mwaandishi mzuri wa vitabu na bado vitabu hivyo vinaendelea kutumika. Je, familia au watoto wa mwandishi huyo Shaaban Robert wanifuafaika vipi na machapisho ya baba au babu yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza timu ya *Twiga Stars* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wanawake wanaweza wapewe nafasi.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa George Mkuchika, Naibu Waziri na wataalam wao kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote linatambuliwa kwa mambo ya msingi kama vile mavazi, lugha, vyakula, ngoma na kadhalika. Inavyoonekana sisi tumeanza kupoteza Utaifa wetu kwa mambo mengi ikiwemo mavazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya magazeti na hasa ya udaku yanaandika mambo na kuonyesha picha za hovyo zikiwemo picha za ngono na kuandika mambo ya watu binafsi. Serikali imeachia uhuru huo kwa baadhi ya vyombo vya habari. Aidha, matangazo yanayopotosha umma hayakemewi ipasavyo mfano ni tangazo la uongo la ujenzi wa nyumba za walimu 22,100 na kwamba zimejengwa 322. Kwa nini Serikali imeshindwa kuleta sheria ya vyombo vya habari Bungeni?

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja hizi kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na Naibu Mawaziri wao, pamoja na watendaji wote wa Wizara hizi kwa namna wanavyojitahidi kutekeleza kwa kusimamia majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana ni jambo la msingi na zinahitaji kusimamiwa kwa umakini mkubwa kwani hata hayo mabilioni ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete hayakuwasaidia ipasavyo walengwa. Kwanza fedha hii ilitegemewa kusaidia vijana ambao wangejiajiri wenyewe binafsi. Lakini taaluma hasa ilikuwa itolewe kwanza kwani inaonekana Watanzania wengi hawana elimu ya kutosha ya kujiajiri wenyewe. Hivyo hata wakipewa fedha za mkopo hawajui namna ya kujiendeleza na matokeo yake ajira zinaendelea kutoweka kwani walengwa huishia kutaifishiwa mali zao kwa kushindwa kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya wasanii wanaelimisha jamii lakini wakati mwengine wanapotosha jamii kutegemea sanaa ama igizo lenyewe ama namna wanavyotoa maonesho yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maigizo mengine yanayooneshwaa kwenye luninga hayafai kwa jamii yetu ya Watanzania kwani maigizo hayo yanatoa mafundisho mabaya kwa vijana wetu wadogo kwani huiga mambo mabaya na hatimaye jamii kupotoka. Naiomba Serikali kuwaomba wasanii wetu pamoja na vyombo vyaa habari kuchuja filamu ama maigizo kabla ya kuoneshwa ama kutolewa hadharani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari kwa namna anavyojitahidi kuhakikisha kwamba taaluma ya wapigakura inawafikia Watanzania popote walipo, lakini bado juhud zaidi inahitajika ili elimu ya wapigakura inawafikie wote hasa wakati huu kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kuwasihii wasanii wetu kuvaav mavazi ya heshima wakati wakiendesha sanaa zao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua leo tuna Wizara mbili na Wizara zenyewe zinavutia. Kwa hiyo, naona sasa niliokuwa nao kwenye orodha nimewaacha tu wale waliokwishachangia zaidi ya mara tatu, kama wawili hivi ama watatu. Kwa hiyo, nitaanza kumwitaa sasa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ana dakika kumi na tano, halafu nitamwitaa Waziri mhusika. Halafu tunaingia kwenye Kamati ya Matumizi, tukishapitisha tunakuja Naibu Waziri wa Wizara inayofuata na Waziri wake, tunaingia tena Kamati ya Matumizi. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuendelea kunipa uhai na afya njema na hivyo kuniwezesha leo hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikupongeze wewe pamoja na Spika, kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya kwa kuendesha Bunge letu kwa ufanisi na kwa viwango wewe pamoja na wenyeviti. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitapongeza timu yangu ya *Bunge Sports Club* pamoja na wanamichezo wa *Bunge Sports Club* kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana kwa miaka mitano kuweka hadhi ya

taasisi hii kwa kuwa washindi na mabingwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mabunge yote, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi aliyoifanya katika kuongoza nchi yetu na kwa amani na utulivu. Aidha, namshukuru kwa imani aliyonayo kwangu kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kipindi hiki cha miaka mtano cha awamu ya nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kazi nzuri aliyoifanya na ushirikiano mzuri katika kuongoza nchi yetu. Vilevile napenda kumpongeza Waziri wangu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika kwa ushirikiano mzuri sana na imani yake kwangu katika kumsaidia kazi ya kuendesha Wizara hii. Kimsingi najivunia sana kufanya kazi naye. (*Makofi*)

Napenda pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Seth Kamuhanda, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri waliota katika utendaji wetu wa kazi za kila siku. Navipongeza vyombo vya habari, radio, televisheni na magazeti kwa kuwapa habari, elimu na burudani wananchi wetu. Pia napenda niwapongeze wafadhili wote ambao wamesaidia michezo mbalimbali katika nchi yetu. Pongezi maalum ziende kwa *TBC*, chombo chetu cha Taifa kwa utangazaji mzuri na mahiri ambao wameuonyesha katika Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Mjini kwa imani yao kwangu kwa ushirikiano wanaonyesha katika kutekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi kwa mwaka 2005/2010 yako mengi yamefanyika tena kwa ufanisi mkubwa na maendeleo makubwa. Nawapenda na naomba waendelee kujenga imani kwangu maana uwezo bado ninao na nawaomba wasiniangushe katika uchaguzi huu ujao wakitaka maendeleo basi chaguo ni Bendera, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kumpongeza mke wangu Flora na watoto wangu Herbert, Yasin na Gloria kwa kunivumilia wakati wote nilipokuwa katika kazi nyingi za kutekeleza majukumu yangu nikiwa Naibu Waziri na Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya utangulizi huo napenda kuchangia hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa napenda kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Aidha, kwa sababu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi mno kwa kuzingatia muda niliopewa wa dakika kumi na tano hatutoweza kuzijibu zote lakini tutahakikisha kwamba baadhi ya hoja na baada ya hoja zote hizo tutawaandikia kwa maandishi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzipata. (*Makofi*)

Hoja zenyewe ni kama ifuatavyo na nitaanza na Kamati yetu ya Bunge ambayo leo amesoma Makamu Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hoja ambayo ameizungumzia kwanza ni ukaguzi wa matumizi ya uwanja wa Taifa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Nataka kumhakikishia kwamba ushauri huo tumeupokea na shughuli hiyo inaendelea kufanyika kila wakati mechii zinapochezwa. (*Makofi*)

Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kuhusiana na suala zima la michezo imezungumzia suala zima la makocha wa kizalendo kwamba watumike katika nchi yetu badala ya kutegemea makocha kutoka nje. Ushauri huo tumeupokea na tunaufanya kazi, napenda pia kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kunipongeza mimi pamoja na Marehemu Ndugu Paul West Gwivaha, kwa kuipeleka timu ya Taifa mwaka 1980 huko Lagos kwenye finali za *Africa Cup of Nations*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa mikakati endelevu, inayoendelea na ya kudumu kwa michezo ya vijana suala hili limezungumzwa na Wabunge wengi na ningependa niwataje kwa sababu wamezungumzia masuala ya shule za msingi, wamezungumzia shule za sekondari, wamezungumzia vipaji na Wabunge ambao wamezungumzia masuala haya ni Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa Nuru Bafadhili. Hawa wote wamezungumzia suala zima la vipaji katika kuwatambua vijana wetu ili waweze kufanya vizuri kuanzia ngazi ya utoto. Nataka kusema kwamba ushauri huo tumeupokea na tunaufanya kazi na kama wanavyofanya sasa hivi hata mashindano ya *Copa Cocacola* ni mashindano ambayo yanafanya ni kuzingatia hilo. *TFF* inafanya kazi nzuri kwenye hilo.

Suala lingine ambalo limezungumziwa na Mheshimiwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ni ukosefu ni ufinyu wa Bajeti, hilo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na ni kweli Wizara yetu ina Bajeti ndogo, lakini jibu ni kwamba hali ikitiruhusu Bajeti itaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya mashindano hayo. (*Makofi*)

Suala lingine ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni migogoro ya mara kwa mara ndani ya vyama vya michezo pamoja na vilabu vyetu, lakini nataka kuwahakishia kwamba hivi sasa migogoro imepungua sana kiasi kikubwa na jitihada zinaendelea kuimarisha utawala bora katika sekta ya michezo. Liko suala ambalo limezungumziwa na Kambi ya Upinzani kwamba Serikali iangalie upya, uendeshaji wa Chama cha Riadha, hilo ni kwamba na sisi tumeliona ni tatizo, Serikali tunasema kwamba tunaendelea kulishughulikia. (*Makofi*)

Lipo suala ambalo limezungumziwa na Kambi ya Upinzani, lakini limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao ni kuhusu viwanja vya michezo nchini, limezungumzwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani lakini limezungumzwa na Wabunge wafuatao, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Diana

Chilolo na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, wote hawa wamezungumzia suala zima la matatizo ya viwanja katika maeneo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba sisi hilo tumelipokea, suala la viwanja ni muhimu na wote mnafahamu mchezo wowote bila kiwanja huwezi ukacheza. Sheria namba moja duniani kwa michezo yote ni kiwanja na hili ni tatizo sugu katika nchi yetu, tunakubaliana na ninyi, lakini nataka niwahakikishie kwamba tumejaribu kutoa ushauri kwenye Halmashauri zetu za Mitaa, za Miji na Vijiji kwamba wajitahidi sasa kuimarisha ujenzi wa viwanja ili angalau kuwe na sehemu za kuchezewa. Si hilo tu limezungumziwa suala la viwanja vinavyomilikiwa na CCM amelizungumza Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, tumeliona hapa kwamba viwanja vya CCM vikabidhiwe Serikalini, viwanja hivyo ni mali ya CCM na ni hiyari yao kuvikabidhi hivyo viwanja Serikalini au kuacha kwa sababu ndiyo wenye hatimiliki. (*Makofî*)

Suala lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi sasa nipongezi za *Twiga Stars*. Ningependa niwataje wale wote ambao wametoa pongezi kwa *Twiga Stars*, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Susan Lyimo. (*Makofî*)

Sisi tumepokea pongezi hizo, lakini pongezi nyingine zimekwenda kwa *Taifa Stars* na Maximo, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Omar Ali Mzee na Mheshimiwa Lucas Selelii. Nataka niseme tu hapa na sisi pia kama Serikali tumeliona hilo tumempongeza Maximo, tumefanya *party* kubwa kwa sababu amefanya kazi nzuri katika nchi hii. Ameifikisha *Taifa Stars* mahali ambapo sasa timu yetu inajulikana duniani, kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli tumelipongeza sana. (*Makofî*)

Suala lingine ambalo limechangiwa sana ni suala zima la sheria ya michezo ihuishwe, hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, tunasema kwamba hilo suala sisi tumelipokea na sheria ya BMT inahuishwa kwa sera ya maendeleo ya michezo kazi inayoendelea hivi sasa ni kuhuisha sasa sheria yetu ya BMT kwa sababu ilitengenezwa mwaka 1971 na napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi kwa sababu yeze wakati alipokuwa Waziri wa Michezo mwaka 1995 yeze ndiyo ameandaa sera akishirikiana na wataalamu wa Wizara ya Maendeleo ya Michezo nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine limezungumzwa na wengi Ndugu Idd Azzan linalohusiana na mechii ya Brazil kwamba kulikuwa na dosari, ni kweli dosari hiyo ilitokana na matatizo ya teknolojia, kasoro hizi zimefanyiwa kazi ili zisijitokeze tena siku zitajazo, aidha, tunaomba radhi, kwa usumbufu wowote uliojitokeza kwa watu wote ambao waliingia pale uwanjani. *TFF* itachukua hatua ili mambo yaende vizuri na suala kwamba timu yetu haikufanya vizuri *CHAN*, hilo linafanyiwa kazi na *TFF* ili timu iweze kufanya vizuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala mengine ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge ni masuala yanayohusiana na michezo mingine kupewa kipaumbele, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Khadija, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, wamezungumzia michezo mingine ipewe kipaumbele. Hilo tumelipa kipaumbele sana na tunalifanyia kazi ili michezo yote ipate huduma sawa na michezo mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala ambalo limezungumziwa sana na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo la kiwanja chake cha *King George Memorial* pale Moshi. Serikali imekwishaeleza kuwasilisha hoja hiyo kwa Madiwani wa Manispaa ya Moshi ili ishughulikiwe lakini napenda nisisitize kwamba suala hilo na si kwa Moshi tu kwa maeneo mengine masuala ya viwanja vya michezo na *open space*, naomba mamlaka husika katika maeneo basi waheshimu maagizo ya wakubwa kwa sababu ni tatizo linalotia aibu sana. *Open spaces* zote zimejengwa ama vimefanyiwa vitu vingine tunasisitiza kwamba bila kuwa na viwanja, watoto watakosa mahali pa kucheza na hili ni suala ambalo lazima tulipe uzito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Diana Chilolo, amezungumzia Serikali isadie kukamilisha ujenzi wa uwanja wa Nafua, Wizara imetoa ushauri na tunaomba Halmashauri ya pale iendelee kujenga kiwanja hiki kwa sababu ni muhimu na sisi tunatilia uzito.

Suala lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Susan Lyimo amezungumzia pia pongezi kwa *Taifa Stars* na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wametoa pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza michezo, hizo pongezi tumezichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala amezungumzia kujua jinsi gani wachezaji wa zamani walioilettea sifa nchi mwaka 1980 wanaenziwa, ushauri umepokelewa tutajitahidi kazi na hata hivyo sasa majina ya wachezaji hao yamewekwa katika kumbukumbu ya Taifa, hicho kwanza ni kitu kikubwa tulishawafanyia *party* kubwa sana wachezaji wote. Aidha, baadhi ya wachezaji hao tunawatumia kuwa makocha au washauri au makamisaa, na wajumbe wa Kamati mbalimbali za *TFF*, lakini wazo lako tunalifanyia kazi la kuweka bango pale ambapo itawezekana basi tutajitahidi ili tuweze kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa nimeshazungumzia suala lake la viwanja kwamba tunamshukuru sana. Mheshimiwa Bujiku Sakila, tumeshamzungumzia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee Mbunge wa Kiswani, timu ya Taifa kutokufanya vizuri katika mashindano ya kKimataifa kutokana na kukosekana na mpango wa kuwa na timu za vijana, ushauri umepokelewa na unafanyiwa kazi, aidha, michezo ya mpira mguu na taratibu mbalimbali zinafanywa ili tuwe na *academias* mbalimbali katika maeneo mbalimbali. Tunashawishi watu binafsi na tunashawishi pia watu wenye uwezo wajenge vituo vya michezo ili angalau vipaji vianze kuibuliwa kutoka katika vituo hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba tutajitahidi kushawishi watu wengi kama wenzetu wa nchi mbalimbali wanavyofanya wenye uwezo wa kifedha watusaidie kujenga vituo hivi ili viweze kusaidia.

Mheshimiwa Bahati Ali Abeid amezungumzia tuenzi wanamichezo wetu, hilo nimeshalizungumzia na Mheshimiwa Mathias Chikawe amezungumza Wizara iangalie uwezekano wa kufanya michezo kuwa sekta yenye kutoa utajiri zaidi hapa nchini. Ushauri na maoni tumeupokea na tutaendelea kuufanya kazi, tunakubaliana naye kwa sababu michezo sasa hivi ni ajira tena ni ajira kubwa kweli kweli, kwa hiyo, na sisi lazima tujipange, tuone namna gani tunaweza tukafanya michezo ni sehemu kubwa ya ajira katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Savelina Mwijage amezungumzia Wizara itasaidiaje vifaa vya michezo kwa shule za walemvu Bukoba, Ngeza Mseto? Kutokana ufinyu wa Bajeti si rahisi kusaidia vifaa vya michezo kwa sasa lakini hata hivyo tunachukua ushauri wake na tutashauriana na wafadhili mbalimbali ili tuone namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema muda hautoshi, lakini napenda nichukue nafasi hii kusema naunga mkono hoja, lakini nataka nimtambue Mheshimiwa Martha Mlata kwamba naye alitoa pongezi kwa *Twiga Star*. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wachangiaji wamekuwa wengi, muda wa kujibu hizi hoja umekuwa mfupi, nimepewa dakika 25 kwa hivyo nitakachofanya kwanza kuwatambua waliochangia. Pili kufafanua yale maeneo ambayo yamerudiwa rudiwa sana ambayo Wabunge wametaka majibu na yale ambayo kama muda hautaturuhusu tutatoa majibu kwa maswali yote ambayo tumeulizwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Muda wa kuwataja wachangiaji hatutahesabu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Haupo?

NAIBU SPIKA: Hatuhesabu huo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Kwa hiyo ruksa.

NAIBU SPIKA: Wataje tu lakini hatuhesabu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Nimewataja, nimewaandika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba wachangiaji wengi wametoa pongezi kwa Wizara yetu kwamba tumepata mafanikio katika maeneo mbalimbali, upande wa *TBC* imepongezwa, vyombo vya habari vimeongezeka viko vingi tumepongezwa, upande wa shughuli za michezo hali kadhalika na upande wa shughuli za utamaduni. Napenda pia tupokee pongezi rasmi za Mkoa wa Singida na Mkoa wa Rukwa

ambao walikuwa hawasikii *TBC* wala hawaoni televishen ya *TBC*, lakini kutokana hatua zilizochukuliwa na Wizara sasa wanapata huduma hiyo muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua wachangiaji wafuatao ambao wamechangia kwa kuzungumza humu ndani katika hotuba ya Wizara yetu kama ifuatavyo, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. (*Makofi*)

Napenda pia kutambua Wabunge waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa CCM, akiliwakilisha maoni ya Kamati ambayo sisi tuko chini yake na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi alichangia kwa kuongea humu ndani akiwakilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi tena ni Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa CCM, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassmy, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mlata, tena kwa maandishi Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Viti Maalum. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba radhi Mheshimiwa Bujiku Sakila kwa sababu hana sifa ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela na Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda nigusie mambo ambayo yamechangiwa katika hotuba yetu, baadhi kama nilivyosema kwa sababu hatuwezi kuyasema yote kutokana na ufinyu wa muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu, jambo la kwanza ambalo limerudiwa sana na ambalo ni la muda mrefu ni kwamba, Serikali itunge sheria ya usimamizi wa vyombo vyahabari. Tumekuwa tukijibu maswali hapa na katika hotuba yangu nimeeleza kwamba kwa upande wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo yale ambayo sisi tunapaswa kufanya tumekwishayafanya. Tumewashirikisha wadau, tumefanya mapendekezo ya Sheria Mpya, imepita ngazi ya Makatibu Wakuu sasa inasubiri kikao cha Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme, nikiwa mmojawapo katika Wajumbe wa Serikali kwa maana ya Baraza la Mawaziri, tunapokaribia kipindi hiki cha uchaguzi tulikuwa na Sheria nyingi za kushughulikia ikiwemo Sheria ya Gharama za Uchaguzi na kadhalika. Kwa hiyo, ilionekana busara tupitishe kwanza zile sheria ambazo lazima ziwe tayari kabla ya uchaguzi na zile nyingine zishughulikiwe mara baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* wapewe hongera kwa kuhama kutokana na teknolojia ya *analogue* kwenda *digital* na imependekezwa *TBC* ipanuke hadi Mikoa mingine. Sikitiko kwamba Serikali kutodhamini *TBC* kupata mkopo, napenda kusema kwamba kama tulivyoeleza kwenye hotuba yetu na kama tulivyokuwa tunajibu maswali mara kwa mara. Serikali imedhamiria kwa kuanzia na redio kwamba Mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar iweze kusikika ndiyo maana tumenunua mitambo ya *FM* imekwishafika na kama tulivyosema mpaka itakapofika mwezi wa tisa watapata kusikia *TBC* katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumzwa suala la lugha ya Kiswahili kwamba, tusiishie kutoa nyaraka na maelekezo bali tuchukue hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba kauli za Serikali zinatekelezwa. Nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba sisi katika Wizara tumejiandaa kauli ile imepelekwa kwa Waziri wa TAMISEMI na yeche amepeleka kwa Halmashauri zote zilizopo chini ya TAMISEMI, tumepeleka kwa Waziri wa Utumishi na yeche pia ameshatoa maagizo kwa Ofisi zote za Serikali kuhakikisha kwamba zinatekelezwa lakini ushauri uliotolewa na Bunge tutaufutilia na tutajitahidi kuhakikisha kwamba maelekezo haya yanatekelezwa ikiwa ni pamoa na kuona kwamba, tunatumia Kiswahili sanifu, saa kumi badala ya masaa kumi, mrabaha badala ya mrahaba na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri kwamba BASATA ipitishe Sheria ya Hatimiliki ili iwe pia chanzo cha mapato kwa Serikali. Sasa hapa nataka nikubali ushauri uliotolewa na baadhi ya wachangiaji. Jambo hili tutalifanyia kazi sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa sababu chombo hiki cha COSOTA kipo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kile ninachotaka kusisitiza ambacho kimeulizwa mara kadhaa wasanii wetu wakongwe wa zamani ambao nyimbo zao mpaka sasa zinatumika wamefaidika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na nchi yetu kwamba inaendeshwa kwa mujibu wa sheria. Sheria zilizokuwepo zamani ukienda kurekodi wimbo Radio Tanzania wakati ule unalipwa, ukishalipwa ile kazi uliyoifanya inakuwa mali ya *Radio Tanzania*. Ndio maana leo ukienda *Radio Tanzania* nyimbo nyingi za zamani wanazo ni kwa sababu walizinunua. Mfano, kuna wimbo aliimba Kungubaya ule unaoashiria kipindi cha wagonjwa: “Wakati umewadnia wa kipindi cha wagonjwa” alilipwa shilingi tano na akaridhika kwa sababu siku zile shilingi tano zilikuwa zinatosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kwamba sisi katika Wizara tutakwenda na wakati. Yale yaliyopita siku zile yalikwenda kwa sheria zilizokuwepo wakati ule, lakini hawa wanaotunga nyimbo au kufanya kazi zao sasa hivi wanashauriwa wazisajili, wawasiliante na *COSOTA* kupata msaada ili wapate Hatimiliki ya kazi walizozifanya. Kwa hiyo, tunakiri kwamba tumepokea ushauri, tutakaa pamoja na wenzetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuona jinsi gani tunatekeleza ushauri wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojitekeza hapa ni Serikali kumiliki vyombo vya habari. Kwamba inamiliiki vyombo, inasajili na inashindana na vyombo vingine. Je, haki itatendeka? Nataka kupitia Bunge lako hapa kueleza kwamba, Serikali ina haki ya kumiliki vyombo vya habari kwa sababu mdau namba mmoja, mtu anayetegemewa na Watanzania milioni 40 kuwahabarisha, kuwaburusha, kuwaelimisha ni Serikali ya Tanzania. Ndiyo maana hapa ndani hata siku moja, si mimi wala Naibu Waziri hatujawahi kujibu swali hapa kwa nini chombo fulani cha mtu binafsi hakipatikani au hakisikiki katika Mkoa wetu. Kwa nini? Ni kwa sababu wale ni wadau, wanashirikiana na Serikali katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba Tanzania sisi siyo kisiwa, yako Mataifa mengi tu duniani ambayo Serikali inamiliiki vyombo vya habari. *Voice of America* inamiliikiwa na Serikali ya Marekani na iko chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. *Voice of Kenya, BBC* na iko mifano mingi sana. Kwa hiyo, ninachotaka kusema inazungumzwa pia kwamba kwa nini tunapeleka fedha kule. Nataka nitoe mfano kwamba, mtoto anapoanza kusimama kabla hajaweza kutembea siku za mwanzo hukamatwa mkono na watu wazima, wanamtembeza akishaweza kutembea mwenyewe unamwacha. Ndio ilivyo kwa shirika letu la *TBC* ambalo bado ni changa. Itakapofika mahali wanajiendesa wenyewe na sisi tunaomba siku moja tufike huko, Serikali itaacha kutoa ruzuku. Lakini ukiacha kutoa ruzuku leo kwa *TBC* utasababisha Watanzania wasihabarishwe, wasiburudishwe, wasielimishwe kwa sababu *TBC* inatoa huduma maeneo mengi na vyombo vilivyobaki havitakidhi mahitaji ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeulizwa tena lini Serikali itafuta sheria kandamizi ya magazeti ya mwaka 1976 ambayo haitoi nafasi kwa wahusika kujitetea? Nataka nirudie maelezo niliyoyatoa, lakini nataka niseme pia kuwa si kweli kama ilivyoolezwa kwamba Serikali sasa hivi kwa sheria ya mwaka 1976 haitoi nafasi kwa wahusika kujitetea. Kila aliyalalamikiwa kwetu tumemwandikia barua ajieleze. Kila yule ambayo tumemng’amuwa sisi kwamba katenda kosa kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1976, ameandikiwa barua

ajieleze. Wamejibu, wengine wanapewa msamaha, wengine wanapewa onyo, wengine wanasimamishwa kwa muda na wengine tumewafuta kabisa na kwa hapa nitumie fursa hii kwamba wale mlioleta hoja kwamba, kwa nini tunaruhusu picha za ngono na kadhalika. Tumefuta magazeti mengi ya aina hiyo na wala hawajalalamika kwa sababu wanajua wametenda makosa. Kwa hiyo, sisi tunaruhusu watu kujieleza baada ya kupata maelezo yao ndiyo tunachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo nataka nirudie ni kwamba, katika uendeshaji wa nchi hauwezi kuwa na *vacuum* kwamba tunaacha kutumia Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 kwa sababu imepitwa na wakati, wakati bado sheria mbadala hajaja. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia sheria iliyopo sasa hivi mpaka siku ile ambapo tutakuwa tumepitisha sheria Bungeni na kumpelekea Mheshimiwa Rais akakakubali mabadiliko yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi sana sheria hiyo itakapokuwa imepita kwa mapendekezo tuliyoyafanya patakuwepo na jambo la kuamua huyu katenda kosa au hakutenda kosa badala ile ya sasa ambayo inasema Waziri mwenye dhamana ya Habari akitosheka kwamba ni lugha ya uchochezi atachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limeulizwa ni kwamba, Serikali hajjawahi kuchukua hatua dhidi ya malalamiko ya baadhi ya Wabunge waliochafuliwa na magazeti. Nataka nieleze kwamba mtu anapoandika habari kwenye magazeti mlalamikaji ruksa kwenda Mahakamani, mlalamikaji ruksa kwenye Baraza la Usuluhisho ambalo ni *Media Council for Tanzania*. Sasa si kweli kwamba hatujawahi kuchukua hatua, tumewahi kuchukua hatua, mmeshuhudia wenyewe tumefunga magazeti, tumefuta magazeti na tumewapa watu maonyo, kwa hiyo tumekuwa tukichukua hatua. Kwa wale Wabunge ambao wamehisni kama hawakutendewa haki tunawashauri kuamua lipi wao wanataka. Ukiwa kwa Waziri wa Habari sisi tutachukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976. Wakienda Mahakamani watakwenda kuhukumiwa na sheria. Kama unataka suluhu unakwenda huko katika *Media Council for Tanzania*. Lakini kwetu sisi Serikali hatuendi *Media Council for Tanzania* kwa sababu si utaratibu Serikali kwenda kulalamika kwenye *NGO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ultakiwa ufanuzi kwamba Habari Leo ilidhalilisha Bunge, malalamiko ya Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Nataka kutoa maelezo kwamba ni kweli nilisimama hapa nikasema Serikali itachukua hatua na Serikali ilichukua hatua. Mhariri alifunga safari kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na barua yake ya kuomba radhi Bunge, akamkabidhi Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Bunge hili aliwapa onyo kwamba wasirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyoulizwa ni kwa nini Mtendaji Mkoo wa Shirika la Magazeti ya Serikali hajateuliwa? Nataka kueleza kwamba, muda wa Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ulikwisha. Kwa hiyo, tuliona ni busara kwanza tupate bodi kwa sababu mnapomtafuta Mtendaji Mkoo mnategemea na mnaomba ushauri wa bodi. Bodi imekwishapatikana kazi ya kumtafuta Mtendaji Mkoo imefanyika, lakini nataka niseme kwamba uteuzi wa Mtendaji Mkoo wa Shirika la Magazeti ya Serikali uko mikononi mwa Rais, sisi tutampokea siku yoyote atakapomteua.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja hapa kwamba Idara ya Habari Maelezo haina kazi. Nataka kusema kwamba, katika Kurugenzi zangu za Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Mkurugenzi wa Habari, Maelezo ana kazi nyingi sana ndiyo tumemwekeea pale Wakurugenzi Wasaidizi watatu. Yeye ni Msemaji wa Serikali, anasajili magazeti, anafuatilia matukio haya ya kila siku kwenye magazeti, anatakiwa kuchukua hatua na kumshauri Waziri juu ya mambo ambayo yamejitokeza katika magazeti ambayo hayaendani na maadili ya nchi yetu. Amekuwa akifanya hivyo na yeye ndio amekuwa mshauri na msaada mkubwa kwangu wa nini tufanye yanapotokea matatizo kama hayo. Lakini uelewe kwamba tuna Gazeti la Serikali linaitwa Nchi Yetu, hilo Gazeti Mhariri wake ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu sisi katika Wizara tumeishauri Serikali kwamba ni vizuri tukarudi utaratibu wa zamani, Maafisa Habari wa Wilaya, Mikoa na Wizara wakawa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kama ilivyokuwa zamani. Kwa siku za nyuma hawa wote niliowataja walikuwa wanafanya kazi chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba Maafisa Utamaduni wanafanya kazi za Uafisa Michezo na Uafisa Vijana. Nataka nikiri kwamba, ni kweli katika kipindi hiki, lakini tatizo limeanzia wapi? Tatizo limeanzia pale tulipofanya zoezi la kupunguza ukubwa wa Serikali, nadhani watalaam wetu kutoka nje wakashauri kwamba hawa waondolewe, kwa hiyo, akaondolewa Afisa Michezo wa Mkoa na pia Afisa Utamaduni wa Mkoa. Sisi katika Wizara tulipoona upungufu huu tumewasiliana na Wizara ya Utumishi, tumewasiliana na TAMISEMI. Utumishi imekubali kwamba kada hiyo irejeshwe kwa kuanzia ngazi ya Mikoa na ngazi ya Wilaya. Baadaye tunakusudia kwamba tukishakuwa tumefundisha wanamichezo wengi na Maafisa Utamaduni tutakwenda mpaka ngazi ya Kata. Kwa hiyo, suala hili tumelifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa hoja alitaka takwimu kwamba je, tunazo Wilaya ngapi na Mikoa ambazo zina Maafisa Utamaduni? Juzi juzi hapa Naibu Waziri Mheshimiwa Bendera alizunguka karibu Mikoa zaidi ya kumi katika kufuatilia suala la uimarishaji na ufu fuaji wa riadha nchini. Asilimia zaidi ya 75 ya Mikoa na Wilaya wamekwishaajiri Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo kutokana na kibali kilichotolewa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo amezungumzia juu ya umuhimu wa vazi la Taifa. Nataka nikiri kwamba kama kuna kitu ambacho sasa hivi Watanzania tunakosa ni vazi la Taifa. Nini kimefanyika? Serikali ilifanya mashindano ya kubaini mitindo gani ya kushona inafaa kuwa vazi la Taifa kwa akina baba na akina mama na washindi wakapatikana. Kazi ile imepelekwa katika Serikali kwa maana ya kikao cha ngazi ya Makatibu Wakuu, nao wametoa ushauri kwamba ni vizuri sisi Tanzania tukaenda katika nchi mbalimbali kuona wenzetu walichukua hatua gani wakapata muafaka wa vazi la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme kwamba katika nchi zingine hawakulazimika kuwa na mjadala au kongamano la vazi la Taifa kwa sababu walichukua nguo zao za asili wakafanya ndiyo vazi la Taifa. Tanzania imekuwa vigumu kwa sababu tuna makabila karibu 127, kila kabila lina mtindo wake, sasa kazi ya kufanya utafiti juu ya ni nguo gani inakubalika kwa wote ndiyo tunaifanya na kama nilivyosema kazi iliyobaki ni kidogo sana ya kwenda katika hayo maeneo ambayo wana nguo za vazi la Taifa. Tutakapokamilisha hiyo nina hakika kabisa na naweza kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, mwaka wa fedha ujao kazi hii tutaimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiwelu ameuliza juu ya suala la haki za wasanii. Nadhani majibu tumekwishayatoa. Waziri alete hatima ya vazi la Taifa, majibu tumekwishayatoa. Kuna hoja ilitoka kwamba Kipindi cha Chereko cha *TBC* kitumike kuelimisha wananchi sheria mbalimbali, siyo sherehe peke yake. Sasa nataka niseme, sisi vyombo vya habari kama alivyoeleza Mheshimiwa Kumchaya vina kazi tatu; kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Hakuna kipindi kinachoweza kuwa mbadala wa mwingine. Sasa kama kipindi hiki cha Chereko kinafurahisha au kuburudisha watu, ni muhimu kikaendelea kuwepo kwa sababu kazi mojawapo ya *TBC* ni kuburudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna haja ya sisi Wizara na *TBC* kukaa pamoja na kuangalia namna gani tunaweza kuongeza vile vipindi vinavyoelimisha jamii, muda mwingi tusiwe tunapiga muziki. Muda wa muziki uwe wa kutosha lakini muda wa kuelimisha na kuhabarisha uwe wa kutosha pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Zungu amewapongeza Waandishi wa *Global Publishers*, wanaandika masuala ya uchunguzi. Tunashukuru kwa pongezi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Martha Mlata, kwanza nataka nimshukuru kwani amekuwa mtetezi mkubwa wa wasanii na kwa kumuona jinsi alivyo na shauku na mambo ya wasanii na anavyowatetea ndiyo maana nikamteua kuwa Mjumbe wa Bodi ya BASATA na nimeambiwa kwamba kule ndani anafanya kazi nzuri. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mlata ameuliza swali hapa kuhusu Nyumba ya Sanaa. Sheria ya nchi yetu inatutaka tusizungumzie mambo yaliyopo Mahakamani. Nyumba ya Sanaa, umiliki wake na uendeshaji wake upo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinaendelea kupitia Sheria ya Kulinda Haki za Wasanii, tumeeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kumchaya alizungumzia umuhimu wa mafunzo kwa waandishi wa habari. Nataka nikushukuru na kukueleza kwamba, sasa hivi tatizo tulilonalo Tanzania ni kuwa, wakati mwengine tunawenza tukakaa tunamlamu mwandishi wa habari aliyeandika habari ile ukadhani ni mwandishi wa habari. Kwa hiyo, tatizo tulilonalo na nadhani hata siku za nyuma niliwahi kulieleza kwamba, wakati kipindi cha utawala wa chama kimoja watu wengi hawakusoma taaluma ya uandishi wa habari kwa sababu vyombo nya habari vilikuwa vichache. Sasa tuliporuhusu watu binafsi kuanzisha vyombo nya habari, wale waliokuwa mahiri katika uandishi wa habari walichukuliwa kwenda kuongoza vyombo nya habari nya watu binafsi ikawa sasa hatuna watu wa kwenda katika shughuli mbalimbali kukusanya habari. Sheria tunayoipendekeza ya usimamizi wa vyombo nya habari inaweka kipengele cha wamiliki wa vyombo nya habari kuchangia mfuko wa elimu kwa ajili ya wanahabari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie Mheshimiwa Anne Killango, Mbunge wa Same Magharibi, Waziri wa Habari atueleze wanaotoa magazeti bure anagharamia nani? Katika sheria tunapoandikisha magazeti yako magazeti mtoaji anasema ya kwangu nayagawa bure na tunayo magazeti bure ambayo yanachapishwa Tanzania hapa na kutolewa bure kwa mfano watu wa utalii na kadhalika. Lakini pia yako magazeti mengine ambayo yanamilikiwa na vyama nya hiari nao pia wanatoa magazeti bure. Lakini niseme hutokea wakati mwengine mtu akanunua magazeti mengi tu akaenda kuyagawa bure kwa shabaha aliyonayo yeye. Kwa hiyo, sitamkataza mtu kugawa magazeti bure kama mtoaji yupo na wapokeaji wapo ili mradi haja ya magazeti ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kusema kwamba, jana tumezindua huduma kwa wateja wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Niliisoma ile hotuba imeandikwa inaweza ikapatikana sikumbuki na sikusema kwamba vyombo nya habari nya Serikali ndiyo nya kuviamini. Maneno hayo sikuyasema na bahati nzuri dada yangu Anne Killango Malecela anakiri kwamba yeye hakuwepo lakini ameambiwa. Sasa huyo aliyekwambia amesema maneno ambayo si ya kweli kwa sababu nina vyombo nya habari ninavyoviheshimu sana nchi hii vinavyomilikiwa na watu binafsi ambavyo havina *disinformation*, vinatoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuyaeleza haya niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Naibu naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 – *Administration and General...Sh. 1,960,430,000/=*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Mpanda, Mheshimiwa Mdee, Mheshimiwa Azzan, Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Dr. Limbu. Tuanze na Mheshimiwa Dr. Limbu sijakuona kwa muda mrefu.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kuuliza swalii moja fupi. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa mgeni rasmi kwenye Tamasha la Bolabo la Wasukuma pale Bujola, Mwanza na alipewa ombi la kufikiria uwezekano wa kukisaidia kituo kile kibajeti na kimiundombinu ili kiweze kudumisha mila na tamaduni za Wasukuma na za Taifa kwa ujumla katika azma nzima ya kuleta mshikamano wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize kwamba nimeangalia katika vitabu vyote sikuona mahali ambako Waziri ametenga fedha kwa ajili ya kukisaidia kituo hicho. Je, Waziri anawenza akanionyesha mahali gani ambapo ametenga na Waziri yuko tayari kwenda kituo cha Bujola ili akaangalie hali halisi na aone jinsi atakavyokisadia kituo hicho kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nuru inakuwaje unapita kati ya msemaji na Mwenyekiti?

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, alinikatisha ulikuwa hunisikii?

MWENYEKITI: Nimekusikia endelea.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuma ujumbe kwenda Bujola kuangalia mahitaji halisi ya kituo kile ili Wizara ione jinsi gani itakisaidia kituo kile. Ahsante.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tamasha la Bolaba ni moja kati ya matamasha ya makabila mbalimbali katika nchi hii. Nakumbuka Mheshimiwa Rais tangu ametoka huko wala mwezi haujapita bado. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Rais angetoa maelekezo tuweke hilo fungu nina uhakika lisingeweza kuwahi mwaka huu. Lakini la msingi ninachotaka kusema, liko tamasha la Wanyamwezi kule Tabora nimealikwa nikawe mgeni rasmi, kuna matamasha ya Makonde na ya Arusha na kila mahali. Kwa sasa hivi uwezo wa Serikali ni kushughulikia matamasha yale ambayo yanaandaliwa na Serikali. Hapo Bunge litakapotuwezesha tukapata fedha za kutosha kusaidia matamasha ya mikoa mbalimbali tutafanya hivyo, lakini kwa sasa hivi kama ulivyoangalia bajeti yetu hatuna mafungu makubwa ya kuweza kusaidia.

La pili, ameuliza kama je, niko tayari kwenda Bujola. Mimi kama Waziri mwenye dhamana ya shughuli za utamaduni pamoja na wastaafu wenzangu katika Wizara tutakuwa tayari kwenda mahali popote tunapoitwa kufanya kazi maana tumekula kiapo cha kufanya kazi hizo.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuuliza swal moja dogo ambalo najua Mheshimiwa Waziri analifahamu vyema sana kuhusu Sherehe za Vita vya Majimaji. Sherehe za Vita vya Majimaji asili yake kubwa vita vile ni Kilwa Kaskazini kwenye Jimbo langu la Kilwa Kaskazini pale Kipatimu na Ndete. Lakini cha ajabu inapotosha inasemekana kwamba sijui imekwenda Songea, Tabora hivi mambo haya mbona hamkanushi? Ahsante sana.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwalimu wa somo la historia. Ni kweli kwamba vita ya Majimaji alianzishwa Kinjeketile Ngwale kule eneo la Kipatimu, pale ndipo ilipoanzia. Lakini vita ile ilienea Kusini yote vikaenda kuishia Songea kule wameweka kumbukumbu sana vita ya Majimaji lakini kule ilikoanzia bado raia au wananchi wa eneo lile hawajachangamka kuweka mnara kama walivyofanya wenzao wa Songea. Kwa hiyo, hakuna kilichopotoshwa ukweli ni kwamba vita imeanzia Kilwa imeishia Songea. Natoa mwito na nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Mpanda na sisi tutashirikiana naye tuwahamasishe wananchi wa Kilwa na wao walichangamkie jambo hili kama walivyochangamkia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nahitaji Mheshimiwa Waziri anipatie ufanuzi wa hoja ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani. Hii ni hoja ambayo imekuwa ikijirudia miaka nenda rudi kuhusiana na suala zima la wanamuziki wa kikazi kipy. Hawa ni vijana amba kwa kiasi kikubwa sana wanaisaidia Serikali katika kutengeneza ile ajira ambazo zisizo rasmi. Lakini cha kusikitisha na kitu ambacho kimejithibitisha hata kwenye hotuba yake hajawazungumzia kabisa. Wakati alipokuwa akijibu maelezo yake alisema kwamba wanafikiria kwenda kukutana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusiana na *COSOTA*. Jibu kama hilo alilitoa Naibu Waziri wake miaka miwili iliyopita baada ya swal la Mheshimiwa Martha Mlata kuuliza kuhusiana na hawa hawa wanamuziki wa kizazi kipy. Sasa ushahidi unaonyesha kwamba wanaibiwa sana na kuna ushahidi unaonyesha kwamba rushwa sana kwenye vyombo vya habari na redio hali inayowapelekea hawa licha ya kwamba wanaauza kazi zao lakini wanaishi maisha magumu kwa sababu kuna wajanja wachache wanaofaidi kupitia mgongo wao.

Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie baada ya kutoa majibu yanayofanana miaka mitano. Sasa hivi mmejiandaaje kuwasaidia kikamilifu wanamuziki wa kizazi kipy ambao wanawasaidia kutengeneza zile ajira milioni moja mnazojivunia. Nashukuru.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Habari ni Waziri wa muziki wa aina zote taarab, kizazi kipy,

muziki wa dansi, ngoma za asili. Katika majibu ya msingi tuliyotoa tumeeleza kwamba tutakaa na Wizara kuangalia uwezekano wa kutunga sheria itakayohakikisha kwamba hao wanamuziki wa aina zote wanapata haki yao hawanyonywi kama ambavyo tumeleza.

Lakini nimesema kwamba la msingi la mwanzo kabla hatujafika huko waanze sasa wanamuziki wa aina zote kujenga tabia ya kusajili kazi zao, maana tukishasajili hata ukimwona mtu anatumia bila kibali kazi yako inakuwa rahisi kumshtaki, inakuwa rahisi kufuutilia. Kwa hiyo, tutatunga sheria itakayohakikisha kwamba wasanii wa aina zote wanatendewa haki.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna ukweli unaosema kwamba kama uongo ukirudiwa rudiwa mara nyingi unakuwa ukweli. Kuna tangazo linalotoka kila siku linalosema “Serikali iliahidi kujenga nyumba 22,000 za walimu”, lakini zimejengwa 320 tu. Kule Rukwa tumejenga nyumba zaidi ya 2,400 sasa hizo 320 inalinganishwa zile za 22,000 zinazosemwa kwamba uongo. Kwa nini Serikali hamkanushi?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna tangazo la Haki Elimu linalopotosha umma kwamba Watanzania wamejenga nyumba 300 tu katika kipindi cha utekelezaji wa mradi wa MMEM. Ukweli ni kwamba zaidi ya nyumba 23,000 zimejengwa katika mpango huu na ujenzi wa nyumba za walimu unaendelea. Tumewapelekea taarifa watu wa Haki Elimu kwamba waache mara moja tangazo hilo na ningependa kupitia kwenye Bunge lako Tukufu kuendelea kuwaamuru watu wa Haki Elimu waache kusema uongo juu ya utekelezaji wa MMEM.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya michezo, nchi hii na leo wakati tunatoa pongezi tumempungeza yeye, tumempungeza Marcio Maximo na wale wote ambao wamehusika sana katika kuinua kiwango cha michezo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ingekuwa vyema na busara kama Wizara hii ingetambua juhudhi hizo za Mheshimiwa Rais ambazo najua imetambua lakini ambacho kingekuwa cha busara zaidi kama vile ambavyo Umoja wa Wabunge wa Kupambana na UKIMWI (*TAPAC*) walivyofanya baada ya kutambua jitihada za Mheshimiwa Rais katika kupambana na UKIMWI waliamua kumpa nishani. Je, Wizara hii inaonaje kama ingetambua juhudhi hizo za Rais kwa kumpa nishani pamoja na kwamba ni Kiongozi wa nchi ambaye ni wajibu wake, lakini wapo Marais ambao walipita pengine hawakufanya kama alivyofanya Mheshimiwa Kikwete. Sasa Wizara inasemaje katika kumtambua Rais kwa kumpa nishani?

MWENYEKITI: Jamani hiyo Wizara ni ya kwake, ajipe nishani mwenyewe. Sasa nyinyi Wabunge tuna taratibu hapa unaweza kutumia azimio mkatengeneza kitu kingine nyinyi wenyewe. Sasa Rais atengeneze nishani ajipe mwenyewe. Mheshimiwa Waziri ningefikiri, mtafute oganaizesheni nyingine, *TAPAC* ilikuwa ni Umoja wa Wabunge Wanaopambana na UKIMWI. Hivyo hivyo hata Bunge hili linaweza kutoa

azimio. Tulishawahi kutoa azimio moja wakati yeye amekuwa Mwenyekiti wa AU yaani *natural* huwezi mwenyewe ukajitengenezea nishani, tena wangemsema tu umejitengenezea hiyo nishani wewe mwenyewe. Sasa ingekuwa haiwezekani. Ama Bunge Social Club ipo tafuteni hiyo taratibu. Tunaendelea.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, naamini wananchi wa Newala watamrudisha ili aje aendeleze hili gurudumu la kuendeleza Wizara hii. Lakini nataka kumwuliza kwa sababu katika kuchangia kwangu nilimwuliza kuhusu suala la maonyesho yanayoendelea kule Sabasaba kwamba kwa sababu yale maonyesho ni kwa ajili ya wafanyabiashara wote na tunaamini kwamba sanaa pia ni biashara na ni ajira. Wasanii walioko pale wamepata shida na wamenyanyaswa. Nilikuwa napenda kujua ni kwa nini? Naomba maelezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo hujalifanya utafiti usilitolee maelezo. Malalamiko hayo nimeyapata nikiwa hapa, ninavyofahamu wamekuwa wakitoa burudani katika miaka ya nyuma. Ninavyofahamu Mbarak Mwinshehe alialikwa Osaka, Japan kwenye maonyesho sasa nini kimesababishwa hao wazuiwe juzi ni jambo ambalo sijalifanya utafiti. Nitawasiliana na Wizara inayohusika na kumpatia Mheshimiwa Martha Mlata majibu sahihi.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze tu Waziri kwa kuomba radhi kwa lile lililotokea Uwanja wa Taifa siku ile. Lakini nina jambo dogo tu, suala la kubadilisha Sera ya Michezo pamoja na ile Sheria ya BMT. Umeizungumza hapa lakini suala ambalo tulianza kulizungumza tangu mwaka 2006 na kila jambo linatakiwa liwe na mwanzo na liwe na mwisho. Sasa je, itachukua muda gani ama hiyo sheria au sera na Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini hasa itakuwa tayari kuliko kuachia jambo linaelea? Sasa ni miaka minne tunazungumza jambo hilo. Nataka kujua ni lini itakuwa iko tayari?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, nataka nikubaliane naye kabisa Sheria ya Baraza la Michezo imepitwa na wakati kama ambavyo amechangia. Tena amechangia kwa kusema na amechangia kwa maandishi. Kuna mabadiliko mengi sana ya michezo katika sera na katika sheria yenye ambayo imetungwa na Baraza la Michezo mwaka 1971. Sasa hivi michezo yote imebadilika sio ya ridhaa tu pamoja na kulipwa. Kwa hiyo, Wizara tumeliona hilo, mchakato unaendelea nataka nimhakikishie kwamba zoezi linamalizika mwaka ujao 2011/2012. Tunaomba utupe muda kwa sababu tuko katika ngazi ya mwisho.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na wa kuzungumza nilizungumzia tahadhari ya alama za *parental guidance* katika tamthilia zinazoonesha ambazo wazazi na vijana hawana tahadhari ya kupewa na

si tu katika suala la kuonesha michezo ya kiutu uzima au hata kuna sinema zingine hazifai kwa watoto wadogo ambazo zinaonesha mauaji mengi sana. Nilitaka kujua Serikali itachukua utaratibu gani wa kufanya sensa katika hizi tamthilia zote zinazooneshwa ziwekewe mwongozo wa kutahadharisha umri wa watazamaji?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Zungu kwamba kwa kweli hali inavyojionesha sasa hivi baadhi ya filamu na baadhi zinaonesha mambo ambayo ni kinyume kabisa na maadili hasa kwa watoto lakini nimekuwa nikijibu swalii hili kila mwaka hapa, kwamba, tunajitahidi Bodi yetu ya Filamu inafanya sensa na Kamati yetu ya maudhui nayo inafanya sensa ili kuondoa yale mambo ambayo ni kinyume cha maadili. Lakini nataka nimhakikishie kwamba kutokana na hali ya utandawazi bado suala hili ni gumu tunaendelea kulifanyia kazi kwa sababu tunalitambua na tunatafuta namna gani ya kuwezesha kuondoa tatizo hili katika nchi. Lakini tukubaliane kwamba ni gumu kutokana na hali ya utandawazi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh 347,114,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh 408,707,000/=
Kif. 1004 - <i>Info, Education and Communication</i>	Sh 202,668,000/=
Kif. 1005 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh 138,535,000/=
Kif. 1006 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh 113,423,000/=
Kif. 6001 - <i>Culture and National Languages</i>	Sh 3,170,690,000/=
Kif. 6004 - <i>Sports Development</i>	Sh 1,925,055,000/=
Kif. 7003 - <i>Information Services</i>	Sh 5,995,198,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	Shs 63,660,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Shs 334,900,000/=
Kif. 6001 - <i>Culture and National Language</i>	Shs 1,716,960,000/=
Kif. 6004 - <i>Sports Development</i>	Shs 1,059,514,000/=
Kif. 7003 - <i>Information Services</i>	Shs 1,307,528,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa taarifa ningependa kuwaomba radhi Wabunge wanne ambao walichangia kwa maandishi dakika za mwisho mwisho. Kwa hiyo, naomba nitambue kwamba wafuatao walichangia kwa maandishi, ambao ni Mheshimiwa Nuru Bafadhir, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Nawaomba radhi lakini kwa maana ya *Hansard* nadhani sasa masuala tumeyaweka sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako tukufu liidhinishe makadirio ya Bajeti hiyo kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari,*
Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa
Fedha 2010/2011 Yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Napenda kuipongeza Wizara, Naibu wake, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri mnayofanya na tunawaombea mrudi tena mkamilishe Sheria ya Habari na mengineyo yaliyozungumzwa hapa na naomba matumizi mazuri ya fedha.

Sasa tunaingia Wizara inayofuata. Ataanza Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye hotuba hii ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na nitangulie kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliendesha vizuri sana Bunge letu. Kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuliongoza

vyema Taifa letu na kwa kuendelea kuniamini katika nafasi yangu ya Unaibu Waziri. Naahidi kuendelea kufanya kazi zangu za kwa bidii, maarifa na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa namna wanavyonisaidia kunilea na kuniongoza katika majukumu yangu katika Wizara hii. Aidha, namshukuru sana mke wangu Florence watoto wetu na wajukuu wetu kwa uvumilivu wao na msaada wao kwangu wakati nikitimiza majukumu yangu ya kikazi na kifamilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Ukonga kwa kuendelea kuniamini na kunisaidia katika kuleta maendeleo makubwa katika Jimbo letu kwa kipindi cha miaka kumi sasa. Msaada wao kwangu umewezesha Jimbo la Ukonga sio tu kuwa Jimbo linalokuwa haraka kwa maendeleo katika sekta zote za miundombinu, elimu, afya, maji, umeme, ujasiriamali na michezo lakini pia tumeweza kupata Majimbo mapya mawili ya uchaguzi ya Ukonga na Segerea. Ninachoweza kuahidi ni kuendelea kuwatumikia kwa bidii zaidi wananchi wa Jimbo langu kwa kadri wananchi watakavyoendelea kuniamini na kunisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ningependa sasa kuchangia kidogo kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kutolea maelezo na ufanuzi baadhi ya hoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge hasa zile zinazohusu Mfuko wa JK, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja mbalimbali ambazo zilitolewa katika nyanja hizi, Mfuko wa JK na zilivyotoa ajira pamoja na sekta ya vijana. Mheshimiwa Zambi alizungumza kwamba fedha hizi za Mfuko wa JK hazirejeshwi na hivyo Benki zinasita kutoa mikopo zaidi. Nataka nimueleze yeye na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa Mujibu wa takwimu zetu wastani wa asilimia 87 zinarudi kutoka kwenye mikopo hii. Kwa hiyo hali si mbaya kiasi hicho. Lakini tunajua kwamba kuna wengine ambao mpaka kwenye asilimia 40 hivi hawarejeshi lakini hawa ni wachache sana. Lakini tutaendelea kuhimiza *SACCOS* na Wajasiriamali waweze kurudisha mikopo. Mheshimiwa Zambi pia alizungumzia kuhusu umuhimu wa kutumia *Pride*, *FINCA* na Asasi zingine za benki kutoa mikopo hii. Tunakubaliana naye na niseme tu kwamba ukiacha *FINCA* lakini *Pride* na Taasisi zingine au Asasi zingine kama 12 zimetumiwa katika awamu ya pili na ukiangalia ukurasa wa 17 wa hotuba yetu utaona hizo Asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Muhonga alizungumzia kwamba tulete taarifa za vikundi na wajasiriamali waliokopa fedha hizi. Nataka nimueleze kwamba, taarifa hizi zipo ila isipokuwa *list* ni ndefu ziko ofisini anaweza akaja ofisini akaziona. Tumeshindwa kuzileta hapa kwa sababu ni ndefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Muhonga pia alizungumzia umuhimu wa ajira kwa wenye ulemavu. Nataka nimhakikishie kwamba mpango wetu wa Taifa wa kukuza ajira unagusia maeneo yote bila ubaguzi na hata walemovu na wengine ambao wako kwenye hali ambazo ni ngumu wanaguswa katika mpango huu. Kitu cha muhimu katika suala hili la ajira si nani mlemavu au hapana, ni kuangalia vile vigezo vyaa uwezo

wa kufanya kazi husika inayotakiwa katika mazingira hayo. Lakini suala la kuwaonea au kuwanyanya au kuwanyanya paa walemau kwenye sekta ya ajira kama ilivyo kwenye sekta nyingine halikubaliki hata kwenye Katiba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Muhonga aliendelea pamoja na Mheshimiwa Salum Abdallah Khalifa ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani wamesema huu Mfuko wa JK umeshiriki vipi katika kutoa ajira. Nataka nieleze kwamba kwa takwimu ambazo tumezitoa watu waliokopeshwa wajasiriamali mmoja mmoja ni 73,113 na *SACCOS* 192 na vikundi 86. Nataka niseme kwamba hata katika hawa wajasiriamali ambao wanafanya biashara na wenyewe wameongeza ajira kwenye shughuli zao. Kwa hiyo, ajira zinaweza kuwa nyingi hapa si hao 73,113 waliopata ajira tu lakini wale waliowaajiri kwenye shughuli wanazozifanya na wenyewe wamefaidika. Hizi *SACCOS* 192 zimekwenda kwa wanachama wengi. Kwa hiyo, ajira nyingi imezalishwa hapo lakini takwimu hatujazipata za kusema kwamba kila *SACCOS* imewafaidisha wajasiriamali na wana-*SACCOS* wangapi na hivi vikundi 86 je, vimeajiri watu wangapi. Lakini niunganishe hilo na la kusema kwamba Serikali imeshiriki vipi katika kutengeneza ajira kama alivyosema Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa kweli katika suala la Serikali kuhusika na ajira hizi milioni 1.3 imehusika sana. Kwanza kuna hizo ajira rasmi ambazo zimejitokeza katika sekta kama ya elimu, afya na kadhalika kwenye utumishi wa Serikali. Lakini vilevile huu Mfuko kama tulivyoona umetoa ajira kwa wingi na hata mifuko ya vijana lakini hata hizo milioni moja ambazo mnasema zimetoka kwenye sekta isiyo rasmi na sekta zingine. Serikali haijaweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi yetu ndio imewezesha biashara kufanyika, imewezesha kilimo, ufgaji, imewezesha miundombinu mawasiliano, hawa watu wanaouza vocha ni mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali ndio maana ajira hizi zimepatikana katika sekta mbalimbali. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali imeshiriki sana katika ajira zote hizi zilizojitokeza milioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Muhonga ameendelea kuzungumzia kwamba katika mifuko hii kuna watu wengine wanatoza au *SACCOS* zinatoza riba asilimia 30 mpaka 50. Kwa kweli kama linafanyika hili ni makosa. Kwa mujibu wa makubaliano hizi *SACCOS* zinatakiwa zitoze asilimia mbili tu. Sasa kama kuna watu kama wanatoza ama wajasiriamali ama *SACCOS* basi tuarifiwe ili tuweze kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar pamoja na Salim Abdallah Khalfani wamezungumzia Mfuko wa JK kule Zanzibar. Niseme tu kwamba kwa upande wa Zanzibar kwa ujumla kama tulivyo sema Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitoa milioni 600 na Mheshimiwa Aman Abeid Karume alitoa milioni 600. Hizi bilioni 1.2 zikajumuishwa na sasa zinadhibitiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Watoto kule Zanzibar. Wanaweza kupata taarifa zote. Lakini niseme tu kwamba kwa upande wa Pembe taarifa ambazo tunazo wakopaji 170 walikopa kule kwenye Wilaya za Pemba. Hivi sasa inawezekana kweli kwa upande wa wanawake na vikundi au Wilaya

moja ilipata kidogo sana lakini ni taratibu tu ambazo zinaweza zikafuatiliwa na awamu nyingine ikarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Al-Qassmy na Mheshimiwa Kimwanga walizungumzia kwamba Mfuko wa JK hazikwenda kwa walengwa. Niseme tu kwamba, kwa kweli kwa kiasi kikubwa zilikwenda kwa walengwa. Ukichukua kwa mfano, fedha zote zilizopitia *CRDB* ambazo zimekopeshwa kwa *SACCOS* wale wanachama wa *SACCOS* ndiyo walengwa tunaowaamini kwa sababu wanachama wa *SACCOS* ni watu wa kawaida. Sasa wala huwezi kusema hazikwenda kwa walengwa. Hata hawa wajasiriamali mmoja mmoja ambao *NMB* walitoa tunaamini kwamba wengi ni wale ambao walilengwa. Lakini ni kweli kwamba kuna watu wachache walitumia ule mwanya kuchukua hiyo mikopo. Lakini nadhani hayo si mambo ambayo unaweza kusema kwa jumla kwamba kwa kiasi kikubwa zilikwenda kwa wasiolengwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aggrey Mwanri katika hili amesema fedha hizi ziende kijijini kule zaidi badala ya kutumika pale mjini hasa kule kwenye Jimbo lake la Siha. Kwa kweli suala hilo ni zuri kama katika awamu zilizopita fedha hizo hazikufika kwa wanakijiji kule Siha basi awamu zinazokuja au hela hizi zikirudi sasa kuwe na utaratibu wa kuzipeleka kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selelii alizungumzia umuhimu wa Kilimo na Ufugaji katika ajira. Sisi tunakubaliana naye kabisa mkazo uelekezwe huko na wadau wote wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salimu Abdallah Khalfani alizungumzia vile vile kwamba hizi ajira zinazozungumzwa hivi ni za staha. Sisi tunataka tumhakikishie kwamba ajira hizi zote milioni 1.3 kwa mujibu wa takwimu tulizonazo ni ajira za staha au *decent work*. Kama ambavyo tafsiri ya ajira inavyoelekeza, kwa sababu kwanza zisingekuwa ajira za staha sisi tusingeweza kuchukua takwimu zake. Serikali inapiga vita ajira ambayo si staha. Kwa hiyo haiwezi kuchukua takwimu za ajira ya aina hiyo na kusema kwamba tumetoa ajira fulani kwa sababu hatuzitambui kwamba ni ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalfani vile vile alizungumzia kwamba, tutapunguza kiwango cha ukosefu wa ajira kutoka asilimia 12.9 mwaka 2001 mpaka asilimia 6.9 mwaka 2010. Ni kweli hiyo na kufikia mwaka 2006 tayari tulishapunguza asilimia 11. Sasa kuanzia hapo kwa sababu tunafanya kila baada ya miaka mitano hii *survey*, tunafikiri kwamba mwaka kesho ni miaka mitano. Kwa hiyo, tutafanya tena tuone kama tumeshatoka kwenye ile 11 tumefikisha ngapi. Lakini tunakwenda vizuri kwa maana ya kuendelea kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya vijana Waheshimiwa kadhaa walichangia, Mheshimiwa Mchemba alizungumzia kuhusu *SACCOS* za kilimo Tabora kwamba zisaidiwe mikopo ya vijana. Sisi tunakubaliana naye kwa sababu kwa kweli ndiyo nia na kwa mujibu wa taarifa tulizonazo na ambazo ni hakika *SACCOS* karibu

mbili mbili karibu za Wilaya zote za Tabora, *SACCOS* za vijana zilipata ile milioni tano tano. Ni mategemeo yangu kwamba kati ya *SACCOS* hizi mbili mbili za kila Wilaya zipo *SACCOS* zinazojishughulisha na Kilimo na Umwagiliaji katika Mkoa wa Tabora. Lakini nadhani ni jambo la msingi sana na tunakubaliana naye Mheshimiwa Mchemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jioni hii amezungumzia umuhimu wa elimu kwa vijana wanaojishughulisha na kilimo na umwagiliaji. Tunakubaliana naye kabisa na sekta zinazohusika, watu wa kilimo na wadau waohusika walizingatие hili suala la elimu kwa vijana hasa kwenye sekta ya kilimo ya umwagiliaji kwa sababu kuna utaalamu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zambi amezungumzia shamba la Sasanda kule Mbozi kuwa Serikali ina mpango gani. Nakubaliana naye kwamba kweli kwa Muda mrefu Serikali ilikuwa haijatilia umuhimu sana kwa sababu ya ufinyu wa bajeti lakini kama ambavyo yeye na mimi ni mashahidi, nilikwenda kule Mbozi Sasanda tukiwa naye na tulizungumzia sana mipango ambayo Serikali inayo na nimhakikishie tu kuwa katika bajeti ya mwaka huu tutakarabati baadhi ya majengo katika kambi ile na gharama zitajulikana baada ya *TBE* kutufanyia tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Salim Abdallah Salim alizungumzia wanafunzi kutokuwa na elimu ya kutosha, wa darasa la saba mpaka *form four* hawajui kusoma na hata wengine wa shahada ya kwanza hawajui kuandika *application letters*, jitihada zifanyike katika elimu hii ya vijana. Tunakubaliana naye lakini hapo kuna mawili; kwanza, kuna suala la elimu ambalo ukiangalia Serikali yetu sasa imeweka mkakati wa kuweka suala la taaluma katika elimu. Nadhani kadri tunavyokwenda hili la kuboresha elimu halitajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujasiriamali ni suala ambalo hata tukielimisha watu kiasi gani kwa kuwapeleka sekondari na *University* bado kutakuwa na watu ambao watatakiwa wafanye ujasiriamali hata hao wanaotoka *University*. Kwa hiyo, tusije kusema kuwa nchi hii inaweza kuwa nchi ya wafanyabiashara wadogowadogo, hapana, tutakazania elimu lakini na vilevile suala la ujasiriamali kwa vijana wetu tatalizingatia. Nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Mudhihir kuhusu ukweli kwamba juhudzi za kuendeleza vijana watu hawazioni, hawaoni mambo yanayofanyika kwenye kilimo kama nilivyo sema mazingira tuliyoweka kwenye kilimo, ufugaji, biashara, miundombinu, mawasiliano na *chain nzima* ya usambazaji wa bidhaa zote hizo imekuza ajira kwa vijana lakini watu hawaoni kuwa Serikali inafanya nini kukuza ajira ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Margaret Sitta, pongezi zake tunazipokea lakini suala la maendeleo ya vijana tunakubaliana na yeye kuwa lazima tulitilie mkazo. Mheshimiwa Dorah Mushi nakubaliana naye kwamba Maafisa Utamaduni ambao ndiyo wanashughulikia masuala ya vijana kwenye Wilaya zetu wapewe mazingira mazuri lakini kama nilivyo sema ni vema tukaajiri Maafisa Vijana katika Halmashauri zetu, tumelisisitiza sana hili na tutaendelea kuwasiliana na TAMISEMI ili kama ambavyo Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zimeajiri Maafisa Vijana na kwingine kote tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selelii amesema kuwa Mwenge unapendelea vijana kutoka Zanzibar. Ttunasema hapana kwa sababu watatu hutoka Tanzania Bara na wawili Tanzania Zanzibar na kuna *rotation* mwaka unaofuata uongozi kutoka Bara. Mheshimiwa Batilda Buriani tunakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nasema mengine yote atajibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Nakuomba wewe usiwataje majina maana wote wametajwa na mwenzio au wamekuja Wizarani maana leo tutalala humu humu, kwanza ili nisimu- *interrupt* Waziri anapoendelea kujibu kwa mujibu wa kifungu cha 104 (1) nitaongeza muda wa dakika 30 baada ya saa mbili kasorobo.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi tena ya kuja kusimama kwenye Bunge lako Tukufu ili niweze kufafanua baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza. Kabla sijafanya hivyo, naomba kwanza niishukuru sana familia yangu ikiongozwa na Mke wangu Tatu kwa kunisaidia sana na kunivumilia kwa kukosekana nyumbani kwa muda mrefu na wao wanafahamu kuwa kila ninapokosekana maana yake niko kazini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wanangu wote Zena, Bahati, Zawadi, Baraka ambaye sasa yuko huko Mahakama Kuu ya Wilaya Mpya Kaliua, mwanangu Athuman, Kulwa na Dotto wote nawashukuruni sana mmevumilia matusi mengi, vurugu nydingi kwa sababu ya Ubunge tu. Vyama visivyojua Siasa vimegeuza hata matusi kuwa ni mtaji, wanatukana biashara mnazofanya lakini vumilieni tu wanangu, narudia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Urambo Magharibi, wananchi hawa wanao mshikamano wa hali ya juu, ni wachapa kazi na wapenda maendeleo sana. Jimbo letu ni changa lakini kasi ya maendeleo yetu inatia moyo sana. Nichukue nafasi hii kuwaomba tena wananchi wa Jimbo la Urambo Magharibi ambao sasa ndiyo Wilaya mpya ya Kaliua kwamba jamani natangaza nia kuwa nakuja tena kuomba ridhaa yenu ya Jimbo kwa sababu nyie ndiyo wenyewe Jimbo, naomba tuanze kumlea mtoto huyu mchanga tuliyempata anayetwa Wilaya mpya ya Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtoto ni mchanga sana na nina hakika uzoefu nilio nao nikishirikiana na nyie ndugu zangu mtoto huyu tutakuwa tumempa mwanzo mzuri, ujenzi wa Wilaya mpya siyo kazi ya lelemama. Naomba sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo imeimariisha muono wa utekelezaji wa malengo na kazi tulizojipangia. Kwanza kabisa naomba niishukuru sana Kamati yangu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wetu Jenista Mhagama ambaye aliwasilishwa hapa. Kwa kweli Kamati hii ni Kamati mahiri sana, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, hoja alizozitoa leo zilikuwa ni za msingi, nashukuru sana hakuweka siasa naomba sana tuendelee kuilea Wizara hii kwa sababu ni Wizara ambayo inasimamia mambo mazito sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa niwatambue wale ambaao wamechangia kwa kuzungumza nao ni:-

Mheshimiwa Fatma Othman Ali kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Salim Khalfan, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Faida Bakari, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Azan Zungu, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Severina Mwijage, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Hemed Hemed, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Muhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hao wote nawapongeza kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii baada ya hapo naomba sasa nijielekeze kwenye hoja ambazo zilikuwa zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara ya kazi hoja ya kwanza iliyojitekeza ilitolewa na Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi na umma hakikidhi mahitaji halisi ya mshahara. Ni kweli kabisa kuwa kima cha chini cha mishahara hakikidhi kwa sekta zote, muhimu ni kuongeza tija kwanza na uchumi wa nchi vile vile majadiliano kati ya Vyama vya Wafanyakazi na waajiri yaendelee kuwepo ili kuboresha kima cha chini kulingana na hali ya uchumi, hoja ya pili ilikuwa majadiliano baina ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi yaendelee kufanyika ili kuboresha kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ushauri kuwa majadiliano kati ya Serikali na Vyama husika vya Wafanyakazi wa umma ni muhimu yaendelezwe ili kuboresha kima cha chini cha mshahara kwa Watumishi wa Umma kadri hali ya uchumi wa nchi itakavyoruhusu nadhani mtakumbuka kuwa Waheshimiwa Wabunge, hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Mei 3, ilikuwa inatoa mwelekeo huo kuwa majadiliano ndiyo ufunguo wa hali yoyote inayojitekeza kati ya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanne Mcchemba alikuwa na michango kadhaa kuboresha utendaji kazi wa Mahakama ya Kazi ikiwa ni pamoja na kuipatia vitendea kazi ili kuondokana na msongamano wa kesi. Ushauri umezingatiwa lakini kwa sasa Mhakama ya Kazi ipo chini ya Mamlaka ya Mahakama Kuu bila shaka watusika wamesikia, yuko hapa Mheshimiwa Chikawe. Nadhani atakuwa amesikia hilo suala.

Mheshimiwa Naibu Spika,, wastaafu kutopewa haki zao kwa wakati muafaka, hii ilikuwa ni hoja ya pili. Serikali itaendelea kuboresha taratibu za kushughulikia stahili za wastaafu kwa wakati na Wizara husika ya fedha na Mamlaka zinginezo zitazingatia wajibu huu. Lakini katika hili nataka niseme kuna *improvement* yaani kuna hali nzuri sana kwa hivi sasa, kwa mfano, wale wanaofanya kazi katika sekta ya umma kabla ya miezi sita kufikia umri wa kustaafu wanapewa *notice* kwamba sasa anza kijiandaa, wakikamilisha ile miezi sita wanakwenda kwa yule Mkurugenzi wa PSPF, cheki yao kama hawakupata siku ile ile wanapata siku ya pili. Katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii wastani wetu ni wiki mbili. Kwa hiyo, kuna maendeleo makubwa sana katika kuboresha hatua hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa kuwepo na Sheria mpya ya fidia ili kuwezesha mfanyakazi kulipwa fidia aumiapo au kupata ajali akiwa kazini. Ni kweli Sheria ya zamani imepitwa na wakati, Sheria mpya ya Fidia kwa wafanyakazi namba 20 ya mwaka 2008 ilishapitishwa na Bunge hili Tukufu, Sheria hii itaanzisha Mfuko Maalumu wa Fidia na kuboresha viwango vya malipo na fidia kwa wafanyakazi na katika kanuni ambazo tumetengeneza, inatengeneza hata namna ya kumlea mfanyakazi kama ana magonjwa ya kudumu mpaka hapo atakapofariki. Kwa hiyo, ni mambo mazuri sana ambayo yapo katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ni mgogoro wa Kiwanda cha Nyuzi Tabora. Wafanyakazi kupewa likizo bila malipo na pia kuachishwa kazi bila stahili. Kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanne Mcchemba katika hili maana yake ni mfuatilaji mzuri sana wa kiwanda hiki. Mgogoro huu Mheshimiwa Mcchemba unahusisha wafanyakazi 126 na siyo 300 uliwasilishwa katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na Tume iliamua kuwa wafanyakazi waachishwe kazi na walipwe haki zao. Mwajiri hakuridhika na uamuzi huo na ameomba marejeo katika Mahakama Kuu, *Division* ya Kazi kwa sababu tunaongozwa na Sheria, acha hilo lichukue mkondo wake, lakini kama Wizara ya Kazi tulishalitolea maamuzi kuwa waachishwe kazi lakini walipwe mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, sababu zinazopelekea kuwapo kwa migogoro baina ya waajiri na wafanyakazi kuhusu mishahara na marupurupu ni ukosefu wa mbinu za majadiliano mionganoni mwa waajiri na wafanyakzi na pia wafanyakazi kutokuwa na uelewa kuhusu tija. Nakubaliana na Mheshimiwa Mudhihir, kwa sababu hizo, Wizara itaboresha mikakati yake katika kuwajengea wadau wote uelewa wa Sheria, kanuni na mbinu mbalimbali na za kisasa kuhusu suala zima la majadiliano ya pamoja na hatimaye ulazima na umuhimu wa tija ufahamike na kueleweka vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii ana hoja mbili, migogoro ya wafanyakazi inapaswa kuangaliwa kwa kina, ushauri umepokelewa na Mamlaka zinazohusika tutaziarifu ikiwemo pamoja na Taasisi za Wizara ya Kazi. Hoja ya pili, malalamiko ya makato ya kodi na fedha wanazopata wafanyakazi baada ya kustaa fu iangaliwe, hii ilikuwa ni moja ya ajenda ambazo wafanyakazi walikuwa wamewasilisha katika yale majadiliano ya pamoja na nina hakika hili lilipatiwa ufumbuzi kwa kiasi fulani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nadhani atalizungumza hili au alishalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khadija Al – Qassmy alisema watoto bado wanatumikishwa na Serikali lazima iongeze jitihada za kutoa elimu kupitia vyombo vya habari na vipeperushi. Ushauri umezingatiwa na Wizara itaendelea na juhudzi za kupambana na ajira mbaya na utumikishwaji wa watoto. Juhudi hizo ni pamoja na kutoa elimu, kuwaondoa watoto walio katika ajira kama nilivyoeleza katika hotuba yangu na kuwapatia mafunzo mbadala, kuwarejesha mashulenii kwa kushirikiana na wadau wengine, Wizara inajenga pia uwezo wa wazazi wa watoto hao ili waweze kujenga uwezo kuondokana na dhana ya kuwategemea watoto wao kupitia ajira zisizofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo anasema Serikali itoe tamko la kima cha chini cha Mshahara. Tangazo la Serikali la Mishahara kwa Sekta Binafsi namba 172 lilitolewa tarehe 30 Aprili, 2010 na kuanza kutumika tarehe 1/5/2010. Kuhusu kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa umma, Waziri mwenye dhamana alishatangaza lakini kuna makubaliano maalum kati ya Serikali na Watumishi wa Umma kwamba usitamke kiwango, unapotamka unatuangamiza, kule tunakotoka mwenye nyumba akisikia kuwa mshahara umepanda na yeze anapandisha kodi, watu wa mabasi na wao wakisikia mshahara umeongezeka na wao wanapandisha. Kwa hiyo, tuambie tu kama tulivyoelewana ndio maana unakuta kwamba hali hii imetulia kwa sababu wafanyakazi wanajua kupitia viongozi wao kuwa walizungumza nini na wakakubaliana nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye hoja ambayo ilijitokeza katika Shirika letu la NSSF. Hatua iliyofikiwa katika uendelezaji wa daraja la Kigamboni, hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Salum Abdalah, Mheshimiwa Khalfan, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Khadija Al- Qassmy, Mheshimiwa Hemed Hemed Mbunge wa Chonga na hao ndiyo waliochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliagiza mradi huu utekelezwe kwa utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP)* kwa kuwa uraratibu huu ni mpya nchini mwetu NSSF ililazimika kuteua Kampuni *CRISIL Risk and Infrastructure Solutions Limited* ya India kwa ajili ya kutoa ushauri kwa ajili ya kumpata mbia wa kushirikiana na NSSF. Majukumu makuu ya mshauri huyu ni kufanya mapitio na upembuzi yakinifu 2005 kutengeneza makabrasha ya kumpata Mbia na kutayarisha rasimu ya mkataba kati ya NSSF na mbia. Aidha, mshauri huyo atasaidia NSSF katika taratibu zetu za kumpata mbia pamoja na wakandarasi wa mradi tunachozungumza hapa ni kwamba itabidi yeze atusaidie kutengeneza *tender documents*, atusaidie kutathmini, atusaidie kuchagua majadiliano na atakayechaguliwa na vile vile asaidie utiwaji saini ili mambo yaanze kwa huyu mbia na vile vile kwa mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yote haya yatakuwa yamekamilika ifikapo mwezi February mwaka 2011 ambapo ujenzi wa daraja utaanza. Gharama za awali za upembuzi yakinifu zitajumuishwa katika gharama za mradi ambazo zimefanywa na NSSF.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa utiaji wa sahihi wa mkopo wa ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma. Ni kweli kabisa kuwa hii hoja imechangiwa na Mheshimiwa Salum Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Khadija Al- Qassmy. Ni kweli lipo tatizo hilo kuhusu mkataba na NSSF Kwa ajili utekelezaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Wizara yangu imekiria kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuhusu mkataba huo. Aidha, tarehe 31 Mei, 2010, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Mkulo kuhusu suala hili na napenda kusema sasa limefikia mahala pazuri kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameahidi kulifua tilia kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu mkopo wa dola za Kimarekani milioni saba kwa kampuni ya makaa Kiwira. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Salum Abdallah Khalfan na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Shirika la NSSF lilitoa mkopo wa dola milioni saba kwa kampuni ya makaa ya Kiwira kwa nia ya kupanua uwezo wa kuzalisha umeme, mkopo huu umedhaminiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Mradi huu ultakiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za NSSF pamoja na mbia *Strategic Investor* kutoka nje, utekelezaji wa mradi umechelewa kutokana na kuchelewa kukamilika kwa upatikanaji wa mbia huyo pamoja na matatizo mengine matatizo haya yaliifanya Serikali kuamua kuuchukua mgodi huu kutoka kwa mwekezaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mdhamini wa mkopo huu ni Serikali kwa asilimia mia moja, tuna uhakika kuwa watakapokuja kumpata mbia NSSF watalipwa dola zao milioni saba baada ya kukamilika kwa kurudishwa mradi Serikalini, Shirika litalipwa fedha zake zote kama ilivyo katika miradi mbalimbali ya Serikali inayofanywa na NSSF.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kupanua huduma ya Hifadhi ya Jamii kwa walio wengi, imechangiwa na Mheshimiwa Fatma Othmani, Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii NSSF pamoja na Taasisi zingine za Hifadhi ya Jamii nchini chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana zinafanya juhudu kubwa kupanua huduma za Hifadhi za Jamii nchini. Idadi ya wanachama imeongezeka kutoka 799,138 mwaka 2007 hadi kufikia 971, 283 mwaka 2009 juhudu hizi ni pamoja na kuongeza utoaji wa elimu ya hifadhi ya jamii, kufanya utafiti kuhusu kuboresha mafao pamoja na kufanya marekebisho mbalimbali ya Sheria kwa nia ya kupanua na kuboresha huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa ofisi ya Mdhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority*).

NAIBU SPIKA: Mtoa hoja wanasema hawakusikii.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatua kubwa katika juhudzi za Serikali za kuboresha na kupanua huduma za Hifadhi ya Jamii nchini. Pongezi kwa jengo la Machinga *NSSF* ijenge *Complex* hizi katika Mikoa mingine na Rukwa. Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Hemed Hemed pongezi zimepokelewa, utafiti utafanyika kubaini faida za kibiashara katika mikoa mingine ukiwemo Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pongezi kwa *NSSF* kwa kazi nzuri na ujenzi wa nyumba za bei nafuu na Chuo Kikuu, Dodoma, ilichangiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti maalum, pongezi zimepokelewa, tunashukuru sana, Mheshimiwa Mhonga anauliza uwekezaji usio na tija katika makampuni ya Tanzania *Oxygen*, *TANRIS*, *First Adili Bank Corporation*, Mbeya *Cement*, *Ubungo Plaza*, *EPZ*, *Quality*, *PPL*, ukiacha Tanzania *Oxygen* ambayo juhudzi za kuifanya itoe faida zinaendelea makampuni mengine yaliyobaki yameanza kutoa faida, *NSSF* tayari imepata imepata gawio kutoka *TANRIS* na *First Adili* ambayo sasa hivi inaitwa *Azania Bank Limited* na vile vile Mbeya *Cement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa kituo cha Kimataifa cha mabasi, Mwandiga Kigoma. Hii ilikuwa ni hoja ya pili. Mheshimiwa Muhonga na Waheshimiwa Wabunge nataka kuwafahamisha kuwa mradi huu utatekelezwa baada ya kukamilika upembuzi yakinifu kwani nia ipo tunachosubiri ni kukamilika tu kwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa *NSSF* kwa kazi nzuri kwa ujenzi wa nyumba za Polisi, Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Hii hoja imetolewa na Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mbunge wa Chonga, pongezi tunazipokea, ahsante sana.

Katika Kitengo chetu cha *CMA*, Mheshimiwa Fatma Athuman Ally, Viti Maalum alikuwa na hoja mbili, Serikali kuongeza fedha kwa ajili ya uimarisaji wa Tume ya Usuluhishi na Uamuza (*CMA*). Nimepokea ushauri huo na naunga mkono kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi ione umuhimu wa kuwaongezesa Tume hii fedha iweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kwa kweli nia ya Serikali ipo ila mwaka huu ni kwa vile majukumu yameongezeka sana na ukizingatia kwamba kunakuwa na Uchaguzi Mkuu. Lakini nina hakika kwa jicho la Wizara ya Fedha na jicho la Serikali kwa ujumla wana nia ya kuimarisha Tume hii ili iweze kufanya kazi yake sawasawa kwa sababu ni mhimili muhimu katika kuimarisha amani na utulivu mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa elimu kwa wafanyakazi na waajiri ili kuwajengea uwezo wa kufahamu haki na wajibu wao mahali pa kazi. Wizara na Taasisi zake zitaendelea kutekeleza jukumu hili la kuelimisha wadau mbalimbali hususan sekta ya kazi na ajira ili kuwajengea uwezo katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika ulimwengu wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shirika letu la aina ya ‘P’ Shirika la Tija la Taifa, kulikuwa na hoja mbili, hoja ya kwanza ni ya Mheshimiwa Salim Abdallah

Khalfan, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani, anasema Wizara ilitakiwa kusimamia mipango ya uboreshaji wa tija na ufanisi kazini ili kukuza uchumi nchini kupitia Shirika la Tija nchini aina ya ‘P’. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu tathmini ya tija ya Watumishi inapimwa vipi kwani suala kubwa ambalo bado linasumbua katika sekta ya umma ni utumishi usiokuwa na tija. Aidha, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwa vipi tija inaweza kupatikana bila kuwepo na motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa motisha kwa wafanyakazi katika sekta zote za uchumi katika Taifa hili, ili utumishi wa wafanyakazi wote uwe na tija. Tathmini ya tija kwa watumishi ni pale ambapo watumishi wametumia nyenzo za kazi kwa ufanisi. Wizara yangu inawahimiza waajiri wapate huduma ya uwekaji wa malengo ya kazi pamoja na utumiaji wa mifumo ya vivutio vya ufanisi kutoka Shirika la Tija la Taifa la aina ya ‘P’ ambalo Wizara yangu iko mbioni kuliimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hoja ya pili ni kutoka kwa Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani, anasema taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkoo wa Hesabu za Serikali imebainisha kwamba matatizo yanayojitokeza ya ubadhirifu yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na watumishi kutokuwa na motisha ya kazi wanayoifanya, jambo ambalo linapelekea kuwa na wizi na udokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na motisha kwa wafanyakazi, tatizo la udokozi na wizi ni la tabia na linahitaji elimu ya wafanyakazi na kuamsha ari ya uzalendo ili kuliondoa, ni muhimu sisi wote Wabunge kwa ujumla wetu tukalipiga vita suala hili, tusilee hali ya udokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia, Mheshimiwa Maida Abdallah amesema tuangalie sana suala la baadhi ya waajiri kupenda kuajiri wageni. Nitasoma hapa hoja ya Mbunge mmoja bila kutaja jina lake anasema hivi, naomba kutoa mchango wangu niliobakiza kwa kuzungumza, tatizo kubwa na uvivu na uzembe kwa vijana wetu wa Kitanzania utakuta hoteli nyingi za kitalii kule Arusha zimejaa waajiriwa wageni, Wakenya mpaka hata wahudumu ukiuliza kulikoni, waajiri wanasema Watanzania wakiajiriwa leo wiki inayofuata wanaacha kazi, kwanini wanasema ni wavivu, hawawajibiki na wanasema kazi hizi za kufanya usafi ni za kuwdhalilisha. Wakenya wanaomba kazi kwa kujitolea lakini wanaajiriwa hata kabla muda wa kujitolea haujakwisha wanapata kuajiriwa moja kwa moja. Wanawajibika sana na wanafanya kazi kwa bidii. Watanzania wanabaki bila ajira kutokana na uvivu na uzembe wao. Vijana wa Kitanzania tusiwaacie ajira zetu wageni. Hii ni hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo kwa vijana wetu. Wanachagua kazi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge hapa, hivyo tunalo tatizo la uadilifu na uaminifu kazini, tuna tatizo la *attitude* katika kufanya kazi. Kwa hiyo, nasema haya yanayoonekana ni bora tuyafanyie kazi kwa pamoja, kianzishwe kituo au chuo cha kushauri vijana waajiri. Nilipokuwa nikitoa hotuba yangu nilisema moja ya vitu ambavyo tunavikusudia kuvifanya katika moja ya vitengo vyetu ni kuratibu mchakato wa uanzishwaji wa kituo cha mafunzo kuhusu masuala ya ajira, *National Centre of*

Employment Studies ambacho kitasaidia kutoa elimu na taarifa kuhusu masuala ya ajira kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Halmashauri, Taasisi za Serikali za binafsi, Vyuo, *NGOs* na washirika wa maendeleo. Kwa hiyo jambo hili tumeshaanza kulishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo cha Ukaguzi kiongozewe fedha ni kweli, kwa Wizara nzima tunahitaji kuongezewa fedha, bodi za kisekta ziboreshweli ili zipange vizuri mishahara, ni kweli mtakumbuka tulipata tatizo sana baada ya kutangaza vima vya mishahara hapo mwanzoni kwa sababu bodi za kisekta ziliundwa haraka zikapewa muda mfupi, fedha chache, matokeo yake mapendekezo yaliyotolewa mengi yalikuwa hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro ya Wafanyakazi inatokana na waajiri wakorofii kutokujali haki za wafanyakazi, *GN* ikishatolewa iheshimike na waajiri. Nasema hivi kama kuna mwajiri ambaye hatekelezi *GN* 172, tuambieni tutakwenda kumshughulikia. Vima vya fidia viro chini, hili nadhani tumeshazungumza kwamba sheria inazingatia. Pia, anaomba wafanyakazi wajijunge na Vyama vya Wafanyakazi, nakupongeza kwa hilo, kwa sababu kwa kweli bila kujiunga wataendelea kubaki dhaifu na hili tunalifanya kazi sana kwa kuwapa elimu wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa ofisi ya kazi Tabora. Nakushukuru Mheshimiwa Mwanne Mchemba kwa kuona kwamba tumefanya kitu vizuri na tutajitahidi kukamilisha mengine kutoana na uwezo au bajeti itakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya kazi imalize kesi haraka.....

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja(*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)
KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tulishaongeza dakika thelathini kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1)

Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kif.1001 - *Administration and General... Sh.1,358,176,000/=*

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

Kif. 1001 - *Administration and General... ... Sh. 2,032,898,200/=*

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Naomba ufanuzi kutoka kwa Serikali kwa sababu toka mwaka 2006 ndani ya Bunge lako Tukufu wakati huo Naibu Waziri akiwa ni Mheshimiwa Nicodem Nsanzugwanko alituahidi kwamba mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana uko katika hatua nzuri na nyaraka zimeandaliwa ziko zinakwenda kujadiliwa katika Baraza la Mawaziri na haraka iwezekanavyo italetwa sheria kuhusu uundwaji wa Baraza la Vijana. Nataka kufahamu uundwaji wa Baraza hilo umeishia wapi? Maana yake sasa ni karibu miaka mitano na hajatekelezeka.

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kati ya maswali ambayo hatukuweza kuyazungumzia kwa sababu ya muda ilikuwa ni hilo la Baraza la Vijana ambalo liliulizwa pia na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani. Nieleze tu kwamba si kweli kwamba kuna mbinu zozote za kukataa kuanzisha Baraza hili, isipokuwa baada ya mchakato kuanza tulipofika katikati kukawa na umuhimu wa kushirikisha zaidi wadau na hasa makundi ya vijana katika mchakato huu. Mikutano ya mwanzo iliyofanyika ilijidhihirisha kwamba kulikuwa na mambo ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuligundua kwamba hata sera ya vijana ya mwaka 2007 ilikuwa hajaeleweka vizuri kwa vijana nchini. Huu ni msingi mkubwa sana wa kuanzisha hata Baraza hilo. Lakini baadaye ikaonekana kwamba mchakato huu unatakiwa uanzie kwenye ngazi za chini Wilayani na Mikoani tupate mapendekezo kutoka chini kuja juu na baadaye tufike mahali tuwe na Baraza ambalo kwa kweli litakuwa linawakilisha maslahi ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu unaendelea vizuri na ushirikishwaji utaendelea. Tumekuwa tukikwazwa na fedha lakini nadhani kadri tunavyokwenda tunafika mahali tutakuwa na Baraza hilo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Waziri alipokemea na akasema kwamba anatafuta njia ya kuondoa watoto katika ajira. Lakini kuna tatizo ambalo lipo mbele yetu mwaka hadi mwaka, tunaona watoto zaidi wa shule za msingi wanatumika kuhamisha Walimu, tunaona watoto wanatumika kuvuna karanga za walimu, tunaona watoto wanatumika kuvuna pamba, kuchota maji na hawalipwi na pia tumetunga sheria ya kuhakikisha watoto wanafanya kazi ya kusoma au kucheza, Serikali inasema nini juu ya hili?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nifafanue suala alilozungumzia Mheshimiwa Cheyo. Sheria ya haki za mtoto ya mwaka 2009 ina kipengele kinachoruhusu watoto kufanya kazi kulingana na umri wao kama zinahusu

faida yao wenyewe. Kwa hiyo, tuangalie sana tunapajaribu kuilewa hii sheria, si kwamba inakataza watoto kufanya kazi kabisa. Kazi zinazokatazwa ni zile za kushurutishwa au za kuzidi umri wao. Lakini kipengele kipo ambacho kinaruhusu watoto nao wasaidie familia zao kulingana na umri wao na uwezo wao. Kwa hiyo, kama Kamati ya shule imeruhusu kwa mfano, labda kuvuna pamba lakini kwa matumizi ya shule basi inaruhusiwa ili mradi tu isizidi umri lakini pia isiwe ya kibiashara. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Halafu usiwatoe watoto darasani wakafanye kazi hiyo.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sheria ukitaka kuzitafsiri vibaya maana yake tutajijengea mazingira ambayo hata watoto wetu majumbani, tutashindwa kuwafundisha kazi. Kwa hiyo, zipo kazi ambazo mtoto atalazimika kufanya ili hatimaye aje kuwa ni mtu anayeweza kujitegemea. Kazi ambazo zinajumuisha katika malezi, hizo hatuzikatazi, tunazozikataza ni kwamba unaamka asubuhi, unamtuma mtoto nenda kaombe barabarani, nenda kavune tumbaku kwa mtu, halafu utaleta hela, tutagawana hiyo tunakataza na kwenye madini na kadhalika.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufanuzi kupitia kwa Waziri kuhusu mfuko wa Vijana ambao unatengwa kwenye Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji, asilimia tano ktokea kwenye vyanzo vyao vya mapato lakini pia huwa kuna *support* ya Serikali kwa kila mwaka. Napenda kujua hiyo *support* ya Serikali katika mfuko huu wa vijana kama wanavyofanya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mpango huo bado upo na ni kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Diana aliuliza swali hilo, labda niseme tu kwamba ile asilimia tano yenyewe hutengwa na Halmashauri zetu kwa mujibu wa taratibu za Wizara ya TAMISEMI. Nadhani tutawasiliana nao tuone kama mifuko hii au asilimia hii inaendelea kwa utaratibu gani. Lakini ninachojuwa hii mifuko ni *revolving*, inatakiwa ifike mahali isiendelee kutengwa, zile zile ambazo zimebekwa ziweze kukopeshwa, lakini kutoka Wizarani sasa ndiyo mfuko wa vijana ambao unatoka kwenye Wizara yetu inasaidia katika huo mfuko. Huu wa kutoka Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana tumewekea sasa utaratibu tofauti ndiyo tunapeleka kwenye SACCOS mbili kila Wilaya kwa sasa, milioni tano, milioni tano zimetoka katika utaratibu ule uliopita. Kwa hiyo, kuna mifuko miwili, mfuko wa Wizara ya Kazi ambao unakwenda kwenye SACCOS mbili kila Wilaya na hiyo ya Halmashauri ambayo inasimamiwa na TAMISEMI.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru sana Naibu Waziri Dr. Mahanga kwamba alikuja Mbozi na akapata nafasi ya kutembelea kambi ya Vijana ya Sasamba, Mbozi.

Pamoja na shukrani hizo, nimepata wasiwasi kwenye majibu yake alipokuwa anazungumzia shamba la kambi hiyo kwamba majengo yatakarabatiwa baada ya TBA kufanya tathmini yake. Hili limenipa wasiwasi na inaonesha kwamba hata pesa kwa ajili

ya kazi hiyo hazijatengwa. Naomba ufanuzi *TBA* watafanya tathmini hiyo lini na kama ni mwaka huu pesa zitapatikana kwa ajili ya kukarabati majengo ambayo yeye mwenyewe ni shahidi aliyona yakiwa katika hali mbaya sana.

NAIBU WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeye. Kwanza nikiri kwamba ni mwaka huu wa fedha kwa sababu ndiyo kwanza tunaanza mwaka na bajeti ndiyo tunaipitisha leo, basi taratibu zitaanza baada ya hapo kutegemea tu na ile *flow* ya pesa na taratibu zingine za kuwaelekeza *TBA* waanze hiyo kazi. Lakini tumesema katika mwaka huu wa fedha wa 2010/2011.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ...	Sh. 283,518,300/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> ...	Sh. 403,936,200/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> ...	Sh. 115,778,900/=
Kif. 1005 - <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh. 150,491,900/=
Kif. 1006 - <i>Information Educat. and Comm. Unit</i> ...	Sh. 97,461,500/=
Kif. 2001 - <i>Labour</i> ...	Sh. 3,025,341,500/=
Kif. 2002 - <i>Employment Division</i> ...	Sh. 1,960,788,100/=
Kif. 2003 - <i>Registrar of Trade Unions</i> ...	Sh. 122,207,200/=
Kif. 5001 - <i>Youth Development</i> ...	Sh. 813,499,200/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 15 - Tume ya Usuluhihi na Uamuzi

Kif.1001 - *Administration and General* ... Sh.676,500,000/=

Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

Kif. 1001 - <i>Admnistration and General</i> ...	Sh.200,000,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> ...	Sh.4,924,567,000/=
Kif. 2001 - <i>Labour</i> ...	Sh.778,463,000/=
Kif. 2002 - <i>Employment Division</i> ...	Sh.0/=
Kif. 5001 - <i>Youth Development</i> ...	Sh.737,627,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge imeyapitia makadirio ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira
na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa
Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana Makadirio yake yamepitishwa rasmi na Bunge hili. Naomba niwapongeze Waziri na Naibu wake na Watalaam wake wote kwa kazi nzuri wanazozifanya na tunaomba waendelee hivyo hivyo. Nilikuwa naongea na Waziri wa Fedha kwamba lile tazito la Mifuko ya Jamii kwamba watu wanafanya kazi halafu wanaingia *bond* na Serikali pengine lipatiwe ufumbuzi kwa sababu litaharibu sifa nzuri ya kazi inayofanyika. Nadhani Waziri ameahidi kwamba atafanya hivyo. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge jambo lingine wiki hii nadhani mliona kwamba Dr. Abdallah Kigoda na Dr. Aisha Kigoda walipotea kwa muda hapa, walikuwa wamefiwa na mdogo wao kabisa. Kwa hiyo, namwona Dr. Aisha Kigoda amerudi lakini tunapenda kwa niaba ya Bunge zima kuwapeni pole sana kwa familia yenu, mvute subira. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa siku ya leo, mimi mwenyewe ilinitanisha sana maana Wizara hizi ni kubwa na zikaunganishwa siku moja, nikawa sielewi kwamba tunakesha humu au vipi. Lakini naona kwa busara yenu hatukuweza kukesha, tuko katika muda tulioomba. Kwa hiyo, kwa sasa naomba nahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.05 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,

Tarehe 9 Julai, 2010, Saa Tatu Asubuhi)